**13 FEBRUARI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 13 Februari, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**MHE. AZIZA S. ALLY K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, namuita Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini, sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Chumi.

Na. 172

**Ujenzi wa barabara za Mradi wa *TACTIC* – Korogwe**

**MHE. COSATO D. CHUMI K.n.y. MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Kibo – Mgombezi – Bagamoyo na *NMB* Benki hadi Magunga hospitali zilizo kwenye mradi wa *TACTIC*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofis ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za Kibo - Mgombezi - Bagamoyo na *NMB* Benki hadi Hospitali ya Magunga zipo kwenye utekelezaji wa mradi wa *TACTIC* kundi la pili *(Tier 2)*. Kundi hili linatekelezwa kwenye Miji 15 ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Korogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kazi ya usanifu wa miradi ya ujenzi wa barabara kupitia kundi la pili *(Tier 2)* unaendelea kutekelezwa na Wahandisi Washauri ambapo tayari walisaini

mikataba tarehe 15 Disemba, 2023 na itafanyika kwa kipindi cha miezi nane ambapo kitakamilika mwezi Agosti, 2024. Aidha, usanifu wa miradi hiyo utakapokamilika Agosti, 2024 kazi ya kutangaza zabuni itaanza Septemba, 2024.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, je, Serikali kwa sababu miradi hii pamoja na mambo mengine itajenga pia vitega uchumi ambavyo vitakuwa vinazisaidia Halmashauri zetu kupata mapato ya ndani. Je, Serikali iko tayari kuharakisha mchakato ule hasa mara baada ya kutangazwa zabuni?

Swali la pili, kwa kuwa Mafinga ni mnufaika wa mradi huu lakini katika *tier* ya tatu; je, Serikali iko tayari ku-*fast track* ili ile *tier* ya tatu na yenyewe iende sambamba na hii *tier* ya pili kusudi kuwawezesha Wananchi wa Mji wa Mafinga kupata barabara na kujengewa stendi na kujengewa pia mradi mmoja ambao utakuwa ni chanzo cha mapato ya ndani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cosato Chumi, kwanza hili la Serikali kuharakisha zabuni hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishasema kwenye majibu yangu ya msingi, mara pale ambapo hawa Wakandarasi Washauri watamaliza kufanya usanifu ule mwezi Agosti mwaka huu, mwezi Septemba zabuni zile zitatangazwa ili waweze kupatikana wakandarasi wa kujenga miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii si tu kwa barabara tayari usanifu unafanyika pia katika ujenzi wa masoko na ujenzi wa

stendi katika maeneo mbalimbali hapa nchini ambayo yamo katika *tier 2*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili ni kwamba Mji wa Mafinga kweli upo kwenye *tier 3* na mara baada ya usanifu kukamilika kwenye *tier 2* mwezi Agosti, sasa usanifu utaanza kwenye *tier 3* ambayo ni Miji 18 ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Mafinga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Barabara ya kutoka Chemba – Soya – Mwailanje – Zajilwa – Dodoma na Zajilwa ni Jimboni kwake, kwa sasa imeharibika sana, naomba sasa *commitment* ya Naibu Waziri mwenyewe, ni lini barabara ile itajengwa ili ipitike wakati wowote? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monni, nikiri kwamba alipotaja Zajilwa na Itiso zimo katika Jimbo langu la Chamwino na barabara hii ya Chemba – Soya – Mwailanje itaanza ukarabati wake mara moja. Ipo katika bajeti ya mwaka huu wa 2023/2024 na tayari Meneja Maganga pamoja na Lamela - Meneja wetu wa Mkoa na Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Chemba, wameshakaa na kuona ni namna gani wanaanza utekelezaji wa ujenzi wa barabara hii, hasa katika maeneo ambayo ni korofi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Hali ya barabara za Halmashauri ya Mji wa Ifakara katika Kata 19 ni mbaya sana kutokana na mvua hizi. Naishukuru Serikali

kwa kutuletea fedha za kujenga kwa lami barabara za Ifakara Mjini, lakini barabara zimejengwa chini ya kiwango na ni mbovu. Naomba kujua Serikali itachukua hatua gani kwa wakandarasi ambao wamejenga Barabara ya Kibaoni na Ifakara Mjini sokoni ambazo mpaka sasa hivi zimeshaharibika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asenga, naomba nitumie Bunge lako Tukufu hili kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Morogoro kuhakikisha Mkandarasi ambaye alijenga barabara hizi alizozitaja Mheshimiwa Asenga, kama mkataba wake ulikuwa bado haujaisha, aweze kurudi na kurekebisha yale maeneo ambayo tayari yameharibika bado barabara ni mpya kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant Daud, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wananchi wa Kata za Igalula, Goweko, Loya, Viswaki na Mienze mpaka leo wanashindwa kupata huduma kwa sababu ya uharibifu wa Barabara za Goweko, Ndevelwa, Mpumbuli, Mienze, Misole na Miswaki na Waziri wa Fedha alituahidi hapa atatoa fedha za ziada za matengenezo kabla ya Bunge hili, mpaka leo fedha hizo hazijaenda na siku tatu Bunge linafungwa.

Je, ni lini fedha zitakwenda haraka kuweza kurekebisha miundombinu ambayo sasa wananchi hawatoki kwa sababu ya uharibifu mkubwa wa barabara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge naona swali hilo ni la Wizara ya Fedha.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Hapana!

**MWENYEKITI:** Sasa usibishane na Kiti ndiyo natoa maelekezo, Naibu Waziri kama una majibu lakini nadhani hilo litaenda Wizara ya Fedha, ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na swali namba 174 halafu tutaenda swali namba 173. Namwita Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, sasa aulize swali lake.

Na. 174

**Barabara ziendazo maeneo yenye mazao ya kimkakati – Lupembe**

**MHE. EDWIN E. SWALLE** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kujenga barabara ziendazo maeneo ya mazao ya kimkakati kama chai, kupitia mradi wa *Agri-Connect* - Lupembe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Jimbo la Lupembe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* imeainisha barabara zinazopita kwenye maeneo ya mazao ya kimkakati, ikiwemo zao la chai katika Jimbo la Lupembe, ambazo zina urefu wa jumla ya Kilometa 182.5. Kwa Mwaka wa fedha 2023/2024, usanifu wa Barabara ya Ukalawa – Kanikelele – Lupembe yenye urefu wa Kilometa 18.5, upo hatua za mwisho kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na mpango wake wa kutenga bajeti ili kuboresha barabara kwenye maeneo ya mazao ya kimkakati ikiwemo Jimbo la Lupembe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Enosy Edwin, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kutukumbuka watu wa Lupembe kupata barabara ya *Agri-Connect*. Sasa, hii Barabara ya Lupembe – Kanikelele – Ukalawa ambayo ni Kilometa 18.5 inaishia nyuma kidogo ya Makao Makuu ya Kata ya Ukalawa, umbali kama wa Kilometa moja tu kwenye Makao Makuu ya Kata ya Ukalawa yenyewe.

Je, Serikali haioni haja ya kuongeza hii Kilometa moja ili wafikishe pale Makao Makuu ya Kata ya Ukalawa yenyewe? *(Makofi)*

Swali langu la pili, ziko barabara kwa mfano ya pale Lupembe Jimboni, kupita kwa Mzee Msambwa kwenda Idamba, kwenda mpaka Mfiriga. Ni lini barabara hii na yenyewe itafanyiwa usanifu na kuanza ujenzi wa lami? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Swalle, swali lake la kwanza hili la kilometa moja hii ya nyongeza katika zile kilometa 18.5 ili kuweza kufika katika Makao Makuu ya Kata ya Ukalawa, nimtoe mashaka Mheshimiwa Swalle kwamba, mradi huu wa *Agri-Connect* upo katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya pamoja na Songwe. Hivyo basi, katika usanifu wa awamu inayofuata nitahakikisha kwamba na hicho kipande pia kinaweza kumalizika kuweza kufika katika Makao Makuu ya Kata ya Ukalawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la usanifu kwa barabara nyingine ambazo amezitaja. Kama ambavyo nimemjibu swali lake la nyongeza la kwanza, katika hatua inayofuata Serikali itaangalia kwa sababu mradi huu bado upo, ni kweli wanazalisha sana chai katika Jimbo lake kule la Lupembe, Serikali itaangalia pia barabara hizi ambazo zimesalia ili ziweze kuweka katika mipango inayofuata. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mrimi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa ajili ya kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii, je Serikali ina mpango gani wa kufanya marekebisho katika barabara za Kata ya Nyamoko, Kisangura, Tarafa ya Ngoreme na Tarafa ya Ikorongo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Dkt. Mrimi, kwanza kuhusu hili la marekebisho, kama ambavyo tulizungumza hapa awali katika Bunge hili ambalo linaendelea kwamba, Serikali ilikuwa katika mchakato wa kuhakikisha *TARURA* inaletewa fedha ya dharura haraka.

Mheshumiwa Mwenyekiti, tathmini imefanyika kote nchini, tathmini ile ilikamilika mwisho wa mwezi Januari mwaka huu wa 2024, ikiwemo kutoka kule kwa Mheshimiwa Mrimi, hivyo basi fedha ile ambayo itapatikana itaenda katika maeneo yale kuweza kuanza kurekebisha barabara zote korofi, ikiwemo kule Jimboni kwa Mheshimiwa Mrimi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lazaro, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kupitia Mradi wa *Agri-Connect* tulikuwa tumeomba Kilometa 15 ambazo zimo tayari kwenye bajeti ya *Agri-Connect* zijengwe kutoka Kilolo hadi Kidabaga ambapo ndiko shamba la chai lilipo.

Je, Serikali ipo tayari kufuatilia ili mradi huo uanze kutekelezwa kwa haraka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Nyamoga kwamba, mradi huu ulipoanza *(Agri-Connect)* Mkoa wa Iringa ulikuwa ni Mkoa wa kwanza kabisa kuanza utekelezaji. Vilevile, niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Mheshimiwa Nyamoga alikuwa *beneficiary* wa kwanza kabisa wa ujenzi wa barabara hizi za *Agri-Connect* katika Jimbo lake. Hivyo basi, Serikali pia italiangalia hili la barabara ya Kilolo kwenda Kidabaga ambapo kuna uzalishaji mkubwa wa chai katika awamu ambayo inafuata kama nilivyomjibu Mheshimiwa Swalle ili kuziweka katika mpango na barabara hizi ziweze kujengwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Barabara ya Orbesh ambayo inatoka kwenye Kata yako kuja Bashneti na kwenda mpaka Haiderere iliahidiwa na Katibu Mkuu kujengwa na sasa hivi hali ni mbaya.

Je, ni lini *TARURA* itakwenda kujenga barabara ile ili wakulima wapate nafuu ya kuleta mazao yao?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri umesikia vizuri eeh? Naomba majibu. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Flatei akiuliza kwamba barabara hii inaanzia kwenye, Jimboni kwako Kata yako ya Orbesh na kuelekea Bashneti ambako anatoka yeye Mheshimiwa Flatei. Nitakaa na Mheshimiwa Flatei ili kuona ni namna gani *TARURA*, *Eng.* Bwaya, Meneja *TARURA* Mkoa wa Manyara pamoja na timu yake walivyojipanga katika kuanza utekelezaji wa matengenezo ya barabara hii mara moja. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea na swali Na. 173. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 173

**Ukarabati wa *OPD* na ujenzi wa uzio Likombe – Mtwara Mikindani**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakarabati Jengo la *OPD* na kujenga uzio katika Kituo cha Afya Likombe - Mtwara Mikindani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Likombe ni moja ya vituo vya afya vilivyonufaika na mpango wa maboresho ambapo katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, kituo hicho kilipokea shilingi milioni 500 na kujenga jengo la wazazi, maabara, jengo la kuhifadhia maiti, stoo ya dawa, nyumba ya mtumishi na kichomea taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maboresho makubwa yaliyofanywa katika kituo hicho, bado kuna uhitaji wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD)* pamoja na uzio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara itatenga shilingi milioni 70 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika Kituo cha Afya cha Likombe. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; jengo ambalo linatumika sasa hivi kama *OPD* ni

jengo la zamani na limechakaa. Kituo kile kimekuwa kikihudumia wagonjwa wengi sana. Mimi nataka kujua, kwa kutenga shilingi milioni 70 kwa mwaka, maana yake tutachukua muda mrefu kukamilisha jengo lile.

Kwa nini Serikali Kuu isipeleke fedha katika kituo hiki ili waweze kujenga *OPD* ya kisasa ambayo itaendana na mahitaji yaliyopo? *(Makofi)*

Swali langu la pili, hoja ya uzio sijajibiwa kabisa bado naendelea kuuliza, kuna mkakati gani wa kujenga uzio katika kituo kile cha afya ili kulinda mali za hospitali pamoja na watu ambao wanahudumiwa pale? Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza Malapo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na miundombinu bora ya kutoa huduma za afya katika vituo vyetu. Ndiyo maana mwaka 2017/2018, Serikali ilipeleka shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga majengo matano. Tunafahamu kwamba Jengo la *OPD* ni chakavu na la siku nyingi na tumeanza na shilingi milioni 70 kwenye bajeti ijayo, mwaka 2024/2024. Hii haimaanishi kwamba hatutapeleka fedha nyingine. Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, huo ni mwanzo tu wa fedha za mapato ya ndani, wakati huo Serikali Kuu inatafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha jengo hilo mapema iwezekanavyo ili liweze kutoa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusiana na uzio, kupanga ni kuchagua. Kwa sababau tuna changamoto ya majengo ya msingi ya kutoa huduma, ni vema tukakamilisha kwanza majengo yale, yaanze kutoa huduma kwa wananchi lakini baadaye tutafuata na hatua ya uzio, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza nianze kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kunipa vituo vya afya viwili, Kituo cha Afya cha Mtii na Kituo cha Afya cha Miamba. Naomba kuiuliza Serikali kwamba, hivi vituo vya afya vimekamilika na vimeshaanza huduma.

Je, Serikali mna mpango gani wa vituo vya afya vyote hivi viwili kujengewa jengo la kuhifadhi maiti kwa sababu, hivi vituo vya afya vyote viwili viko milimani sana? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nampongeza Mheshimiwa Mama Anne Kilango Malecela kwa namna ambavyo amefuatilia sana ubora wa huduma katika vituo vyake vya afya, vikiwemo vituo hivi viwili. Nimhakikishie kwamba baada ya kukamilisha majengo yale kuanza kutoa huduma kwa wananchi, tunaendelea na ujenzi wa miundombinu mingine ambayo haijakamilika yakiwemo majengo ya kuhifadhia maiti. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba lipo kwenye *pipeline* na litafanyiwa kazi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya swali la nyongeza. Kata ya Likawage katika Jimbo la Kilwa Kusini haina kituo cha afya na ipo mbali kutoka katika maeneo ya kutolea huduma, na Mheshimiwa Naibu Waziri alishatoa maelekezo kwa Mkurugenzi aandike andiko ili litumwe Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Andiko hilo tayari limekamilika, sasa tunataka kupata *commitment* ya Serikali, lini Kituo cha Afya Likawage kitajengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kassinge. Ni kweli alishafuatilia mara kadhaa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhusiana na ujenzi wa kituo cha afya katika kata hiyo na tayari Mkurugenzi alishawasilisha andiko ambalo tuna makadirio ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie, kwa sababu tayari ameshaleta kama kipaumbele na katika mwaka ujao wa fedha Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatupa idhini ya kutenga bajeti ya vituo vya afya kila jimbo na katika Jimbo lake la Kilwa Kusini tutahakikisha tunapeleka fedha kwa ajili ya kituo hiki cha afya, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 175

**Kuwanyima safari wafanyakazi wanaonyonyesha**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza: -

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa waajiri wanaowanyima safari watumishi wanaonyonyesha kwa kigezo cha kutumia fedha nyingi kujikimu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,

naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2008 aya ya 5(1) ikisomwa pamoja na Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 zinaelekeza watumishi wanaosafiri safari za kikazi wakiwemo wanaonyonyesha kupewe posho ya kujikimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maelezo hayo, Serikali inaelekeza tena na kusisitiza kwa waajiri wote wa watumishi wa umma kuwa watumishi wa umma wahudumiwe kwa usawa na haki kwa kuzingatia sera na kanuni zilizopo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu ya Serikali. Pamoja na majibu hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. Je, Serikali inawachukulia hatua gani waajiri wale ambao hawawapi safari hawa wanawake wanaonyonyesha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, je, Serikali haioni imefikia wakati wa kuwa na takwimu sahihi ya wanawake wanaonyonyesha ili kupanga bajeti kuepukana na kisingizio cha ufinyu wa bajeti? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali haya ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hatua gani zimechukuliwa na Serikali, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba hatua zimeendelewa kuchukuliwa kwa waajiri wote ambao hawatekelezi majukumu kwa mujibu wa sheria tulizoziweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu takwimu, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba takwimu

tumeendelea kuzichukua na kama zipo kesi zozote zile ambazo sisi kama Serikali hatuzifahamu au yeye kama Mbunge anazifahamu, basi ofisi yangu ipo wazi nakaribisha malalamiko hayo ili tuweze kuyashughulikia mara moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tatizo linalowakuta wamama wanaonyonyesha limewakuta pia wamama waliopata watoto njiti. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu wamama hawa ambao wana nafasi ya kukaa muda mrefu na wale watoto, lakini mara nyingi waajiri wamekataa kuwalipa na kuwasaidia ili waweze kutekeleza wajibu wao wa kuwalea wanadamu hawa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wa Bunge lako, swali la pili lililoulizwa na Mheshimiwa Santiel ndiyo lipo katika eneo hilo. Sasa naogopa sana kujibu hapa halafu Mheshimiwa Santiel, tukamwambia kama tulivyojibu swali la nyongeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante. Basi ngoja tuendelee. Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 176

**Likizo ya uzazi kwa wanaojifungua watoto njiti**

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuwapa Likizo ya uzazi zaidi ya siku 120 wanaojifungua watoto njiti ili kuwa na muda wa kutosha kuwatunza watoto hao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa tuwatendee haki Wananchi wa Shinyanga waliyomchagua Mbunge Santiel Eric Kirumba, kwa kujibu swali Na. 176 kama lilivyoelekezwa kwenye Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali Na. 176 lililoulizwa na Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Utumishi wa Umma, likizo ni miongoni mwa haki za watumishi wa umma ambazo wanastahili kupewa na waajiri wao kwa mujibu wa Kanuni H.12 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma mwaka 2009, kanuni hiyo ikisomwa pamoja na Kanuni ya 97 ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la likizo ya mtumishi aliyejifungua mtoto njiti halijaelezwa bayana katika Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 135 ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2022, linapotokea suala ambalo halikuelezwa bayana katika Kanuni ya Utumishi wa Umma, mtumishi atamtaarifu mwajiri kuhusu suala hilo. Mwajiri anaweza kutumia busara kulitatua pale inapobidi na anaweza kutumia sheria nyingine au kushauriana na Katibu Mkuu Utumishi kwa ufafanuzi wa suala hilo ikiwemo nyongeza ya siku katika likizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Santiel Eric, swali la nyongeza.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema inategemea na busara; je, haoni kwamba Serikali inahitajika

kuweka mkazo kwenye suala hili, kwa sababu siku 90 zile mama hazimtoshi kwa kipindi kile anapomlea mtoto njiti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Serikali pia haioni haja ya kuweka mkazo kwa wanaume pia kuwasaidia wanawake kwa kuwaongezea likizo ya uzazi wanaume wanaopata watoto njiti? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kuhusu kuweka utaratibu, nataka nilihakikishie Bunge lako kwamba maelekezo ya Bunge lako yalishatoka, lakini pia ni nia ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye alituelekeza sisi aliotupa dhamana ya kusimamia Ofisi ya Rais, Utumishi, kuyaangalia mazingira yote yatakayomwezesha mtumishi wa Umma kufanya kazi yake akiwa yupo na furaha ya kutimiza hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hivyo, Serikali imeandaa mwongozo wa ujumuishwaji wa jinsia katika Utumishi wa Umma mwaka 2023 ambao pamoja na masuala mengineyo tunazungumzia jambo la kutoa likizo kwa wazazi wanaopata watoto njiti likiwemo pia jambo hili la kuingiza wanaume katika sehemu ya watu watakaochukua likizo katika kipindi hicho cha kusaidiana kulea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo Serikali italeta mwongozo huu mbele ya Bunge lako, tutajadili kwa pamoja na tukubaliane kimsingi ni njia gani nzuri au ni kipindi gani kizuri cha kuwawekea wazazi hawa ili tuweze kufikia ulezi ulio bora usiochosha kwa mzazi mmoja au kwa mzazi mwingine, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 177

**Usambazaji wa umeme Tarafa ya Mgeta – Morogoro**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza: -

Je, lini Kata za Tchenzema, Lingali, Kikeo na Lwale katika Tarafa ya Mgeta - Morogoro zitapatiwa umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI** alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inaendelea kutekeleza mradi wa kupeleka umeme vijijini katika Mkoa wa Morogoro hususan Tarafa ya Mgeta ambapo mradi unahusisha kusambaza umeme katika Kata za Tahenzewa, Langala, Kikea na Kwale. Mkandarasi anayetekeleza mradi huo katika Tarafa ya Mgeta amekamilisha kazi ya mradi katika Kata ya Tahenzewa katika vijiji vya Tahenzewa na Kibuko na Kata ya Langala, Kijiji cha Pinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Mkandarasi anaendelea na kazi katika Kata ya Tahenzewa, vijiji vya Bumu, Lusungi, Mwarazi na Kata ya Kikea, vijiji vya Lukunguni, Kododo, Chohelo, Mhale, Kikeo na Ng'owo. Utekelezaji wa mradi katika Tarafa ya Mgeta unatarajia kukamilika mwezi Juni, 2024.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, licha ya kupeleka umeme katika Kata za Chenzema, Langala na hizo nyingine zote, naishukuru Serikali

kwa sababu inachukua huduma sana kwenye umeme: Je, ni lini vijiji vya Kidunda pamoja na Ngolehanga vitaweza kupatiwa umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini vijiji na vitongoji vya Morogoro vijijini vitaweza kupata umeme? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro kwa ujumla wake una vijiji vilivyohitaji kupatiwa umeme takribani 668. Vijiji ambavyo vilikuwa vipo katika mpango wa kupelekewa umeme ni vijiji 239. Mpaka sasa tumeshapeleka umeme kwenye vijiji takribani asilimia 90. Makusudio yetu ni kwamba vijiji vyote vya Mkoa wa Morogoro ikifika mwezi Juni mwaka huu viwe vimepatiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba tupo katika hatua ya mwisho ya kupeleka umeme kwenye vitongoji 15 vya kila jimbo la nchi yetu na matarajio yetu ni kwamba kazi hii itakamilika, uratibu wa kazi hii utakamilika hivi karibuni na tutaweza kuanza kufanya kazi hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ndani ya Halmashauri ya Mji wa Njombe Kata ya Kambarage kuna mitaa miwili ya Pemba na Unguja mpaka leo haina umeme: Ni lini mitaa hiyo itapata umeme? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itahakikisha kwamba vijiji vyote ambavyo havina umeme, kufika mwezi Juni vinapata umeme na vile vile kufika Juni kazi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote nchini, vile 15 kama nilivyosema awali, itakuwa imefanyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata za Mwamashele, Lagana pamoja na Mwasubi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mnzava, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusudio yetu ni kuhakikisha kwamba mikataba yote ya ukandarasi wa kupeleka umeme kwenye vijiji vyetu, ile mikataba iliyowahi kufika mwezi Juni mwaka huu 2024, umeme utakuwa umepatikana. Mikataba ambayo imechelewa tutasogea mbele kidogo ikiwezekana kufika mwishoni mwa mwaka huu wa fedha (2023/2024). *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni lini Serikali itatekeleza mpango wake wa *peri urban* kupeleka umeme katika mitaa yenye sura za vijiji katika miji yetu ikiwepo katika Manispaa ya Iringa Mtaa wa Ugere, Mosi, Msisina na Mtalagala.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kupeleka umeme kwenye maeneo ya miji yenye sura za vijiji *(peri urban)* na kazi hiyo inaendelea kwa sasa. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na Subira, kazi hii itakamilika, maeneo haya yatapatiwa umeme.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 178

**Idadi ya magari ya Zimamoto nchini**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza: -

Je, magari mangapi ya Zimamoto yanahitajika kukidhi mahitaji halisi nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linahitaji jumla ya magari 237 ya kuzima moto, magari 168 ya uokoaji, magari 28 ya *HAZMAT*, *Crane* 38, *ambulance* 168 na magari 28 ya ngazi ya kuzima moto katika majengo marefu *(Turn table ladder)*. Serikali imeendelea kuliimarisha Jeshi la Zimamoto

na Uokoaji kwa kutenga fedha za maendeleo katika bajeti kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kuzima moto pamoja na vifaa vingine vya uokoaji ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Jeshi limetengewa shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ununuzi wa magari matano ya kuzima moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kupata mkopo wenye masharti nafuu wa Dola za Kimarekani milioni 100 utakaowezesha kupata vitendea kazi mbalimbali ikiwemo magari zaidi ya 100 ya kuzima moto na uokoaji kwa nchi nzima, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya moto yamekuwa mengi sana katika nchi yetu na hasa katika maeneo ya shule na masoko, lakini kumekuwa na changamoto kubwa ya magari ya zimamoto kufika maeneo ya tukio bila ya kuwa na maji. Tatizo hili limekuwa ni kubwa kiasi kwamba watu wanakata tamaa na Jeshi lao la Zimamoto. Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusiana na changamoto hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa katika nchi yetu kumekuwa na miradi mingi ya kimkakati ya Serikali kama vile *standard gauge*, Bwawa la Mwalimu Nyerere pamoja na bomba lile la mafuta la Chongoleani Hoima, je, Serikali imejipanga vipi katika kuweka tahadhari ya moto katika maeneo hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la mwanzo la kwamba magari yanafika yakiwa hayana maji, naomba leo nisaidie kuweka sawa hisia hizo kwa kusema yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida gari lenye uwezo wa kubeba lita 5,000 litakapofika kwenye eneo lenye athari ya moto,

kwa *pressure* yake linaweza likazima moto kwa dakika mbili maji yale huwa yamekwisha. Sasa wananchi wana-*tend* kuamini kwamba halina maji linaenda kutafuta maji mengine. Ila ni kwa sababu dakika mbili tu lita 5,000 zinakuwa zimemalizika. Haiwezekani gari yetu iende kwenye tukio la kuzima moto halafu haina maji na kiuzoefu gari linapokuwa lime-*park, always* linakuwa na maji. Kwa hiyo, wananchi waondoe dhana hiyo potofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya kuchelewa kufika ni changamoto ya miundombinu yetu, lakini na shughuli za kibinadamu zinazofanyika kwenye maeneo ambayo gari hilo linapita. Kama kila mwananchi ataelewa na akasaidia kufungua njia wakati wa dhararu kama hizo, tatizo kama hili litapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali kuzingatia miradi ya kimkakati ikiwemo Bwawa la Mwalimu Nyerere, *SGR*, bomba la Chongoleani, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kwamba maeneo yenye uwekezaji wa kimkakati kama hizi kwa maana ya *vital installation* kuweka tahadhari ya kudhibiti matukio ya kuzima moto ni kipaumbele cha juu cha Serikali. Kwa hiyo, namhakikishia Bwawa la Mwalimu Nyerere na miradi mingine kama hiyo itazingatiwa katika kuwekewa magari na vifaa vya kuzima moto na uokoaji, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Wilaya ya Muleba ni kati ya wilaya kubwa lakini haina gari la zimamoto. Ni lini Serikali itatupatia gari la zimamoto? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya msingi nimeeleza mpango wa Serikali kutumia zaidi ya dola za Kimarekani milioni 100 kununua magari ya kuzima moto na vifaa vingine kwa ajili ya uokoaji, na tutakapokuwa tumepata mkopo huo na kununua magari hayo, Wilaya ya Muleba anapotoka Mheshimiwa Kikoyo itazingatiwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninashukuru kwa kunipa nafasi.

Ni lini Serikali itanunua gari la Zimamoto katika Mkoa wa Rukwa, kwa sababu Mkoa wa Rukwa hauna gari la Zimamoto hata moja? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba Rukwa haina gari kwa maana ya gari zima linalofanya kazi. Gari lipo ni bovu linaendelea kutengenezwa hatua kwa hatua. Ninamhakikishia Mheshimiwa Bupe kwamba mara magari haya yatakaponunuliwa Mkoa wako utazingatiwa katika mgao, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, Mbunge wa Kiteto, sasa aulize swali lake.

Na. 179

**Kumaliza ujenzi wa Kituo cha Polisi Magungu Kiteto**

**MHE. EDWARD O. KISAU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatenga fedha kumalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi Kijiji cha Magungu – Kiteto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisua, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Magungu Kiteto ulianza mwaka 2015 kwa kutumia michango na nguvu za wananchi. Ujenzi huo ulisimama ukiwa kwenye hatua ya lenta kutokana na kukosa fedha. Wakati ujenzi unasimama kiasi cha shilingi 20,000,000 zilikuwa zimetumika. Tathmini ya kumaliza ili kuunga mkono nguvu za wananchi imeshafanyika na kiasi cha fedha shilingi 33,985,000 kinahitajika. Fedha hizo zitatengwa kwenye mfuko wa Tuzo na Tozo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edward Olelekaita. Swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri sana. Hata hivyo, kwa ajili ya kuweka *record* sawa ni Kituo cha Magungu, siyo Magugu, Magugu ni kwa Mheshimiwa Mwenyekiti pale. Vilevile, jina langu ni Kisau siyo Kisua, Kisua kwa Kichaga ni yule beberu mdogo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, baada ya kusema hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza. Ninawapongeza Wananchi wangu wa Kiteto ni waungwana sana, unajua wananchi kujenga Vituo vya Polisi siyo jambo dogo sana. Kwa kuwa Wananchi wa Kijungu nao wamejenga Kituo cha Polisi na imefikia lenta wametumia milioni 15 mpaka 20. Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa nini, msiweke hiyo bajeti ya 2024/2025 ili kumalizia kama mlivyofanya kwa wenzao wa Magungu hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa aliyekuwa *IGP,* 2014/2015 alitoa ahadi ya kujengwa Kituo cha Polisi Kijiji cha Chekanoa, na kwa kuwa Mji Mdogo wa Matui unahitaji kituo chenye hadhi ya polisi. Ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri utatembelea Kiteto ili tukague vituo hivi vya polisi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali ya Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninawapongeza wananchi wa Jimbo la Kiteto, kwa juhudi hizi wanazozifanya kwa ajili ya kuhakikisha uwepo wa usalama wa wananchi na mali zao kwa kujenga vituo hivi vya polisi. Ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa wito wako na nipo tayari baada ya Bunge hili kuunga nawe kutembelea eneo lako la Kiteto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kata hii ambayo pia wameanza, ni ahadi yetu kwamba wananchi walionesha juhudi za kuanza tutawaunga mkono kwa kutenga fedha za maendeleo na fedha nyingine kutoka Mfuko wa Tuzo na Tozo ili kukamilisha majengo hayo yaweze kufanya kazi iliyokusudiwa. Kuhusu ahadi ya *IGP* aliyepita nitamkumbusha *IGP* aliyepo madamu ilikuwa ni ahadi ya Jeshi la Polisi, ili aweze kusaidiana na wananchi hawa wa Chekanao kujenga kituo hicho kilichoahidiwa, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipata nafasi hii. Kituo cha Polisi cha Sanza, ni chakavu sana ambacho kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. Nini mkakati wa Serikali wa kuwasaidia Wananchi wa Sanza kujenga kituo kipya cha Polisi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchakavu wa Kituo hiki na Mheshimiwa ameomba tujenge Kituo Kipya. Naomba anikubalie tufanye tathmini ya kiwango cha uchakavu wa kituo kilichopo. Tutakapobaini gharama za kufanya ukarabati ni kubwa au zinakaribia kulingana na ujenzi wa kituo Kipya. Basi tutaunga mkono juhudi zako kwa kujenga kituo kipya, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, Wilaya ya Mbulu ni Wilaya kongwe Serikali ina mkakati gani wa kujenga vituo vya polisi katika Tarafa za Nambis na Tarafa ya Daudi, ili kuweza kupeleka huduma karibu na wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu**.**

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali kila mara tunapokuwa na Vijiji au Miji Midogo inayokuwa kwa kasi hasa katika shughuli za kiuchumi na kuvutia vitendo vya uhalifu kuzingatia kwamba maeneo hayo tunayapa miundombinu ya kulinda usalama wa maisha ya watu na mali zao. Kwa hiyo, Tarafa alizo zitaja Mheshimiwa Mbunge tutazifanyia tathmini na wenzetu wa Mkoa wa Manyara kwa maana ya *RPC,* kuona kama pana mahitaji tuweze kuzitengea fedha kwenye bajeti zetu ili vituo hivyo viweze kujengwa, ninashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kituo cha Polisi Konde kilitengewa bajeti katika mwaka 2022/2023, hakikukarabatiwa, kikatengewa bajeti 2023/2024 mpaka leo hakijakarabatiwa. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, atafahamu kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya juhudi za kujenga na kukarabati vituo katika maeneo mbalimbali yakiwemo maeneo ya Pemba na Unguja. Ni bahati mbaya kwamba bajeti haikutoka ndio maana ukarabati haukuweza kufanyika. Ninaomba nimuahidi bajeti ya mwaka huu itakapotoka Kituo cha Konde kitapewa kipaumbele, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 180

**Kuimarisha mawasiliano Kondoa**

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaimarisha Mawasiliano ikiwemo Minara ya Simu na usikivu wa Radio ya Taifa *(TBC)* – Kondoa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa *Engineer* Andrea Kundo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* wakishirikiana na Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* imekamilisha ujenzi wa majengo ya mitambo ya redio pamoja na miundombinu ukiwemo mnara wa redio wilayani Kondoa ambapo kwa sasa *TBC* wanasubiria vifaa ambavyo vipo katika hatua ya manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* itafanya tathmini katika jimbo la Kondoa Mjini na kuona maeneo yaliyobaki yenye changamoto za mawasiliano na kuviingiza vijiji husika katika orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Juma Makoa, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, kuuliza maswali ya nyongeza. Nina maswali mawili, kama Mbunge wa Jimbo la Kondoa Mjini, nimewauliza wenzangu kule Kondoa, kwamba yapo majengo yaliyokamilika na mitambo na vitu vingine kama hivi vimejengwa Kondoa, lakini sifahamu huo mradi mkubwa namna hiyo umefanywa halafu Mwakilishi wa Wananchi na hata Mkuu wa Wilaya hana habari. Sasa ninataka kujua, je, majengo haya yamejengwa wapi? Na mitambo hii imejengwa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, majibu ya kusema tathmini itaanza, ninapenda kufahamu hapa nyuma tumeambiwa Serikali imetoa minara mingi sana kwenye nchi hii karibu wilaya zote. Hapa ninapokuambia jimbo langu si vijiji ni mitaa, kwenye minara mitano iliyokwenda Kondoa hakuna mnara hata mmoja ambao unakwenda kwenye Mtaa wa Jimbo la Kondoa Mjini. Wewe ni shahidi ukitoka Dodoma kilomita 30 tu, kuelekea huko tayari mawasiliano yote yanakatika barabara hii ni kubwa. Sasa ninataka nijue Serikali inawaambia nini Wananchi wa Kondoa Mjini na Mitaa yake ambayo haina mawasiliano? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli alivyoingia tu Bungeni hoja yake ya kwanza ilikuwa nikuhakikisha kwamba Kondoa wana Mtambo ambao utaenda kuhudumia Wananchi wa Kondoa, ili *TBC* iweze kusikika kwa ajili ya wananchi wake. Serikali ilipokea ombi lake na tayari Serikali imeshajenga, imejenga mnara imejenga jengo na pia, imeshaweka jenereta. Eneo gani mtambo huu umejengwa?

Ukiwa unaelekea Arusha upande wa kulia pale ambapo majengo ya halmashauri yanapojengwa pale, kwenye kona pale na ndio mtambo wetu upo na mnara wetu upo pale. Mimi mwenyewe ninaufahamu na nilishafika pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoweza kusema ni jambo moja kwamba ninawaomba *TBC* wanapoenda kutekeleza miradi ya maendeleo ndani ya Majimbo ya Waheshimiwa Wabunge wahakikishe wanawashirikisha Waheshimiwa Wabunge pamoja na Madiwani na Ofisi za Halmashauri ili kuhakikisha kwamba miradi hii inakuwa nishirikishi. Kwa hiyo, hayo ni maelekezo yangu kwa *TBC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni kweli tumeshafanya tathmini. Tunapofanya tathmini hatua ya pili nikupata fedha kwa ajili ya kufikisha huduma ya mawasiliano. Maeneo yetu bado ni mengi ambayo bado yana changamoto. Kipaumbele cha Mheshimiwa Rais, ilikuwa ni kuhakikisha maeneo ya mipakani, kuhakikisha maeneo ambayo yapo vijijini. Vile vile, kuhakikisha tunawashawishi watoa huduma wakawekeze katika maeneo ya mjini ili kuhakikisha kwamba haya maeneo yote yana huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninampa matumaini Mheshimiwa Mbunge, kwamba jambo lake la Kondoa ni jambo la Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na tunalipokea tutaenda kulifanyia kazi na kuchukua hatua stahiki ili wananchi wa Kondao wapate huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize Serikali swali moja. Usikivu wa *TBC* ndani ya Mkoa wa Rukwa ni wa taabu na hususani katika Wilaya ya Kalambo hakuna kabisa, najua kuna juhudi za Serikali kujenga mtambo pale Kijiji cha Mkoi. Je, ujenzi

huo utaanza lini ili Wananchi wa Mkoa wa Rukwa wapate usikivu wa *TBC? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa amekuwa mstari wa mbele kuwatetea sana wananchi wake na anahitaji wasikilize *TBC* Taifa. Sisi kama Serikali tulilipokea ombi lake na tulishaliingiza kwenye bajeti. Hivyo, ninamuomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati utekelezaji utakapoanza basi tunashirikisha kwa hatua zaidi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza**.**

**MHE. STELLA S. FIYAO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Maeneo mengi ya Wilaya ya Ileje, kuna changamoto kubwa ya mawasiliano ni upi mpango wa Serikali kupeleka miundombinu ya mawasiliano ya kutosha ili kurahishisha huduma kwa wananchi wa Wilaya ya Ileje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu na kwa bahati nzuri amekuwa mshauri mzuri sana katika Wizara yetu kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto za mawasiliano. Jambo jema kabisa ni kwamba katika minara ile 758, kati ya Majimbo ambayo yamebahatika sana ni Jimbo la Ileje ambalo limepata minara mitano. Kwa hiyo, ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, hivyo, tumuombe Mheshimiwa Mbunge aendelee kutupatia ushirikiano kuhakikisha kwamba wananchi wanatoa maeneo bila kuwa na masharti magumu ili tuhakikishe kwamba miradi hii

inaanza kwa wakati na kukamilika kwa wakati, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, sasa aulize swali lake**.**

Na.181

**Uhaba wa Masoko ya Samaki Nkasi**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Masoko ya Kuuzia Samaki katika Kata za Ninde, Wampembe na Kala Wilayani Nkasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mnyeti, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo**,** Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuboresha na kujenga miundombinu ya uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo katika mwambao wa Ziwa Tanganyika. Katika mwaka 2023/2024, Serikali inajenga masoko ya samaki saba na mialo mitatu ambapo Wilaya ya Nkasi imepangiwa kujengewa mwalo wa Karungu. Aidha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeingia Mkataba na Mkarandarasi *Nice Construction and General Supplies Ltd*. wenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya kujenga mwalo wa Karungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalo huo wa Karungu utakaojengwa utakuwa na miundombinu ya soko ikiwemo

chumba cha ubaridi, mtambo wa kuzalisha barafu na sehemu ya kuuzia samaki. Aidha, nimuombe Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Nkasi kutumia miundombinu hiyo kwa pindi itakapokamilika wakati Serikali inatafuta fedha za kujenga masoko ya samaki katika kata zingine zilizosalia. Vilevile, Serikali itaendelea kujenga miundombinu ya uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini kuendana na upatikanaji wa fedha na mahitaji ya maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vincent Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Nina maswali mawili ya nyongeza. Ziwa Tanganyika, Wilaya Nkasi hakuna vizimba hata kimoja . Ni lini Serikali mtapeleka vizimba Wilaya ya Nkasi hasa Jimbo la Nkasi Kusini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la namba mbili, lini Serikali itamalizia ujenzi wa Bwawa la Kacheche la kunyweshea mifugo pamoja na ujenzi wa majosho mawili Chala *B,* Kata ya Chala pamoja na Kijiji cha Kitosi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza na hili la vizimba, tumeshatoa maelekeza kwamba mvuvi yeyote ama mwananchi yeyote ambaye ana shida na vizimba ama boti au nyenzo zozote zinazohusiana na uvuvi, aombe haraka iwezekanavyo milango ipo wazi kwa Watanzania wote. Kwa kweli Mheshimiwa Rais, ametufungulia njia kama mnavyokumbuka Tarehe 30, aligawa kule Mwanza vizimba na boti za kutosha na Wizara ipo katika mchakato wakutafuta vizimba vingine ili kuwagawia wananchi watakaohitaji kwa awamu ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge aendelee kuhamasisha Wananchi wake wenye uhitaji. Tupo tayari kupeleka Ziwa Tanganyika na tayari tumeshaanza Ziwa Victoria  na kwa kweli vijana wote na wavuvi wote wenye shida na wenye uhitaji wa nyenzo za uvuvi Serikali ipo tayari kuwagawia. Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili, kuhusiana na lini bwawa litakamilika na majosho. Hapa katikati tulisimama kidogo kwa sababu ya upatikanaji wa fedha. Mara tu Serikali itakapopata fedha tutakwenda kukamilisha ujenzi wa majosho hayo. Mheshimiwa Mbunge atakumbuka katika Wilaya yake tumemtengea jumla ya shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya ujenzi wa soko la samaki katika eneo hilo. Tukapopata fedha nyingine tutakwenda kukamilisha ujenzi wa majosho hayo na mabwawa ambayo yapo katika Wilaya yake, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninashukuru kwa kunipa fursa na mimi niulize swali la nyongeza. Kwanza, ninashukuru kwa huduma tuliyoipata miundombinu katika Ziwa Victoria. Wilaya ya Ilemela asilimia 87 ni eneo la maji, na wanawake na vijana wengi wanashughulika na mazao ya samaki hususani dagaa lakini miundombinu yao ya kukausha samaki si mizuri hasa kwa afya ya binadamu. Ni lini Wizara itasaidia kuweka miundombinu kwa ajili ya kukausha samaki kwa wafanyabiashara hao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimesema kwamba Serikali imeshaanza na katika Ziwa Victoria tumeshaanza kuwasaidia Wavuvi namna ya kuvua zile samaki lakini pia kuhifadhi samaki. Hili wazo la Mheshimiwa Mbunge tumelichukua tutakwenda kulifanyia kazi kuwasidia Wavuvi wakanda ya ziwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simon Songe, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye orodha ya masoko ya Samaki yatakayojengwa katika mpango ambao ameusema Mheshimiwa Naibu Waziri kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni pamoja na Nyamikoma, Jimbo la Busega. Mpaka sasa soko hili halijaanza kujengwa na imebaki miezi minne kukamilika kwa mwaka wa fedha. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa soko hili la Nyamikoma? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaanza ujenzi wa Soko Nyamikoma mara tu fedha zitakapokuwa zimepatikana. Tayari Serikali imeshaanza ujenzi wa masoko katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Tunduma, Muleba, Momba, Ludewa, Busega, Nkinga na Kalambo. Kwa hiyo, mara tu tutakapopata fedha Serikali itaanza ujenzi haraka sana iwezekenavyo katika Kijiji cha Nyamikoma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, sasa aulize swali lake.

Na. 182

**Ujenzi wa malambo ya kunyweshea mifugo – Mwibara**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Malambo ya kunyweshea mifugo katika Jimbo la Mwibara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto ya upatikanaji wa maji ya mifugo katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwa ni katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda; na aidha katika mwaka 2022/2023 Serikali ilianza ujenzi wa bwawa la maji ya mifugo katika Kijiji cha Kihumbo Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ambapo ujenzi wa bwawa hilo umefikia asilimia 95. Kazi inayoendelea kwa sasa ni ujenzi wa mabirika ya kunyeshea maji ya mifugo kabla ya bwawa kuanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali za kujenga mabwawa na kuchimba visima virefu kwa ajili ya maji ya mifugo bado mahitaji ni makubwa. Hivyo nitoe wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya kuhamasisha wafugaji na wadau wengine kuwekeza kwenye miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kajege swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, kwanza nataka nikiri kwamba Serikali haijajibu swali langu. Mimi nimeuliza ni lini? Yeye ananiambia ujenzi wa bwawa katika Halmashauri nyingine ambayo wala Jimbo langu halihusiki. Kwa hiyo swali langu halijajibiwa, lakini vilevile nina swali moja na ombi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile wananchi wa Vijiji vya Kamreja Kigaga Lagata wakishirikiana na mimi tumeanza kuchangia ujenzi wa malango ya…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge samahani, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu swali lake halijajibiwa *then* hamna haja la swali la nyongeza, hivyo swali lake linaweza likajibiwa tena upya tupate majibu ya swali hilo, ahsante sana.

Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na

naishukuru Serikali kwa kuchimba Bwawa la Kihumbu. Sasa nataka kuuliza, kwa sababu bwawa limechukua muda mrefu kidogo pamoja na kwamba jitihada zipo.

Je, ni lini sasa hilo bwawa litakamilika ili wananchi watumie maji ya bwawa hilo na mifugo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli bwawa halijakamilika; Serikali tayari imeshakutana na mkandarasi na imeshampa *deadline* juu ya lini bwawa linatakiwa kukamilika na tayari tumeshakubaliana. Mara tu mkataba utakapokuwa umekamilika bwawa hilo litakuwa limekamilika na atatukabidhi Serikallini kwa ajili ya kuendelea kulitumia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, sasa aulize swali lake.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba sasa swali langu namba 182 liweze kupewa majibu ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge ni swali namba 183.

Na. 183

**Ukarabati wa Ghala Kata ya Ludewa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakarabati ghala la mazao lililopo katika kata ya Ludewa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Jimbo la Ludewa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatambua umuhimu wa ghala la Ludewa katika kuwezesha soko la mahindi kwa wakulima wa Kata ya Ludewa. Ghala hilo lilikuwa kituo muhimu cha ununuzi wa mahindi kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* lakini kwa sasa halitumiki kwa kuwa limechakaa na kupata nyufa kubwa kiasi cha kutokidhi vigezo vya uhifadhi mazao ya kilimo. Aidha, uwezo wa ghala hilo ni mdogo (tani 150) ikilinganishwa na uzalishaji wa mahindi katika Kata hiyo ambao ni takriban tani 27,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia changamoto hiyo, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kwa kushirikiana na uongozi wa kata hiyo tayari imeainisha eneo lenye ukubwa wa ekari 4 kwa ajili ya ujenzi wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,000. Aidha, michoro na makadirio ya mahitaji ya ujenzi *(BoQ)* vimeandaliwa na hivyo ghala hilo litaingizwa kwenye mpango wa ujenzi kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza; na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na kawaida wakati fulani kuzuia mahindi ya Tanzania kuuzwa nje ya nchi, jambo ambalo linaadhiri sana bei ya zao hili la mahindi kwa wakulima.

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba mahindi ya Tanzania yanaruhusiwa kwenda kuuzwa nje ya nchi ili wakulima wapate bei nzuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; bei za mbegu za mazao mbalimbali zimekuwa zikipanda kwa kasi sana.

Je, Serikali ina mpango gani walao kwa kuanzia na zao la mbegu za mahindi, Serikali ina mpango gani wakuweka ruzuku kwenye bei ya mbegu ya mahindi ili wakulima waache kurudia mbegu au kutegemea mbegu za asili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jambo la kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake ya msingi. Nimuondoe shaka kwamba moja ya wajibu wetu sisi kama Wizara ya Kilimo tunapokuwa tunazuia wakati fulani mahindi kuuzwa nje ya nchi lengo letu linakuwa kwanza, kujiridhisha kupata tathmini halisi ya usalama wa chakula nchini; na tunafanya hivyo ikiwemo kwa kutumia wakala wetu wa hifadhi ya chakula nchini kununua. Tukishamaliza jambo hilo ndipo ambapo huwa tumekuwa tukiruhusu wananchi kufanya biashara. Kwa hiyo tunaendelea kulizingatia ili kuleta namna bora ambayo itasaidia soko kwa wakulima wa mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuweka ruzuku katika bei ya mahindi, kwa maana ya mbegu mbalimbali ikiwemo mahindi, jambo hilo tumelipokea. Ndiyo maana katika mipango yetu ya awali, mwazo tumeanza na ruzuku katika upande wa mbolea na pembejeo nyinginezo zikiwemo viuwatilifu; lakini *next* maana yake tutakuja katika pembejeo nyinginezo zikiwemo bei za mahindi. Kwa sasa tumeanza na hizo *items* mbili *then* tutakuja katika hilo jambo lingine. Kwa hiyo, hilo tumelipokea na lipo katika mipango yetu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa pale Vwawa eneo Isangu kuna maghala yalikuwa yanajengwa na Serikali ambayo yametelekezwa; na tangu mwaka 2020 mkandarasi aliondoka akaacha ule mradi.

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba maghala yale ambayo ni ya kisasa kwa maana ya vihenge yanatekelezwa ili yaweze kuchangia katika uchumi wa taifa letu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mpango wa Serikali kwa Maghala ya Vwawa na maeneo mengine yakiwemo yale ya Songea ni kwamba tulishawapa kazi *NFRA* kufanya tathmini halisi ya gharama ya maghala yote nchini, kuhakikisha tunayamaliza katika mwaka wa fedha unaokuja kwa kutumia fedha zetu za ndani. Huo ndiyo mpango wetu, kwa sababu lengo la Serikali ni kuongeza uhifadhi wa chakula kutoka tani laki 3 za sasa walao mpaka mwakani tuende kwenye tani laki saba na mwaka 2030 tufikie tani milioni tatu. Kwa hiyo mpango tulionao wa muda mfupi ni kuyamaliza yote kwa fedha za ndani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Soko la Kimataifa ya Mazao la Lemagu ambalo lipo mpaka wa Sirali ni soko la kimkakati katika kukuza uchumi wa Taifa letu. Soko hilo lilijengwa na kutelekezwa zaidi ya miaka 12 iliyopita; na katika kufuatilia Serikali iliahidi kulifufua. Nataka kujua mchakato umefikia hatua gani katika kufufua soko lile?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, bahati nzuri hili soko mimi nalifahamu. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba alishapatikana mkandarasi anaitwa *Nice Construction.* Soko hilo litagharimu karibu bilioni 1.04 kwa ajili ya kulijenga na kulimaliza. Kwa hiyo hatua ipo vizuri na kazi itaendelea muda mfupi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsnate. Wananchi wa Kijiji cha Kambi ya Simba Kata ya Bulumbulu

wamejenga ghala kubwa ya kuhifadhia mazao yao lakini halijakamilika.

Je, lini Serikali itaweza kwenda kukamilisha lile ghala iliyopo katika Kijiji cha Kambi ya Simba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali la awali. Ni kwamba *NFRA* wamefanya tathmini ya maghala yote nchini na wameshatupatia hiyo taarifa, tunachokifanya sasa hivi sisi tunatafuta fedha na maghala yote nchini tutamaliza kwa fedha za ndani, likiwemo ghala hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisema.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 184

**Serikali kununua pamba toka kwa wakulima**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza kununua pamba toka kwa wakulima pindi bei ya pamba inapoporomoka katika soko la dunia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya pamba nchini hufanyika kwa kuzingatia hali halisi ya soko ilivyo. Serikali imekuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa bei inayotolewa kwa wakulima inaakisi uhalisia wa bei katika soko la dunia kwa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kutokuwiana kati ya uzalishaji na mahitaji ya pamba duniani, bei ya pamba hupanda na kushuka kulingana na hali ya wakati huo. Mathalani, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita bei ya pamba kwa ratili katika soko la dunia, kwa mfano kwa mwaka 2020, ilifikia Senti 50 za dola ya Marekani; na mwaka 2021 bei ilipanda hadi kufikia dola 1.5 kwa ratili. Mwaka 2023 hadi mwanzoni mwa mwaka 2024 bei ilikuwa wastani wa senti 84 za dola ya Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua athari ya mabadiliko ya bei kwa wakulima wa pamba nchini, Serikali ipo katika hatua za awali za uanzishaji wa Mfuko wa Kinga ya Bei *(Price Stabilization Fund)* utakaotumika kumfidia mkulima wakati bei inaposhuka kwa kiasi kitakachokubalika kwa mujibu wa Sheria ya kuanzishwa kwake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, swali la nyongo swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza ninakubaliana na majibu ya Serikali, wamefanya *analysis* vizuri lakini jinsi bei inavyopanda katika soko la dunia kama Serikali ilivyoeleza, hata gharama za ulimaji au za kilimo zinapanda vile vile.

Je, kwa nini basi Serikali isiangalie namna ya ku-*subsidize* hili zao la pamba kwamba mkulima anapolima ukatengeneza bei fulani ambayo kama itashuka katika bei ya dunia basi mkulima huyo aweze kuuza kwa bei ambayo imepangwa hata kabla hajaenda kwenye kilimo, kwa sababu analima kwa gharama kubwa wakati wa kuvuna bei inakuwa imeshuka na inawaumiza sana wakulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mmesema wenyewe mtakuja na kitu kinaitwa *price stabilization fund,* mtatunga sheria mtaileta Bungeni.

Je, ni lini sheria hiyo itatungwa ili sisi wadau wa pamba tuweze kuchangia katika sheria hiyo na tuje na sheria ambayo ni nzuri kwa mkulima wa pamba nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, cha kwanza nikubaliane vile vile na maoni ya Mheshimiwa Mbunge ya kuhakikisha tuna-*subsidize* katika zao la pamba katika kuhakikisha tunamsaidia mkulima. Sisi kama Serikali jambo hili tumelipokea. Tunachofanya ni tathmini, tutatafuta fedha ili kuhakikisha jambo hili linafanikiwa na kuwa lenye mantiki kwa faida ya wakulima wote wa pamba nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lini sheria hiyo tutaleta, nafikiri kwa sababu tupo katika mchakato wa kuanzisha huu mfuko wa kinga ya bei. Tutakapomaliza huu mchakato ninaamini kabisa kwamba kabla hatujafika mwaka 2025 jambo hili litakuwa limekamilika na limeanza kufanyiwa kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, Mbunge wa Lupembe, Mheshimiwa Swalle amekuwa akihangaika sana na wananchi wake juu ya chai. Sasa, tangu juzi viwanda vya chai kule Lupembe vimesimama, wakulima hawana mahala pa kwenda kuuza chai kule Lupembe.

Je, ni lini Serikali itatupa jibu la viwanda vile viweze kufanya kazi wakulima waweze kuuza chai yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jambo hili sisi kama Wizara tunalifahamu na Waziri wa Kilimo tayari ameshatuma timu ya wataalamu kwenda kushughulikia changamoto hiyo. Kwa hiyo, mara baada ya kurudi kwa tume hiyo tutakuwa katika nafasi ya kujibu na kuwasaidia wakulima wa Lupembe hususani wa zao la chai. Kwa hiyo jambo hili tunalifahamu na tunalifanyia kazi; na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan haitaacha jambo hili liende ili kuwaumiza wakulima wa chai nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga Mpina, swali la nyongeza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa sababu kubwa ya kushuka kwa bei ya pamba ni makato makubwa yanafanywa na Bodi ya Pamba, ambapo mwaka 2021 kwa kilo moja walikata shilingi 400; mwaka 2022 walikata shilingi 300 kwa kilo moja; na mwaka huu 2024 napo watakata.

Je, ni nani anayeruhusu viwango hivi kukatwa na kusababisha wananchi kupata bei ndogo ya pamba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninafahamu Mheshimiwa Mpina anatambua kwamba kuna makato ambayo yapo katika kanuni, kuna makato ambayo wakulima wanakubaliana wao wenyewe na kuna makato ambayo yapo kisheria. Kwa hiyo sisi ambacho tunakipokea ni kwamba, panapotokea malalamiko kila baada ya msimu wa zao ambalo linakuwa limelimwa ama limefanyiwa biashara, Wizara tunakuwa tunapitia na kuangalia yale makato. Yale ambayo tunaona yanamuumiza mkulima tunashauri Bunge lako Tukufu tunayaondoa. Kwa hiyo sisi jambo hili tuseme tumelipokea na baada ya huu msimu utapokwisha basi tutapitia yale makato yote na kuangalia yale ambayo yanawaumiza wakulima.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendela na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na.185

**Kumaliza tatizo la mimba za utotoni**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo la mimba za utotoni kwa watoto wa kike?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na wadau, imekuwa ikitekeleza afua mbalimbali kupitia Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA). Ambapo Serikali inatarajia kuzindua Awamu ya Pili ya Mpango Kazi huo mwezi Machi, 2024; ambapo moja ya kipaumbele chake ni mikakati ya kudhibiti mimba za utotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na afua zinazotekelezwa katika mpango huo Serikali itaendelea kutekeleza afua mambo yafuatayo: -

(i) Kufanya kazi kwa mapitio ya Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 ambayo imeongeza adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela kwa atakayepatikana na hatia ya kumpa mimba mtoto/mwanafunzi shule/.

(ii) Kuendelea kutoa elimu ya stadi za maisha kwa watoto kupitia madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto na kutoa elimu ya malezi na makuzi ya watoto kwa wazazi au walezi na jamii kupitia kampeni katika vyombo vya habari na majukwaa ya madhehebu ya dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imepanga kuzindua Kampeni ya Usalama wa Mtoto Mtandaoni kwa ajili ya kuelimisha wazazi, walimu na watoto kuhusu athari za matumizi yasiyofaa ya mitandao ambayo pia yanachangia mimba za utotoni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, nini mkakati wa Serikali kushirikisha taasisi mbalimbali zinazojihusisha na elimu ya masuala ya afya ya uzazi. Je, Serikali haioni haja ya taasisi hii kupata vipindi kwenye mashule mbalimbali ili kutoa elimu kwa watoto wa kike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa vile mimba za utotoni zinaenda sambamba na ndoa za utotoni. Nini sasa baada ya Serikali kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali. Lini Serikali italeta Muswada wa ndoa za utotoni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Janeth, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na wadau tunaimarisha mikakati ya uratibu za afua na kutoa huduma za afya shuleni kwa kushirikiana na majukwaa ya watoto walioko shuleni, vitabu vya watoto, madawati, ulinzi na usalama, mabaraza ya watoto, na kutumika katika elimu ya afya shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili. Wizara ya Maendeleo ya Jamii ikishirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria inaendelea na mchakato wa kukusanya maoni juu ya kujua umri wa kuolewa kwa mtoto wa kike. Pia, mchakato huo ukimalizika Muswada huu utaletwa katika Bunge lako Tukufu na kujadiliwa na kupitishwa sheria ya kuthibiti ndoa za utotoni.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga Mbunge wa Kalenga sasa aulize swali lake.

Na. 186

**Mpango wa Serikali wa kuenzi tamaduni za makabila**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inaenzi Tamaduni za Makabila ili kulinda maadili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waiziri, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, kama ifutavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha tunaenzi tamaduni za makabila kwa lengo la kulinda maadili ya Mtanzania Serikali inafanya yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamza ni kuendesha Tamasha la Kitaifa la Utamaduni ambalo hufanyika kila mwaka. Tamsha hilo linashirikisha vikundi vya utamaduni kutoka Mikoa yote ya Tanzania bara na Visiwani, ambalo linahusisha shughuli mbalimbali za kiutamaduni, kama vile maonesho ya vyakula vya asili, urembo na utanashati, michezo ya jadi, teknolojia na sayansi jadia. Pia, Tamasha hilo linahusisha mashindano ya ngoma za asili, upishi na uandaaji wa vyakula vya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sambamba na hayo, Tamasha hilo huambatana na mdahalo wa namna ya kupambana na mmomonyoko wa maadili. Hivyo kupitia tamasha hilo, wananchi

wanasherehekea, wanaenzi, wanatunza na kuendeleza tamaduni zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili Serikali inaendelea kutumia majukwaa mbalimbali kama vile makongamano, semina, mikutano na warsha kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuthamini utamaduni na maadili ya Mtanzania

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, inaendelea kufanya Tafiti mbalimbali ili kubaini mila na desturi zinazo kubalika katika jamii ili ziendelezwe na zisizofaa waachane nazo, ambapo hadi sasa jumla ya tafiti 286 kuhusu mila na desturi za maeneo ya Kihistoria zimefanyika;

Mheshimiwa Mwenyekiti na mwisho inaendelea kushirikiana na wadau na kuwahimiza kufanya matamasha mbalimbali ya utamaduni nchini kote, ili kuhakikisha mila, desturi na tamaduni zetu zinalindwa na kuendelezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jimbo la Kalenga limekuwa kinara wa kuendeleza mila na tamaduni; je, Serikali haioni haja sasa ya kutujengea hata kituo cha utamaduni katika Jimbo hilo la Kalenga ili tuweze kuendeleza utamaduni wetu wa Kihehe? *(Makofi)*

Swali namba mbili, kwa kuwa Makumbusho ya Mkwawa ambayo ndiyo sehemu ya kuenzi mila na tamaduni zetu yako katika eneo la makaburi ya familia ya Mkwawa na Uchifu wa Mkwawa upo hai. Je, Serikali haioni haja sasa katika vile viingilio wakawa wanatupa hata asilimia moja au mbili ili kuendelea kuimarisha ule utamaduni wetu na uchifu wetu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza ni kuhusuana na kujenga kituo cha utamaduni pele Kalenga, namuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, inaendelea kufanya tathmini ya kutambua maeneo ya kiutamaduni ili kutoa maelekezo mahsusi kwa mamlaka husika za mikoa na wilaya, namna ya kuyaenzi na kuyahifadhi maeneo haya. Kwa hiyo, hili la kujenga kituo cha utamaduni pale Kalenga, namuahidi Mheshimiwa Mbunge ninalichukua na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo italifanyia kazi na muda utakaporuhusu tutaweza kufanya hivyo. *(Makofi)*

Swali lake la pili kuhusuana na sehemu ya malipo ya maonesho ya kaburi la Chifu Mkwawa kwenda kwa familia, namuahidi Mheshimiwa Mbunge pia nalichukua na tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Makumbusho ya Taifa kuona namna ambavyo hili linaweza kufanyika na familia ya Chifu Mkwawa ikaweza kufaidika na sehemu ya kiingilio cha makumbusho yale, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya utafiti gani ili kujua makabila yaliyoko nchini, kuweza kuyasaidia na kuyaendeleza kuwa kivutio ili kuweza kuiingiza Serikali Pato la Taifa na watalii zaidi ya Wamasai? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi, mpaka sasa tafiti 286 zimeshafanyika, tunachofanya ni

mwendelezo wa tafiti hizo na kuona namna ambavyo tunaweza kutumia ufahamu tulioupata kupitia tafiti hizo ili kuyaenzi na kuhifadhi tamaduni za makabila mbalimbali zaidi ya Wamasai hapa nchini, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, sasa aulize swali lake.

Na. 187

**Uchimbaji wa visima vya maji Jimbo la Buchosa**

**MHE. ERIC J. SHIGONGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha uchimbaji wa visima vya maji vilivyoanza kuchimbwa katika Jimbo la Buchosa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Jimbo la Buchosa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2023/2024 Serikali inaendelea na zoezi la utafiti wa maji chini ya ardhi pamoja na uchimbaji wa visima 13 katika Jimbo la Buchosa Wilayani Sengerema. Hadi sasa jumla ya visima sita vimechimbwa, ambapo kati ya visima hivyo tulivyopata maji ni visima vinne vilivyochimbwa katika vijiji vya Bulolo, Nyonga, Bulyahilu na Izindabo. Aidha, kazi ya utafiti wa maji ardhini na uchimbaji wa visima inaendelea katika Vijiji vya Kisaba, Busikimbi, Kasalaji, Nyamiswi, Luharanyonga, Irenza na Bugoro ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eric Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali.

Swali la kwanza, ni kweli kwamba visima hivi vimechimbwa, lakini kwa hivi sasa vimesimama na hakuna fedha ya kuendeleza. Je, Serikali italeta lini fedha ili kukamilisha uchimbaji wa visima hivyo?

Swali la pili, mradi wa maji kutoka Kijiji cha Lumeya, Nyakalilo, Kalebezo, Mizolozolo mpaka Nyehunge haufanyi kazi ipasavyo kwa sababu mambomba yake yanapasuka. Je, Serikali iko tayari pia kuukarabati mradi huu ili uweze kufanya kazi kwa ukamilifu wake? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, lini fedha itakwenda kwa ajili ya kuendeleza visima. Tayari Mheshimiwa Waziri ametoa maagizo kwa Mameneja wa Mikoa wote kuhakikisha hivi visima vinaweza kuendelezwa na tija ya uchimbaji visima hivi kunaweza kupatikana kwa maji bombani kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukarabati mradi ambao umekamilika lakini mabomba yanapasuka, hapa kwanza tumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kutupatia fedha na kuhakikisha miradi inakamilika. Unapoona mabomba yanapasuka maana yake maji yamekuwa ni mengi tofauti na ilivyokuwa nyuma. Kwa hiyo, tuko tayari kukarabati ili kuhakikisha maji mengi yaliyopatikana sasa yanawafikia wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 188

**Kubadili muonekano wa sarafu na noti**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itabadili muonekano wa Noti na Sarafu ili kutoa fursa ya kuweka picha ya Rais Mwanamke wa kwanza Tanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa kuondoa picha ya Rais kwenye noti ulifanyika katika kipindi cha Awamu ya Tatu chini ya Rais mstaafu Hayati Benjamin Mkapa. Miongoni mwa sababu ya kuondoa picha za viongozi kwenye sarafu yetu ilikuwa ni gharama za mara kwa mara za uchapishaji wa noti kwa ajili ya kubadilisha picha za viongozi mara muda wao wa kuwa madarakani unapokoma. Hivyo, kuanzia toleo la noti la mwaka 1997, picha ya Kiongozi Mkuu wa Nchi iliondolewa na badala yake picha za wanyama kama vile tembo (shilingi 10,000), kifaru (shilingi 5,000) na simba (shilingi 2,000) zimeendelea kuonekana kwenye sarafu ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuenzi michango ya waasisi wa Taifa letu, noti ya shilingi 1,000 imeendelea kuchapishwa ikiwa na picha ya baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na noti ya shilingi 500 ilichapichwa ikiwa na picha ya Rais wa awamu ya kwanza wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume. Hata hivyo, noti ya shilingi 500 ilibadilishwa kuwa *coin* mwaka 2014 ambapo picha ya Hayati Sheikh Abeid Amani Karume imeendelea kuwepo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, swali la nyongeza.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya

nyongeza. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yametuwekea kumbukumbu kwamba, mara ya mwisho tulibadilisha fedha mwaka 1997 lakini jibu langu bado sijalipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, ni mara ya kwanza kupata Rais Mwanamke Tanzania na Afrika Mashariki, ambaye ni mchapa kazi, jasiri na ameonyesha uwezo wa wanawake. Ambaye ameweza kutupa sifa Tanzania, Afrika na dunia nzima. Je, Serikali haioni kwamba, sasa ni wakati mwafaka wa kuweka sura ya Rais wa Kwanza Mwanamke katika Noti za Tanzania? *(Makofi)*

Swali langu la pili, kwa kuwa, Rais wa Kwanza wa Zanzibar amepewa nafasi katika sarafu ya Shilingi 500 na kutokana na kupanda kwa uchumi sasa hivi, Shilingi 500 haitumiki sana. Je, Serikali haioni kwamba sasa hivi ni fursa pekee ya kupandisha pia hadhi ya Rais wa Kwanza wa Zanzibar, kumuongezea noti juu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Angelina kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala hili zipo taratibu mbalimbali ambazo hutumika katika uwekaji wa alama kwenye noti zetu au sarafu yetu. Hizi lazima zizingatie kufuata Taratibu, Sheria na Kanuni. Muda wa suala hili ukifika basi, maoni yake tumeyachukua na tunaenda kuyafanyia kazi. Muda ukifika zitawekwa, *Inshallah. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu.

Tunaenda Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, sasa aulize swali lake.

Na. 189

**Malipo ya fidia kwa waliopisha mradi wa barabara Kibamba**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza: -

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya malipo ya fidia kwenye miradi ya barabara za *TANROADS* zinazopita kwenye makazi ya watu Kibamba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulipaji wa fidia kwa wananchi ambao mali zao zinaathiriwa na miradi ya ujenzi wa barabara hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Namba 13 ya mwaka 2007. Wananchi wote ambao mali zao ziko nje ya eneo la hifadhi ya barabara wanalipwa fidia na wale ambao mali zao zimo ndani ya eneo la hifadhi ya barabara hawastahili kulipwa fidia. Hii ni kwa wananchi wote nchi nzima ikiwemo na wananchi wa Jimbo la Kibamba, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya jumla ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; ipo barabara ya Makabe – Msakuzi kuelekea Mpiji Magoe ambayo ina sifa hizo ambazo amezizungumza na sasa barabara hii imeanza kutengenezwa, wananchi bado wako kwenye sintofahamu kama

watalipwa fidia au lah! Je, ni ipi kauli ya Serikali kwenye barabara hii. *(Makofi)*

Swali la pili, ipo barabara ya Victoria au inaitwa Mbezi Shule – Mpiji Magohe, kilometa 9.5; ni barabara ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais lakini ipo ndani ya bajeti kwa kipindi cha miaka miwili, lakini ina watu takribani 50,000 ambao ni wengi zaidi hata ya majimbo mengine.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Makabe – Msakuzi, ni barabara ambayo tangu kuwepo kwake iko chini ya *TANROADS* na wakati ule ilikuwa chini ya ujenzi Mkoa wa Dar es Salaam, *TANROADS* ilipoanzishwa ikawa imehamia moja kwa moja *TANROADS*. Kwa hiyo, kwa wananchi ambao watakuwa ndani ya mita 22.5 kutoka katikati hawatastahili kulipwa, ila pale ambapo tutakwenda 7.5 wananchi ambao wako katika barabara hii watalipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Victoria, pale kuna barabara mbili, kuna barabara ya Kibamba Shule – Magoe Mpiji na Victoria kwenda Magoe Mpiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kibamba Shule tayari imeshaanza kujengwa kwa awamu, pia, ndiyo tunayoitegemea itakuwa *outer ring road* ya Mkoa wa Dar es Salaam na usanifu unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Victoria imekuwa ni barabara ambayo inahitajika sana hasa baada ya kuanzisha stendi ya Magufuli, tunavyoongea sasa hivi Mhandisi Mshauri yuko *field* kufanya usanifu na tunategemea baada ya kukamilisha kwa

bajeti ambayo tunaiandaa iweze kuingia ili ijengwe kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 190

**Ujenzi wa Chuo cha *VETA* Mkoa wa Songwe**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha *VETA* Mkoa wa Songwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa sasa inatekeleza azma ya kujenga Chuo cha Ufundi katika kila Mkoa na Wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali ilitenga shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kujenga vyuo vya ufundi stadi katika Wilaya 64 ambazo zilikuwa hazijajengewa Vyuo vya Ufundi Stadi ikiwamo Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Songwe. Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Songwe kimetengewa fedha shilingi bilioni 6.53 kwa ajili ya ujenzi wa jumla ya majengo 25 ikijumuisha jengo la utawala,

karakana, madarasa, maktaba, bwalo la chakula, vyoo, stoo pamoja na nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshapeleka shilingi bilioni 1.14 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Songwe ambapo kwa sasa ujenzi umefikia hatua ya kukamilika kwenye baadhi ya majengo na kazi ya ujenzi wa kuta inaendelea. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, fedha iliyokuwa imetengwa ni shilingi bilioni 6.53 lakini mpaka sasa fedha iliyotolewa ni shilingi bilioni 1.14 hasa ukizingatia sasa hivi tuko mwezi wa Nane wa mwaka wa kibajeti bado miezi minne tu ili tuweze kumaliza mwaka wa fedha. Nataka kujua ni mpango upi wa Serikali kuhakikisha mnapeleka fedha zote kwa wakati ndani ya mwaka huu wa bajeti ili chuo hiki kiweze kujengwa kwa wakati?

Swali langu namba mbili, nataka kujua, je, Serikali mna mkakati gani sasa wa kuhakikisha mnapata wakufunzi wa kutosha na wanafunzi ili chuo hiki kitakapoanza kiweze kufunguliwa kwa muda na kuanza kwa wakati, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Stella Fiyao, kama alivyouliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza ni kweli kwamba kulikuwa na ucheleweshaji kidogo wa upelekaji wa

fedha katika fedha ambayo ilikuwa imetengwa ya shilingi bilioni 6.53 lakini mpaka hatua hii ninavyosema shilingi bilioni 1.14 imekwenda na katika mwaka huu wa fedha katika hatua hii ya mwisho tayari kuna fedha zingine ambazo tunatarajia kuzitoa kwenye *disbursements* nyingine. Changamoto tu ilikuwa ni ya upatikanaji wa fedha lakini azma ya Serikali na dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassani ya kujenga imeendelea kuwepo na siyo tu kwa Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge atakumbuka kuwa tunajenga eneo la Mbozi katika Halmashauri ile lakini pia kwenye Mikoa mingine ujenzi unaendelea. Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi nafurahia kwamba ana dhamira ya dhati kuona kwamba chuo kile kinaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, fedha zitapelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ameuliza kama tunao mpango gani kuhusiana na kupeleka wakufunzi pamoja na wanafunzi wa kujifunza pale. Dhamira ya Serikali ya kujenga vyuo hivi katika andiko lake kuu ni pamoja na uwepo wa vitendeakazi, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanakuwepo lakini pia vifaa vya kijifunzia na mashine za wanafunzi hawa kujifunza, yote haya yako katika mpango wa bajeti na kwamba tutaenda kukamilisha mara pale chuo kitakapokamilika ili wanafunzi hawa wa Kitanzania waweze kupata fursa hiyo ya kujifunza na kuchangia katika ujenzi wa Taifa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, sasa aulize swali lake.

Na. 191

**Kurejesha eneo la RUBADA kwa wananchi – Mlimba**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itarejesha eneo lililokuwa linamilikiwa na *RUBADA* kwa wananchi wa Utengule – Mlimba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shamba Namba 949 linalojulikana kwa jina la Ngalimila lina ukubwa wa hekta 5,128.483 (sawa na ekari 12,820). Shamba hili lipo Mkoa wa Morogoro katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba katika Kata ya Utengule. Shamba hili limezungukwa na Vijiji vya Ngalimila, Ipugasa, Ngombo, Mpanga, Miembeni na Viwanja Sitini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya mwaka 2009 ardhi hii ilikuwa inamilikiwa na Kijiji cha Ngalimila ambapo tarehe 18 Mei, 2009 kilifanyika kikao maalum kwa ajili ya kujadili maombi ya ardhi kwa ajili ya *RUBADA* kutoka kijiji cha Ngalimila kwa ajili ya uwekezaji. Wanakijiji walikubali kutoa ardhi hiyo kutokana na manufaa ambayo walielezwa yangepatika na kutokana na uwekezaji mkubwa katika kilimo cha mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 16 Aprili, 2014 iliandaliwa taarifa ya kusudio la kuhaulisha ardhi ya kijiji kuwa ya kawaida. Baada ya *RUBADA* kufutwa, mali mbalimbali ikiwemo shamba la Ngalimila zilirejeshwa Wizara ya Fedha na Mipango na kuwa chini usimamizi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ardhi ya shamba hili kutoendelezwa kwa muda mrefu, Serikali ilipokea maombi ya wananchi kurejeshewa shamba hili. Hata hivyo, uchambuzi wa maombi hayo ulibaini kuwa eneo lenye ukubwa wa hekta 1,820.494 sawa na asilimia 35 ya shamba hilo lipo katika eneo la Pori Tengefu la Kilombero. Aidha, ili kufika katika shamba hili, sharti

kuvuka Mto Mpanga na Mto Mnyera ambayo ndiyo chanzo cha kupeleka maji katika mradi wa ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme wa maji wa Julius Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa wananchi wanaotumia shamba hili kwa sasa ambao ni wavamizi kutokuweka miundombinu ya kudumu ili kuepusha hasara inayoweza kujitokeza endapo Serikali itatoa maamuzi tofauti na maombi yao. Aidha, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa suala hili litashughulikiwa na kutolewa maamuzi kwa uharaka unaohitajika kwa maslahi mapana ya jamii na Taifa kwa ujumla, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi, swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba hapo awali shamba hili lilikuwa linamilikiwa na Kijiji cha Utengule, na kwa kuwa wananchi hawa kwa nia njema kabisa waliridhia shamba hili litwaliwe na Serikali kwa ajili ya uwekezaji, lakini sasa yapata miaka 13 hamna uwekezaji wowote: Swali langu, ni lini Serikali itakabidhi shamba hili kwa wananchi wa Kata ya Utengule? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Kunambi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla ya kutoa maelezo ya majibu, nampongeza sana Mheshimiwa Kunambi na wananchi wa Mlimba kwa kumpata kiongozi ambaye ni mfuatiliaji, ana hamasa ya kweli kwa maendeleo ya wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi ni kwamba Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, wanaendelea na mchakato wa jinsi ya kuharakisha maamuzi ya shamba hili aidha kurudishwa sehemu ya shamba hilo kwa wananchi na ile sehemu ambayo imewekwa kwa ajili ya

uwekezaji mkubwa wa bwawa letu la Mwalimu Nyerere, nalo kuangaliwa katika umbo zima la namna ya kulilinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe tu *comfort* Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itatoa maamuzi kwa haraka ili kuharakisha manufaa yatakayotokana na matumizi ya ardhi hii ambayo kimsingi haijatumika ipasavyo kwa muda mrefu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu kwa upande wa Serikali. Ninayo matangazo, nitaanza na tangazo la wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Nitaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika ambao ni wageni wanne wa Mheshimiwa Spika na Rais wa Mabunge Duniani *(IPU)* kutoka Bunge la Jimbo la Makueni nchini Kenya ambaye kwanza ni Mheshimiwa Urbanus Manzu Yulu ambaye ni Mwenyekiti; Mheshimiwa Darius Kioko Mainga ambaye ni Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Janiffer Kamanthe Mwanthi ambaye ni Mjumbe; na Ndugu Griffins Ndungi Mutevu ambaye ni Katibu wa Msafara, karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni wageni watatu wa Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ambao ni Mabalozi wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira walioshiriki kwenye Mkutano wa Mazingira Dubai *(COP 28),* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambao ni wapiga kura wake kutoka Geita Mjini, Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Rehema Migilla ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Dorothy Kilave ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani ambao ni marafiki zake kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Abubakari Asenga ambao ni rafiki zake kutoka Jimbo la Kilombero, Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambao ni ndugu zake kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunaye mgeni mmoja wa Mheshimiwa Vedastus Manyinyi ni *campaigner* wake mkuu kutoka Jimbo la Musoma Mjini, Mkoa wa Mara, karibu sana *campaigner* mkuu wa Mheshimiwa Mathayo. *(Makofi)*

Tunaye mgeni mmoja wa Mheshimiwa Maryam Omar Said ambaye ni mtoto wake kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Tunao wageni 103 wa Mheshimiwa Dkt. Mathayo David Mathayo ambao ni Makatibu wa CCM kutoka Jimbo la Same Magharibi, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana na tusikilizane, matangazo yanaendelea.

Tunao wageni 83 wa Mheshimiwa Husna Sekiboko ambao ni Wajumbe wa UWT kutoka Wilaya ya Handeni, Mkoani Tanga, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 63 wa Mheshimiwa Amina Daud ambao ni wanafunzi wa Chuo cha *SAMAIT University* kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ambaye ni mdogo wake kutoka Kampuni ya *Yuho Agro processing Industries*

*Ltd*. iliyopo Manyoni, Mkoa wa Singida, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023**
**na**
**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, awasilishe hoja yake. Mheshimiwa Dennis Londo, karibu.

**MHE. DENNIS L. LONDO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha kwako Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kipindi cha kuanzia Februari 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha kwa Bunge lako Tukufu, Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kipindi hicho nilichotaja hapo juu Februari, 2023 mpaka Januari 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Taarifa yangu yote, iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge, kama ilivyowasilishwa mezani kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, taarifa hii imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo: -

(i) Sehemu ya Kwanza, inatoa maelezo ya jumla ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, mbinu na njia zilizotumika pamoja na orodha ya shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja;

(ii) Sehemu ya Pili, inafafanua shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi na yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto;

(iii) Sehemu ya Tatu, inatoa maoni ya jumla na mapendekezo ili kuliwezesha Bunge lako kufanya maamuzi; na

(iv) Sehemu ya Nne, ni hitimisho na kutoa hoja kwa ajili ya Bunge kuweza kujadili na kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia iliyotumika kutekeleza majukumu ya Kamati. Katika kutekeleza majukumu yake, kama ilivyotajwa na Kanuni ya 142(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilitumia njia kuu tatu kama ifuatavyo: -

(i) Kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara pamoja na Taasisi inazozisimamia;

(ii) Kusoma na kuchambua taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi inazozisimamia; na

(iii) Kuandaa na kutoa maoni na ushauri kuhusu yatokanayo na taarifa za Wizara na Taasisi inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shughuli zilizotekelezwa kipindi cha 2023/2024, Kamati ilipata wasaa wa kutekeleza majukumu yake mbalimbali ambayo imepewa kwa mujibu wa Kanuni ya 137 na Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya 7 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanikiwa kufanya ziara katika Mikoa 11 ambayo ni Mwanza, Mara, Tabora, Singida, Iringa, Morogoro, Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Arusha, Tanga na Mbeya ambako kote Kamati ilikagua miradi zaidi ya 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza na kusimamia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, fungu la bajeti Na. 56, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Ofisi hii ilipokea ama iliidhinishiwa fedha zaidi ya shilingi trilioni moja kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Desemba 21, Ofisi hii ilipokea jumla ya shilingi bilioni 733.6 sawa na asilimia 68 ya fedha iliyoidhinishwa kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu namba mbili - Tume ya Utumishi wa Walimu, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 17.2 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya Fedha hizo, mishahara ni shilingi bilioni 8.8 sawa na asilimia 41, matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 7.7 sawa na asilimia 33 na miradi ya maendeleo ni shilingi milioni 670 sawa na asilimia 26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliarifiwa kuwa, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2023 Tume ya Utumishi wa Walimu ilipokea na kutumia jumla ya shilingi bilioni 7.9 sawa na asilimia 46 ya kiasi cha bajeti ambayo iliidhinishwa na Bunge lako. Kati ya Fedha hizo shilingi bilioni 4.7 ni mishahara, shilingi bilioni 2.7 ni matumizi mengineyo na shilingi milioni 509 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kama ilivyo katika kielelezo Na. 2 cha Taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati yetu iliangalia fungu Na. 26 la Sekretarieti za Mikoa, ambalo liliidhinishiwa shilingi bilioni 281.3. Kati kati ya fedha hizo, mishahara ni shilingi bilioni 73.7, matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 107.7 na fedha za miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 99.8 kama ilivyo kwenye kielelezo Na. 3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 31 Desemba, 2023 jumla ya shilingi bilioni 117 sawa na asilimia 41 ya fedha zote

zilizoidhinishwa zimepokelewa kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi za Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri za Wilaya, Majiji na Miji), katika bajeti ya 2023/2024 Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 7.7. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 5.3 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 2.4 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi Desemba, 2023 jumla ya shilingi trilioni 3.5 zilipokelewa sawa na asilimia 45.2 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya Fedha hizo zilizopokelewa, kiasi cha shilingi bilioni 2.6 sawa na asilimia 49.9 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 835 sawa na asilimia 34 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla hali ya utolewaji wa fedha ambazo zimeidhinishwa na Bunge lako kupitia bajeti ya Ofisi hii kinaridhisha, kwani katika uchambuzi wa Kamati, tumebaini fedha zilizotolewa katika Fungu 56 pamoja na Fungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa kwa jumla ni asilimia 21.9 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Taarifa ya Kamati kwa ajili ya Wizara na Taasisi ambazo tunazisimamia; katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Oktoba na Januari, 2024, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa miradi ya Ofisi za Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa, Kamati ilijadili Taarifa ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhusu ujenzi wa Ofisi za Halmashauri ili kujua hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati imebaini kuwa Serikali imefanya juhudi kubwa sana katika kuimarisha utendaji wa Sekretarieti za Mikoa na Halmashari za Wilaya, jambo ambalo limeleta tija kubwa na urahisishaji wa huduma kwa wananchi nchini. Kamati inaipongeza Serikali kwa ujenzi wa ofisi mbalimbali za Mikoa na Halmashauri za Wilaya na Miji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya elimu, madarasa, madawati, maabara na

maktaba; Kamati ilipokea taarifa za Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhusiana na utekelezaji wa miundombinu hiyo. Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ilitamka wazi kuunda Serikali itakayoimarisha rasilimaliwatu kama inavyotamkwa na Ibara ya 80(a) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka juhudi kubwa katika kuhakikisha kuwa miundombinu ya elimu inaimarishwa katika shule za msingi na sekondari nchini ili kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya wanafunzi kujifunza. Uwekezaji huu kupitia miradi mbalimbali kama vile *SEQUIP, BOOST na EP4R* imelifanya Taifa kushuhudia mabadiliko makubwa ya mazingira ya kutolea elimu kwa shule za msingi na sekondari nchini hali iliyosababisha ongezeko la wanafunzi katika shule za msingi na sekondari na kusababisha upungufu wa madawati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya upandaji wa miti, utunzaji wa mazingira na uwezekano wa miradi ya hewa ya ukaa katika Halmashauri zetu. Halmashauri nyingi nchini zimekuwa zikikumbwa na uharibifu wa mazingira kwa ukataji miti ovyo. Hali hii imekuwa ikisababisha pamoja na mambo mengine, ongezeko la hewa ukaa angani, halikadhalika kukosekana kwa misitu kulisababisha Halmashauri nyingi kushindwa kutekeleza jukumu lake la utengenezaji wa madawati kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona kuwa ni wakati muafaka sasa kwa Halmashauri kuweka mikakati ya kuanzisha misitu ya Halmashauri itakayowezesha upatikanaji rahisi wa mbao kwa ajili ya samani mbalimbali katika Ofisi za Halmashauri na katika shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imebaini uwepo wa misitu katika Halmashauri unaweza kuleta faida kubwa kwa Halmashauri kwa kufanya biashara ya hewa ukaa. Mfano mzuri ni Halmashauri za Tanganyika, Mbulu na Katavi, ambazo zinatarajia kukusanya mabilioni ya pesa kutokana na biashara ya hewa ukaa kutoka kwenye misitu ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ina jukumu la kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa na tulipokea taarifa na kujadili katika maeneo mbalimbali. Katika uchambuzi wa Kamati ilibaini mambo mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Kamati imebaini kuwa katika baadhi ya Halmashauri, watumishi hudumu kwa muda mrefu na hivyo kufanya kazi kwa mazoea na jambo hilo halikubaliki. *(Makofi)*

(ii) Kamati imebaini kuwa Serikali hupeleka fedha nyingi katika Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuwaletea maendeleo wananchi. Hata hivyo, imebainika kuwa wasimamizi na watekelezaji wa miradi hiyo hasa watendaji na wanasiasa katika ngazi ya kata na vijiji, ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hawana utaalam au taaluma ya miradi wanayoisimamia, hivyo kupelekea usimamiaji na ufuatiliaji wa miradi hiyo kuwa mgumu

(iii) Imebainika kuwa maslahi ya viongozi katika ngazi za kata, mitaa na vijiji hapa nchini bado yapo chini. Hata hivyo, imebainika kuwa hata utoaji wa maslahi hayo hutofautiana kati Halmashauri moja na nyingine. Aidha, baadhi ya Halmashauri hazina utaratibu wa kutoa posho ya aina yoyote kwa Watendaji wa Vijiji na Mitaa. Kamati inashauri Serikali kutoa mwongozo kwa Halmashauri zote nchini kuweka utaratibu wa ulipaji wa posho za viongozi katika ngazi za Kata, Mitaa na Vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la matumizi mengineyo ya fedha za mapato ya ndani, Kamati ilijadili taarifa kuhusu ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri na upangaji wa matumizi mengineyo. Kwanza Kamati inaipongeza Serikali kwa kupeleka fedha nyingi kwenye miradi ya maendeleo katika Halmashauri zetu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kwamba moja ya majukumu makuu ya Halmashauri ni kupeleka maendeleo mijini na vijijini. Hata hivyo, kutokana na Serikali Kuu kupeleka fedha nyingi kwenye miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kuwa

Halmashauri nyingi zimeongeza utegemezi kwa Serikali Kuu na kujiondoa katika jukumu lake la msingi kwa kutumia mapato ya ndani kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Hali hii imesababisha miradi mingi ya maendeleo ambayo imeanzishwa kutokamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini upungufu katika mifumo na miundo ya watumishi wasio waaminifu katika suala zima la ukusanyaji na usimamizi wa mapato katika ngazi mbalimbali. Kutokana na matumizi ya mifumo ambayo inasababisha uwezekano wa kuwepo kwa mianya ya upotevu wa ukusanyaji wa mapato, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua madhubuti kudhibiti watumishi wasio waaminifu na kuweka mifumo inayofaa ili kuziwezesha Halmashauri kukusanya mapato kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la michezo katika shule za msingi na sekondari, Kamati inatambua kuwa Serikali imeweka Sera na Miongozo mbalimbali inayopaswa kutekelezwa ili kukuza michezo kwenye shule zetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemo wa Kilatini unasema *mens sana in corpore sano* yaani *a healthy mind in a healthy body*, kwa tafsiri isiyo rasmi maana yake ni akili safi inakaa kwenye mwili safi, na ujenzi wa Taifa hili la vijana na wenye afya na siha njema, inategemea sana kujishughulisha sana hasa katika ya michezo hii, hivyo basi, Serikali inapaswa kuwekeza zaidi katika miundombinu ya michezo ili kujenga Taifa imara lenye vijana ambao wanaweza kuwa na tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa Mradi wa *SEQUIP*, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa kuhusiana na miradi hiyo ambayo ina thamani ya zaidi ya dola za Kimarekani milioni 500 sawa na fedha za Kitanzania shilingi trilioni 1.2. Lengo la mradi huu ni kuboresha elimu ya sekondari nchini na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari ili kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya sekondari, kuweka mazingira salama ya elimu kwa wasichana waliopo katika shule za sekondari pamoja na kuhakikisha wanafunzi wote wanaoanza masomo ya sekondari wanamaliza elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchambuzi tulibaini kwamba changamoto kubwa ambayo ipo ni miradi kutokumalizika kwa wakati;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(Tanzania Rural and Urban Roads Agency – TARURA),* Kamati ilipokea taarifa hiyo na katika uchambuzi wa Kamati kupitia Taarifa ambayo iliwasilishwa kwetu ama TAMISEMI ambayo ni msimamizi wa Taasisi hii ya *TARURA*, Kamati imebaini kuwa uwiano wa viwango vya barabara kati ya barabara za udongo, changarawe na lami ni mdogo sana. Kamati imebaini kuwa sehemu kubwa ya barabara zinazohudumiwa na *TARURA* 69% ni za udongo. Hali hii ikisababisha barabara nyingi zinazosimamiwa na *TARURA* kuharibika kila wakati hasa katika misimu ya mvua zinazoendelea kama sasa. Katika muktadha huu, Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kwa matengenezo makubwa ya mara kwa mara kwa barabara zile zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii, Kamati inashauri *TARURA* kupandisha barabara nyingi za udongo kwenda kuwa barabara za changarawe zikijumuisha ujenzi wa mifereji ili kuzuia athari za mmomonyoko wakati wa mvua nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 *TARURA* iliidhinishiwa na Bunge lako shilingi bilioni 818 kwa ajili ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara katika halmashauri zetu. hadi kufikia Disemba, 2023 fedha zilizopokelewa na Wakala (*exchequer*) ni shilingi bilioni 339.23 sawa na asilimia 47.75% ya bajeti ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pesa taslimu ambazo zilizopokelewa hadi tarehe 31 Disemba, 2023 ni shilingi bilioni 82.50 sawa na 12% ya bajeti ya mwaka. Upokeaji huo wa fedha umewezesha utekelezaji wa kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kufikia asilimia 38.84% ya malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haijaridhishwa kabisa na hali hii ya upelekaji wa fedha za bajeti kwa *TARURA*, hasa ukizingatia kuwa katika kipindi cha hivi karibuni kumeripotiwa

kuwepo kwa uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara nchini kulikotokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali ya nchi. Ikumbukwe kuwa Bunge lako lilipitisha bajeti hii ya bilioni 808.02 na Serikali ilihaidi ndani ya Bunge lako kutoa bilioni 350 za ziada kwa *TARURA*. Kamati inasikitika kwamba hata fedha hizi pia bado hazijapokelewa mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Masoko ya Kariakoo, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Shirika la Masoko ya Kariakoo na kuijadili. Tuchambuzi Taarifa Kamati na tulibaini mambo mbalimbali pamoja na changamoto nyingi ambazo Kariakoo inaendelea kukumbana nazo Maafisa wengi wanaokaimu nafasi zao bado hawajawa *confirmed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swala la mabasi yaendayo kasi *DART*, Katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa, *DART* imeendelea kutekeleza vyema majukumu yake tangu awamu ya kwanza mpaka awamu ya tatu. Imebaini kuwa utekelezaji na utoaji wa huduma zinazotokana na mradi huu na namna mradi ulivyo umeifanya Tanzania kuwa ya mfano. Hii imefanya nchi takribani 12 kuja nchini kwetu kujifunza kuhusu uendeshaji wa usafiri mijini kwa kutazama mafanikio ya *DART*. Pamoja na mradi wa *DART* kuwa wa mfano kwa nchi kadhaa Afrika, bado umekumbwa na changamoto nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya kina kuhusiana na uendeshaji wa mradi huu wa mabasi ya mwendokasi. Aidha, Serikali itazame upya uendeshaji wa *DART*, ili kuona namna bora ya kuimarisha usafiri ambao kwa sasa umekuwa ni adha kwa wananchi wa Jiji la Dar es Salaam. Ikiwezekana kwa kufungua milango kwa kampuni na sekta binafsi kutumia miundombinu ya mwendokasi kwa utaratibu ambao wakala utapanga ama utaona unafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilipitia maazimio ya Bunge lako yaliyotokana na Taarifa ya mwaka ya ile Kamati iliyokuwa inaitwa USEMI iliwasilishwa kwako mwaka 2023. Kamati ilipokea na kujadili taarifa za Wizara inayoisimamia na tuliona kwamba kati ya Maazimio ya saba yaliyotolewa na Bunge kupitia

Kamati ya Kudumu ya Bunge iliyokuwa inaitwa *USEMI* Maazimio hayo yametelekezwa kwa kiasi kikubwa, aidha Maazimio yaliyobaki Kamati imefahamishwa kuwa mchakato wake wa utekelezaji unaendelea. Maazimio ambayo bado utekelezaji wake unaendelea;

(i) Azimio kuhusu migogoro ya ardhi katika halmashauri nchini;

(ii) Migogoro wa ardhi katika Jiji la Dodoma;

(iii) Uanzishwaji wa Shirika la Masoko Tanzania; na

(iv) Utungaji wa Sheria ya Usafiri wa Umma mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo. Kufuatia utekelezaji wa majukumu ya Kamati, mafanikio na changamoto zilizobainika katika kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024, Kamati inatoa maoni yafuatayo: -

(a) Upungufu wa watumishi katika sekta ya utawala, afya na elimu ni changamoto kubwa katika maeneo mengi nchini, Kamati inashauri, Serikali kuendelea na utaratibu wa kutoa ajira kwa watumishi wa kada ya afya, elimu na watendaji wa kata na vijiji ili kupunguza tatizo hili. Aidha, ajira hizo zizingatie maeneo yenye upungufu zaidi ili wananchi waweze kufikiwa na huduma; *(Makofi)*

(b) Bajeti zinazopitishwa na Bunge kwaajili ya utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa shule, barabara na vituo vya afya, zipelekwe kwa wakati ili kuleta tija katika uendelezaji wake. Aidha, Serikali inapaswa kuongeza nguvu katika usimamizi wa miradi ya maendeleo na kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wazembe wanaoshindwa kusimamia matumizi ya Fedha zilizopelekwa kwaajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali; *(Makofi)*

(c) Uharibifu wa miundombinu ya barabara ni changamoto iliyojitokeza kwa kiasi kikubwa hususani katika kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kunyesha kwa kiasi kikubwa, Kamati inashauri kuwa, Serikali ichukue hatua za dharura na madhubuti katika maeneo yaliyoharibika zaidi kutokana na mvua hizi ikiwemo kufanya ukarabati wa haraka ili kupunguza athari na wananchi kukosa huduma. Aidha, kutumia bajeti ya dharura ambayo ililengwa kwa ajili ya kuendelea kukarabati maeneo ambayo miundombinu inaendelea kuharibika; *(Makofi)*

(d) Serikali inapaswa kuendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji na utumiaji wa fedha za kodi na ushuru katika halmashauri zote nchini ili kuziba mianya kwa Halmashauri kukusanya mapato kidogo au kutumia mapato kiholela;

(e) Maagizo yote yanayotolewa na Viongozi Wakuu wa Serikali yanapaswa kuwekewa utaratibu wa ufutiliaji na mipango madhubuti ya utekelezaji wake ili kufanya maelekezo na maagizo haya kuwa na tija pale ambapo Viongozi wanapotoa ahadi hizo kwa wananchi wao;

(f) Serikali kupitia upya kanuni za uendeshaji wa Halmashauri kuona nafasi ya Mbunge katika usimamizi wa shughuli za maendeleo ndani ya Halmashauri. Kwani Sheria ya sasa inamtambua Mbunge kama mjumbe katika baraza la madiwani, jambo ambalo linaathiri maamuzi ya Mbunge katika mchango wake; *(Makofi)*

(g) Serikali kuendelea kuwekeza katika teknolojia na matumizi ya TEHAMA kama njia mbadala ya kuongeza tija katika utendaji kazi kwa watumishi katika sekta zote. Aidha, matumizi haya yaendane na utoaji fursa za mafunzo mbalimbali kwa watumishi ili kuendana na kasi ya teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekeozo, Kamati inatoa mapendekezo yafuatayo ili kuboresha utekelezaji bora wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu, Wakala wa barabara Vijijini na Mijini *(TARURA*): -

Kwa kuwa, Malengo ya uanzishwaji wa Wakala wa barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*) yalikuwa ni uboreshaji wa mtandao wa barabara wilayani ili kukabiliana na changamoto za mapungufu kwenye sekta ya barabara za vijijini na mijini;

Na kwa kuwa, pamoja na jitihada mbalimbali za kuijengea uwezo *TARURA* bado wakala unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile uhaba wa fedha za utekelezaji wa miradi kusua sua kwa wakandarasi na baadhi ya wakandarasi kutokua na uwezo, mitambo, mitaji ya kutekeleza miradi pamoja na uzembe wa makusudi wa watendaji wa Serikali katika usimamizi wa miradi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Bajeti iliyopitishwa na Bunge kutekeleza miradi ipelekwe kama ilivyoidhinishwa na Bunge;

(b) Serikali iongezee *TARURA* Bajeti kufikia shilingi trilioni 1.64 kutoka shilingi Bilioni 710 kwa miaka minne mfululizo ili kufikia malengo ya asilimia 70 ya barabara kuwa za changarawe, asilimia tatu kuwa barabara za lami na kujenga vivuko vyote vya barabara zetu;

(c) Serikali kusimamia kwa makini taratibu za manunuzi kulingana na uwezo wa wakandarasi wanaoomba kazi na utekelezaji wa miradi husika;

(d) Serikali kutekeleza mchakato wa kuanzisha hati Fungani (*TARURA* SAMIA *INFRASTRUCTURE BOND)* kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara;

(e) Serikali kutafuta vyanzo vya fedha mbadala ikiwemo kushirikisha sekta binafsi ili kuiwezesha *TARURA* kuwa na fedha za uhakika za kutekeleza miradi yake;

(f) Kuandaa na kuwawezesha makandarasi wazawa kushiriki kwenye ushindani katika utekelezaji wa miradi ya *TARURA*; na

(g) Barabara za vijijini kusimamiwa na jumuiya za watumia barabara wa vijijini kama zilivyo katika jumuiya ya watumia maji, na bajeti za matengenezo ziende kwa jumuiya hizo badala ya wakandarasi kutoka mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la utawala: -

Kwa kuwa, Sera ya Ugatuaji wa Madaraka *(D by D)* ambayo dhumuni lake ni kuiwezesha TAMISEMI kusimamia na kupeleka maendeleo vijijini imedhoofika;

Na kwa kuwa, hali hiyo imesababishwa na TAMISEMI kujikita zaidi katika jukumu la utawala na kuacha eneo la maendeleo vijijini bila usimamizi madhubuti;

Na kwa kuwa, hali hiyo inaleta ombwe linalopelekea Taasisi zingine za Serikali kutumia mwanya huo kunyofoa majukumu ya TAMISEMI na kukinzana na Sera ya Ugatuaji wa madaraka unaoelekeza TAMISEMI kusimamia maendeleo vijijini,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(a) Serikali isimamie kikamilifu utekelezaji wa Sera ya *D by D* na misingi yake;

(b) Serikali idhibiti mwenendo wa baadhi ya taasisi zake wa kuhamisha Mamlaka za Utumishi ambazo ndiyo msingi wa utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka;

(c) Serikali irejeshe Idara muhimu zinazowezesha utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka, zikiwemo Idara ya Uratibu wa Sekta na Idara ya ujenzi ndani ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya Elimu: -

Kwa kuwa, Serikali kuwekeza kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika Sekta ya Elimu nchini, bado maeneo mengi yanakabiliwa na uhaba wa madawati, upungufu wa watumishi (walimu), kutokumalizika kwa maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi, nyumba za watumishi; vifaa na viwanja vya michezo;

Na kwa kuwa, uhaba wa miundombinu hiyo unapelekea elimu kutotolewa kwa kiwango kinachostahili;

Hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali kusimamia vizuri matumizi ya fedha za ndani ili fedha hizi ziweze kutekeleza ukamilishaji wa miradi na uendelezaji wa miundombinu ya Elimu;

(b) Serikali kutoa ajira kwa walimu kwa kuzingatia maeneo ambayo yana upungufu zaidi; na

(c) Serikali ije na suluhisho la kudumu la kuhakikisha kwamba halmashauri zote nchini zinaanzisha programu maalum ya kumaliza tatizo la uhaba wa madawati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya afya: -

Kwa kuwa, Serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha katika miradi ya sekta ya afya kama vile hospitali, vituo vya afya na zahanati;

Na kwa kuwa, kuna changamoto ya uhaba wa vifaa tiba na upungufu wa wataalam katika vituo vya afya nchini;

Na kwa kuwa, upungufu huo unasababisha huduma za afya kutolewa kwa kiwango duni**;**

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali ifanye tathmini ya gharama na mahitaji ya vifaa vinavyohitajika katika kila kituo cha afya nchini ili kujua ukubwa wa tatizo;

(b) Serikali iandaae mpango kazi na kutafuta ufumbuzi wa kibajeti ili kumaliza tatizo hili; na

(c) Serikali ifanye uwekezaji wa rasilimali watu (watalaam) katika maeneo ya hospitali, vituo vya afya na zahanati zote nchini, hasa kwa maeneo yale ambayo vifaa vimenunuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu lishe na michezo: -

Kwa kuwa, maeneo ya lishe na michezo shuleni hayapewi kipaumbele;

Na kwa kuwa, kuna madhara ya wazi kama vile udumavu, miili kutokuwa imara na magonjwa yasiyoambukiza kutamalaki;

Na kwa kuwa hali hiyo inasababisha Serikali kutumia rasilimali watu na fedha nyingi kushughulikia matokeo ya kutokuwekeza kwenye maeneo ya lishe na michezo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(a) Serikali iangalie namna bora ya kupunguza gharama ya vifaa vya michezo mashuleni;

(b) Serikali iweke mkakati wa kuwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye viwanja vya michezo pamoja na walimu wa michezo mashuleni;

(c) Serikali ione namna bora ya kuanzisha idara ya michezo na utamaduni katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI

itakayosimamia masuala ya michezo kuanzia ngazi ya vijiji;

(d) Serikali iweke mpango madhubuti na unaotekelezeka wa kuboresha suala la lishe shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa niaba ya Kamati napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa Mbunge – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu Mawaziri Mheshimiwa Deogratius John Ndenjembi, na Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, kwa ushirikiano wao kwa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Adolf Ndunguru, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee niwashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa shughuli za Kamati. Aidha, natambua na kuthamini michango yao adhimu na kujitoa kwao kikamilifu katika kuhakikisha Kamati yetu inatekeleza wajibu wake kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba orodha ya majina yao iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee pia napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Wankanga Mwihambi, *ndc,* kwa ushirikiano wake kwa Kamati katika kipindi chote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake, pamoja na Sekretarieti ya Kamati hii, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa

hii. Sekretarieti hii ilikuwa na ndugu yetu Emmanuel Mdidi na Dada Sikudhani Mbinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARI, 2023 HADI JANUARI, 2024 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024.

**1.1 Muundo wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Taarifa hii imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo: -

i) **Sehemu ya Kwanza**, inatoa maelezo ya jumla ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, mbinu na njia zilizotumika pamoja na orodha ya shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja;

ii) **Sehemu ya Pili**, ambayo inafafanua shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto zilizojitokeza;
iii) **Sehemu ya Tatu**, inatoa maoni ya jumla na mapendekezo ili kuliwezesha Bunge kufanya maamuzi; na

iv) **Sehemu ya Nne,** ni Hitimisho na kutoa hoja kwa ajili ya Bunge kuweza kujadili na kufanya maamuzi.

## 1.2 Njia iliyotumika kuteleleza Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake, kama ilivyo takwa la Kanuni ya 142(a) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Kamati ilitumia njia kuu tatu kama ifuatavyo: -

i) Kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara pamoja na Taasisi inazozisimamia;

ii) Kusoma na kuchambua taarifa za utekelezaji wa majukumu zilizowasilishwa na Wizara na Taasisi zake; na

iii) Kuandaa na kutoa maoni na ushauri kuhusu yatokanayo na taarifa za Wizara na Taasisi inazozisimamia.

## 1.3 Madhumuni ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyoelekezwa katika Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Madhumuni ya Taarifa hii ni kubainisha mambo yanayohusu uendeshaji wa shughuli za Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024. Lengo ni kuonesha mambo yanayohitaji kuboreshwa ili Bunge liyajadili kwa kuzingatia majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba[1].

[1] 63._ *(2) Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano* na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii.

## 1.4 Msingi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge kwa niaba ya wananchi, lina jukumu kubwa la kuisimamia na kuishauri Serikali. Aidha, Ibara ya 96(1) ya Katiba inaweka utaratibu na msingi wa uwepo wa Kamati za Bunge na utekelezaji wa majukumu ya Kamati ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Kanuni ya 137 kwa pamoja na Nyongeza ya Nane zinaweka msingi wa utekelezaji wa shughuli za Kamati za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane 5(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na taasisi zake.

Aidha, Nyongeza ya Nane, 7(1) (a-d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, imeainisha majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge ikiwemo Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuwa ni pamoja na: -

a) Kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Maazimio na Mikataba inayopendekezwa, kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zilizo chini yake; na

d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Taasisi na Idara zilizo chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA

**Mheshimiwa Spika,** katika Kipindi cha Mwaka 2023/2024, Kamati ilipata wasaa wa kutekeleza majukumu yake mbalimbali ambayo imepewa kwa mujibu wa Kanuni ya 137 na Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 7 (1) (a-d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Shughuli ambazo Kamati imezitekeleza ni pamoja na: -

a) Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa Fedha 2023/2024;

b) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa Fedha 2023/2024;

c) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji wa Wizara na Taasisi inazozisimamia;

d) Kupokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya USEMI iliyowasilishwa Bungeni Februari, 2023; na

e) Kushiriki Semina za mafunzo.

### 2.1 Kufanya ziara za ukaguzi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilipata wasaa wa kupokea na kujadili taarifa mbalimbali za miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara na Taasisi inazozisimamia. Aidha, Kamati ilifanikiwa kufanya ziara katika Mikoa kumi na moja (11) ambayo ni Mwanza, Mara, Tabora, Singida, Iringa, Morogoro,

Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Arusha, Tanga, na Mbeya ambako Kamati ilikagua jumla ya Miradi 49.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi mitano (5) Mkoa wa Mwanza, miradi mitatu (3) Mkoa wa Mara, miradi mwili (2) Mkoa wa Tabora, miradi mitano (5) Mkoa wa Singida, miradi sita (6) Mkoa wa Morogoro, mradi mmoja (1) Mkoa wa Dar es Salaam (Mradi wa DART Lot II na Lot III), miradi mitatu (3) Mkoa wa Mtwara, miradi mine (4) Mkoa wa Lindi, miradi mitano (5) Mkoa wa Arusha, miradi mitano (5) Mkoa wa Tanga, miradi sita (6) Mkoa wa Iringa na miradi minne (4) Mkoa wa Mbeya na kupokea taarifa za maendeleo ya miradi hiyo. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

i) Mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Mwanza inayojengwa katika Wilaya ya Magu (Machi, 2023);

ii) Mradi wa matengenezo kwa kiwango cha lami ya Barabara ya Kisesa – Bujora (Magu) yenye urefu wa km 1.32 (Machi, 2023);

iii) Mradi wa ujenzi wa Soko la Mjini Kati lililopo Jijini Mwanza (Machi, 2023);

iv) Mradi wa ujenzi wa jengo la Utawala la Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime (Machi, 2023);

v) Mradi wa ujenzi wa barabara za Kwangwa – Mkirira na Mwisenge – Nyamlasa Mkoani Mara (Machi, 2023);

vi) Mradi wa Matengenezo Maalumu ya barabara yenye urefu wa Km. 39.5, Ujenzi wa Mifereji kwa urefu wa M.800 na ujenzi wa Kalavati (8Nos) katika barabara za Bukima – Bulinga – Bwasi, Nyegugu – Rusoli – Makojo, Kwikerege P/s na Busungu – Bulinga – Bujaga (Machi, 2023);

vii) Mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Bariadi Mkoani Simiyu (Machi, 2023);

viii) Mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Shinyanga (Machi, 2023);

ix) Mradi wa Uboreshaji wa Kituo cha Afya Kambarage kilichopo Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga (Machi, 2023);

x) Mradi wa ujenzi wa Soko la Wamachinga la Halmashauri ya Shinyaga (Machi, 2023);

xi) Mradi wa Ujenzi wa Mabanda 106 ya Biashara Soko Kuu Manispaa ya Shinyanga (Machi, 2023);

xii) Mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Ikungi iliyoko Mkoani Singida (Machi, 2023);

xiii) Mradi wa ujenzi wa Shule ya Wasichana ya Mkoa wa Singida (Machi, 2023);

xiv) Mradi wa Ujenzi wa Soko la kisasa la Mlandenge katika Manispaa ya Iringa (Oktoba, 2023);

xv) Mradi wa ujenzi wa Barabara ya Don Bosco – Mawelewele Halmashauri ya Manispaa ya Iringa chini ya TARURA (Oktoba, 2023);

xvi) Mradi wa Soko la Kisasa la Kingalu katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro (Oktoba, 2023);

xvii) Mradi wa ujenzi wa Stendi ya Mabasi ya Abiria ya Mafiga katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro (Oktoba, 2023);

xviii) Mradi wa ujenzi wa Barabara ya Barakuda yenye urefu wa Km. 2.4 katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro chini ya TARURA (Oktoba, 2023);

xix) Mradi wa ujenzi wa Barabara ya Tubuyu yenye urefu wa Km. 2.4 katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro chini ya TARURA (Oktoba, 2023);

xx) Mradi wa ujenzi wa Barabara ya Nane Nane yenye urefu wa Km. 1.6 katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro chini ya TARURA (Oktoba, 2023);

xxi) Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Kibiashara katika eneo la Stendi ya Kange (Kange business Complex) katika Halmashauri ya Jiji la Tanga (Oktoba, 2023);

xxii) Mradi wa Barabara za kuelekea Kituo cha Mabasi na sehemu ya maegesho ya malori katika Halmashauri ya Jiji la Tanga chini ya TARURA (Oktoba, 2023);

xxiii) Mradi wa ujenzi wa Dampo la Kisasa la Mpirani katika Halmashauri ya Jiji la Tanga (Oktoba, 2023);

xxiv) Mradi wa ujenzi wa Barabara ya Msambweni katika Halmashauri ya Jiji la Tanga, chini ya TARURA (Oktoba, 2023);

xxv) Mradi wa ujenzi wa Dampo la Kisasa la Muriet katika Halmashauri ya Jiji la Arusha (Oktoba, 2023);

xxvi) Ujenzi wa Uwanja wa Kisasa wa Michezo Shule ya Msingi Ngarenaro katika Halmashauri ya Jiji la Arusha (Oktoba, 2023);

xxvii) Ujenzi wa Barabara ya Oljoro Muriet katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, chini ya TARURA, (Oktoba, 2023);

xxviii) Mradi wa upanuzi wa Barabara ya Njiro, Krokon, Sombetini – FFU katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, iliyo chini ya TARURA, (Oktoba, 2023);

xxix) Mradi wa ujenzi wa Barabara ya Bypass ya Kisongo – Airport yenye urefu wa Km. 1.7 katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, iliyo chini ya TARURA, (Oktoba, 2023);

xxx) Mradi wa ujenzi wa Barabara ya magari yaendayo kwa kasi Mkoa wa Dar es Salaam (Dar es Salaam Rapid Transport – DART) Awamu ya Pili na Awamu ya Tatu Jijini Dar es Salaam (Juni & Oktoba, 2023);

xxxi) Mradi wa ukarabati wa jengo la zamani na ujenzi jengo jipya katika Shirika la Masoko la Kariakoo Jijini Dar es Salaam (Oktoba, 2023);

xxxii) Mradi wa ujenzi wa Barabara za Mkwajuni (Mbweni) yenye urefu wa Km. 7.85, Barabara ya Toure Drive yenye urefu wa Km. 3.5 na Barabara ya Mbweni JKT yenye urefu wa Km. 3.91 Jijini Dar sa Salaam zilizo chini ya TARURA (Oktoba, 2023);

xxxiii) Mradi wa ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari ya Kata ya Isuna katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi Mkoani Singida (Oktoba, 2023);

xxxiv) Mradi wa ujenzi wa Shule mpya ya Msingi katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida (Oktoba, 2023);

xxxv) Mradi wa ujenzi wa jengo la OPD na RCH katika Zahanati ya Mkwajuni, Manispaa ya Lindi (Novemba, 2023);

xxxvi) Mradi wa ujenzi wa OPD na RCH katika Zahanati ya Banduka, Manispaa ya Lindi (Novemba, 2023);

xxxvii) Mradi wa ujenzi wa OPD, Maabara, Wodi ya akina mama (maternity), chumba cha upasuaji (theatre), chumba cha kufulia nguo (laundry) pamoja na kichomea taka (incinerator) katika Kituo cha Afya Mtama, Halmashauri ya Wilaya ya Mtama Mkoani Lindi (Novemba, 2023);

xxxviii) Mradi wa ujenzi wa OPD, Maabara, chumba cha kufulia nguo (laundry), kichomea taka (incinerator) pamoja na njia za watembea kwa miguu (walk ways) katika Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea, Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea Mkoani Lindi (Novemba, 2023);

xxxix) Mradi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), Maabara na Kichomea taka katika kituo cha Afya Kitaya, Halmashauri ya Mji Nanyamba Mkoani Mtwara (Novemba, 2023);

xl) Mradi wa ujenzi wa jengo la Wagonjwa wa nje (OPD), maabara na kichomea taka katika Kituo cha Afya Mtandi, Halmahauri ya Mji Masasi Mkoani Mtwara (Novemba, 2023);

xli) Mradi wa ujenzi wa OPD, EMD, jengo la wazazi, Wodi ya wanawake na wanaume, jengo la kufulia, stoo ya dawa na ununuzi wa vifaatiba katika Hospitali ya Wilaya ya Newala (Mchemo), Halmashauri ya Wilaya ya Newala Mkoani Mtwara (Novemba, 2023);

xlii) Mradi wa ujenzi wa zahanati, jengo la OPD na jengo la mama na mtoto katika Zahanati ya Nkomo iliyopo Halmashauri ya Mji wa Nanyamba Mkoani Mtwara (Novemba, 2023);

xliii) Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Kata ya Kitwiru – Manispaa ya Iringa (Januari, 2024),

xliv) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Wenda – Mgama (km 19) kwa kiwango cha lami (Agriconnect) (Januari, 2024),

xlv) Mradi wa ujenzi wa Barabara ya Mtiri – Ifwagi (Km 14) kwa kiwango ch lami (Agriconnect) Januari, 2024

xlvi) Mradi wa Ujenzi wa Barabara Lupeta – Wimba – Izumbwe (10.1kms) kwa kiwango cha lami (Agri-connect) (Januari, 2024)

xlvii) Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Mwasanga na Barabara ya Mwasanga – Tembela (Januari, 2024),

xlviii) Mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Kata ya Nsalaga (SEQUIP) (Januari, 2024); na

xlix) Barabara ya Inyala – Simambwe (16.7kms) kwa kiwango cha lami (Agriconnect) (Januari, 2024).

**Mheshimiwa Spika,** miradi iliyotajwa baadhi yake ilitolewa taarifa wakati wa vikao vya Bunge la Bajeti. Aidha, miradi iliyosalia

ilitembelewa na kukaguliwa wakati vikao vingine vya Kamati vilivyofanyika baada ya Bunge la Bajeti.


## 2.2 Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara na taasisi zilizo chini yake (Fungu 56)

### 2.2.1 Makao Makuu ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Fungu Namba 56) na Taasisi zilizo chini yake ziliidhinishiwa jumla ya **Shilingi Trilioni 1.074** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2023 Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu Na. 56) na Taasisi zake zilipokea jumla ya **Shilingi bilioni 733.601** sawa na **asilimia 68.24** ya Fedha iliyoidhinishwa, kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 1

***Kielelezo Na. 1***

***Ulinganisho wa Fedha zilizotengwa na Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai-Disemba, 2023) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zilizo chini yake (katika bilioni).***




**Chanzo:** *Taarifa ya OR-TAMISEMI na usanifu wa Kamati (Februari, 2024)*


### 2.2.2 Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu 02)

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Tume ya Utumishi wa Walimu iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 17,203,948,300** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, Mishahara ni **shilingi 8,819,516,000** sawa na **asilimia 41,** matumizi mengineyo ni **shilingi 7,714,432,300** sawa na **asilimia 33** na Miradi ya Maendeleo ni **shilingi 670,000,000** sawa na **asilimia 26.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitarifiwa kuwa, hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2023 Tume ya Utumishi wa Walimu ilipokea na kutumia jumla ya **Shilingi 7,947,416,357** sawa na **asilimia 46** ya kiasi cha Bajeti yake iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya Fedha hizo **shilingi 4,728,826,000** ni Mishahara, **shilingi 2,708,733,508** ni matumizi Mengineyo na **shilingi 509,847,849.38** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, *kama ilivyo katika kielelezo Na. 2*

***Kielelezo Na. 2***

***Ulinganisho wa Fedha zilizotengwa na Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai-Disemba, 2023) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa - Tume ya Utumishi wa Walmu Tanzania.***




**Chanzo:** *Taarifa ya OR-TAMISEMI na usanifu wa Kamati (Februari, 2024)*


## 2.2.3 Sekretarieti za Mikoa (Mafungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa) 2.2.4

### a) Makao Makuu ya Sekretrieti za Mikoa

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mikoa iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 281,304,416,000.00.** Kati ya Fedha hizo Mishahara ni **shilingi 73,778,256,000.00,** Matumizi Mengineyo ni **shilingi 107,706,120,000.00,** na Fedha za Miradi ya Maendeleo ni **shilingi 99,820,040,000.00** ambapo kati ya Fedha za maendeleo zilizoidhinishwa, Fedha za Ndani ni **shilingi 69,618,865,000.00** na Fedha za Nje **ni shilingi 30,201,175,000.00.** Aidha, jumla ya **shilingi 261,890,400.00** ziliidhinishwa kama maduhuli ya Mikoa (Tazama Kielelezo Na. 3).

**Mheshimiwa Spika,** hadi tarehe 31 Disemba, 2023 jumla ya **shilingi 117,732,502,208.79** sawa na **asilimia 41.48** ya Fedha zilizoidhinishwa zimepokelewa. Kati ya Fedha hizo **shilingi 30,601,903,293.00** ni Mishahara, **shilingi 44,693,064,359.00** ni Matumizi mengineyo na **shilingi 42,437,534,556.79** ni Maendeleo. Aidha, **shilingi 51,112,000.00** za Maduhuli zimekusanywa (Tazama Kielelezo Na. 3).

***Kielelezo Na. 3***
***Ulinganisho wa Fedha zilizotengwa na Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai-Disemba, 2023) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri).***





**Chanzo:** *Taarifa ya Wizara ya OR-TAMISEMI na usanifu wa Kamati (Februari, 2024)*

**b) Ofisi za Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri za Wilaya)**

**Mheshimiwa Spika,** katika bajeti ya Mwaka 2023/2024 Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 7,770,394,930,000.00.** Kati ya Fedha hizo **shilingi 5,364,151,698,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 2,406,243,232,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi Disemba, 2023 jumla ya **Shilingi 3,510,000,781,083.92** zimepokelewa sawa na **asilimia 45.2** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya Fedha hizo zilizopokelewa kiasi cha **Shilingi 2,674,617,144,338.65** sawa na **asilimia 49.9** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 835,383,636,745.27** sawa na **asilimia 34.7** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Kielelezo Na. 4**

**Ulinganisho wa Fedha zilizotengwa na Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai-Disemba, 2023) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri).**




***Chanzo:*** *Taarifa ya OR-TAMISEMI na usanifu wa Kamati (Februari, 2024)*

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla hali ya utolewaji Fedha kwa Wizara hii ni ya kuridhisha kwani katika uchambuzi wake Kamati imebaini Fedha zilizotolewa kwa Wizara (Fungu 56, Fungu 02 pamoja na Mafungu 26 ya mikoa) kwa ujumla ni asilimia **51.9**.

## 2.3 Taarifa za Utendaji za Wizara na Taasisi inazozisimamia

**Mheshimiwa Spika,** Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Agosti na Oktoba, 2023 na Januari, 2024, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa za Utendaji wa Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na Taasisi zake. Taarifa zilizowasilishwa na kuchambuliwa na Kamati ni kama ifuatavyo: -

### 2.3.1 Taarifa ya Utendaji ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Makao Makuu ya Wizara)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua taarifa zifuatazo: -

**i) Utekelezaji wa shughuli na Miradi ya Ujenzi wa Ofisi za Halmashauri na Sekretarieti za mikoa nchini**

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa Serikali inaziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini ili kutekeleza jukumu lake la kufikisha huduma kwa wananchi, Serikali imekuwa ikitekeleza miradi ya ujenzi wa ofisi za Halmshauri za Wilaya pamoja na ofisi za mikoa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijadili taarifa ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu ujenzi wa Ofisi za Mikoa na Halmashauri nchini ili kujua hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati imebaini kuwa Serikali imefanya juhudi kubwa sana katika kuimarisha utendaji wa Sekretarieti za Mikoa na Halmashari za Wilaya nchini. Jambo ambalo lilileta tija kubwa sana katika upelekaji wa huduma kwa wananchi nchini. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa ujenzi wa ofisi mbalimbali za mikoa na halmashauri za wilaya na miji nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijadili na kuichambua taarifa hii kwa kina. Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini mambo muhimu kama ifuatavyo: -

a. Katika utekelezaji wa miradi hii Halmashauri zimekuwa zikikosa wazabuni wenye uwezo wa kutekeleza majukumu ya

ujenzi wa miradi hiyo kwa wakati kutokana na wazabuni hao kuwa na uwezo mdogo wa kutekeleza miradi ya Halmashauri;

b. Kamati pia ilibaini kuwa halmashauri nyingi nchini zimekuwa zikitumia baadhi ya Fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo kwa shughuli nyingine kama ujenzi wa barabara za kufikisha vifaa vya ujenzi eneo la ujenzi;

c. Kukosekana kwa huduma nyingine kama vile umeme, maji pamoja na miundombinu ya barabara kumepelekea kuongezeka kwa gharama katika utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati imebaini kuwa wakati wa usanifu wa miradi hii, taasisi nyingine za Serikali kama vile TARURA, Mamlaka za Maji pamoja na Ofisi za TANESCO Mikoa na Wilaya hazishiriki, jambo ambalo Kamati inaona kuwa si sahihi kwa mustakabali mzuri wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa majengo ya ofisi za mikoa na halmashauri za wilaya na miji nchini; na

d. Kumekuwa na ucheleweshaji wa ujenzi wa majengo haya kutokana na kuwa na bajeti ndogo na Fedha zilizotengwa awali kutotosheleza kutokana na kuongezeka kwa gharama za ujenzi kulikotokana na kupanda kwa gharama za manunuzi ya vifaa mbalimbali vya ujenzi na uchepushaji wa Fedha za mradi kwa ajili ya matumizi mengine kama vile kugharamia uwekaji wa miundombinu ya maji, umeme na barabara kuelekea maeneo ya miradi.

**ii) Utekeleaji wa Miradi ya ujenzi wa miundombinu ya elimu nchini (Madarasa, madawati, maabara na maktaba)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea taarifa za Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya kutolea elimu nchini (madarasa, madawati, maabara na maktaba).

**Mheshimiwa Spika**, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 imetamka kuunda Serikali itakayoimarisha rasilimaliwatu. Ibara ya 80 Ibara ndogo (a) Ilani inatamka kuwa katika kipindi cha kuanzia 2020 hadi 2025" Chama

*kitaielekeza Serikali kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu pamoja na kuhifadhi na kuendeleza mazingira ya shule hizo*[2]*".*

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeweka juhudi kubwa katika kuhakikisha kuwa miundombinu hii inaimarishwa katika shule za msingi na sekondari nchini ili kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya wanafunzi kujifunza. Uwekezaji huu kupitia miradi mbalimbali kama vile *SEQUIP, BOOST na EP4R* imelifanya taifa kushuhudia mabadiliko makubwa ya mazingira ya kutolea elimu kwa shule za msingi na sekondari nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanya uwekezaji mkubwa sana wa ujenzi wa miundombinu ya elimu ikiwemo ujenzi wa madarasa katika shule za msingi na sekondari nchini hali iliyopelekea ongezeko la wanafunzi katika shule za msingi na sekondari na kusababisha upungufu wa madawati. Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya halmashari zimefanya vizuri kwa kuongeza Fedha za miradi pale pesa kutoka Serikali Kuu zilipoishia. Aidha, Kamati inazipongeza sana Halmashauri hizo. Miongoni mwa halmashauri zilizofanya vizuri kwenye uwekezaji wa miundombinu hiyo ya elimu kwa upande wa ujenzi wa maboma kwa kutumia vyanzo vya ndani ni Halmashauri za Mkoa wa Katavi.

**iii) Upandaji wa miti, utunzaji wa mazingira na uwezekano wa miradi ya hewa ya ukaa katika halmashauri**

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri nyingi nchini zimekuwa zikikumbwa na uharibifu wa mazingira kwa ukataji miti hovyo. Hali hii imekuwa ikisababisha pamoja na mambo mengine ongezeko la hewa ukaa angani. Hali kadhalika kukosekana kwa misitu kunasababisha halmashauri nyingi kushindwa kutekeleza jukumu lake la utengenezaji wa madawati kwa gharama nafuu kutokana na kukosa mbao zinazofaa karibu na maeneo ya Halmashauri. Kamati inaona kuwa ni wakati mwafaka sasa kwa halmashauri kuweka mikakati ya kuanzisha misitu ya halmashauri itakayowezesha upatikanaji rahisi wa mbao kwa ajili ya samani mbalimbali katika ofisi za halmashauri na katika shule za msingi na sekondari.

[2] Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia imebaini uwepo wa misitu katika halmashauri unaweza kuleta faida kubwa kwa halmashauri kwa kufanya biashara ya hewa ukaa. Mfano mzuri ni Halmashauri ya Tanganyika ambayo katika mwaka 2023 imefanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 14, Halmashauri za Mbulu na Katavi zimekusanya kiasi cha shilingi bilioni 4.7 kutokana na biashara ya hewa ukaa kutoka kwenye misitu ya vijiji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa masuala ya mabadiliko ya tabianchi na biashara ya hewaukaa (carbon credit) yanaendelea vizuri na tuna misitu ya halmashauri takriban 154, hivyo basi kama halmashauri zikiwekeza kwenye upandaji na utunzaji wa miti utaziwezesha halmashauri kufanya biashara ya hewaukaa, na kupata fedha ambazo zitaziwezesha halmashauri hizo kutekeleza miradi ya maendeleo bila kutegemea zaidi fedha kutoka Serikali Kuu.

**iv) Utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**a) Sekretarieti za Mikoa**

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi za Wakuu wa Mikoa ni chombo kilichoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 61(1) na (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977[4] [3]pamoja na marekebisho yake. Majukumu na muundo wa Tawala za Mikoa yameainishwa katika Sheria ya Tawala za Mikoa Sura 97 (Sheria Na. 19 ya Mwaka 1997).

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa uanzishwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kukuza na kuharakisha maendeleo kwa wananchi kwa kupitia mamlaka za miji na vijiji kwa kuwapa nguvu wananchi

[3] **61.**-(1) Kutakuwa na Mkuu wa Mkoa kwa kila mkoa katika Jamhuri ya Muungano ambaye, bila ya kuathiri ibara ndogo ya (3), atakuwa ni kiongozi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (5), kila Mkuu wa Mkoa, atakuwa na wajibu wa kusimamia utekelezaji wa kazi na shughuli zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika mkoa aliokabidhiwa; na kwa ajili hiyo, atatekeleza kazi na shughuli zote zilizotajwa na sheria, au kwa mujibu wa sheria kama hizi au shughuli za Mkuu wa Mkoa na atakuwa na madaraka yote yatakayotajwa na sheria yoyote iliyotungwa na Bunge.

katika maamuzi kuhusu maendeleo yao wenyewe. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 imeweka kipaumbele katika kuongeza nguvu na kuzifanya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa ndicho chombo kinachowawezesha wananchi kuwa na nguvu na sauti katika kuwezesha maendeleo yao kiuchumi na na kijamii.

> ***122.*** *Kwa kutambua umuhimu wa kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi katika hali iliyo shirikishi, Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kitahakikisha kuwa Serikali za Mitaa zinaendelea kuboreshwa kwa lengo la kuinua ubora wa huduma kwa wananchi*[4].

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inasimamia uendeshaji wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa 26 zenye jumla ya Wilaya 139, Mamlaka za Serikali za Mitaa 184, Tarafa 570, Kata 3,956, Vijiji 12,318, Mitaa 4,263 na Vitongoji 64,355. Kwa mujibu wa Hati idhini ya kuunda Ofisi / Wizara na mgawanyo wa majukumu ya Mawaziri kupitia Tangazo la Serikali la **tarehe 30 Agosti, 2023,** Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na majukumu mengine ina majukumu makubwa yafuatayo: -

i. Usimamizi wa Sera ya Kupeleka Madaraka kwa Wananchi **(Decentralisation by Devolution - D - D)**;
ii. Usimamizi wa Sera ya Maendeleo Vijijini na Mijini;
iii. Usimamizi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa;
iv. Usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa;
v. Kuratibu ujenzi wa miundombinu, utoaji wa huduma Mijini na Vijijini hususani barabara, afya, elimu na usafi wa mazingira; na
vi. Maboresho ya utendaji kazi na Maendeleo ya rasilimali watu.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yaliyotajwa hapo juu, Ofisi ya Rais TAMISEMI ina jumla ya Idara 8 na Vitengo 8 ikiwemo Idara ya Tawala za Mikoa.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa majukumu ya Idara ya Serikali za Mitaa ni kuratibu na kusimamia uendeshaji wa shughuli za

[4] Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020

Serikali katika Mikoa na Wilaya ikiwemo, uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa masuala ya Utawala, Miradi ya Maendeleo na utoaji wa huduma za jamii katika Mikoa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Idara ya ya Serikali za Mitaa. Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini mambo yafuatayo: **-**

i) Kwa muundo wa Sekretarieti za Mikoa zinapaswa kuwa na jumla ya watumishi wataalam 2,678. Hata hivyo, taarifa ya Wizara inaeleza kuwa hadi kufikia Disemba, 2023 idadi ya watumishi waliopo ni 1,534. Hii inafanya Sekretarieti za Mikoa kuwa na upungufu wa **watumishi 1,144 sawa na asilimia 43;**

ii) Utaratibu wa Sekretarieti za Mikoa umewezesha kupatikana kwa mafaniko na kuongeza uwajibikaji na usimamizi katika ngazi ya mikoa ambapo kwa mwezi Septemba, 2023 miradi 884 ilikaguliwa;

iii) Kutokana na uratibu wa Sekretarieti za Mikoa, kero za wananchi zilishughulikiwa kwa mafanikio makubwa ambapo taarifa iliyowasilishwa inaonesha kuwa kwa kipindi cha Septemba hadi Novemba, 2023 kero zilizoshughulikiwa ni 2,199. Aidha, kero hizo zipo katika sekta za ardhi, utawala bora, biashara na maji; na

iv) Imebainika kuwa hakuna utaratibu maalum kwa mamlaka mbalimbali ambazo zinashughulika na kusimamia Watumishi, kuwatembelea na kuzungumza na kusikiliza kero zao kwenye Halmashauri. Hali hiyo imepelekea kuwa na malalamiko mengi ya Watumishi.

## b) Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM)

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Ibara ya 145 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inaweka misingi ya uanzishwaji wa vyombo vya Serikali za Mitaa katika kila Mkoa, Wilaya, Mji na Kijiji ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambavyo vitakuwa vya aina na majina yatakayowekwa na Sheria iliyotungwa na Bunge au Baraza la Wawakilishi. Aidha, Ibara ya 145(2) inasema Bunge au Baraza la Wawakilishi kadri

itakavyokuwa, litatunga Sheria itakayofafanua utaratibu wa kuanzisha vyombo vya Serikali za Mitaa, miundo na wajumbe wake, njia za mapato na utaratibu wa utekelezaji wa shughuli za vyombo hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali za Mitaa. Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini mambo mbalimbali kama ifuatavyo: -

i) Kamati imebaini kuwa katika baadhi ya halmashauri, watumishi hudumu kwa muda mrefu na hivyo kufanya kazi kwa mazoea. Kamati inaona kuwa hili si sawa kwa ustawi wa halmashauri nchini kwa kuwa kufanya kazi kwa mazoea kunaweza kudhoofisha utoaji huduma bora kwa wananchi;

ii) Kamati imebaini kuwa Serikali hupeleka Fedha nyingi katika Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuwaletea maendeleo wananchi. Hata hivyo, imebainika kuwa wasimamizi na watekelezaji wa miradi hiyo (watendaji na wanasiasa katika ngazi ya kata na vijiji), ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hawana ujuzi wa kiuongozi, usimamiaji na ufuatiliaji wa miradi. Kamati imebaini kuwa kutokana na udhaifu huo miradi mingi ndani ya halmashauri hutekelezwa kwa viwango duni. Kamati inashauri kuwa Serikali itoe mafunzo ya mara kwa mara kwa viongozi na watendaji hao kuhusu uongozi, ufuatiliaji na usimamizi wa miradi ndani ya halmashauri ili kuwajengea uwezo wa uongozi, usimamizi na ufuatiliaji mzuri wa miradi ya Serikali; na

iii) Imebainika kuwa maslahi ya viongozi katika ngazi za kata, mitaa na vijiji ni ya chini. Hata hivyo, imebainika kuwa hata utoaji wa maslahi hayo hutofautiana kati halmashauri moja na nyingine. Aidha, baadhi ya halmashauri hazina utaratibu wa kutoa posho ya aina yoyote kwa watendaji wa vijiji na mitaa. Hali hii imekuwa ikisababisha watendaji wengi kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kamati inadhani kuwa hali hii inaweza kusababisha ushawishi wa utoaji na upokeaji wa rushwa kwa watendaji hao. Kamati inashauri Serikali kutoa mwongozo kwa halmashauri zote nchini kuweka utaratibu wa ulipaji wa posho za viongozi katika ngazi za kata, mitaa na vijiji.

### c) Matumizi mengineyo ya Fedha za mapato ya ndani

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijadili taarifa kuhusu ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri na upangaji wa matumizi mengineyo. Kwanza Kamati inaipongeza Serikali kwa kupeleka Fedha nyingi kwenye miradi ya maendeleo katika halmashauri zetu nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba, moja ya majukumu makuu ya halmashauri ni kupeleka maendeleo mijini na vijijini. Hata hivyo, kutokana na Serikali kuu kupeleka fedha nyingi kwenye miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kuwa halmashauri nyingi nchini zimeongeza utegemezi kwa Serikali kuu na kujiondoa katika jukumu lake la msingi kwa kutumia makusanyo ya ndani kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Hali hii imesababisha miradi mingi ya maendeleo ambayo inaanzishwa kutokamilika.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati pia imebaini kuwa Fedha za asilimia 20 kutoka mapato ya ndani zinazotakiwa kupelekwa kwenye vijiji na kata kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa ofisi hizo nazo hazipelekwi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini mapungufu katika mifumo, miundo na watumishi wasio waaminifu katika suala zima la ukusanyaji na usimamizi wa mapato katika ngazi mbalimbali za Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kutokana na matuizi ya mifumo ambayo inapelekea uwezekano wa kuwepo kwa mianya ya upotevu wa ukusanyaji wa mapato. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua Madhubuti kudhibiti watumishi wasio waaminifu na kuweka mifumo inayofaa ili kuziwezesha halmashauri kukusanya mapato kwa ufanisi.

### iv) Utekelezaji wa program za michezo katika shule za msingi na sekondari nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa **Serikali** imeweka Sera na miongozo mbalimbali inayopaswa kutekelezwa ili kukuza michezo kwenye shule zetu nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kuna msemo wa Kilatini unaosema kuwa (***mens sana in corpore sano*** – **a healthy mind in a healthy body**), kwa tafsiri isiyo rasmi maana yake ni akili safi inakaa kwenye mwili safi. Katika ujenzi wa taifa la vijana wenye afya na siha njema, suala la michezo hatuwezi kuliweka kando.

**Mheshimiwa Spika**, Wasomi mbalimbali wamefanya tafiti za kutosha kuhusu uhusiano wa kufanya mazoezi na uwezo wa akili wa mtoto. Watafiti **Fedewa and Soyeon** wamefanya utafiti wa kina kwa kufanya uchambuzi wa kina wa maandiko *(studies)* 59 yaliyochapishwa kuanzia mwaka 1947 hadi Mwaka 2009 na kugundua kuwa mtoto anayefanya mazoezi shuleni ana uwezo wa kuwa na akili kubwa yenye ugunduzi *(childrend cognitive outcome)* kuliko mtoto asiyefanya mazoezi shuleni. Ninaomba nimnukuu: -
*Not only is physical activity worth the time, but it appears to benefit those children who need it most, particularly in the areas where high stakes testing demands proficient achievement: mathematics and reading. Out of the various physical activity interventions, programs that emphasized aerobic training exerted the largest effect on children's cognitive and achievement outcomes. For children with learning disabilities who struggle in meeting mathematics and reading benchmarks, physical activity interventions appeared to improve these children's academic abilities tremendously*[55]. (Fedewa and Soyeon 2013)

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 inatamka wazi kuwa mambo yafuatayo yanapaswa kufanyika ili kukuza maendeleo ya michezo shuleni. Sera inatamka mambo hayo kuwa ni: -

i) Kuandaa utaratibu wa kufundisha Elimu kwa michezo na michezo kuanzia shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu hadi Chuo Kikuu;

ii) Kutekeleza kwa ukamilifu azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Elimu kwa Michezo na Michezo (Physical Education Charter) la 1978 kwa kushirikiana na mashirika ya kitaifa na kimataifa

[5] Fedewa, Alicia L., and Ahn Soyeon. 2013. "The Effects of Physical Activity and Physical Fitness on Children's Achievement and Cognitive Outcomes." *Research Quarterly for Exercise and Sport*, January 23: 37-41.

yanayojihusisha na michezo na utamaduni kama vile Tume ya Taifa ya Sayansi Elimu na Utamaduni na UNESCO;

iii) Kuhakikisha kwamba walimu wa kufundisha somo la Elimu kwa Michezo na Michezo katika Shule na Vyuo wanaandaliwa vya kutosha;

iv) Kuhakikisha kwamba mashindano ya michezo yanayoendeshwa katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya *Ualimu yanaimarishwa ili yaendelee kuchangia upatikanaji wa wachezaji bora wa taifa, pia wenye uwezo wa kuendeleza taaluma ya michezo;*

v) Kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya Michezo kutayarisha mitaala pamoja na kuandika vitabu ambavyo vitatumika kufundisha Elimu kwa Michezo na Michezo shuleni na vyuoni kwa misingi ya kuoanisha mafunzo haya na yatakayotolewa na Vyama vya Michezo nje ya taasisi hizo ili kuweka msingi imara wa michezo; na

vi) *Kuhakikisha kwamba viwanja vya michezo vya shule na vyuo vinaendelea kutunzwa na kutumika kwa madhumuni ya shughuli za michezo pamoja na Kufuatilia utekelezaji wa mitaala na mipango yote ya michezo shuleni na vyuoni.*

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo Katika uchambuzi wake kwa taarifa ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

a) Kuna upungufu mkubwa wa viwanja na vifaa vya michezo katika shule za msingi na sekondari nchini. Aidha, kuna ukosefu wa walimu wa masomo ya michezo katika shule za msingi na sekondari nchini;

b) Kamati imebaini pia kuwa mashindano ya michezo katika shule za msingi na sekondari nchini (UMITAMSHUMTA na UMISETA) hayatiliwi mkazo kama sera inavyotamka. Kutokana na hilo Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati maalum wa kuimarisha viwanja vya michezo, walimu wa kufundisha masomo ya michezo, kupunguza ama kuondoa kodi kwenye vifaa vya michezo vinavyoagizwa kwa ajili ya shule za msingi na sekondari nchini pamoja na kuimarisha mashindano ya michezo shuleni. Aidha,

Serikali iimarishe mabaraza ya michezo ya mikoa na wilaya ili mabaraza haya yaweze kutimiza wajibu wake kama yalivyokusudiwa katika uundwaji wake na kama yalivyopewa majukumu yake katika **Tangazo la Serikali Na. 471 la tarehe 16 Novemba, 1990.**

**v) Utekelezaji wa Mradi wa SEQUIP**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Kuboresha Ilimu ya sekondari (SEQUIP).

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wanatekeleza Mradi wa Kuboresha elimu ya sekondari (SEQUIP) kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia 2020/2021 hadi 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kuboresha elimu ya sekondari unafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa mkopo wa **Dola** za Kimarekani **milioni 500** sawa na Fedha za Kitanzania **Shilingi Trilioni 1.2**.

**Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la mradi wa Kuboresha Elimu ya sekondari nchini ni kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari ili kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya sekondari, kuweka mazingira salama ya elimu kwa Wasichana waliopo katika shule za sekondari pamoja na kuhakikisha wanafunzi wote wanaoanza masomo ya sekondari wanamaliza elimu ya sekondari.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto zilizobainika kuhusu mradi wa SEQUIP ni kama ifuatavyo: -

i) Miradi mingi inayofadhiliwa na Mradi wa SEQUIP imekuwa na changamoto ya kutomalizika kwa wakati. Hii inatokana na changamoto zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi. Kwa mfano sehemu ya Fedha za kutekeleza miradi zimekuwa zikitumika kugharamia shughuli nyingine ambazo si sehemu ya andiko la mradi kama kuchimba visima vya maji katika eneo la

mradi kwa ajili ya ujenzi na ujenzi wa miundombinu ya barabara na umeme kwenye eneo la mradi;

ii) Kamati imebaini kuwa kumekuwa na utolewaji wa Fedha za kugharamia ujenzi wa miundombinu ya shule ambao unafanana kwa kila halmashauri zote nchini. Kamati inatambua kuwa halmashauri nchini hazifanani katika ugharamiaji wa miradi ya maendeleo kwa kuwa kila halmashauri ina mazingira yake, hasa utofauti wa kijiografia, hali inayosababisha miradi kuwa na gharama tofauti. **Kamati inaona ipo haja kwa Serikali wakati wa kusanifu miradi ya aina hii, iweke pia kigezo cha jiografia katika utengaji wa bajeti ya kutekeleza miradi yake.**

**vi) Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tanzania Rural and Urban Roads Agency – TARURA)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), ambapo pamoja na mambo mengine Kamati ilielezwa kuwa mtandao wa barabara za Wilaya chini ya TARURA una jumla ya **kilomita 144,429.77**, kati ya barabara hizo, **kilomita 3,224.12** ambazo ni sawa na **asilimia 2.23** ni barabara za lami, **kilomita 41,107.52** ambazo ni **asilimia 28.46** ni za Changarawe na **kilomita 100,098.13** ambazo ni sawa na **asilimia 69.31** ni za udongo kwenye mtandao wa barabara za Wilaya.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa Taarifa ya TARURA Kamati imebaini kuwa uwiano wa viwango vya barabara kati ya barabara za udongo, changarawe na lami ni mdogo sana. Kamati imebaini kuwa sehemu kubwa ya barabara zinazohudumiwa na TARURA (**asilimia 69**) ni za vumbi. Hali hii imekuwa ikisababisha barabara nyingi zinazosimamiwa na TARURA kuharibika kila wakati hasa katika misimu ya mvua kubwa zinaponyesha. Katika muktadha huu, Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kwa matengenezo makubwa ya mara kwa mara kwa barabara zile zile.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hali hii, Kamati inashauri TARURA kupandisha barabara nyingi za udongo kwenda kuwa barabara za changarawe zikijumuisha ujenzi wa mifereji ili kuzuia athari za

mmomonyoko wakati wa mvua nyingi, hali ambayo itawezesha barabara hizo kudumu kwa muda mrefu na hivyo kuondoa adha kwa wananchi na pia kupunguza gharama za matengenezo ya mara kwa mara katika barabara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa Fedha 2023/2024 TARURA iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 818.02 kwa ajili ya ukarabati na shilingi bilioni 3 katika matengenezo ya miundombinu ya barabara za Wilaya. Kati ya Fedha hizo shilingi bilioni 710.31 ni Fedha za ndani na Shilingi bilioni 107.71 ni Fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Disemba, 2023 Fedha zilizopokelewa na Wakala (exchequer) ni Shilingi bilioni 339.23 sawa na asilimia 47.75 ya bajeti ya mwaka. Hata hivyo, Fedha taslimu zilizopokelewa hadi tarehe 31 Disemba, 2023 ni Shilingi bilioni 82.50 sawa na **asilimia 12** ya bajeti ya mwaka. Upokeaji huo wa Fedha umewezesha utekelezaji wa kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 kufikia asilimia 38.84 ya malengo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa kabisa na hali hii ya upelekaji wa fedha za bajeti kwa TARURA, hasa ukizingatia kuwa katika kipindi cha hivi karibuni kumeripotiwa kuwepo kwa uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara nchini kulikotokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika sehemu kubwa ya nchi. Ikumbukwe kuwa Serikali iliahidi ndani ya Bunge lako kuwa pamoja bajeti ya Bilioni 808.02 Serikali ingetoa Bilioni 350 za ziada kwa TARURA. Kamati inasikitika kwamba, hata fedha hizi pia hazijapokelewa.

**Mheshimiwa Spika,** ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ione umuhimu wa kuwapelekea TARURA fedha za kutosha kwa kadiri ya bajeti ilivyoidhinishwa na Bunge; ili TARURA iweze kukabiliana na hali mbaya ya miundombinu inayoikabili nchi, na hivyo kuweza kuwaondolea adha wanazozipata wananchi katika maeneo ambayo uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara na madaraja umefanyika**.**

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati inaamini kuwa ukamilishaji na maboresho ya miundombinu katika Barabara zinazosimamiwa na TARURA kunakwenda kupunguza muda wa safari, kuongeza tija kwa wananchi kuwahi kwenye shughuli zao za kiuchumi, jambo ambalo litaongeza tija katika uchumi wa taifa.

**vii) Shirika la Masoko ya Kariakoo**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Masoko ya Kariakoo lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 36 ya mwaka 1974. Mnamo mwaka 1985, Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho kwa kurekebisha Kifungu Namba 8. Katika marekebisho hayo, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam lilimilikishwa **asilimia 51** ya hisa na Msajili wa Hazina anabaki na hisa **asilimia 49**. Sheria ya Shirika la Masoko ya Kariakoo pia imefanyiwa marejeo mwaka 2002 na kutambulika kama *The Kariakoo Market Corporation Revised Edition No.132 of 2002.*

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Masoko Kariakoo linaendelea na mradi wa ukarabati wa soko kuu na ujenzi wa soko jipya la Kariakoo. Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 07 Januari, 2022 kufuatia jengo la soko kuu kupata ajali ya moto tarehe 10 Julai, 2021. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuamua kutekeleza mradi huu mkubwa na muhimu kwa wafanyabiashara wa Jiji la Dar es Salaam na kukuza uchumi wa watu wa Dar es Salaam. Aidha, soko ili ni alama (symbol) kubwa ya nchi kwa mataifa ya nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Shirika la Masoko ya Kariakoo na kuijadili. Katika uchambuzi wa taarifa hii Kamati ilibaini mambo mbalimbali. Pamoja na Shirika la Masoko ya Kariakoo kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio bado kuna changamoto ya uwepo wa **Maafisa wengi wanaokaimu nafasi wanazozitumikia.**

**Mheshimiwa Spika,** katika taarifa iliyowailishwa mbele ya Kamati mwezi Agosti, mwaka 2023 Kamati ilibaini kuwa Shirika la Masoko ya Kariakoo lina watendaji wengi ambao wanakaimu nafasi za uongozi. Hali hii inapunguza kasi ya utendaji wa shirika hilo kutokana na watendaji wengi kushindwa kuwa na maamuzi ya

mwisho yanayoathiriwa na kukosa mamlaka kamili ya maamuzi. Kamati inaishauri Serikali kushughulikia changamoto hii.

**viii) Utekelezaji wa Miradi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea, kujadili na kuifanyia uchambuzi taarifa ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kuhusu utekelezaji wa miradi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi nchini kama sehemu ya jitihada za Serikali katika kuongeza thamani ardhi, kurasimisha maeneo, kuboresha vijiji na miji inayokuwa kwa kasi na kumaliza migogoro ya ardhi ambayo inaendelea kushamiri katika halmashauri zetu.

**Mheshimiwa Spika**, migogoro ya ardhi inayoendelea nchini inazidisha umasikini kwa watu wetu pamoja na upotevu wa amani nchini, jambo ambalo halina afya kabisa kwa usalama wa nchi yetu. **Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa mpango wa matumizi bora ya ardhi unaendelezwa na kuimarishwa ili kuhakikisha kila anayehitaji ardhi anaipata kwa haki kwa ajili ya matumizi yake, ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla.**

**Mheshimiwa Spika,** migogoro hii inasababishwa na mipango mibaya, kukosa uadilifu, uaminifu na weledi, kutozingatia maadili ya taaluma inayohusika inayosimamia mipango miji, upimaji wa ramani, uthamini na umilikishaji wa ardhi. Mambo haya yamepelekea matumizi mabaya yasiyo ya mpangilio ya ardhi kati ya makundi mbalimbali nchini. Katika kulitatua hili, Serikali imekuwa ikichukua juhudi mbalimbali za kupanga, kupima na kumilikisha ardhi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika kipindi cha mwaka 2023 imepokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mtaa kuhusu utekelezaji wa program ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi kwa kutumia Fedha za mkopo kutoka Serikalini. Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini mambo kadhaa kama ifuatavyo: -

i) Baadhi ya halmashauri zilitumia fedha za mkopo kutoka Wizara ya Ardhi kwa ajili ya Kupanga, Kupima, na Kumilikisha ardhi

kwa matumizi ambayo hayakuwa malengo kusudiwa, kwa mfano kulipia fidia ya maeneo ya ardhi iliyotwaliwa, ujenzi wa majengo ya biashara na ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na umeme kwenye maeneo ya mradi;

ii) Maeneo yaliyopimwa kwa ajili ya viwanja vya makazi na biashara katika baadhi ya halmashauri hayawavutii wananchi kutokana na aidha kuwa mbali zaidi na huduma mbalimbali za kijamii kama vile umeme, barabara, maji, shule, hospitali, maeneo ya makaburi, maeneo ya wazi na masoko. Hali hii imesababisha wananchi wengi kushindwa kununua viwanja hivyo na hivyo kuzikosesha halmashauri mapato stahiki na kuzisababishia halmashauri hizo ugumu wa kulipa madeni yaliyotokana na fedha zilizokopwa kwa ajili ya upimaji huo;

iii) Kamati imebaini kuwa Serikali imekuwa ikitumia gharama kubwa kutekeleza miradi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi kutokana na kutumia fedha nyingi iliyopaswa kutumika kwa ajili ya upimaji na umilikishaji kwa ajili ya kulipa fidia hizo. Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe inatekeleza program hii kwa kadri ya malengo kusudiwa; na

iv) Baadhi ya halmashauri zimekuwa na tafsiri potofu na dhana hasi kuhusiana na mradi wa KKK kuwa ni chanzo cha mapato ya halmashauri, jambo ambalo si lengo la mradi huu, kwa kuwa zimekuwa zikitoza gharama zisizo na uhalisia kwa viwanja vilivyopimwa, hali iliyosababisha viwanja vingi kukosa masoko. Kamati inashauri Serikali iweke mwongozo wa usimamizi kwenye utekelezaji wa mradi huu wa KKK kuwa endelevu.

**ix) Utekelezaji wa Mradi wa Mabasi yaendayo kwa Haraka (DART)**

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa malengo ya kuanzishwa kwa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) ni kurahisisha usafiri wa abiria Jijini Dar es Salaam pamoja na kuwa DART ni taasisi ya umma inayowezesha upatikanaji wa faida kwa ajili ya kuliwezesha shirika kutoa mchango mkubwa katika mapato ya taifa.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa, DART imeendelea vyema kutekeleza miradi yake tangu awamu ya kwanza (Lort I) inayohusisha miundombinu kutoka Kivukoni hadi Kimara na baadaye hadi Mbezi na matawi yake; awamu ya pili (Lort II) miundombinu ya Barabara kutoka Mbagala hadi Stesheni, na sasa awamu ya Tatu (Lort III) kutoka Stesheni hadi Gongolamboto. Kamati imebaini kuwa utekelezaji na utolewaji wa huduma zinazotokana na mradi huu na namna mradi ulivyo kumeifanya Tanzania kuwa ya mfano. Hii imefanya nchi takriban 12 kuja nchini kwetu kujifunza kuhusu uendeshaji wa usafiri mijini kwa kutazama mafanikio ya DART. Nchi hizo ni pamoja na Nchi ya Zambia, Zimbabwe, Uganda, Kenya, Ethiopia, Senegal, Ghana, Rwanda, Angola, Botswana, Nigeria na Liberia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kuwa, matumizi ya teknolojia katika usimamizi na uendeshaji wa mradi pamoja na uwepo wa Program tumizi (mobile application) vikiunganishwa Pamoja na Mfumo wa usimamizi na uongozaji wa mabasi *(ITS)* mradi utakuwa bora zaidi na kuifanya nchi yetu kuendelea kupigiwa mfano katika usafiri wa umma katika majiji.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mradi wa DART kuwa wa mfano kwa nchi kadhaa Afrika, bado umegubikwa na changamoto nyingi. Baada ya uchambuzi wa kina wa taarifa ya Wakala iliyowasilishwa mbele ya Kamati, changamoto zifuatazo zilibainika:-

i) Watu binafsi wamekuwa wakivamia miundombinu ya mradi hali inahosababisha ugumu kwenye uendeshaji wa mradi;

ii) Wakala ameshindwa kupanga bei za nauli (*autonomasly*) bila kutegemea mamlaka zingine hali inayopelekea mradi kushindwa kujiendesha wenyewe kwa faida;

iii) Pamoja na Serikali kununua mabasi mengi kwa ajili ya mradi wa mwendokasi, wakala umeshindwa kuhakikisha kuwa mabasi hayo yanatoa huduma ipasavyo, kwani bado kumekuwa na shida ya mabasi mengi kupaki maeneo ya karakana na hivyo kusababisha upungufu wa mabasi barabarani. Hali hii imekuwa

ikisababisha usafiri kuwa mgumu na hivyo kusababisha adha kubwa kwa abiria.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya kina kuhusiana na uendeshaji wa mradi huu wa mabasi ya mwendokasi. Aidha, Serikali itazame upya uendeshaji wa DART, ili kuona namna nzuri ya kuimarisha usafiri ambao kwa sasa umekuwa ni adha kwa wanachi wa Jiji la Dar es Salaam; ikiwezekana kwa kufungua milango kwa kampuni na sekta binafsi kutumia miundombinu ya mwendokasi kwa utaratibu ambao wakala utapanga;

i) Shirika limeomba kutengeneza sheria kwa ajili ya kuifanya taasisi hii kuweza kufanya kazi katika majiji na miji mingine hasa katika majiji ya Arusha, Mbeya, Mwanza na Dodoma. Hata hivyo, Kamati inatia shaka uwezo wa taasisi hii kutanua utekelezaji na uendeshaji wa miradi kama hii katika miji na majiji mengine kwa kuwa hata mradi huu wa DART kwa Jiji la Dar es Salaam utekelezaji wake na utoaji wake wa huduma hauna ufanisi uliokusudiwa. Kamati inashauri kuwa DART ijiimarishe kwanza katika Jiji la Dar es Salaam kabla ya kuanza kutanua huduma kwenye miji na majiji mengine nchini.

### 2.3.2 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya iliyokuwa Kamati ya USEMI iliyowasilishwa Bungeni Februari, 2023

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa za Wizara inayoisimamia kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa (USEMI) ya Mwaka 2022/2023. Maazimio hayo yalitolewa kwa msingi wa matarajio ya watu kuhusu shughuli za umma na ustawi nchini. Kwa ufupi mambo matatu yamehusianishwa ambayo ni matarajio (maazimio), matokeo yaliyofikiwa yaani mafanikio na changamoto. (*Utaratibu huu unatokana na kawaida ya uzingatiaji wa dhamana ya Bunge katika usimamizi wa shughulli za umma*)

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ilipokea jumla ya Maazimio saba (7)

yaliyotolewa na Bunge kupitia kwa iliyokuwa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa (USEMI). Maazimio hayo yametekelezwa na Wizara kwa asilimia 90. Aidha, yaliyobaki Kamati imefahamishwa kuwa michakato ya utekelezaji wake inaendelea. Maazimio ambayo bado utekelezaji wake unaendelea ni: -

i) Azimio kuhusu migogoro ya ardhi kwenye halmashauri nchini;
ii) Migogoro ya ardhi katika Jiji la Dodoma;
iii) Migogoro ya ardhi kwenye halmashauri nyingine nchini;
iv) Uanzishwaji wa Shirika la Masoko Tanzania; na
v) Utungaji wa Sheria ya Usafiri wa Umma mijini;

### 2.4 Kushiriki katika Semina

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa walipata fursa ya kushiriki katika semina na mafunzo mbalimbali zilizoandaliwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Taasisi zilizo chini yake.

Semina na mafunzo hayo yalilenga kuwaongezea ujuzi na uelewa Wajumbe wa Kamati katika nyanja mbalimbali pamoja na kuwakumbusha kuhusu wajibu na majukumu ya Kibunge ambayo wanayatekeleza katika kuisimamia na kuishauri Serikali. Aidha, Semina na mafunzo yaliyotolewa kwa nyakati mbalimbali yalilenga katika kuimarisha stadi za kazi za wabunge, ufuatiliaji wa matumizi ya Fedha na usimamizi wa miradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kutoa shukrani zake za dhati wa Ofisi ya Raisi - TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii kwa kutoa fursa za mafunzo na kuwajengea uelewa waheshimiwa wabunge juu ya masuala mbalimbali yanayohusu sekta wanazozisimamia.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia utekelezaji wa majukumu ya Kamati, Mafanikio na Changamoto zilizobainika katika kipindi cha

Februari, 2023 hadi Januari, 2024, Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

i) Upungufu wa watumishi katika sekta ya utawala, afya na elimu ni changamoto kubwa katika maeneo mengi nchini, **Kamati inashauri,** Serikali kuendelea na utaratibu wa kutoa Ajira kwa watumishi wa kada ya afya, elimu na watendaji wa kata na vijiji ili kupunguza tatizo hili, Aidha, Ajira hizo zizingatie maeneo yenye upungufu zaidi ili wananchi waweze kufikiwa na huduma;

ii) Bajeti zinazopitishwa na Bunge kwaajili ya utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa shule, barabara na vituo vya afya, zipelekwe kwa wakati ili kuleta tija katika uendelezaji wake. Aidha, Serikali inapaswa kuongeza nguvu katika usimamizi wa miradi ya maendeleo na kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wazembe wanaoshindwa kusimamia matumizi ya Fedha zilizopelekwa kwaajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali;

iii) Uharibifu wa miundombinu ya barabara ni changamoto iliyojitokeza kwa kasi kubwa hususan katika kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kunyesha kwa kiasi kikubwa, **Kamati inashauri kuwa**, Serikali ichukue hatua za dharura na madhubuti katika maeneo yaliyoharibika zaidi kutokana na mvua hizi ikiwemo kufanya ukarabati wa haraka ili kupunguza athari na wananchi kukosa huduma. Aidha, kutumia bajeti ya dharura ambayo ilitengwa kwajili ya kuendelea kukarabati maeneo ambayo miundombinu inaendelea kuharibika;

iv) Serikali inapaswa kuendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji na utumiaji wa Fedha za kodi na ushuru katika Halmashauri zote nchini ili kuziba mianya kwa Halmashauri kukusanya mapato kidogo au kutumia mapato kiholela;

v) Maagizo yote yanayotolewa na Viongozi wakuu wa Serikali yanapaswa kuwekewa utaratibu wa ufutiliaji na mipango madhubuti ya utekelezaji wake ili kufanya maelekezo na maagizo haya kuwa na tija pale ambapo Viongozi wanapotoa ahadi hizo kwa wananchi wao;

vi) Serikali kupitia upya kanuni za uendeshaji wa Halmashauri kuona nafasi ya mbunge katika usimamizi wa shughuli za maendeleo ndani ya Halmashauri. Kwani Sheria ya sasa inamtambua Mbunge kama mjumbe katika baraza la madiwani, jambo ambalo linaathiri maamuzi ya Mbunge katika mchango wake kwa wananchi wote wa Halmashauri; na

vii) Serikali kuendelea kuwekeza katika teknolojia na matumizi ya TEHAMA kama njia mbadala ya kuongeza tija katika utendaji kazi kwa watumishi katika sekta zote. Aidha, matumizi haya yaendane na utoaji fursa za mafunzo mbalimbali kwa watumishi ili kuendana na kasi ya teknolojia.

### 3.2 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa mapendekezo yafuatayo ili kuboresha utekelezaji bora wa Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kama ifuatavyo: -

#### 3.2.1 Wakala wa barabara Vijijini na Mijini (TARURA)

**KWA KUWA** Malengo ya uanzishwaji
wa Wakala wa barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) yalikuwa ni uboreshaji wa mtandao wa barabara wilayani ili kukabiliana na changamoto za mapungufu kwenye sekta ya barabara za vijijini na mijini;

**NA KWA KUWA** pamoja na jitihada mbalimbali za kuijengea uwezo TARURA bado wakala unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile uhaba wa Fedha za utekelezaji wa miradi (Bajeti hadi sasa Fedha zilizopelekwa kutekeleza miradi ni asilimia 12% tu), kusua sua kwa wakandarasi na baadhi ya wakandarasi kutokua na uwezo, mitambo, mitaji ya kutekeleza miradi pamoja na uzembe wa makusudi wa watendaji wa Serikali katika usimamizi wa miradi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -
a) Bajeti iliyopitishwa na Bunge kutekeleza miradi ipelekwe kama ilivyoidhinishwa na Bunge;

b) Serikali iongezee TARURA Bajeti kufikia Shilingi Trilioni 1.64 kutoka Shilingi Bilioni 710 kwa miaka minne mfululizo ili kufikia malengo ya asilimia 70 ya barabara kuwa za changarawe, asilimia 3 kuwa barabara za lami na kujenga vivuko vyote vya barabara zetu;

c) Serikali kusimamia kwa makini taratibu za manunuzi kulingana na uwezo wa wakandarasi wanaoomba kazi na utekelezaji wa miradi husika;

d) Serikali kutekeleza mchakato wa kuanzisha hati Fungani (TARURA SAMIA INFRASTRUCTURE BOND) kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara;

e) Serikali kutafuta vyanzo vya fedha mbadala ikiwemo kushirikisha sekta binafsi ili kuiwezesha TARURA kuwa na fedha za uhakika za kutekeleza miradi yake;

f) Kuandaa na kuwawezesha makandarasi wazawa kushiriki kwenye ushindani katika utekelezaji wa miradi ya TARURA; na

g) Barabara za vijijini kusimamiwa na jumuiya za watumia barabara wa vijijini kama zilivyo katika jumuiya ya watumia maji, na bajeti za matengenezo ziende kwa jumuiya husika.

**3.2.2** Eneo la Utawala

**KWA KUWA** Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) ambayo dhumuni lake ni kuiwezesha TAMISEMI kusimamia na kupeleka maendeleo vijijini imedhoofika;

**NA KWA KUWA, hali hiyo imesababishwa na** TAMISEMI kujikita zaidi katika jukumu la utawala na kuacha eneo la maendeleo vijijini bila usimamizi madhubuti;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inaleta ombwe linalopelekea Taasisi zingine za Serikali kutumia mwanya huo kunyofoa majukumu ya TAMISEMI na kukinzana na Sera ya Ugatuaji wa madaraka unaoelekeza TAMISEMI kusimamia maendeleo vijijini,

**KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;**

a) Serikali isimamie kikamilifu utekelezaji wa Sera ya D by D na misingi yake;

b) Serikali idhibiti mwenendo wa baadhi ya taasisi zake wa kuhamisha Mamlaka za Utumishi ambazo ndiyo msingi wa utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka;

c) Serikali irejeshe Idara muhimu zinazowezesha utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka, zikiwemo Idara ya Uratibu wa Sekta na Idara ya Ujenzi.

### 3.2.3 Sekta ya Elimu

**KWA KUWA Pamoja na Serikali kuwekeza kiasi kikubwa** cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika Sekta ya Elimu nchini, bado maeneo mengi yanakabiliwa na uhaba wa madawati, upungufu wa watumishi (walimu), kutokumalizika kwa maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi, nyumba za watumishi; vifaa na viwanja vya michezo;

**NA KWA KUWA,** uhaba wa miundombinu hiyo unapelekea elimu kutotolewa kwa kiwango kinachostahili;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -
a) Serikali kusimamia vizuri matumizi ya fedha za ndani ili Fedha hizi ziweze kutekeleza ukamilishaji wa miradi na uendelezaji wa miundombinu ya Elimu;

b) Serikali kutoa ajira kwa walimu kwa kuzingatia maeneo ambayo yana upungufu zaidi; na

c) Serikali ije na suluhisho la kudumu la kuhakikisha kwamba Halmashauri zote nchini zinaanzisha programu maalum ya kumaliza tatizo la uhaba wa madawati.

### 3.2.4 Sekta ya Afya

**KWA KUWA** kuna changamoto ya uhaba wa vifaa tiba na upungufu wa wataalam katika vituo vya afya nchini;

**NA KWA KUWA,** upungufu huo unasababisha huduma za afya kutolewa kwa kiwango duni**;**

**KWAHIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: -

a) Serikali ifanye tathmini ya gharama na mahitaji ya vifaa vinavyohitajika katika kila kituo cha afya nchini ili kujua ukubwa wa tatizo;

b) Serikali iandaae mpango kazi na kutafuta ufumbuzi wa kibajeti ili kumaliza tatizo hili; na

c) Serikali ifanye uwekezaji wa Rasilimali watu (Watalaam) katika maeneo ya hospitali, vituo vya afya na zahanati zote nchini, hasa kwa maeneo yale ambayo vifaa vimenunuliwa.

**3.2.5 Lishe na Michezo**

**KWA KUWA**, maeneo ya lishe na michezo shuleni hayapewi kipaumbele;

**NA KWA KUWA**; kuna madhala ya wazi kama vile udumavu, miili kutokuwa imara na magonjwa yasiyoambukiza;

**NA KWA KUWA** hali hiyo inapelekea Serikali kutumia rasilimali watu na fedha nyingi kushughulikia maatokeo ya kutokuwekeza kwenye maeneo ya Lishe na Michezo;

**KWAHIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba;

a) Serikali ingalie namna bora ya kupunguza gharama ya vifaa vya michezo shuleni;

b) Serikali iweke mkakati wa kuwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye viwanja vya michezo pamoja na walimu wa michezo shuleni;

c) Serikali ione namna ya kuanzisha idara ya michezo na utamaduni katika Ofisi ya Rais TAMISEMI itakayosimamia masuala ya michezo shuleni; na

d) Serikali iweke mpango madhubuti na unaotekelezeka wa kuboresha suala la lishe shuleni.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu Mawaziri Mhe. Deogratius John Ndenjembi (Mb) na Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb) kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Aidha, nawashukuru watendaji wote wa ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndg. Adolf Ndunguru kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee niwashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Justin Lazaro Nyamoga, kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa shughuli za Kamati. Aidha, natambua na kuthamini michango yao adhimu na kujitoa kwao kikamilifu katika kuhakikisha Kamati yetu inatekeleza wajibu wake kikamilifu. Orodha ya majina ya Wajumbe wa Kamati ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dennis Lazaro Londo, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Lazaro Justin Nyamoga, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. William Vangimembe Lukuvi, Mb. – **Mjumbe**
4. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb. “
5. Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi, Mb. “
6. Mhe. Sylvestry Francis Koka, Mb. “
7. Mhe. Zuberi Mohammed Kuchauka, Mb. “
8. Mhe. Zacharial Paulo Issaay, Mb. “
9. Mhe. Salome Wycliff Makamba, Mb. “
10. Mhe. Mwita Mwikabe Waitara, Mb. “
11. Mhe. Sebastian Simoni Kapufi, Mb. “
12. Mhe. Amandus Julius Chingulile, Mb. “
13. Mhe. Doroth George Kilave, Mb. “

14. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb. "
15. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb. "
16. Mhe. Mwantum Mzamili Zodo, Mb. "
17. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis, Mb. "
18. Mhe. Erick James Shigongo, Mb. "
19. Mhe. Ameir Abdalla Ameir, Mb. "
20. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb. "

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee pia ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa Wankanga Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano wake kwa Kamati katika kipindi chote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake, pamoja na Sekretarieti ya Kamati hii, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Dennis Lazaro Londo (Mb),
**MWENYEKITI**
**KAMATI YAKUDUMU YA BUNGE YA TAWALA**
**ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

13 Februari, 2024

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, awasilishe hoja yake.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Taarifa hii inahusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara zifuatazo:-

(i) Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;
(ii) Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji;
(iii) Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano;
(iv) Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Uratibu na Bunge; na
(v) Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli ambazo zimetekelezwa na Kamati katika kipindi hiki; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria shughuli ya kwanza ni kujadili Miswada ya Sheria, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ilijadili Miswaya ya Sheria 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miswada hiyo ni;

(i) Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa mwaka, 2023;

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa mwaka, 2023;

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali yatokanayo na Urekebu wa Sheria wa mwaka 2023;

(iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023;

(v) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2023;

(v) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023;

(vi) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2023;

(vii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2023;

(viii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2023;

(ix) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023;

(x) Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023;

(xi) Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023;

(xii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023; na

(xiii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya kina kuhusu uchambuzi na maudhui ya Miswada hiyo ya Sheria yanapatikana katika taarifa husika zilizowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli ya pili ilikuwa ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Lengo la ziara hizo lilikuwa ni kuona hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi husika ili Kamati iweze kupata nafasi nzuri zaidi ya kuzishauri Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara hizo za ukaguzi zilifanyika katika Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Mwanza kati ya tarehe 13 – 18 Machi, 2023 ambapo miradi ifuatayo ilitembelewa: -

(a) Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya Mahakama Kuu, Tabora;

(b) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Shinyanga;

(c) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi cha Taasisi za Kisheria, Mwanza;

(d) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi cha kutoa haki, Mwanza

(e) Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji Nyaraka za Serikali, Dodoma;

(f) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Dodoma;

(g) Mradi wa Ujenzi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya TAKUKURU, Dodoma;

(h) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za bei nafuu 188, Dodoma; na

(i) Ukaguzi wa utekelezaji wa mradi wa mfuko wa maendeleo ya Jamii (TASAF), Mikoa ya Tabora na Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu masuala mbalimbali yaliyobainika katika ziara za ukaguzi wa miradi hiyo, yanapatikana katika Taarifa za Kamati zenye maoni na ushauri kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa kila Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa isipokuwa kwa miradi michache ambayo Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo mahsusi katika taarifa iliyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli ya nne ya Kamati ilikuwa ni uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, baada ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu uchambuzi wa bajeti za kila Wizara husika, pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ziliwasilishwa kwa nyakati tofauti katika Mkutano wa Kumi na moja wa Bajeti uliomalizika Mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli ya nne ilikuwa ni Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka mmoja Kamati ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa za taasisi zifuatazo: -

(a) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambapo taasisi zifuatazo zilileta taarifa:-

(i) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa;

(ii) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(iii) Taasisi ya Uongozi;

(iv) Wakala wa Ndege za Serikali;

(v) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF);*

(vi) Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa;

(vii) Tume ya Utumishi wa Umma;

(viii) Chuo cha Utumishi wa Umma;

(ix) *Watumishi Housing Investment*;

(x) Sekretarieti ya Ajira; na

(xi) Mamlaka ya Serikali Mtandao *(eGA)*.

(b) Ofisi ya Rais –Mipango na Uwekezaji, taasisi ambazo ziliwasilisha taarifa ni: -

(i) Ofisi ya Msajili wa Hazina;

(ii) Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC);* na

(iii) Mamlaka ya Eneo Huru la Uwekezaji;

Pia, tulipokea taarifa kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Masuala na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara hiyo.

(c) Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, taasisi ambazo ziliwasilisha taarifa zao: -

(i) Tume ya Taifa ya Uchaguzi;

(ii) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya;

(iii) Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa;

(iv) Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

(d) Wizara ya Katiba na Sheria, taasisi ambazo ziliwasilisha taarifa zao kwenye kamati ni: -

(i) Tume ya Utumishi wa Mahakama;

(ii) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(iii) Ofisi ya Taifa ya Mashitaka;

(iv) Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;

(v) Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *(RITA);*

(vi) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;

(vii) Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania;

(viii) Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania; na

(ix) Chuo cha Uongozi wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge katika Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Katika vikao vya Kamati za Bunge vilivyofanyika kuanzia tarehe 15 – 24 Januari, 2024, Kamati ilipokea Taarifa za Wizara na taasisi zinazosimamiwa na Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Maazimio hayo yalitokana na Taarifa za Mwaka ya zilizokuwa Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa za Februari, 2022 hadi Januari, 2023 ambazo zilizowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sehemu kubwa, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa maazimio ya Bunge uliofanywa na Wizara na taasisi hizo. Kwa yale maeneo ambayo yanahitaji kutiliwa mkazo zaidi katika utekelezaji wake, Kamati imetoa ushauri mahsusi kwa kila Wizara na taasisi zake kama itakavyowasilishwa hapo mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kamati imepitia utekelezaji wa maazimio yote na imeridhika kwa namna ambavyo imetekelezwa; na taarifa hii iko mezani kwako kwa ajili ya rejea lakini pia kwa ajili ya Kumbukumbu za *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano. Katika Wizara hii Bunge liliazimia masuala yafuatayo: -

(i) Kuharakisha utekelezaji wa utatuzi wa hoja zote za Muungano pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu hatua zilizochukuliwa kwenye utatuzi wa hoja hizo; na

(ii) Kuhakikisha kwamba Taasisi zote za Muungano zinakuwa na Ofisi pande zote za Muungano mapema iwezekanvyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mahojiano na Serikali kuhusiana na maazimio haya ya Bunge, Kamati ilielezwa kuwa Wizara iliratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kushughulikia Masuala ya Muungano kwa lengo la kutafuta ufumbuzi wa changamoto za Muungano. Tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa kushughulikia hoja za Muungano kupitia vikao vya Kamati ya pamoja ya Serikali ya Zanzibar na ya Muungano mwaka 2006, hoja 25 zimejadiliwa, na hadi kufikia uwaandishi wa taarifa hii hoja 22 zimepatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya Hoja za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azimio la Bunge, hadi sasa Taasisi za Muungano 33 kati ya Taasisi 36 zina Ofisi Zanzibar. Taasisi ambazo hazina Ofisi Zanzibar ni Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania *(TCU),* Mamlaka ya Elimu Tanzania *(TEA)* na Ofisi ya Taifa ya Takwimu *(NBS)*. Hata hivyo Taasisi hizo zipo katika hatua

mbalimbali za kukamilisha zoezi hilo. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kuzisisitiza Taasisi hizo kuharakisha ufunguzi wa Ofisi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kulikuwa na maazimio matatu na kati ya hayo matatu mawili yametekelezwa kikamilifu, azimio moja bado halijatekelezwa kikamilifu na ninaomba nilisome mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azimio hili la pili lilihusu uendeshaji wa shughuli za Baraza la Taifa la Biashara katika ngazi za Mikoa na Wilaya ambapo kamati ilitaka kuwa na mkakati wa haraka na endelevu wa kuongeza watumishi kulingana na mahitaji ya Baraza hili katika ngazi za mikoa na wilaya, na kuhakikisha kuwa kuna ushiriki wa kutosha wa wadau muhimu katika Mikutano yaBaraza katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azimio hilo, Serikali imekuwa ikiongeza watumishi katika ngazi mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji. Watumishi hao wameendelea kutekeleza majukumu na maazimio mbalimbali yanayotolewa na Baraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kuwa azimio hili halijatekelezwa kikamilifu na Serikali, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuleta taarifa kikamilifu kuhusu utekelezaji wa Azimio kama ilivyo elekezwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria; Katika Wizara hii, Bunge liliazimia masuala yafuatayo: -

(i) Lugha ya Uandishi wa Sheria;

(ii) Lugha ya Mahakama;

(iii) Ushiriki wa Wadau katika Kuandaa Miswada ya Sheria;

(iv) Uendeshaji wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

(v) Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai;

(vi) Umuhimu wa Kutilia Mkazo Suala la Utatuzi wa Migogoro Nje ya Mahakama;

(vii) Shule ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo na Ufaulu wa Wanafunzi; na

(viii) Ucheleweshwaji wa kuridhia Mikataba ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maslahi ya muda nitasoma maeneo matatu ambayo nadhani yanagusa maslahi mapana ya Bunge lako kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; Utekelezaji kuhusu umuhimu wa kutilia mkazo suala la utatuzi wa migogoro nje ya Mahakama. Kamati ilielezwa kuwa Serikali inaendelea kuweka kipaumbele katika kutoa elimu kwa wadau na wananchi kuhusu umuhimu na faida za utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zilizochini ya Wizara imekuwa ikitumia matukio ya kitaifa kama vile Wiki ya Sheria, Wiki ya Msaada wa Kisheria, Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, Maonesho ya Wakulima ya Kitaifa na Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Kitaifa kila mwaka kutoa elimu ya sheria pamoja na utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala kwa umma na wadau wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria imefanya marekebisho ya Sheria ya Usuluhishi Sura ya 15 ya mwaka 2020 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Sekta ya Sheria ya mwaka 2023 kwa madhumuni ya kuimarisha mfumo wa usuluhishi wa migogoro kwa njia mbadala nchini. Aidha, Wizara imetafsiri Kanuni za Upatanishi na Maridhiano ambazo zinalenga kufanikisha utekelezaji wa Sheria ya Usuluhishi. Vile vile, katika Mahakama ya Tanzania upo utaratibu wa utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Pia, jumla ya watatuzi wa migogoro 576 wamesajiliwa, vilevile, jumla ya vituo binafsi vinne vya utatuzi wa migogoro vimesajiliwa na vinafanya kazi. Sambamba na hilo Serikali imepanga kufungua kituo cha Usuluhishi wa Migogoro Tanzania *(Tanzania Arbitration Centre)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilipenda nieleze kuhusu Shule ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo na Ufaulu wa Wanafunzi kadri ambavyo Kamati ilitaka Serikali itekeleze azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliieleza Kamati kuwa italeta marekebisho ya Sheria ya Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Sura ya 425, pamoja na Tume ya Kurekebisha Kufanya Utafiti Kuhusu Mitaala na Uwezo wa Vyuo Katika Kufundisha Taaluma ya Sheria Nchini ili marekebisho yatakayofanyika yawe na tija na manufaa mapana kwa taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Baraza la Elimu ya Sheria linafanya ukaguzi wa vyuo vikuu vinavyotoa elimu ya sheria nchini ili kusimamia ubora wa elimu ya Sheria nchini. Kupitia kaguzi hizo, mapendekezo yanatolewa ili kufanya marekebisho katika maeneo mbalimbali ikiwemo miundombinu (majengo), idadi ya walimu wanaofundisha katika vyuo hivyo na sifa za walimu wanaohitajika kufundisha katika vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine yanayokaguliwa ni maktaba za vyuo, kama kuna vitabu vya kutosha na vya kisasa, matumizi ya *online* kwa wanafunzi katika kutafuta vitabu kwa ajili ya kujisomea, namna ya utungaji wa mitihani ya sheria kwa wanafunzi, ofisi za walimu vyuoni na mabweni ya wanafunzi. Aidha, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo inaendelea kufanya maboresho mbalimbali katika kuinua ubora wa utoaji wa mafunzo ya sheria ikiwemo kuhuisha mtaala wake ili kuendana na mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilipenda kugusia eneo linalohusu ucheleweshwaji wa uridhiaji wa mikataba ya kimataifa kama ambavyo Bunge lako liliitaka Serikali kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeanza kufanyia kazi suala hili ambapo uchambuzi wa awali umebainisha kuwa hadi kufikia Mwezi Septemba 2023 jumla ya Mikataba 59 imesainiwa lakini bado haijaridhiwa. Mikataba hiyo inahusisha mikataba 15 ya *SADC,* 3 Umoja wa Afrika, na 41 Umoja wa Mataifa. Ofisi ya

Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa ikitoa ushauri ipasavyo kuhusu mikataba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2022/23 jumla ya mikataba 13 ya kimataifa imesainiwa. Moja ya sababu za msingi ya kuchelewa kuridhiwa kwa Mikataba ya Kimataifa ni kutoa fursa kwa Serikali kufanya uchambuzi na tathimini ya kina kuhusu Mikataba husika baada ya kusainiwa ili kufahamu umuhimu na manufaa yake kwa nchi na kutoa fursa kwa ushirikishwaji wa wadau husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba, Kamati imeridhishwa na namna ambavyo Serikali inatekeleza maoni na ushauri unaotolewa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo; maoni ya jumla; kufuatia utekelezaji wa majukumu ya Kamati, mafanikio, changamoto na yaliyobainika katika kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024, Kamati ina maoni yafuatayo: -

(a) Suala la upungufu wa rasilimali watu limekuwa ni changamoto ya muda mrefu kwa baadhi ya Taasisi na hivyo kuathiri utendaji kazi wa Taasisi hizo, Wizara na Serikali kwa ujumla. Pamoja na kwamba Kamati inatambua juhudi za Serikali kuongeza idadi ya watumishi ili kutatua changamoto hii, kuna umuhimu pia kwa Serikali kuwa na mahitaji ya msingi, hasa vifaa, vitendea kazi na miundombinu ya mazingira ya kazi vikaboreshwa pia.

(b) Kamati inapongeza Wizara na taasisi zake kwa kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kuna baadhi ya Wizara na taasisi za Serikali hazina utamaduni wa kutenga fedha za kufanya ukarabati mdogo mdogo wa mara kwa mara kwa miradi hiyo. Kamati ina maoni kwamba, kwa kutotenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa aina hiyo, miradi hiyo inaweza kuanza kupoteza ubora wake. Hivyo basi, ni vema Wizara na taasisi zake zikajenga utamaduni wa kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kwa baadhi ya Wizara na taasisi za Serikali hazina utamaduni wa kutenga fedha za kufanya ukarabati mdogo mdogo wa mara kwa mara kwa miradi hiyo. Kamati ina maoni kwamba, kwa kutotenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa aina hiyo, miradi hiyo inaweza kuanza kupoteza ubora wake. Hivyo basi, ni vema Wizara na taasisi zake zikajenga utamaduni wa kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo mahususi kuhusu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

(a) Udahili wa watu wenye ulemavu katika mfumo wa ajira nchini.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kutokuwepo kwa miundombinu inayojitosheleza na taratibu rafiki kwa watu wenye ulemavu katika mchakato wa ajira nchini. Usaili wa watahiniwa walio wengi haujazingatia watu wenye uoni hafifu na ukaaji wa muda mrefu kwenye foleni za usaili kwa watu wenye mahitaji maalum;

Na kwa kuwa, changamoto hiyo inawanyima fursa ya kushiriki kikamilifu na wakati mwingine kutokushiriki kabisa kwenye mchakato wa usaili wa ajira nchini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali iboreshe miundombinu na taratibu zitakazo wawezesha watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika mchakato wa ajira bila vikwazo vyovyote.

(b) Utunzaji wa historia za Viongozi wa Jadi na Waasisi wa nchi yetu.

Kwa kuwa, Tanzania ina historia pana na ya muda mrefu, historia hiyo imejengwa na matukio mbalimbali ambayo yameathiri maendeleo, utamaduni, uchumi na umoja wa Kitaifa;

Na kwa kuwa, Kumbukumbu za matukio ya kihistoria zinaweza kupotea kutokana na sababu mbalimbali kama vile uharibifu wa nyaraka, mabadiliko ya teknolojia, mabadiliko ya

tabianchi, majanga ya asili na kutokuwepo kwa watu wenye kumbukumbu hizo. Vilevile, kumbukumbu za kihistoria zinaweza kupotoshwa na kufanywa kuwa hadithi za uwongo na kukosa urithi wa kihistoria kwa vizazi vijavyo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali ifanye jitihada za kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu za tamaduni, viongozi wa jadi na kuhifadhi taarifa hizo kidigitali

(ii) Serikali ifanye kampeni maaluum ya kuhamasisha wananchi kuenzi utamaduni, historia na mchango wa Waasisi wa Taifa letu.

(c) Malimbikizo ya madeni ya mishahara kwa Watumishi

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwepo kwa malimbikizo ya madeni ya mishahara kwa Watumishi wa umma hususan wale wanaopandishwa vyeo na wanaobadilishiwa muundo wa utumishi;

Na kwa kuwa, Changamoto hiyo husababishwa na mifumo iliopo ya upandishwaji vyeo na mabadiliko ya kimuundo ya watumishi wa umma ambapo baadhi ya waajiri huchelewa kuwasilisha taarifa za watumishi wanao stahili kupanda vyeo ama kubadilishiwa miuundo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mifumo ya upandishaji vyeo na mabadiliko ya kimuundo kwa watumishi iboreshwe ili iende sambamba na mabadiliko ya mishahara.

(d) Wakala wa Ndege za Serikali kufanya ununuzi wa Ndege mpya kwa ajili ya Viongozi wa Kitaifa**.**

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwepo kwa ndege tatu zinazowahudumia Viongozi wa Kitaifa, ndege moja aina ya *Gulfstream* G550 inamuhudumia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndege nyingine *Fokker* F50 na *Fokker* 28 zinawahudumia Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Waziri

Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Kwanza na wa pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Viongozi wengine wa Kitaifa;

Na kwa kuwa, Kamati imebaini kuwa, ndege aiNAya *Fokker* 28 ambayo ilinunuliwa mwaka 1978 ilitumika kuwahudumia Viongozi Wakuu wa Kitaifa hadi kufikia mwaka 2015. Ndege hiyo imefanya kazi ya kuwahudumia Viongozi wa Kitaifa kwa miaka 35, kwa sasa ndege ya *Fokker* F50 inaendelea kuhudumia Viongozi Wakuu wa Kitaifa isipokuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hali hii husababisha Wakala kutekeleza jukumu la kuwahudumia Viongozi kwa kuchelewa pindi zinapotokea safari za Viongozi wote kwa wakati mmoja;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ione umuhimu wa kufanya ununuzi wa ndege zingine ili kuboresha utoaji huduma za usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu).

(a) Ongezeko la Matumizi ya dawa za kulevya.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kwamba ipo changamoto ya ongezeko la matumizi ya dawa za kulevya nchini. Pamoja na jitihada nzuri zinazofanywa na Serikali, tafiti mbalimbali ikiwemo ripoti ya dawa za kulevya ya dunia ya mwaka 2021 inaonesha kumekuwa na ongezeko la matumizi na mauzo ya dawa za kulevya hasa katika tovuti za siri, tafiti hizo zinaonesha kuwa ongezeko hilo ni mara nne zaidi kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na mwaka 2017. Aidha, idadi ya watumiaji wa dawa hizo wanakadiriwa kufikia milioni 200 hadi kufikia mwaka 2019 ambayo ni asilimia Nne ya watu wote duniani. Ongezeko la utumiaji wa dawa za kulevya ni asilimia 18 katika kipindi cha miaka 10 iliyopita;

Na kwa kuwa, changamoto ya ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevya katika jamii linaathari nyingi hasi ambazo zinaweza kuathiri afya, kuongezeka kwa uhalifu na kuvuruga maendeleo ya nchi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Kuhakikisha elimu ya madhara ya dawa za kulevya inaendelea kutolewa husasan kwenye mashule, vyuo vya elimu ya juu na programu za redio, televisheni na mitandao ya kijamii.

(ii) Kampeni za uhamasishaji wa kupinga matumizi ya dawa za kulevya kuanzia ngazi za Vitongoji, Vijiji, Mitaa, Tarafa, Wilaya, Mikoa na Taifa.

(iii) Kuongeza vituo vya matibabu na msaada wa kisaikolojia kwa waraibu wa dawa za kulevya.

(iv) Kuimarisha udhibiti wa uingizwaji wa dawa za kulevya nchini kwa kutumia mifumo ya kisasa.

(b) Uendeshaji wa mashauri ya dawa za kulevya.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kwamba katika mashauri 1,158 ya dawa za kulevya yaliofunguliwa kwenye Mahakama mbalimbali nchini, mashauri 64 pekee ndiyo yaliomalizika hadi sasa;

Na kwa kuwa, ucheleweshwaji wa mashauri ya dawa za kulevya unapelekea kupungua kwa imani kwenye mfumo wa haki jinai, kuendelea kwa biashara haramu na kuathiri juhudi za kupambana na dawa za kulevya;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:

(i) Kuanzisha divisheni maalum ya kimahakama ya kushughulikia mashauri ya dawa za kulevya.

(ii) Kuwajengea uwezo watumishi na watendaji wa Mahakama kwa kuwapa mafunzo maalum ya uendeshaji wa mashauri yanayohusu dawa za kulevya kwenye mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria.

(a) Ukarabati wa Majengo na Mindombinu ya Mahakama za Mwanzo

Kwa kuwa, Kamati imebaini kwamba Mahakama ya Tanzania imefanya maboresho makubwa ya matumizi ya TEHAMA kwenye uendeshaji na usajili wa mashauri kwenye Mahakama za Wilaya, Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama za Rufani;

Na kwa kuwa, Mahakama za Mwanzo kwa sehemu kubwa zinawahudumia wananchi walio wengi zaidi na kwamba Mahakama za Juu yake ni Mahakama za Rufani kwa Mahakama ya Mwanzo. Kamati imebaini kuwa Mahakama za Mwanzo zinamapungufu makubwa kwenye ubora wa majengo kwani majengo mengi ni chakavu sana na maeneo mengine Mahakama hizo zimekodi majengo ya Halmashauri pamoja na kwamba majengo mengi ya Mahakama za Mwanzo haya na miundombinu kama vile umeme na vifaa vya TEHAMA;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:

(i) Majengo ya Mahakama ya Mwanzo yaboreshwe kwa kufanyiwa ukarabati unaostahili.

(ii) Serikali ijenge majengo ya Mahakama za Mwanzo kwenye maeneo ambayo haya na Mahakama za mwanzo.

(iii) Serikali ihakikishe Mahakma za Mwanzo zinakuwa na Miundombinu ya TEHAMA ili kuwezesha utendaji bora wa kazi.

(b) Serikali iwaongeze majukumu Wanasheria wa halmashauri kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi.

Kwa kuwa, Serikali imefanya jitihada kubwa ya kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi wasio na uwezo wa kupata msaada wa kisheria kutoka kwa Mawakili kupitia mradi wa Mama Samia *Legal Aid Campaign;*

Na kwa kuwa, Watoa msaada wa Kisheria *(Para – Legals*) hawajapatikana katika Wilaya zote Tanzania;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iwaongeze Jukumu Wanasheria wa halmashauri kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi kwenye baadhi ya maeneo yasio na watoa huduma wa msaada wa kisheria.

(c) Serikali iwajengee uwezo Taasisi zinazohusika na Mfumo wa Haki Jinai

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwa Taasisi za mfumo wa Haki Jinai kama vile Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali zina upungufu mkubwa wa ikama ya watumishi na miundombinu ya utendaji wa kazi kama vile vifaa vya TEHAMA, magari na Ofisi;

Na kwa kuwa, changamoto hii husababisha ofisi hizo kutotekeleza majukumu yao kwa ufanisi unaotegemewa na kupelekea huduma zisizoridhishwa kwa wananchi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:

i) Serikali itenge Bajeti itakayo boresha Miundombinu ya Taasisi hizo ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao.

ii) Serikali iajiri watumishi wa kutosha kwenye Taasisi hizo kwa kuzingatia ikama ya taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kamati inamshukuru sana Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa ushirikiano wao wakati wa utekelezaji wa majukumu haya na ninaomba

majina yao yaingie kwenye Kumubukumbu za Kudumu za Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninawashukuru viongozi wote kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Kwa kipekee naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa George Huruma Mkuchika - Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais; Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama - Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais; Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana - Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi - Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga – Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete – Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis – Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwashukuru watendaji wote wa Mhimili wa Utendaji *(The Executive)* na Mhimili wa Mahakama *(The Judiciary)* kwa ushirikiano walioupatia Kamati, kwa niaba yao wote, naomba niwatambue viongozi hawa kama ifuatavyo: -

Dkt. Jim James Yonazi – Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; Ndugu Juma Selemani Mkomi – Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ndugu Mary Ngelela Maganga – Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; Ndugu Mary Gabriel Makondo – Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria; Dkt. Tausi Mbaga Kida – Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; na Profesa Elisante Ole Gabriel – Mtendaji Mkuu wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndugu

Nenelwa Mwihambi, *ndc,* na kwa kipekee Sekretarieti ya Kamati, kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba Bunge lako sasa lipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARI, 2023 HADI JANUARI, 2024 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1. Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Taarifa hii inahusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Tano zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi ambapo pamoja na masuala mengine, inaelezea kwa muhtasari kuhusu muundo na majukumu ya Kamati, pamoja na kuainisha mbinu zilizotumika kutekekeleza majukumu hayo.
b) Sehemu ya Pili inabainisha majukumu/shughuli zilizotekelezwa na kutoa ufafanuzi wa uchambuzi kuhusu masuala mbalimbali yaliyobainika.
c) Sehemu ya Tatu inahusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliotolewa kwenye Mkutano wa Kumi
d) Sehemu ya Nne ni Maoni na Mapendekezo ya Kamati; na

e) Sehemu ya Tano ni Hitimisho.

### 1.2. Muundo na Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta ambayo imeundwa chini ya Kifungu cha 5 (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni, Kamati hii imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara zifuatazo:-

a) Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;
b) Ofisi ya Rai – Mipango na Uwekezaji;
c) Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano;
d) Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Uratibu na Bunge; na
e) Wizara ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Kamati za Kisekta yameainishwa katika Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kwa msingi huo Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria ina majukumu yafuatayo: -

a) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;
b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo; na
d) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo.

### 1.3. Njia na Mbinu Zilizotumika Kutekeleza Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hutekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 96 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Majukumu hayo ni sehemu ya utekelezaji wa Madaraka ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) na (3) ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 136 (3) na (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kutumia mbinu na njia zifuatazo: -

a) Kufanya vikao vya kupokea, kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali za wizara na taasisi zake kwa lengo la kufahamu utendaji wa majukumu, mafanikio na changamoto wanazokumbana nazo;
b) Kuchambua na kujadili miswada ya sheria mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusikiliza maoni ya wadau kuhusu miswada hiyo;
c) Kufanya ziara za mafunzo katika taasisi na maeneo mbalimbali ya kisekta kwa lengo la kuona na kujifunza namna ambavyo taasisi hizo zinatekeleza majukumu yake;
d) Kutembela na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha ili kujiridhisha kuhusu hatua mbalimbali za utekelezaji na ufanisi wa miradi hiyo; na
e) Kupokea semina na mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujenga uelewa wa masuala mahsusi yanayotekelezwa na Wizara na taasisi zake, pamoja na wadau wengine.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA MASUALA YALIYOBAINIKA

### 2.1 Uchambuzi wa Miswada ya Sheria

**Mheshimiwa Spika**, Jukumu la utungaji wa Sheria za Nchi limeainishwa kwenye Ibara ya 64 ya Katiba, ambapo Bunge limepewa madaraka ya kutunga sheria za Tanzania Bara katika Ibara ya 64(1) na Sheria za kimuungano katika Ibara ya 64(4). Aidha, Ibara ya 97 inaweka utaratibu kwamba, Bunge litatumia madaraka hayo kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria kabla ya kibali cha Rais ili kuwa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo na kwa kuzingatia Kanuni ya 97, katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Februari 2023 hadi Januari 2024, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na

Sheria ilijadili Miswada ya Sheria kumi na mbili (12). Miswada hiyo ni: -

a) **Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa mwaka, 2023;**

b) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa mwaka, 2023** [*The Tanzania Intelligence and Security Services (Amendment) Bill, 2023*]

c) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali yatokanayo na Urekebu wa Sheria wa mwaka 2023** *[The Laws Revision (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023]* ambao ulikuwa unafanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

i) Sheria ya Uanzishwaji wa Mashirika Binafsi, Sura ya 119 (*The Corporations Sole (Establishment) Act, Cap. 119*);
ii) Sheria ya Usimamizi na Tozo ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 (*The Excise (Management and Tariff) Act, Cap. 147*);
iii) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 (The Income Tax Act, Cap. 332);
iv) Sheria ya Tafsiri za Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap. 1*);
v) Sheria ya Urekebu, Sura ya 4 (*The Laws Revision Act, Cap. 4*);
vi) Sheria ya Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135 (*The Social Security Act, Cap. 135*);
vii) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399 (*The Tanzania Revenue Authority Act, Cap. 399*); na
viii) Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263 *(The Workers' Compensation Act, Cap. 263*).

d) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023** *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023]* ambao ulikuwa unafanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

i) Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Sura ya 269 [*The Architects and Quantity Surveyors (Registration) Act, Cap. 269*];
ii) Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229 [*The Media Services Act, Cap. 229*];

iii) Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70 [*The Medical Stores Department Act, Cap. 70*];
iv) Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa, Sura ya 419 [*The National Leaders' Funerals Act, Cap. 419*];
v) Sheria ya Reli, Sura ya 170 [*The Railways Act, Cap. 170*];
vi) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Sura ya 277 [*The Tanzania Forestry Research Institute Act, Cap. 277*];
vii) Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370[*The Treasury Registrar (Powers and Functions) Act, Cap. 370*]; na
viii) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 [*The Value Added Tax Act, Cap. 148*].

e) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2023** *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2023]* ambao ulikuwa unafanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

i) Sheria ya Nguvu ya Atomu, Sura ya 188 [*The Atomic Energy Act, Cap. 188*];
ii) Sheria ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam, Sura ya 253 [*The Dar es Salaam Maritime Institute Act, Cap. 253*];
iii) Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449 [*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, Cap. 449*];
iv) Sheria ya Mapitio na majadiliano kuhusu masharti Hasi katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 450 [*The Natural Wealth and Resources (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, Cap. 450*]; na
v) Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda, Sura ya 159 [*The Tanzania Industrial Research and Development Organisation Act, Cap. 159*].

f) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2023** *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2023]* ambao ulikuwa unafanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

i. Sheria ya Kanda Maalum za Uwekezaji kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi, Sura ya 373 [*The Export Processing Zones Act, Cap. 373*] na
ii. Sheria ya Kanda Maalum za Kiuchumi, Sura ya 420 [*The Special Economic Zones Act, Cap. 420*].

g) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2023** *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2023]* ambao ulikuwa unafanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

i) Sheria ya Leseni za Biashara, Na. 25 ya mwaka 1972 [*The Business Licensing Act, Act No. 25 of 1972*];
ii) Sheria ya Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, Sura ya 144 [*The Dar es Salaam Institute of Technology Act, Cap. 144*];
iii) Sheria ya Stahili na Mafao ya Majaji, Sura ya 424 [*The Judges (Remuneration and Terminal Benefits) Act, Cap. 424*];
iv) Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Sura ya 93 [*The Mwalimu Nyerere Memorial Academy Act, Cap. 93*];
v) Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa, Sura ya 225 [*The Political Service Retirement Benefits Act, Cap. 225*];
vi) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 [*The Public Service Act, Cap. 298*];
vii) Sheria ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo, Sura ya 112 [*The Small Industries Development Organisation Act, Cap. 112*];
viii) Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, Sura ya 155 [*The Tanzania Trade Development Authority Act, Cap. 155*];
ix) Sheria ya Usajili wa Wataalamu wa Mipango Miji, Sura ya 426 [*The Town Planners (Registration) Act, Cap. 426*]; na
x) Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 [*The Weighs and Measures Act, Cap. 340*].

h) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023** *[The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023]* ambao ulikuwa unafanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

i. Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 [*The Advocates Act, Cap. 341*];
ii. Sheria ya Mamlaka ya Rufaa, Sura ya 141[The Appellate Jurisdiction Act, Cap 141];
iii. Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15 [*The Arbitration Act, Cap. 15*];
iv. Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391 [*The Commission for Human Rights and Good Governance Act, Cap.391*];
v. Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20 [*The Criminal Procedure Act, Cap. 20*];
vi. Sheria ya Uhujumu Uchumi na Makosa ya Kupanga, Sura ya 200 [*The Economic and Organised Crime Control Act, Cap. 200*];
vii. Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442 [*The Electronic Transactions Act, Cap. 442*];
viii. Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 [*The Evidence Act, Cap. 6*];
ix. Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Mahakama Lushoto, Sura ya 405 [*The Institute of Judicial Administration Lushoto Act, Cap. 405*];
x. Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Sura ya 237 [*The Judiciary Administration Act, Cap. 237*];
xi. Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 [*The Land Disputes Courts Act, Cap. 216*];
xii. Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171 [*The Law Reform Commission of Tanzania Act, Cap. 171*];
xiii. Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania, Sura ya 425 [*The Law School of Tanzania Act, Cap. 425*];
xiv. Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21[*The Legal Aid Act, Cap. 21*];
xv. Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11[*The Magistrates' Courts Act, Cap. 11*];
xvi. Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430 [*The National Prosecutions Service Act, Cap. 430*];
xvii. Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 [*The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act, Cap. 268*];
xviii. Sheria ya Bodi ya Msamaha wa Wafungwa, Sura ya 400 [*The Parole Boards Act, Cap. 400*];

xix. Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 [*The Penal Code, Cap. 16*];
xx. Sheria ya Uthibitishaji Wosia na Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352 [*The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352*];
xxi. Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256 [*The Proceeds of Crime Act, Cap. 256*];
xxii. Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, Sura ya 307 [*The Tanganyika Law Society Act, Cap. 307*]; na
xxiii. Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318 [*The Trustees' Incorporation Act, Cap. 318*].

i) **Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023**.

j) **Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023**.

k) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023** [*The Political Parties Affairs Laws (Amendment) Bill, 2023*] ambao ulikuwa unafanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

i) Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278 [*The Election Expenses Act, Cap. 278*]; na

ii) Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 [*The Political Parties Act, Cap. 258]*.

l) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023** [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill, 2023*] ambao ulikuwa unafanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

i) Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442 [*The Electronic Transactions Act, Cap. 442*];
ii) Sheria ya Taifa ya Leseni na Usajili wa Viwanda, Sura ya 46 [*The National Industries (Licensing and Registration) Act, Cap. 46*];

iii) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 [*The Public Audit Act, Cap. 418*]; na
iv) Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sheria Na. 10 ya Mwaka 2022 [*The Tanzania Investment Act, Act No. 10 of 2022*].

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya kina kuhusu uchambuzi wa maudhui ya Miswada hiyo ya sheria yanapatikana katika taarifa husika zilizowasilishwa Bungeni.

**2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Lengo la ziara hizo lilikuwa ni kuona hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi husika ili Kamati iwe katika nafasi nzuri zaidi ya kuzishauri Wizara inazozisimamia katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, ziara hizo za ukaguzi zilifanyika katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Mwanza na Dodoma kati ya tarehe 13 – 18 Machi, 2023 ambapo miradi ifuatayo ilitembelewa: -

a) Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya Mahakama Kuu, Tabora (Mradi Na. 6314);
b) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Shinyanga (Mradi Na. 6389);
c) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi cha Taasisi za Kisheria, Mwanza (Mradi Na. 6389);
d) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi cha kutoa haki, Mwanza (Mradi Na. 6389);
e) Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji Nyaraka za Serikali, Dodoma (Mradi Na. 4937);
f) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Dodoma (Mradi Na. 6389);
g) Mradi wa Ujenzi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya TAKUKURU, Dodoma (Mradi Na. 6203);
h) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za bei nafuu 188, Dodoma; na

i) Ukaguzi wa utekelezaji wa mradi wa mfuko wa maendeleo ya Jamii (TASAF), Mikoa ya Tabora na Shinyanga (Mradi Na. 6220).

**Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina kuhusu masuala mbalimbali yaliyobainika katika ziara za ukaguzi wa miradi hiyo, yanapatikana katika Taarifa za Kamati zenye maoni na ushauri kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa kila Wizara husika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa isipokuwa kwa miradi michache ambayo Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo mahsusi katika taarifa iliyowasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya masuala ambayo yalibainika katika baadhi ya taasisi ni kutokuwa na utamaduni wa kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ukarabati mdogo wa mara kwa mara *(regular maintenance)* wa miradi ya ujenzi. Kwa sababu hiyo, miradi hiyo ambayo inatumia fedha nyingi za umma, huanza kupoteza ubora wake na kuchakaa katika muda mfupi.

**2.3 Uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mara baada ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Bajeti ya Serikali ni sehemu ya utekelezaji wa Madaraka ya Bunge katika Mchakato wa Bajeti *(the budget cycle)* kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Katika uchambuzi wake, Kamati ilizingatia kikamilifu masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya

Kanuni za Bunge kwa kufanya ulinganisho baina ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha unaoisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha unaofuata. Aidha, Kamati iliangalia mwenendo wa makusanyo ya maduhuli, na upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha unaoisha ili kupima ufanisi wa utekekelezaji wa bajeti husika.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge hili kupata picha ya masuala yaliyobainika katika uchambuzi wa Bajeti ya Serikali 2023/2024, ufuataο ni muhtasari wenye kuonyesha mwenendo wa Bajeti ya Wizara/Taasisi zinazosimamiwa na Kamati: -

<u>**Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**</u>

a) Kwa upande wa Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, uchambuzi wa Kamati ulibaini yafuatayo: -

i) Kwa ujumla, Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 iliongezeka kwa wastani wa **asilimia 17.18** ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Ongezeko hili liliakisi maoni ya Kamati kwamba Serikali iongeze fedha kwa taasisi mbalimbali za Wizara ili kuboresha ufanisi wa utendaji wake.

ii) Kwa upande wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Bajeti ya Ofisi hiyo iliongezeka kwa **asilimia 8.53** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023. Kamati ilibaini kwamba ongezekeo la bajeti ilitokana na miradi mipya ya ujezi wa ofisi zinazosimamiwa na Wizara hii.

<u>**Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)**</u>

b) Katika bajeti Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Kamati ilibaini yafuatayo: -

i) Katika Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 bajeti iliongezeka kwa **asilimia 1.58** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Ongezeko hili ni matokeo ya ushauri uliotolewa na Kamati ili kuwezesha Ofisi hiyo na taasisi zake ziwe na fedha ya kutosha kutekeleza majukumu yake.

ii) Kwa upande wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo, Kamati ilibaini kwamba fedha iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni pungufu kwa **asilimia 40.9** ukilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa sababu ya upungufu wa bajeti ya maendeleo nikutokana na kutokuwepo kwa mradi mpya unaotekelezwa na Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi hii inaomba fedha za ukamilishaji wa mradi wa ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais Dodoma, Dar es salaam na Pemba ulioanza kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

<u>**Ofisi ya Waziri Mkuu**</u>

c) Katika bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake, Kamati ilibaini yafuatayo: -

i) Kwa ujumla wake, hali ya upatikanaji wa fedha katika Ofisi ya Waziri Mkuu ilikuwa ya kuridhisha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Hadi wakati taarifa ya Kamati inawasilishwa Bungeni, Ofisi hiyo na Taasisi zake zilipokea wastani wa **asilimia 66** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

ii) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 iliongezeka kwa **asilimia 9.2** ukilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023. Moja kati ya sababu ya ongezeko hilo ilikuwa ni utekelezaji wa maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi.

iii) Kwa upande wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Bajeti ya Ofisi hiyo iliongezeka kwa **asilimia 16.77** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023. Kamati ilibaini kwamba ongezekeo la bajeti ilitokana na miradi mipya ya ujezi wa ofisi zinazosimamiwa na Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo: -

i) Serikali ijiwekee malengo ya ukusanyaji maduhuli ambao yanaakisi uwezo wa ukusanyaji, na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

ii) Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati Fedha za Maendeleo na Matumizi Mengineyo ili kuwezesha Wizara hii, taasisi na idara zilizoko chini yake kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi.

**<u>Wizara ya Katiba na Sheria</u>**

d) Kwa upande wa Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zake, uchambuzi wa Kamati ulibaini yafuatayo: -

i) Kwa ujumla, Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 iliongezeka kwa wastani wa **asilimia 62.13** ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Ongezeko hili liliakisi maoni ya Kamati kwamba Serikali iongeze fedha kwa taasisi mbalimbali za Wizara ili kuboresha ufanisi wa utendaji wake.

ii) Kwa upande wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo, Kamati ilibaini kwamba fedha iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni pungufu kwa **asilimia 4.2** ukilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Sababu ya kupungua huku kunatokana na miradi 30 mingi iliyopangwa

Kwenda kutekelezwa kwa mwaka 2023/2024 tayari ipo katika hatua za utekelezaji kutoka mwaka 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina kuhusu Uchambuzi wa Bajeti za kila Wizara husika, pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ziliwasilishwa kwa nyakati tofauti katika Mkutano wa Kumi na moja wa Bajeti uliomalizika Mwezi Juni, 2023.

**2.4 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na Taasisi zake**

**Mheshimiwa Spika**, kwa nyakati tofauti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake. Msingi wa shughuli hii umejengwa katika utekelezaji wa Madaraka ya Bunge kama chombo kikuu kwa niaba ya wananchi cha kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha mwaka mmoja Kamati ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa za taasisi zifuatazo:

**a) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.**

i. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).
ii. Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.
iii. Taasisi ya Uongozi.
iv. Wakala wa Ndege za Serikali.
v. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)
vi. Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.
vii. Tume ya Utumishi wa Umma.
viii. Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC).
ix. Watumishi Housing Investment (WHI).
x. Sekretarieti ya Ajira.
xi. Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA).

**b) Ofisi ya Rais –Mipango na Uwekezaji.**

i. Ofisi ya Msajili wa Hazina.
ii. Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).
iii. Mamlaka ya Eneo Huru la Uwekezaji (EPZA).

**c) Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu**

i. Tume ya Taifa ya Uchaguzi.
ii. Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA).
iii. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.
iv. Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

**d) Wizara ya Katiba na Sheria**

i. Tume ya Utumishi wa Mahakama.
ii. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
iii. Ofisi ya Taifa ya Mashitaka.
iv. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.
v. Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA)
vi. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.
vii. Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania.
viii. Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania.
ix. Chuo cha Uongozi wa Mahakama.

**SEHEMU YA TATU**

**3.0 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge katika Wizara zinazosimamiwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika Vikao vya Kamati za Bunge vilivyofanyika kuanzia tarehe 15 – 24 Januari, 2024, Kamati ilipokea Taarifa za Wizara na taasisi zinazosimamiwa na Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Maazimio hayo yalitokana na Taarifa za Mwaka ya zilizokuwa Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa za Februari, 2022 hadi Januari, 2023 zilizowasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sehemu kubwa, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa maazimio ya Bunge uliofanywa na Wizara na taasisi hizo. Kwa yale maeneo ambayo yanahitaji kutiliwa mkazo zaidi katika utekelezaji wake, Kamati imetoa ushauri mahsusi kwa kila Wizara na taasisi zake ili yakafanyiwe kazi zaidi.

**3.1 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge liliazimia Uanzishwaji wa Programu za Vituo vya kukuza vipaji vya TEHAMA (*incubation centers*) kwa vijana waliohitimu masomo ya TEHAMA ili kutoa fursa za ajira kwa vijana ndani na njee ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanzisha vituo vinavyopokea watanzania wenye kuonesha vipaji katika TEHAMA kutoka katika Vyuo Vikuu na Vyuo mbali mbali kwa ushindani kwa kupokea maombi kimtandao, na baada ya kujiunga wanajengewa uwezo katika Utafiti na Ubunifu ili kuongeza umahili wao na kuwawezesha kuajirika au kujiajiri wenyewe. Hivyo, Utafiti na Ubunifu unawajengea uwezo vijana na kutengeneza fursa za ajira ndani na nje ya nchi kwenye sekta ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inaratibu uanzishwaji wa vituo vya ubunifu katika maeneo ya Zanzibar, Arusha, Dodoma, Tanga, Kilimanjaro, Morogoro, Mbeya, Iringa, Mtwara, Mwanza na Dar-es-Salaam. Vituo hivi vitatumika kukuza na kuendeleza bunifu za TEHAMA kwa vijana. Vituo hivi vinatarajia kuhudumia takribani ya Vijana 5000 kwa mwaka. Aidha, kupitia Tume ya TEHAMA, kwa mwaka 2023/24 jumla ya Kampuni changa 12 ziliwezeshwa kushiriki kwenye Mikutano ya Kimataifa nje ya Nchi ikiwa ni mkakati wa kuwatengenezea fursa nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kuboresha sera na miongozo kwa ajili ya kuwatambua, kuwaendeleza na kuwasimamia wabunifu mbali mbali wa TEHAMA. Nyaraka hizi zitaimarisha ushiriki wa kiufanisi wa Wadau wa sekta Binafsi na Umma katika kuendeleza bunifu za TEHAMA nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ilianzisha Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji Mifumo

ya Serikali Mtandao (*e-Government Research, Innovation and Development Center* – eGovRIDC) kwa ajili ya kuandaa wabunifu na waendelezaji wa Mifumo maalum ya Serikali Mtandao ili kurahisisha na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma na utendaji kazi Serikalini. Kituo hiki kipo katika Chuo Kikuu cha Dodoma ndaki ya Sayansi na Teknolojia (UDOM CIVE) na kilizinduliwa Mwezi Agosti, 2019.

**Mheshimiwa Spika,** Kituo hicho kinafanya tafiti na bunifu mbalimbali za kiteknolojia zikiwemo teknolojia mpya kama vile:

i. Blockchain;
ii. Artificicial Intellgence (AI);
iii. Machine Learning (ML);
iv. Internet of Things (IoT);
v. Usalama wa kimtandao (*Cyber Security*);
vi. Ujenzi wa mifumo (*Software development*); na Uchambuzi wa taarifa (*Data analytics*).

### 3.1.1 Ofisi ya Makamu wa Rais

**Mheshimiwa Spika,** Katika Wizara hii Bunge liliazimia masuala yafuatayo:

i) Kuharakisha utekelezaji wa utatuzi wa hoja zote za Muungano pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu hatua zilizochukuliwa kwenye utatuzi wa hoja hizo; na

ii) kuhakikisha kwamba Taasisi zote za Muungano zinakuwa na Ofisi pande zote za Muungano mapema iwezekanvyo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mahojiano na Serikali kuhusu maazimio haya ya Bunge, Kamati ilielezwa kuwa Wizara iliratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ya Kushughulikia Masuala ya Muungano kwa lengo la kutafuta ufumbuzi wa changamoto za Muungano. Tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa kushughulikia hoja za Muungano kupitia vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ mwaka 2006, hoja 25

zimejadiliwa na hadi kufikia uwaandishi wa taarifa hii hoja 22 zimepatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya Hoja za Muungano.

**Mheshimiwa Spika**, Hoja za Muungano ambazo zimepatiwa ufumbuzi ni kama ifuatavyo:

i. **Utekelezaji wa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Hoja: Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura Namba 391 inayosimamiwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilikuwa haitekelezwi Zanzibar kwa kuwa haikuwa suala la Muungano na pia haikumshirikisha Waziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwenye dhamana ya mambo ya Haki za Binadamu.

Ufumbuzi: Baada ya majadiliano katika vikao vya Kamati ya Pamoja, suala hilo limepatiwa ufumbuzi kwani Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawal a Bora ilifanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali 'Written Laws Miscellaneous Amendments', Namba 8 ya mwaka 2006. Kwa sasa Tume inafanya kazi pande zote mbili za Muungano.

ii. **Utekelezaji wa Sheria ya Usafirishaji Majini (Merchant Shipping Act) katika Jamhuri ya Muungano na Uwezo wa Zanzibar Kujiunga na International Maritime Organisation (IMO)**

Kwa mujibu wa sheria na taratibu za 'IMO' Zanzibar haiwezi kujiunga na 'IMO' kwani mwanachama lazima awe Dola. Katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, utaifa ni mmoja na kwamba, pamoja na kuwa na serikali mbili, utaifa huu unawakilishwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hoja: Zanzibar ilikuwa na sheria yake ya usafiri baharini "Maritime Transport Act, 2006" ambayo imekuwa ikitumika kwa masuala yote yanayohusu uchukuzi na usalama wa njia ya majini katika mikataba yote ya SMZ chini ya (Zanzibar Maritime Administration). Aidha, ilikuwa na mpango wa kuanzisha chombo chake cha

kusimamia masuala ya usafiri majini. Kwa upande wa Tanzania Bara, sheria ya 'Merchant Shipping Act' ya mwaka 2003 ambayo ilikuwa ikitumika katika masuala yote yanayohusu uchukuzi na usalama wa njia ya majini katika mikataba yote ya kimataifa na katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hali hii ilizusha utata pale ambapo Zanzibar ilipoomba uanachama kwenye taasisi ya International Maritime Organisation (IMO).

Ufumbuzi: Ingawa uanachama wa 'IMO' ni wa kitaifa, baada ya mashauriano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na 'IMO', imekubalika Zanzibar kuwa na Mamlaka yake ya usafiri majini (Zanzibar Maritime Administration) ambayo itatekeleza baadhi ya majukumu kulingana na mikataba ya kimataifa.

iii. **Ushirikishwaji wa SMZ kwenye Masuala ya Kimataifa na Kikanda**

Hoja: kulikuwa na hoja kwamba, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki haiipi nafasi ya kutosha Zanzibar ya kuwa na ushirikiano wa kiuchumi unaohitajika na Taasisi za Kimataifa.
Ufumbuzi: Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) zimetayarisha Mwongozo wa Ushirikishwaji wa SMZ Kwenye Masuala ya Kimataifa na Kikanda ambao umezingatia maeneo ya ziara za viongozi wa kitaifa; mikutano ya kimataifa; nafasi za masomo ya elimu ya juu nje ya nchi na utafutaji wa fedha za misaada au mikopo ya kutekeleza miradi mbalimbali kutoka nje ya nchi. Mwongozo huu ulipitishwa na kuridhiwa na Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano tarehe 9 Februari, 2019. Mwongozo umesambazwa kwa Wizara husika za SJMT na SMZ tarehe 21 Juni, 2019.

iv. **Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki**

Hoja: Nafasi ya Zanzibar kuwasilisha miradi ya maendeleo ya kiuchumi kwa ajili ya kujumuishwa katika miradi ya kikanda inayotekelezwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Ufumbuzi: SMZ iliwasilisha miradi minane ya maendeleo kwa ajili ya kujumuishwa katika Miradi ya Kikanda inayotekelezwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miradi minne ya kikanda kati ya minane ilipewa kipaumbele kwa ajili ya kuandaliwa maandiko ya miradi, usanifu na tathmini ya gharama tayari kwa kuombewa fedha za utekelezaji. Mradi wa Uwanja wa ndege Pemba na Bandari ya Mpigaduri, Maruhubi iliyokuwa inatafutiwa ufadhili chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imepatiwa ufadhili kupitia vyanzo vingine. Taratibu za utafutaji rasilimali kwa ajili ya miradi ya Ujenzi wa Chelezo (Dry Dock Construction) na Kivuko (Roll ON Roll Off – RORO) kati ya Bandari ya Dar es Salaam, Zanzibar, Pemba, Tanga na Mombasa kutoka vyanzo vingine bado zinaendelea. Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ kilichofanyika Dodoma tarehe 9 Februari, 2019 kilikubaliana kuwa, changamoto hii iondolewe katika orodha ya changamoto za Muungano.

v. **Gharama za Kushusha Mizigo Bandari ya Dar es Salaam kwa Mizigo inayotoka Zanzibar**

Hoja: Kulikuwa na hoja kwamba, gharama za kushusha mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam (Landing Fees) kwa mizigo inayotoka Zanzibar ni kubwa ikilinganishwa na mizigo inayotoka nje ya nchi yaani shilingi 4,000 kwa mizigo ya nje ya nchi inayoingia Tanzania Bara na shilingi 11,000 kwa mizigo ya Zanzibar inayoingia Tanzania Bara.

Ufumbuzi: Kwa mujibu wa Tariff Book of Port Dues and Charges ya Aprili, 2013 iliyopitishwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) viwango vinavyotozwa kwa mizigo inayotoka Zanzibar ni vya chini ikilinganishwa na viwango vinavyotozwa kwa mizigo inayotoka nchi nyingine kuingia Tanzania Bara au mizigo inayotoka nchi nyingine kupitia Bandari ya Dar es Salaam kwenda nchi nyingine (Transit Cargo). Viwango vinavyotozwa ni kama ifuatavyo: - Shore handling ni USD 7 kwa mizigo inayotoka nje ya nchi wakati kwa mizigo kutoka Zanzibar ni USD 2; Wharfage ni USD 1.6% kwa thamani ya mzigo kwa mizigo kutoka nje wakati kwa mizigo kutoka Zanzibar ni USD 2 CBM/tani

moja; na Stevedoring ni USD 6 kama mzigo unachukuliwa eneo la kushushia na USD 7 kama mzigo unachukuliwa eneo la yadi wakati kwa mizigo kutoka Zanzibar ni USD 2 CBM/tani moja.

vi. **Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia**

Hoja: Namna ya kugawana mapato ya rasilimali ya mafuta na gesi asilia itakapopatikana.
Ufumbuzi: Serikali zetu baada ya kujadiliana, ziliamua kutumia Kampuni ya ushauri elekezi Aberdeen University Petroleum and Economic Consultants (AUPEC) ya Uingereza ili kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu mgawanyo wa mapato ya rasilimali ya aina hiyo kwa nchi zilizoungana. Kampuni ya AUPEC ilikamilisha kazi hiyo na mapendekezo kuwasilishwa SJMT na SMZ. Baada ya majadiliano baina ya Viongozi wa SJMT na SMZ, pande zote mbili zimekubaliana kuliondoa suala la utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia katika orodha ya mambo ya Muungano. Hivyo, Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 ilitungwa na kuipa Zanzibar Mamlaka ya kuanzisha chombo/vyombo vya kusimamia masuala ya mafuta na gesi asilia kwa kutumia Sheria ya Zanzibar na Zanzibar ilitunga Sheria yake ya Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2016.

vii. **Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano**

Hoja: Kulikuwa na hoja kuhusu kutokuwepo kwa Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano.

Ufumbuzi: Katika Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano kilichofanyika tarehe 9 Februari, 2019 katika Ukumbi wa Kambarage, Hazina Square, Dodoma chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kilipitisha Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano na kuagiza kwamba, Utaratibu huo uliandaliwa na kusambazwa Wizara zote za SJMT na SMZ mwezi Aprili, 2019.

viii. **Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu**

Hoja: Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu ilikuwa haitekelezwi Zanzibar kutokana na kutozihusisha taasisi za SMZ zinazoshughulikia masuala ya Uvuvi katika Bahari Kuu.

Ufumbuzi: Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mwezi Februari, 2007 kupitia Sheria Na. 4 ya mwaka 2007 na kuzitambua taasisi zinazohusika na matumizi ya Bahari Kuu kwa upande wa Zanzibar na kuzijumuisha katika Kamati ya Utendaji ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Marekebisho hayo yameiwezesha Mamlaka kuanza kazi zake rasmi mwaka 2010. Sambamba na marekebisho ya Sheria, hatua nyingine muhimu zilizochukuliwa ni pamoja na kufunguliwa kwa akaunti ya amana kwa ajili ya kuweka mapato yatokanayo na shughuli za Uvuvi wa Bahari Kuu, kufikiwa kwa makubaliano ya kugawana mapato kuwa, asilimia 50 ni kwa ajili ya uendeshaji wa Mamlaka ya Uvuvi na asilimia 50 itagawanywa kwa asilimia 30 Tanzania Bara na asilimia 20 Zanzibar. Mkubaliano mengine ni mgao wa wafanyakazi wa Mamlaka kwa pande zote za Muungano. Aidha, Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sheria Na. 5 ya mwaka 2020 ilitungwa na Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kusainiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria hiyo imeorodheshwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 23 Februari, 2021. Kwa sasa Mamlaka ya kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu ni moja yenye makao makuu yake katika Kijiji cha Fumba, Zanzibar na Mamlaka hiyo ina majukumu ya kutoa leseni za uvuvi katika Bahari kuu, kudhibiti viwango vya uvuvi, kusimamia rasilimali ya uvuvi na hifadhi ya mazingira ya Bahari na uendelezaaji wa rasilimali za Bahari Kuu.

ix. **Uingizaji wa maziwa kutoka Zanzibar**

Hoja: Kikwazo cha kuzuiwa kwa maziwa ya AZAM kuingia katika soko la Tanzania Bara kinachotokana na Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Sura ya 156 na Kanuni zake

Ufumbuzi: Kikwazo cha kuzuiwa kwa maziwa ya AZAM kuingia katika soko la Tanzania Bara kimepatiwa ufumbuzi baada ya

Kanuni kufanyiwa marekebisho, ikiwa ni pamoja na kupunguziwa tozo kutoka shilingi 2000 hadi shilingi 250 kwa lita ya maziwa yanayotengenezwa kutokana na unga wa maziwa unaoagizwa nje ya nchi. Aidha, Tarehe 25 Februari, 2019 Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) - SJMT iliingia Mkataba wa Makubaliano ya uingizaji wa maziwa ya AZAM katika soko la Tanzania Bara na tayari yameshaanza kuingizwa katika soko la Tanzania Bara.

x. **Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano**

Hoja: Kupungua kwa kiwango cha ushindani katika soko la ajira kwa Wazanzibari kunatokana na tofauti ya mitaala ya elimu ya msingi na sekondari kati ya Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, hoja nyingine ilikuwa ni kuendeleza Ari na Dhamira ya Muungano katika kufanya uteuzi wa nafasi mbalimbali katika Taasisi za Muungano.

Ufumbuzi: Kamati ya Kukuza Mitaala iliyoundwa ikiwa na wajumbe kutoka pande mbili za Muungano ililinganisha mihutasari ya ngazi zote za elimu (Msingi hadi Vyuo) ya Tanzania Bara na Zanzibar na kubaini kuwa tatizo sio tofauti ya mitaala bali ni nafasi ya Wazanzibari katika Taasisi za Muungano. Hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kutatua changamoto zikiwemo kuhamasisha Wazanzibari kuomba ajira zinazotangazwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Taasisi za Muungano; Matangazo ya ajira kutangazwa kupitia vyombo vya habari vya Tanzania Bara na Zanzibar; Taasisi za Muungano kufungua Ofisi Zanzibar ikiwa ni pamoja na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na usaili kufanyika Zanzibar pia. Utaratibu wa mgao wa ajira uliokubalika kutumika kuhusu nafasi za Watumishi wa kawaida kwenye Taasisi za Muungano (isipokuwa kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama) ni asilimia 79 kwa Tanzania Bara na asilimia 21 kwa Tanzania Zanzibar. Kikao cha Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ kilichofanyika tarehe 2 Desemba, 2019 Zanzibar kiliagiza Wizara husika kuendelea kushughulikia suala hili na kufanya tathmini ya utekelezaji kila mwisho wa mwaka wa fedha ili kujua mafanikio na changamoto zilizopo. Pande mbili zimekubaliana kuwa na mfumo shirikishi katika mchakato mzima wa ajira katika Taasisi za Muungano.

xi. **Mgawanyo wa Mapato Yatokanayo na misaada ya kibajeti (General budget support-GBS)**

Hoja: Mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada kutoka nje ni asilimia 95.5 kwa SJMT na asilimia 4.5 kwa SMZ ambapo mgawanyo huu ndiyo unaotekelezwa hadi sasa. Hata hivyo, suala la mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada ya kisekta bado halijafanyiwa kazi.

Ufumbuzi: Utaratibu wa kupokea fedha za misaada ya kisekta kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo umeelekezwa kwenye kifungu cha 15 (1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura 134, ambapo SMZ ina jukumu la kupokea misaada hiyo bila kutafuta idhini ya Waziri wa Fedha na Mipango wa SJMT.

xii. **Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja**

Hoja: Kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kutokana na mkataba huo kuwa na kipengele Na. 4.01 ambacho kinaitaka Serikali iweke baadhi ya Mali zake kama dhamana ya mkopo.

Ufumbuzi: Baada ya mazungumzo baina ya SJMT na Saudi Fund kuhusu kipengele Na. 4.01, Saudi Fund ilikubali mapendekezo ya kufanya marekebisho katika kipengele hicho kilichohusu kuweka mali za Serikali kama dhamana ya mkopo huo. Hivyo, Serikali ilisaini mkataba na Saudi Fund tarehe 19 Aprili, 2020.

xiii. **Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake hadi Wete – Pemba**

Hoja: Kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Mkopo wa Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake hadi Wete – Pemba kutokana na mkataba huo kuwa na kipengele Na. 4.01 ambacho kinaitaka Serikali iweke baadhi ya Mali zake kama dhamana ya mkopo.

Ufumbuzi: Baada ya mazungumzo baina ya SJMT na Saudi Fund kuhusu kipengele Na. 4.01, Saudi Fund ilikubali mapendekezo ya kufanya marekebisho katika 11 kipengele hicho kilichohusu

kuweka mali za Serikali kama dhamana ya mkopo huo. Hivyo, Serikali ilisaini mkataba na Saudi Fund tarehe 19 Aprili, 2020.

xiv. **Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri**

Hoja: Kuchelewa kukamilishwa kwa Mkataba wa Mkopo kutoka Exim Bank ya China kwa ajili ya Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri.
Ufumbuzi: Serikali iliunda Timu ya wataalamu ili kupitia upya Andiko la Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. Pamoja na mambo mengine, Timu hiyo ilibaini kuwa andiko la mradi liliandaliwa na kampuni ya China Harbour Engineering Company (CHEC) ambaye ndiye mkandarasi tarajiwa wa mradi kwa mujibu wa hati ya makubaliano (MoU) ya mwaka 2012 baina ya kampuni hiyo na SMZ. Suala hili lingeweza kusababisha mgongano wa kimaslahi. Hivyo Timu ilishauri andiko la mradi liandaliwe na mtaalamu elekezi huru ili kuepusha mgongano wa kimaslahi. Baada ya ushauri huo, SMZ ilisitisha makubaliano na CHEC na kutafuta mtaalamu elekezi huru wa kuandaa andiko jipya.

xv. **Usimamizi wa Ukokotoaji na Ukusanyaji wa Kodi kwenye Huduma za Simu unaofanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar (Zanzibar Revenue Board - ZRB)**

Hoja: Kulikuwa na hoja kwamba, baada ya kuzimwa mfumo uliokuwa unatumika kukokotoa kodi kwenye huduma za simu (Electronic Revenue Collection System - eRCS) ambao ulikuwa unatumika kukusanya na kugawana kodi baina ya pande mbili za Muungano, ZRB iliendelea kutumia mfumo huo kukusanya kodi jambo lililoleta malalamiko kutoka kwa Kampuni za Simu.
Ufumbuzi: Mfumo wa ukokotoaji na ukusanyaji wa kodi kwenye huduma za simu umepatiwa ufumbuzi baada ya Timu ya Wataalamu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango SJMT na SMZ kufanya maboresho ya mfumo huo. Hivyo, mfumo ulianza kufanya kazi rasmi mwezi Januari, 2020. 12

xvi. **Mapato Yanayokusanywa na Uhamiaji kwa Upande wa Zanzibar**

Hoja: Mapato yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji Zanzibar yanapaswa kuwekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti na kutumika katika kugharamia shughuli za Muungano kulingana na bajeti zilizotengwa. Hivyo, kulikuwa na hoja kwamba, mapato yanayokusanywa na idara ya Uhamiaji upande wa Zanzibar kubakizwa Zanzibar ni kinyume na sheria ya bajeti.

Ufumbuzi: Katika hotuba ya bajeti 2021/22 iliyosomwa na Waziri wa Fedha na Mipango (SJMT) tarehe 10 Juni, 2021 ilipendekezwa kutekeleza utaratibu wa kuruhusu mapato yanayotokana na Tozo za VISA kutumika pale yalipokusanywa kama ilivyo kwenye mapato mengine ya Muungano. Mapendekezo haya yalipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Juni 2021.

xvii. **Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Tax Revenue Appeal Tribunal (TRAT) kutoka Zanzibar**

Hoja: Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchelewa kuwasilisha jina kwa ajili ya uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa TRAT.

Ufumbuzi: Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa TRAT ulifanyika tarehe 24 Aprili 2029.

xviii. **Uteuzi wa Mjumbe wa Bodi ya Bima ya Amana (Deposit Insurance BoardDIB) Kutoka Zanzibar**

Hoja: Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchelewa kuwasilisha jina kwa ajili ya uteuzi wa mjumbe wa Bodi ya Bima ya Amana.

Ufumbuzi: Uteuzi wa mjumbe wa Bodi ya Bima ya Amana ulifanyika tarehe 22 Marchi 2019.

xix. **Malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar Kutozwa Kodi mara mbili**

Hoja: Kuhusu kuwepo kwa utofauti wa ukadiriaji wa viwango vya thamani za bidhaa, na kodi ya forodha baina Tanzania Bara na Zanzibar. Tofauti hii inayosababisha wafanyabiashara wa Zanzibar kulipa kodi ya ziada kwa bidhaa zinazotoka Zanzibar Kwenda katika soko la Tanzania Bara. Hali hii ilileta malalamiko kwa wafanyabiashara wa Zanzibar, ambao nao walitumia kipengele cha Sheria ya Kodi kinachosema kwamba, "Bidhaa zinazoingizwa nchini na kukamilisha taratibu zote za kiforodha kupitia kituo chochote rasmi cha forodha zihesabike kuwa zimeingizwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania", na kwamba hakuna haja ya kufanya upya makadirio kwa bidhaa zinazoingizwa Tanzania Bara.

Ufumbuzi: Imebainika kwamba, wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa Zanzibar kutoka nje ya nchi na kupeleka Tanzania Bara hulazimika kulipia tofauti ya kodi iliyoachwa kukusanywa kutokana na tofauti ya tathmini ya bidhaa iliyofanywa Zanzibar. Hivyo, suala hilo haliwafanyi wafanyabiashara kulipa kodi mara mbili badala yake kulipa kodi inayostahili kulipiwa kwa tathmini ya bidhaa inayotumika Tanzania Bara. Kwa muktadha huo, suala la ulipaji wa tofauti ya kodi kwa bidhaa zinazotoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara linaeleweka vizuri kwa wafanyabiashara wa Zanzibar.

xx. **Kodi ya Mapato – (Pay as You Earn - PAYE) na Kodi ya Zuio (Withholding Tax)**

Hoja: Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hainufaiki ipasavyo na kodi ya mapato yatokanayo na mishahara ya wafanyakazi (PAYE) wa Taasisi za Muungano waliopo Zanzibar pamoja na kodi ya zuio (Withholding Tax) itokanayo na kampuni na mashirika yanayofanya kazi Zanzibar.

Ufumbuzi: Kuhusu Kodi ya Mapato yatokanayo na mishahara ya watumishi wa Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar ufumbuzi ni kwamba kiasi cha shilingi bilioni 1.75 ambacho kimekuwa kikitolewa kwa SMZ kila mwezi kuanzia mwaka 2012/13 kama

malipo ya PAYE kiendelee kutolewa kila mwezi kwa SMZ. Kuhusu Kodi ya Zuio (Withholding Tax) kwa Kampuni zinazofanya kazi Tanzania Bara na zenye matawi Zanzibar, Wizara zinazohusika na masuala ya Fedha za SJMT na SMZ mnamo mwezi wa Juni, 2022 zilikubaliana kufanya marekebisho 14 katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Tax Administration Act) Sura ya 438, na Sheria ya Kodi ya Mapato (Income Tax Act) Sura ya 332 kupitia Sheria ya Fedha Na.5 ya Mwaka 2022 ili Kampuni zilizosajiliwa Tanzania Bara na zenye matawi Zanzibar kuweza kulipa Kodi ya zuio Zanzibar.

xxi. **Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (Terminal III)**

Hoja: Kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Mkopo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Exim ya China kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (Terminal III), kutokana na Mkataba kuhusisha vipengele vya kuweka mali za Serikali kama dhamana ya mkopo.

Ufumbuzi: Baada ya SJMT na Mkopeshaji - Benki ya Exim ya China kukubaliana kuondoa kipengele kinachohusu kuweka mali za Serikali kama dhamana ya mkopo huo, SJMT ilisaini Mkataba wa Mkopo huo tarehe 03 Novemba, 2022.

xxii. **Ongezeko la gharama za umeme kutoka TANESCO kwenda ZECO**

Hoja: Kuongezeka kwa bei ya umeme kwa wateja wa TANESCO ikiwemo Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO), kulitokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usambazaji wa umeme. Ongezeko hilo liliibua malalamiko kwa watumiaji wa umeme kwa upande wa Zanzibar.

Ufumbuzi: Menejimenti ya ZECO na TANESCO zilikutana tarehe 15 Novemba, 2021 kujadili taarifa iliyoandaliwa na wataalamu wa Mashirika yote mawili. Katika kikao hicho suala la bei ya kuuziana umeme kati ya TANESCO na ZECO lilipatiwa ufumbuzi ambapo

Wajumbe walikubaliana ZECO kununua umeme kwa shilingi 130 kwa uniti moja.

**Mheshimiwa Spika**, Hoja za Muungano ambazo hazijapatiwa ufumbuzi ni kama ifuatavyo:

i. **Uingizaji wa Sukari katika Soko la Tanzania Bara**

Hoja: SMZ ina hoja kwamba sukari inayozalishwa na Kiwanda cha Mahonda iruhusiwe kuuzwa katika soko la Tanzania Bara.

ii. **Usajili wa Vyombo vya Moto**

Hoja: Sheria za Vyombo vya moto ziainishwe ili gari likitoka upande mmoja kwenda upande mwingine ijulikane kuwa imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu na faida za Muungano ikiwemo hatua zilizochukuliwa kutatua Hoja za Muungano. Elimu hiyo imetolewa kupitia machapisho mbalimbali, Vyombo vya Habari, Makongamano, Maonesho ya shughuli mbalimbali za kitaifa, Majarida na Vipeperushi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza azimio la Bunge, hadi sasa Taasisi za Muungano 33 kati ya Taasisi 36 zina Ofisi Zanzibar. Taasisi ambazo hazina Ofisi Zanzibar ni Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS). Hata hivyo Taasisi hizo zipo katika hatua mbalimbali za kukamilisha zoezi hilo. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kuzisisitiza Taasisi hizo kuharakisha ufunguzi wa Ofisi Zanzibar.

### 3.1.2 Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)

**Mheshimiwa Spika,** Katika Wizara hii Bunge liliazimia masuala yafuatayo:

i) Katika mradi wa upanuzi wa eneo la mji wa Serikali

a. Kuhakikisha fedha zote zilizopangwa kutekeleza Mradi huu zinatolewa kwa wakati

b. Serikali ihakikishe inapotekeleza zoezi la utwaaaji ardhi inazingatia taratibu zote za kisheria ikiwemo kushirikisha Wananchi.

ii) Uendeshaji wa shughuli za Baraza la Taifa la Biashara katika ngazi za Mikoa na Wilaya

a. kuwa na mkakati wa haraka na endelevu wa kuongeza watumishi kulingana na mahitaji ya Baraza hili katika ngazi za Mikoa na Wilaya.

b. kuhakikisha kuna ushiriki wa kutosha wa wadau muhimu katika Mikutano ya TNBC katika ngazi hizo.

iii) Ufanisi wa utendaji wa Idara ya Mpiga chapa Mkuu wa Serikali, Serikali ifanye utafiti na kuja na mapendekezo ambayo yatasababisha Idara hiyo kuongezewa uwezo, uhuru na miundombinu yote muhimu ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi na viwango bora.

**Mheshimiwa Spika**, Kuhusu utekelezaji wa upanuzi wa eneo la mji wa serikali Kamati ilipata fursa ya kutembelea mradi wa ujezi wa mji wa serikali na kujiridhisha juu ya utekelezaji wa upatikanaji wa fedha kwa wakati wa kukamilisha mradi huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa Serikali imetoa jumla Shilingi **28,237,647,798.19** kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wa Kata ya Mtumba ambao maeneo yao yametwaliwa kwa ajili ya kuendeleza Mji wa Serikali, Mtumba. Fedha hizo zinajumuisha Shilingi **26,651,005,135.75** zilizolipwa Februari, 2023 kwa wananchi wapatao **1,479** ambao madai yao yalihakikiwa na kustahili kulipwa na Shilingi **1,586,642,662.44** zilitolewa Septemba 2023 kwa ajili ya wananchi **88**.

**Mheshimiwa Spika**, taratibu za uthamini na uhakiki kwa wananchi ambao hawakujitokeza katika awamu zote unaendelea na madai yao yatawasilishwa kwa ajili ya malipo baada taratibu

kukamilika. Aidha, Taratibu za kisheria kuhusu utwaaji wa ardhi zilizingatiwa ikiwemo kushirikisha wananchi ambao maeneo yao yaliathirika na utwaaji ulifanyika kupitia mikutano ya hadhara katika Kata ya Mtumba kwa kuhusisha mitaa ya Vikonje A, Vikonje B, Mtumba, Mahoma Makulu na Chibefu. Lakini pia, ushirikishaji wa viongozi katika ngazi zote ulizingatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kuhusu utekelezaji wa uendeshaji wa shughuli za baraza la taifa la biashara katika ngazi za mikoa na wilaya, Kamati ilielezwa kuwa Kimuundo Baraza ngazi ya Taifa linaongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Mkuu wa Mkoa ni Mwenyekiti ngazi ya Mkoa na Mkuu wa Wilaya ngazi ya Wilaya. Mfumo wa utekelezaji wa majukumu ya mabaraza unazingatia mfumo wa utendaji serikalini kuanzia ngazi ya Taifa, Mikoa na Wilaya kwa watumishi waliopo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikiongeza watumishi katika ngazi mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji. Watumishi hao wameendelea kutekeleza majukumu na maazimio mbalimbali yanayotolewa na Baraza.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inamaoni kuwa azimio hili halijatekelezwa kikamilifu na Serikali, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuleta taarifa kikamilifu kuhusu utekelezaji wa Azimio kama iliivyo elekezwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Utekelezaji wa mapendekezo ambayo yatasababisha Idara ya mpiga chapa wa Serikali kuongezewa uwezo, uhuru na miundombinu yote muhimu ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi na viwango bora. Ofisi ya Waziri Mkuu imeanza kuchukua hatua za muda mfupi na muda mrefu za kutatua changamoto zinazoikabili Idara ya Kupiga Chapa ya Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu yake kama ifuatavyo; -

i) **Mpango wa maboresho wa muda mfupi**

a) Ununuzi wa mashine saba (7) za gharama nafuu na zenye teknolojia rahisi inayokwenda na wakati;

b) Ununuzi wa malighafi za uchapishaji wa nyaraka mablimbali kwa Pamoja (bulk procurement);
c) Matengenezo ya mashine 13 za uchapishaji zinazohitaji matengenezo madogo ili kuongeza uwezo wa Idara kuchapa nyaraka za Serikali; na
d) Kuongeza Idadi ya Watumishi kulingana na Ikama iliyopo.

ii) **Mpango wa maboresho wa muda mrefu**

a) Kukamilisha ujenzi wa Kiwanda cha Serikali cha uchapishaji kinachojengwa Dodoma ambao umefikia asilimia 98 hadi Novemba 2023. Aidha, awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la utawala la kiwanga unaendelea kwa gharama ya shilingi bilioni 5.01;
b) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika shughuli za uchapishaji wa nyaraka za Serikali sambamba na kuweka alama za usalama (*Security features*). Aidha, Ofisi ya Waziri mkuu ipo kwenye mchakato wa kuboresha muundo wa Idara ya Kupiga Chapa ya Serikali kuwa wakala wa uchapaji wa Serikali ili kuiwezesha Idara kufanya kazi zake kwa ufanisi na tija.

**3.1.3 Wizara ya Katiba na Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Wizara hii Bunge liliazimia masuala yafuatayo:

i) Lugha ya Uandishi wa Sheria - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ifanye utafiti wa kutosha kuhusu namna bora ya matumizi ya Lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika uandishi wa sheria na Taarifa ya Utafiti huo iwasilishwe Bungeni kwa lengo la kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu matumizi ya lugha ya uandishi wa sheria;

ii) Lugha ya Mahakama - Serikali iharakishe mchakato wa kusanifu programu ya kutafsiri mwenendo wa mashauri na hukumu za Mahakama kutoka katika Lugha ya Kiingereza kwenda katika Lugha ya Kiswahili ili kurahisisha upatikanaji wa haki kwa haraka;

iii) Ushiriki wa Wadau katika Kuandaa Miswada ya Sheria - Serikali ihakikishe na kuthibitisha kuhusu ushirikishaji wa wadau husika katika maandalizi ya awali ya miswada ya Sheria;

iv) Uendeshaji wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka - Serikali iandae mpango wa haraka na endelevu wa kuhakikisha kwamba Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inapatiwa miundombinu yote muhimu ikiwemo mifumo wezeshi ya kielektroniki, majengo ya ofisi na vitendea kazi.

v) Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai;

a. Serikali ihakikishe inatekeleza maamuzi yote ya Mahakama ili kulinda haki za raia, ikiwemo kurejesha mali zilizotaifishwa iwapo mtuhumiwa ameshinda kesi na pale ambapo hatua zote za rufaa zimekamilika.

b. Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, kwa kushirikiana na taasisi nyingine zinazohusika katika upelelezi, ukamataji, na utaifishaji wa mali za watuhumiwa, kulinda haki za watuhumiwa hao na mali zao bila kuathiri thamani ya mali zao endapo watuhumiwa hao watashinda kesi.

vi) Umuhimu wa Kutilia Mkazo Suala la Utatuzi wa Migogoro Nje ya Mahakama;

a. Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wadau na wananchi kwa ujumla kuhusu umuhimu na faida za utatuzi wa migogoro nje ya Mahakama.

b. Serikali iimarishe mifumo ya kisheria na kiutendaji ambayo itachochea utatuzi wa migogoro nje ya Mahakama kwa ufanisi zaidi.

vii) Umuhimu wa Kuiwezesha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (Solicitor General);

a. Serikali iongeze ukomo wa bajeti (budget ceiling) ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kuiwezesha Ofisi hiyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

b. Serikali itathimini uwezekekano wa kuajiri Mawakili wa kujitegemea ambao wana stadi maalum katika maeneo maalum yenye maslahi kwa Serikali ili kuongeza uwezo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kusimamia mashauri kwa weledi na ufanisi zaidi.

viii) Shule ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo na Ufaulu wa Wanafunzi;

a. Serikali ifikirie na ikibidi ianzishe mitihani ya kuingia (entry examinations) ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaojiunga na Taasisi hiyo wana ujuzi wa nadharia unaotosheleza kufanya mafunzo kwa vitendo kwa ufanisi.

b. Mamlaka husika ifanye utafiti wa kutosha kuhusu mitaala na uwezo wa vyuo katika kufundisha taaluma ya sheria nchini.

ix) Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania;

a. Serikali itenge fedha za kutosha kwa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

b. Tume ya Kurekebisha Sheria ibuni njia mbadala za zitakazohusisha matumizi ya teknolojia ya mtandao, kuhusisha washauri elekezi (consultants) na taasisi za utafiti wa kisheria ili kufanya marekebisho ya sheria yanayoenda na mabadiliko na mazingira yaliyopo sasa.

x) Ucheleweshwaji wa kuridhia Mikataba ya Kimataifa:

a. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na taasisi husika za kisekta, kuhakikisha kwamba inafanya utafiti kuhusu mikataba yote ya kimataifa ambayo nchi yetu inahusika lakini bado haijaridhiwa, ili kutoa ushauri stahiki kuhusu umuhimu wa kuridhia au kutoridhia mikataba hiyo.

b. Kwa ile mikataba ya kimataifa ambayo haijaridhiwa na ina maslahi kwa nchi yetu, Serikali ihakikishe mikataba hiyo inaridhiwa mapema iwezekanavyo.

**3.1.3.1 Utekelezaji kuhusu Lugha ya Uandishi wa Sheria.**

**Mheshimiwa Spika**, Uandaaji na uwasilishaji wa Miswada Bungeni kwa lugha ya Kiswahili ni utekelezaji wa masharti ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1. Kwa mujibu wa kifungu cha 84 kama kilivyofanyiwa marekebisho na Sheria Na. 1 ya Mwaka 2021 lugha ya kutungia sheria ni Kiswahili. Hata hivyo, baada ya kuanza kutekeleza masharti haya Kamati ilibaini kuwa ni muhimu mara tu sheria inapotungwa kwa lugha ya Kiswahili kutafsiriwa ili kuwasaidia watumiaji wasiojua lugha ya Kiswahili. Hivyo, kifungu cha 84 kilifanyiwa tena marekebisho kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 ya mwaka 2023 ili kuitaka Serikali kuhakikisha kuwa Sheria yoyote inayotungwa kwa lugha ya Kiswahili kutafsiriwa kwenda Lugha ya Kiingereza ndani ya siku 90 baada ya kuanza kutumika.

**Mheshimiwa Spika**, Tangu kufanyika kwa mabadiliko ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1 Kiswahili kilifanywa kuwa lugha ya kutungia sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeandika sheria sita (6) kwa lugha ya Kiswahili ambapo Sheria Nne (4) kati ya hizo zimetafsiriwa kwenda lugha ya Kiingereza Serikali inaendelea kutekeleza masharti ya Sheria ili kuhakikisha kuwa sheria zote zinazotungwa kwa lugha ya Kiswahili zinatafsiriwa ndani ya muda ulioainishwa na sheria.

**3.1.3.2 Utekelezaji kuhusu Lugha ya Mahakama.**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kurahisisha tafsiri ya hukumu na kumbukumbu za mashauri, Mahakama imejenga Mfumo wa Kunukuu na Kutafsiri Kumbukumbu za Kimahakama (Transcription and Transalation Sytem - TTS). Mfumo huo una uwezo wa kutafsiri kumbukumbu za kimahakama kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili na Kiswahili kwenda Kiingereza. Hadi sasa, mfumo umefungwa katika Mahakama 11 nchini ambapo katika kila Mahakama zimefungwa seti 4 za vifaa vya kuwezesha kutumika kwake. Mahakama hizo ni Mahakama Kuu Masjala

Ndogo ya Dodoma, Arusha, Dar es Salaam, Bukoba, Mwanza, Musoma, Morogoro, Kituo Jumuishi cha Utoaji haki Temeke, Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara na Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Mahakama nyingine ni Mahakama ya Hakimu Mkazi Kivukoni/Kinondoni.

**Mheshimiwa Spika**, Ufungaji wa Mfumo huu na vifaa vyake pamoja na kutoa mafunzo kwa watumiaji vilikamilika Desemba 2023. Aidha, mfumo wa TTS ili uweze kunukuu mwenendo wa Mahakama unahitaji vifaa vya kurekodi sauti ambavyo tayari vimefungwa kwenye Mahakama 11 zilizotajwa hapo juu. Hata hivyo, pale ambapo hukumu ama mwenendo umeshaandikwa, TTS inaweza kutumika katika kutafsiri tu. Hivyo, pamoja na Mahakama hizo zilizofungwa vifaa vya kurekodi, kwa sasa Mahakama inafanya utaratibu wa kutumia mfumo wa kutafsiri katika Mahakama zote zenye miundombinu ya internet nchini. Mfumo huu utaongeza kasi ya maamuzi na mienendo ya kimahakama kupatikana kwa lugha ya kiswahili maana tafsiri ya nyaraka hizo huchukua dakika chache kukamilika ikilinganishwa na tafsiri kwa njia ya kawaida. Aidha, Serikali inaendelea na uhakiki wa Sheria 258 zilizotafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ili zitangazwe katika Gazeti la Serikali na kuanza kutumika. Pia, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imepanga kutafsiri sheria kuu 188 zilizobakia.

### 3.1.3.1 Utekelezaji kuhusu Ushiriki wa Wadau katika Kuandaa Miswada ya Sheria

**Mheshimiwa Spika**, Mchakato wa utungaji wa sheria (legislative process) umegawanyika katika hatua kuu mbili. Hatua ya kwanza ni mchakato wa awali kabla ya Muswada kusomwa mara ya kwanza. Hatua ya pili ni baada ya Muswada kusomwa mara ya kwanza bungeni ambapo katika hatua hii utaratibu wake unasimamiwa na Kanuni za Kudumu za Bunge. Uandaaji wa Miswada ya Sheria katika hatua ya awali unasimamiwa na sheria na miongozo mbalimbali ya Serikali. Sheria na miongozo hiyo ni pamoja na Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Sura ya 268, Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1, Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma Toleo la Mwaka 2009, Miongozo ya Uandaaji wa Nyaraka za Baraza la

Mawaziri toleo la mwaka 2014 na Miongozo ya Uandishi wa Sheria ya Mwaka 2023. Sheria na Miongozo hii hususan Miongozo ya Uandaaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri inazitaka Wizara na Taasisi kushirikisha wadau wote muhimu wakati wa uandaaji wa mapendekezo ya sheria mpya au marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikiwasilisha uthibitisho wa ushirikishwaji wa wadau sambamba na maoni ya wadau husika katika hatua zote za maamuzi ndani ya Serikali. Serikali itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha wadau wote kushiriki na kutumia fursa hizi katika kutoka maoni yao.

**3.1.3.2 Utekelezaji kuhusu Uendeshaji wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeandaa Mpango Kabambe wa miaka mitano (2023/2024 - 2027/2028) wa ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ambao unahusisha ujenzi wa majengo ya ofisi, upatikanaji wa vitendea kazi pamoja ununuzi wa vifaa vya TEHAMA. Kupitia utekelezaji wa mpango huu Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuanza ujenzi wa Ofisi za Taifa za Mashtaka katika mikoa 10 (Kibaha-Pwani, Ilala-Kinyerezi, Geita, Shinyanga, Manyara, Rukwa, Katavi, Mbeya, Morogoro na Njombe) na Wilaya moja (1) ya Serengeti na Jengo la Makao Makuu Dodoma; ambapo ujenzi wa jengo la Ilala-Kinyerezi na Kibaha pwani na Serengeti yamekamilika kwa 100% na yameanza kutumika na majengo mengine yapo hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, Serikali imeanza mchakato wa ujenzi wa Ofisi ya Mkoa wa Kimashtaka wa Temeke na Kinondoni pamoja na Wilaya ya Hai.

**3.1.3.3 Utekelezaji kuhusu Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa Serikali itaendelea kulinda haki za raia kisheria kwa kuzingatia utaratibu wa urejeshwaji wa mali zilizotaifishwa iwapo mtuhumiwa ameshinda kesi na pale ambapo hatua zote za rufaa zimekamilika.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kuhakikisha wadau wote katika mnyororo wa haki jinai hususan katika eneo la upelelezi,

ukamataji na utaifishaji mali unazingatia haki za watuhumiwa na mali zao kwa kuzingatia sheria zilizopo. Katika kutekeleza hilo mwezi Mei 2023 Mkurugenzi wa Mashtaka alitoa mwongozo wa utaifishaji mali, urejeshaji na usimamizi wa mali zilizotaifishwa (Asset Forfeiture, Recovery and Managament Guidleines) kwa ajili ya waendesha mashataka na wapelelezi. Mwongozo huu ni kwa ajili ya kuwasaidia waendesha mashataka na wapelelezi katika utekelezaji wa majukumu yao kuhusiana na utaratibu wa kisheria ambao wapelelezi na waendesha mashtaka wanatakiwa kuufuata tangu mali inapokamatwa hadi inapoondoshwa (disposed off).

### 3.1.3.4 Utekelezaji kuhusu Umuhimu wa Kutilia Mkazo Suala la Utatuzi wa Migogoro Nje ya Mahakama

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa Serikali inaendelea kuweka kipaumbele katika kutoa elimu kwa wadau na wananchi kuhusu umuhimu na faida za utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zilizochini ya Wizara imekuwa ikitumia matukio ya kitaifa kama vile Wiki ya Sheria, Wiki ya Msaada wa Kisheria, Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, Maonesho ya Wakulima ya Kitaifa na Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Kitaifa kila mwaka kutoa elimu ya sheria pamoja na utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala kwa umma na wadau wengine.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Katiba na Sheria imefanya marekebisho ya Sheria ya Usuluhishi Sura ya 15 ya mwaka 2020 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Sekta ya Sheria ya mwaka 2023 kwa madhumuni ya kuimarisha mfumo wa usuluhishi wa migogoro kwa njia mbadala nchini. Aidha, Wizara imetafsiri kanuni za Upatanishi na Maridhiano ambazo zinalenga kufanikisha utekelezaji wa Sheria ya usuluhishi. Vile vile, katika Mahakama ya Tanzania upo utaratibu wa utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala (Court Annex) Pia, jumla ya Watatuzi wa Migogoro 576 wamesjaliwa, vilevile, jumla ya vituo binafsi vinne (4) vya utatuzi wa migogoro vimesajiliwa na vinafanya kazi. Sambamba na hilo Serikali imepanga kufungua kituo cha Usuluhishi wa Migogoro Tanzania (Tanzania Arbitration Centre).

### 3.1.3.5 Utekelezaji kuhusu Umuhimu wa Kuiwezesha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (Solicitor General)

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuongeza wigo wa Ukomo wa bajeti kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali iliitengea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jumla ya Shilingi 12,812,816,000 na mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya shilingi 17,075,830,000. Aidha, Serikali itaendelea kuongeza wigo wa bajeti kwa Ofisi hii kulingana na upatikanaji wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imepanga kutenga fedha katika Mpango na Bajeti kwa ajili ya kufanya tafiti kuhusu uwezekano wa kuajiri mawakili wa kujitegemea ambao wana stadi maalum katika maeneo maalum yenye maslahi kwa Serikali ili kuongeza uwezo wa Ofisi hii kusimamia mashauri kwa weledi na ufanisi zaidi.

### 3.1.3.6 Utekelezaji kuhusu Shule ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo na Ufaulu wa Wanafunzi

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iliieleza Kamati kuwa italeta marekebisho ya Sheria ya Taasisi ya mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Sura ya 425, pamoja na Tume ya Kurekebisha kufanya tafiti kuhusu mitaala na uwezo wa vyuo katika kufundisha taaluma ya sheria nchini ili marekebisho yatakayofanyika yawe na tija na manufaa mapana kwa taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Baraza la Elimu ya Sheria linafanya ukaguzi wa Vyuo Vikuu vinavyotoa elimu ya Sheria nchini ili kusimamia ubora wa elimu ya Sheria nchini. Kupitia kaguzi hizo, mapendekezo yanatolewa ili kufanya maboresho katika maeneo mbalimbali ikiwemo miundombinu (majengo), idadi ya Walimu wanaofundisha katika Vyuo hivyo na sifa za Walimu wanaohitajika kufundisha Vyuo Vikuu. Maeneo mengine yanayokaguliwa ni maktaba za Vyuo, kama kuna vitabu vya kutosha na vya kisasa, matumizi ya online kwa wanafunzi katika kutafuta vitabu kwa ajili ya kujisomea, namna ya utungaji wa mitihani ya Sheria kwa Wanafunzi, ofisi za Walimu Vyuoni na

mabweni ya Wanafunzi. Aidha, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo imeendelea kufanya maboresho mbalimbali katika kuinua ubora wa utoaji wa mafunzo ya sheria ikiwemo kuhuisha mtaala wake ili uendana na mahitaji ya soko.

### 3.1.3.7 Utekelezaji kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuiwezesha Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilitenga ukomo wa bajeti ya shilingi 3,154,329,000 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya tume na katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali ilitenga ukomo wa bajeti ya shilingi 5,195,945,000 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Tume. Serikali itaendelea kuongeza wigo wa bajeti kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria inajenga Mfumo wa kielektroniki (Law Reform Management Information System) utakaorahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume kidigitali. Aidha, Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171 katika Kifungu cha 10 kinaruhusu Tume kuazima watalaam kutoka Taasisi mbalimbali kwa lengo la kutekeleza majukumu ya maboresho ya Sheria kwa ufanisi. Hivyo, Tume huazima au kushirikiana na watalaam kutoka Taasisi mbalimbali ikiwemo vyuo vikuu na wadau wengine katika shughuli za utafiti. Tume itaendelea kushirikiana na wadau hao katika maboresho ya sheria mbalimbali.

### 3.1.3.8 Utekelezaji kuhusu Ucheleweshwaji wa uridhiaji wa Mikataba ya Kimataifa

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeanza kufanyia kazi suala hili ambapo uchambuzi wa awali umebainisha kuwa hadi kufikia Mwezi Septemba 2023 jumla ya Mikataba 59 imesainiwa lakini bado haijaridhiwa. Mikataba hiyo inahusisha mikataba 15 ya SADC, 3 Umoja wa Afrika, na 41

Umoja wa Mataifa. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa ikitoa ushauri ipasavyo kuhusu mikataba hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha mwaka 2022/23 jumla ya mikataba 13 ya kimataifa imesainiwa. Moja ya sababu za msingi ya kuchelewa kuridhiwa kwa Mikataba ya Kimataifa ni kutoa fursa kwa Serikali kufanya uchambuzi na tathimini ya kina kuhusu Mikataba husika baada ya kusainiwa ili kufahamu umuhimu na manufaa yake kwa nchi na kutoa fursa ya ushirikishwaji wa wadau husika.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba, Kamati imeridhishwa na namna ambavyo Serikali inatekeleza maoni na ushauri unaotolewa na Bunge.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia utekelezaji wa majukumu ya Kamati, Mafanikio, Changamoto na yaliyobainika katika kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024, Kamati ina maoni yafuatayo: -

a) Suala la upungufu wa rasilimali watu limekuwa ni changamoto ya muda mrefu kwa baadhi ya Taasisi na hivyo kuathiri utendaji kazi wa Taasisi hizo, Wizara na Serikali kwa ujumla. Pamoja na kwamba Kamati inatambua juhudi za Serikali kuongeza idadi ya watumishi ili kutatua changamoto hii, kuna umuhimu pia kwa Serikali kuwa na mahitaji ya msingi hasa vifaa, vitendea kazi na miundombionu ya mazingira ya kazi vinaboreshwa pia.

b) Kamati inapongeza Wizara na taasisi zake kwa kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kwa baadhi ya Wizara na taasisi za Serikali hazina utamaduni wa kutenga fedha za kufanya ukarabati mdogo mdogo wa mara kwa mara kwa miradi hiyo. Kamati ina maoni kwamba, kwa kutotenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa aina hiyo, miradi hiyo inaweza kuanza kupoteza

ubora wake. Hivyo basi, ni vema Wizara na taasisi zake zikajenga utamaduni wa kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa namna hiyo.

## 4.2 Mapendekezo

### 4.2.1 Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora

a) **Udahili wa watu wenye ulemavu katika mfumo wa ajira nchini.**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kutokuwepo kwa miundombinu inayojitosheleza na taratibu rafiki kwa watu wenye ulemavu katika mchakato wa ajira nchini. Usaili wa watahiniwa walio wengi haujazingatia watu wenye uwoni hafifu na ukaaji wa muda mrefu kwenye foleni za usaili kwa watu wenye mahitaji maalum.

**NA KWA KUWA** Changamoto hiyo inawanyima fursa ya kushiriki kikamilifu na wakati mwingine kutokushiriki kabisa kwenye mchakato wa usaili wa ajira nchini.

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba Serikali iboreshe miundombinu na taratibu zitakazo wawezesha watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika mchakato wa ajira bila vikwazo vyoyote.

b) **Utunzaji wa Historia za Viongozi wa Jadi na waasisi wa nchi yetu.**

**KWA KUWA** Tanzania ina historia pana na ya muda mrefu, historia hiyo imejengwa na matukio mbalimbali ambayo yameathiri maendeleo, utamaduni, uchumi na umoja wa kitaifa.

**NA KWA KUWA** Kumbukumbu za matukio ya Kihistoria zinaweza kupotea kutokana na sababu mbalimbali kama vile uharibifu wa nyaraka, mabadiliko ya teknolojia, mabadiliko ya tabia nchi, majanga ya asili na kutokuwepo kwa watu wenye kumbukumbu hizo. Vievile kumbukumbu za kihistoria zinaweza kupotoshwa na

kufanywa kuwa hadithi za uwongo na kukosa urithi wa historia kwa vizazi vijavyo.

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba:

i) Serikali ifanye jitihada za kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu za tamaduni, Viongozi wa Jadai na kuhifadhi taarifa hizo kidigitali

ii) Serikai ifanye kampeni maaluum ya kuhamasisha Wananchi kuenzi utamaduni, historia na mchango wa waasisi wa Taifa letu.

c) **Malimbikizo ya Madeni ya Mishahara kwa Watumishi**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kuwepo kwa malimbikizo ya madeni ya mishahara kwa Watumishi wa umma hususan wale wanaopandishwa vyeo na wanaobadilishiwa muundo wa utumishi.

**NA KWA KUWA** Changamoto hiyo husababishwa na mifumo iliopo ya upandishwaji vyeo na mabadiliko ya kimuundo ya watumishi wa umma ambapo baadhi ya Waajiri huchelewa kuwasilisha taarifa za watumishi wanao stahili kupanda vyeo ama kubadilishiwa miuundo.

**KWA HIVYO BASI** Bunge linaazimia kwamba mifumo ya upandishaji vyeo na mabadiliko ya kimuundo kwa Watumishi iboreshwe ili iende sambamba na mabadiliko ya mishahara

d) **Wakala wa Ndege za Serikali kufanya ununuzi wa Ndege mpya kwa ajili ya Viongozi wa Kitaifa.**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kuwepo kwa ndege tatu zinazowahudumia Viongozi wa Kitaifa, Ndege moja aina ya Gulfstream G550 inamuhudumia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ndege zingine Fokker F50 na Fokker 28 zinawahudumia Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Kwanza na wa pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Viongozi wewngine wa Kitaifa.

**NA KWA KUWA** Kamati imebaini kuwa, ndege aina ya Fokker 28 ambayo ilinunuliwa mwaka 1978 ilitumika kuwahudumia Viongozi Wakuu wa Kitaifa hadi kufikia mwaka 2015. Ndege hiyo imefanya kazi ya kuwahudumia Viongozi wa Kitaifa kwa miaka 39, kwa sasa ndege ya Fokker F50 inaendelea kuhudumia Viongozi Wakuu wa Kitaifa isipokuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hali hii husababisha Wakala kutekeleza jukumu la kuwahudumia Viongozi kwa kuchelewa pindi zinapotokea safari za Viongozi wote kwa wakati mmoja.

**KWA HIVYO BASI** Bunge linaazimia kwamba Serikali ione umuhimu wa kufanya ununuzi wa ndege zingine ili kuboresha utoaji huduma za usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

**4.2.2 Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)**

a) **Ongezeko la Matumizi ya dawa za kulevya**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba ipo changamoto ya ongezeko la matumizi ya dawa za kulevya nchini. Pamoja na jitihada nzuri zinazofanywa na Serikali, tafiti mbalimbali ikiwemo Ripoti ya dawa za kulevya ya Dunia ya mwaka 2021 inaonesha kumekuwa na ongezeko la matumizi na mauzo ya dawa za kulevya hasa katika tovuti za siri (dark web), tafiti hizo zinaonesha kuwa ongezeko hilo ni mara nne (4) Zaidi kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na mwaka 2017. Aidha, idadi ya watumiaji wa dawa hizo wanakadiriwa kufikia milioni 200 hadi kufikia mwaka 2019 ambayo ni asilimia 4 ya watu wote duniani. Ongezeko la utumiaji wa dawa za kulevya ni asilimia 18 katika kipindi cha miaka 10 iliyopita.

**NA KWA KUWA** Changamoto ya ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevya katika jamii lina athari nyingi hasi ambazo zinaweza kuathiri afya, kuongezeka kwa uhalifu na kuvuruga maendeleo ya nchi.

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba:

i) Kuhakikisha elimu ya madhara ya dawa za kulevya inaendelea kutolewa husasani kwenye mashule, vyuo vya elimu ya juu na programu za (redio, tevisheni na mitandao ya kijamii).

ii) Kampeni za uhamasishaji wa kupinga matumizi ya dawa za kulevya kuanzia ngazi za vitongoji, vijiji, mitaa, tarafa, wilaya, mikoa na taifa.

iii) Kuongeza vituo vya matibabu na msaada wa kisaikolojia kwa waraibu wa dawa za kuelvya.

iv) Kuimarisha udhibiti wa uingizwaji wa dawa za kulevya nchini kwa kutumia mifumo ya kisasa (*Cargo scanners*).

b) **Uendeshaji wa mashauri ya Dawa za Kulevya**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba katika mashauri 1,158 ya dawa za kulevya yaliofunguliwa kwenye Mahakama mbalimbali nchini, mashauri 64 pekee ndio yaliomalizika hadi sasa.

**NA KWA KUWA** Ucheleweshwaji wa mashauri ya dawa za kulevya unapelekea kupungua kwa Imani kwenye mfumo wa haki jinai, kuendelea kwa biashara haramu na kuathiri juhudi za kupambana na dawa za kulevya.

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba: -

ii) Kuanzisha divisheni maalum ya kimahakama ya kushughulikia mashauri ya dawa za kulevya.

iii) Kuwajengea uwezo watumishi na watendaji wa Mahakama kwa kuwapa mafunzo maalum ya uendeshaji wa mashauri yanayohusu dawa za kulevya kwenye mitandao (*dark web*).

### 4.2.3 Wizara ya Katiba na Sheria

a) **Ukarabati wa Majengo na Mindombinu ya Mahakama za Mwanzo**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba Mahakama ya Tanzania imefanya maboresho makubwa ya matumizi ya TEHAMA kwenye uendeshaji na usajili wa mashauri kwenye Mahakama za Wilaya, Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama za Rufani.

**NA KWA KUWA** Mahakama za mwanzo kwa sehemu kubwa zinawahudumia Wananchi walio wengi zaidi na kwamba Mahakama za Juu yake ni Mahakama za Rufa kwa Mahakama ya Mwanzo. Kamati imebaini kuwa Mahakama za mwanzo zinamapungufu makubwa kwenye ubora wa majengo kwani majengo mengi ni chakavu sana na maeneo mengine Mahakama hizo zimekodi majengo ya Halmashauri pamoja na kwamba majengo mengi ya Mahakama za mwanzo hayana miundombinu kama vile umeme na vifaa vya TEHAMA.

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba:

i) Majengo ya Mahakama ya Mwanzo yaboreshwe kwa kufanyiwa ukarabati unaostahili.

ii) Serikali ijenge majengo ya Mahakama za mwanzo kwenye maeneo ambayo hayana Mahakama za mwanzo.

iii) Serikali ihakikishe Mahakma za mwanzo zinakuwa na Miundombinu za TEHAMA zitakazowezesha Mahakama hizo kutoa huduma za TEHAMA kama ilivyo kwenye Mahakama zingine.

b) **Serikali iwaongeze Majukumu Wanasheria wa Halmashauri kutoa huduma za Msaada wa Kishereia kwa Wananchi**

**KWA KUWA** Serikali imefanya jitihada kubwa ya kutoa huduma za msaada wa Kisheria kwa Wananchi wasio na uwezo wa kupata

msaada wa Kisheria kutoka kwa Mawakili kupitia mradi wa Mama Samia Legal Aid Campaing

**NA KWA KUWA** Watoa msaada wa Kisheria (Para – Legals) hawapatikani katika Wilaya zote Tanzania

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba Serikali iwaongeze Jukumu Wanasheria wa Halmashauri kutoa msaada wa Kisheria kwa Wananchi kwenye baadhi ya maeneo yasio na Watoa huduma wa msaada wa Kisheria (Para legals)

c) **Serikali iwajengee Uwezo Taasisi zinazohusika na Mfumo wa Haki Jinai**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kuwa Taasisi za mfumo wa Haki Jinai kama vile Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali zina upungufu mkubwa wa ikama ya Watumishi na Miundombinu ya Utendaji wa Kazi kama vile vifaa vya TEHAMA, magari na Ofisi.

**NA KWA KUWA** Changamoto hii husababisha Ofisi hizo kutotekeleza majukumu yao kwa ufanisi unaotegemewa na kupelekea huduma zisizoridhishwa kwa Wananchi.

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba:-

i) Serikali itenge Bajeti itakayo boresha Miundombinu ya Taasisi hizo ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao; na

ii) Serikali iajiri Watumishi wa Kutosha kwenye Taasisi hizo kwa kuzingatia ikama ya Taasisi.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 HITIMISHO
### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Muungano wa Mabunge Duniani (IPU) na kuwa Mwanamke wa kwanza kutoka Barani Afrika kushika wadhifa huo. Kamati inakuahidi kuendelea kukupa ushirikiano na tunakuombea kila kila la kheri katika utekelezaji bora wa majukumu yako. Aidha, namshukuru na kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati hii kwa muda wote.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo: -

1) Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2) Mhe. Florent Laurent Kyombo Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
3) Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb – **Mjumbe**
4) Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - **Mjumbe**
5) Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb – **Mjumbe**
6) Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb – **Mjumbe**
7) Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb – **Mjumbe**
8) Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb – **Mjumbe**
9) Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb – **Mjumbe**
10) Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb – **Mjumbe**
11) Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb – **Mjumbe**
12) Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb – **Mjumbe**
13) Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb – **Mjumbe**
14) Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb – **Mjumbe**
15) Mhe. Omar Issa Kombo, Mb – **Mjumbe**
16) Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb – **Mjumbe**
17) Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb – **Mjumbe**
18) Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb – **Mjumbe**
19) Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb - **Mjumbe**
20) Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb - **Mjumbe**
21) Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb - **Mjumbe**

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa, niwashukuru viongozi wote wa Mhimili waMh Utendaji *(The Executive)* kwa ushirikiano ambao

wameipatia Kamati hii katika kutekeleza majukumu yake. Kwa kipekee, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. George Huruma Mkuchika, Mb. – **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais**
2. Mhe. Jenista Joakim Mhagama, Mb. – **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)**
3. Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb. – **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti,ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora)**
4. Mhe. Dkt. Selemani Said Jafo, Mb. – **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)**
5. Mhe. Dkt. Balozi Pindi Hazara Chana, Mb. – **Waziri wa Katiba na Sheria**
6. Mh. Prof Kitila Alexander Mkumbo, Mb. – **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji )**
7. Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mb. – **Mwanasheria Mkuu wa Serikali**
8. Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga, Mb. – **Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)**
9. Mhe. Ridhiwan Kikwete, Mb. – **Naibu Waziri Ofisi ya Rais (Menejimenti,ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora)**
10. Mhe. Khamis Hamza Khamis, Mb. - **Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)**

**Mheshimiwa Spika**, vile vile niwashukuru Watendaji wote wa Mhimili wa Utendaji *(The Executive*) na Mhimili wa Mahakama *(The Judiciary)* kwa ushirikiano walioipatia Kamati. Kwa niaba yao wote naomba niwatambue viongozi wao kama ifuatavyo: -

1. Dkt. Jim James Yonazi – **Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)**

2. Ndg. Juma Selemani Mkomi – **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Menejimenti,ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora)**
3. Ndg. Mary Ngelela Maganga – **Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)**

4. Ndg. Mary Gabriel Makondo – **Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria**

5. Dkt. Tausi Mbaga Kida – **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji)**

6. Prof. Elisante Ole Gabriel – **Mtendaji Mkuu wa Mahakama**

**Mheshimiwa Spika**, Nawashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya uonghozi thabiti wa Katibu wa Bunge **Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*,** na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa Uratibu wa Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**5.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naliomba Bunge lako sasa liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb.
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**
**UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
13 Februari, 2024

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, hoja imeungwa mkono, tunakushukuru sana kwa taarifa ya Kamati yako.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea taarifa zote mbili sasa ni muda wa kuchangia hizi hoja, ninayo majina hapa ya wachangiaji, tutaanza na Mheshimiwa Janejelly James Ntate, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mheshimiwa Florent Kyombo, ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa wasaa huu wa kuchangia. Kwanza, nianze kwa kusmhukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa afya njema na uhai. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi alivyoboresha hizi Wizara hasa upande wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma, upande wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja taarifa za Kamati hizi mbili. Zote zimejishibisha na zote zimekuja na taarifa iliyokamili. Nianze na Menejimenti ya Utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana kwa marekebisho mnayofanya kwenye utumishi wa umma. Hata hivyo, nina machache ya kuwashauri. Leo asubuhi mmeulizwa swali kuhusu safari ya watumishi wanawake wanaonyonyesha, ule mwongozo uko vizuri kabisa lakini Maafisa Utumishi wanachokwenda nacho wanaenda pale mwisho kwenye mwongozo kwa sababu inasemwa; "Endapo hakuna mtu wa kufanya kazi hiyo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo "endapo" imewatesa watumishi wanawake wenye watoto wanaonyonyesha kwa kiasi kikubwa sana. Nishauri, kama "endapo" inaweza ikatoka kwenye huo mwongozo basi itoke, kwa sababu si kwamba inawatesa hawa watumishi wanawake tu inatesa na wale watoto, sasa ili mtu aweze kuendelea na hizo kazi, mwisho anamwachisha mtoto kunyonya kabla hajafika miaka miwili ili aendelee na hizo kazi. Niwaombe mkaliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeletwa suala la njiti, ninawaomba ni wakati sasa wa kuleta sheria humu kwenye Bunge hili Tukufu ya kuwalinda wanawake hawa watumishi wanaojifungua njiti. Sheria hiyo basi iseme kwamba siku ambayo yule mtoto njiti anapokuwa amefikisha umri wa kuzaliwa, sasa ndiyo aanze kuhesabiwa likizo yake ya uzazi, lakini watumishi hawa wanahesabiwa likizo ya uzazi pale anapojifungua kumbe amejifungua mtoto njiti, mtoto yule huwezi kumwachia msaidizi nyumbani, niwaombe sasa ni wakati wa kuleta hiyo sheria ili kuwalinda hawa watumishi wenzetu wanaojifungua watoto njiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee madeni ya mishahra ya watumishi. Mheshimiwa Rais alifanya maksudi mazima, akatoa bajeti ya kulipa madeni ya watumishi, hata hivyo, leo hii bado kuna baadhi ya watumishi wanadai madeni ya mishahara tangu mwaka 2017. Sasa, sielewi utumishi mnatumia kigezo gani, madeni ya 2020, 2019 analipwa, unakuta mwingine wa 2017 hajalipwa. Yawezekana ni mitandao yenu kati ya Wizara ya Utumishi na Idara zinazojitegemea haisomani. Niwaombe mitandao yenu isomane ili watumishi hawa wapate haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa TAMISEMI. TAMISEMI mmesema ukweli kwamba utendaji kule chini umekuwa hauridhishi. Hata hivyo, nini kinafanya utendaji usiridhishe? Ni upunguaji wa watumishi walioko chini hasa upande wa Watendaji wetu wa Kata, Vijiji na Vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii baadhi ya Walimu, baadhi ya Maafisa Ugani ndiyo wamekuwa Watendaji wa Kata, Watendaji wa Vitongoji na Serikali za Mitaa. Sasa, huyu hawezi akatoa huduma kama inavyotakiwa kwa sababu yeye hiyo siyo kazi yake. Niiombe Serikali sasa, ni wakati wa kuboresha watumishi wa Serikali za Mitaa hasa kwenye Utendaji wa Kata, Vitongoji na Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha hata maelekezo yanayotolewa na Bunge lako, bajeti inayopitishwa na Bunge lako, haitekelezwi ipasavyo kwenye Serikali za Mitaa. Bajeti ya Serikali ilipitishwa hapa kwamba, Watendaji wa Kata walipwe posho ya 100,000. Posho hiyo imekuwa kitendawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mtandao na Watendaji wa Kata, kuna wengine toka posho hiyo ipitishwe hawajawahi kulipwa. Wengine wanadai miezi 11, wengine wanadai miezi 12. Si vizuri kutaja hizo Halmashauri. Nimeshakaa na Waziri wa TAMISEMI, nimemueleza suala hilo, nimekaa na Naibu Waziri wa TAMISEMI, nimemueleza suala hilo, niiombe leo Serikali kupitia Wizara ya TAMISEMI, itoe tamko kwa hizi posho za Watendaji wa Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefikia sehemu nyingine wanaambiwa mkakusanye ushuru wa matrekta msipofikia

malengo hatuwalipi hiyo posho. Sisi hatukupitisha hiyo posho kwamba wanakwenda kufikia malengo, ni haki yao. Wengine wameambiwa hizo hela zitapitia kwenye akaunti za *WDC*! Hili ni jambo la kushangaza, haki ya Mtumishi anayo akaunti ya mshahara unamwambia hela yake ipitie *WDC,* ikishapitia *WDC* ataipata kwa uhakika? hawezi kuipata kwa uhakika.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watumishi wanaolipwa na *own sources* za Halmashauri, badala kuwa mishahara yamekuwa mateso. Kuna watumishi wengine wanakaa miezi mitatu mpaka minne hajalipwa ule mshahara. Hivi kweli tunategemea huyu atafanya kazi ipasavyo! Maana haki na wajibu vinaendana. Naiomba Serikali iangalie hawa watumishi wanaolipwa mishahara kupitia kwenye Halmashauri, wanateseka. Sasa mtoe azimio, mtoe maelekezo, kama Halmashauri haziwezi kulipa, basi ndio hawa wapate ajira za kudumu, walipwe na Serikali Kuu kama walivyo watumishi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niongelee *TARURA*. *TARURA* tumewapa kazi kubwa sana, kwa hiyo, tuwaongezee bajeti, tuwaongezee rasilimali watu, tuwape mamlaka yaliyo makuu ya kuweza kufanya hizi kazi. Utashi wa kisiasa umeingia sana kwenye *TARURA*. *TARURA* wanaweza wakasema barabara hii ndiyo ingestahili kujengwa, lakini utashi wa kisiasa ukasema ijengwe barabara sehemu nyingine. Kwa hiyo, nao wanakuwa kwenye mchanganyiko wa kushindwa kuamua ni kipi wafanye na kipi waache. Naomba kama tumeamua *TARURA* ndiyo ihusike na barabara za Serikali za Mitaa, basi tuamue kuongeza bajeti ya kutosha ili barabara hizi ziweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri, Dar es Salaam siasa zake ni Barabara na miundombinu, lakini ukiangalia barabara zilizoko Dar es Salaam ni za kitaifa. Kwenye mitaa kule ni hatari, na tunategemea hizo barabara ndiyo zitusaidie kupata kura za wananchi. Kama tukichukua uthubutu wa kutengeneza barabara za Dar es Salaam tunaweza tukaongea mengine kwenye uchaguzi. Barabara zinatisha, hazipitiki. Nawaomba... *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janejelly kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mabula.

**TAARIFA**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa mchango mzuri wa Mheshimiwa Mbunge. Nataka tu nimpe taarifa kwamba umuhimu wa barabara zinazojengwa na *TARURA* siyo kwa Dar es Salaam peke yake, ni nchi nzima, kwa sababu ushindi wa CCM utatokana na kura zitakazopigwa nchi hii na barabara zina hali mbaya. *TATURA* inahitaji fedha nyingi zaidi kuliko sasa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Janejelly, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea, lakini nawaomba Wabunge, tunapoongelea suala la Dar es Salaam kila Mbunge atuunge mkono, kwa sababu hakuna Mbunge ambaye hana makazi Dar es Salaam ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kabisa!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapoongelea suala la Dar es Salaam mtuunge mkono, mkubali barabara za Dar es Salaam zitengenezwe. Mwache kutujia *inbox*. *Inbox* wanakuja na kusema ongeleeni barabara ile, ongeleeni barabara ile, hata kwa *message,* lakini sasa hapa tukiongea, wanaona kama tunajipendelea Dar es Salaam. Hatujipendelei, Dar es Salaam ndiyo kioo cha Taifa, Dar es Salaam ndiyo Mji Mkuu wa kibiashara, lazima barabara za Dar es Salaam zitengenezwe. *(Makofi)*

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janejelly kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Lazaro Nyamoga.

**TAARIFA**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tu kuweka kumbukumbu sawa, tupo Wabunge wengi ambao hatuna makazi Dar es Salaam, tunaishi majimboni, mmojawapo ni mimi. Naomba kutoa taarifa hiyo ili wananchi wasije wakaelewa tofauti na hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Janejelly taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana mdogo wangu huyu, lakini hiyo taarifa siwezi kuipokea, sijasema hawakai kwenye majimbo yao, lakini nimesema wana makazi Dar es Salaam. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu. Naomba Barabara za Dar es Salaam ziangaliwe kwa umuhimu wa kipekee.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea haya, mnafanya utani, mnanipiga taarifa, lakini Dar es Salaam tuelewe ndiyo ina asilimia 15 ya kura za nchi hii, tunazozitegemea. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, alishapewa taarifa mbili zinatosha.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoongea ninamaanisha. Ni lazima Dar es Salaam iangaliwe

kwa jicho lingine, ni lazima Dar es Salaam barabara zitengenezwe. *(Makofi*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuweza kuchangia taarifa za Kamati hizi muhimu sana; Kamati ya TAMISEMI na Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla kwamba wamepeleka fedha nyingi sana majimboni kwetu kufanya kazi ya kuhudumia watu wetu katika sekta mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naunga mkono Taarifa na maazimio ya Kamati zote mbili, nami ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi taarifa ni muhimu sana kwa sababu zina *cut across* katika maeneo yote katika nchi yetu, sasa zikishasomwa napendekeza kwamba kuwe na utaratibu tu wa kujua kwamba yale tuliyotoa mwaka jana yametekelezwa mpaka leo kwa kiwango gani? Tusiwe tunasoma taarifa halafu tunafunika tu halafu tunaacha, hapana tuweke utaratibu wa kufuatilia mambo haya mazito ambayo tumeazimia kwa kila Kamati. Kwa sababu ni mambo ya msingi Wabunge wamechangia, na yameletwa katika Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, ni muhimu sana

tupate mrejesho, maazimio ya mwaka jana, mwaka juzi na haya ya leo mwakani tupate mrejesho kujua utekelezaji wake umefikia hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mapendekezo ya Kamati ya TAMISEMI tumesema ni vizuri Serikali ikaweka utaratibu. Mheshimiwa Rais, Mama Samia amepeleka fedha nyingi sana kujenga miundombinu ya elimu msingi, sekondari na afya, lakini unaweza ukashangaa shule ambayo imejengwa kwa zaidi ya shilingi milioni 500 mpaka shilingi milioni 600 na nyingine zimejengwa kwa shilingi bilioni moja na zaidi, lakini watoto wanakaa chini, hawana madawati, viti au meza, au shule inataka kufungwa kwa sababu wamefunga ya vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali iweke utaratibu wa kuhakikisha kwamba matundu ya vyoo isiwe ajenda ya kujadili kwenye Bunge hili, ni aibu. Habari ya madawati ya watoto kukaa chini tunapigiwa picha, tunaoneshwa, siyo sawa sawa. Kwa hiyo, jambo hili liwekewe nguvu na litekelezwe na tupate mrejesho kwamba hatua zimechukuliwa kwa kiwango gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya *TARURA,* kila Mbunge hapa jimboni kwake hata watu wa Dar es Salaam pia maeneo mengi hayapitiki. Sasa maana yake ni kwamba, kama hatutaki mwaka huu kupata ushindi mgumu wa uchaguzi, Serikali kwa makusudi iongeze fedha ya dharura ili wakarekebishe maeneo ambayo hayapitiki, warejeshe madaraja, wajenge mitaro, walete makalvati ili wananchi waweze kuwasiliana katika maeno hayo, na ni majimbo yote. Kila Mbunge akijieleza hapa, kuna malalamiko makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wabunge wengine sasa hivi wameahirisha kwenda majimboni kwa sababu ukifika pale hata nyumbani kwako huwezi kwenda. Kwa hiyo, ni vizuri hiyo hoja itolewe. Kibaya zaidi, fedha iliyotengwa, mwaka wa bajeti huu shilingi bilioni 808 ni asilimia ndogo sana imeenda na Serikali iliahidi kuongeza shilingi bilioni 350. Kwa hiyo, ni lazima kwanza fedha yote waliyobajeti iende na fedha ya dharura ambayo tuliahidiwa hapa iende ikafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina Kata ya Matongo na Kibazuka ambako ng'ombe za watu zimeenda, mazao yameenda, watu wamepoteza maisha, hakuna mawasiliano kabisa katika Mto Tigite. Kwa hiyo, tunaomba fedha ikienda maeneo hayo pia ni muhimu kuzingatia na Wabunge washirikishwe katika kuboresha mawasiliano katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Vita Kawawa.

**TAARIFA**

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa msemaji, ni kweli anayoyasema namuunga mkono. Ni kwamba hata kwetu Jimbo la Namtumbo, barabara zinaharibika sana hasa barabara ya kutoka Lusewa kwenda Msisima na tulitengewa shilingi milioni 216 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo lakini fedha bado hazijaenda na kwa hiyo, mkandarasi hajaenda kazini. Kwa hiyo, barabara imekatika kabisa kutoka Lusewa kwenda Kata ya Msisima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waitara, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hiyo taarifa iwe ya mwisho kwangu, kwa sababu mimi siyo mzuri sana katika mambo hayo ya kutoa taarifa. Ndiyo maana huwa siwapi taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotaka kufanya kazi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa nimeipokea, lakini iwe ya mwisho hiyo. Sitaki nyingine tena. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unataka kufanya kazi ya maendeleo katika vijiji vyetu, vijiji na mitaa, yaani Serikali za Mitaa, imetambuliwa kwenye Katiba Ibara ya 145, lakini pia ikaongeza kazi zake Ibara ya 146, ambako kuna Umma wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango yote ya Serikali, hakuna mahali kwenye bajeti wamewahi kuonesha namna ambavyo wanasaidia vijiji, mitaa na vitongoji madiwani kufanya kazi yake. Hata namna ya kupata kazi za kawaida, hata posho ambazo wanafanya kwenda kusimamia miradi zinapangwa kutoka Ofisi ya TAMISEMI, zinaenda Mkoani, zinaingia kwenye Wilaya na Halmashauri. Kwenye vijiji pale watu wanashinda kutwa nzima hakuna hata maji ya kunywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema asilimia 20 inaenda kwenye vijiji, tungeomba tupate takwimu ya Halmashauri ipi imerejesha asilimia 20 kwenye vijiji kusaidia viongozi wale kuendesha Halmashauri zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho za Madiwani zimeongezwa mara ya mwisho tarehe 16 Agosti, 2012, miaka 12 mpaka leo. Hao Madiwani, wanalipwa shilingi laki tatu na nusu, na Wabunge ni mashahidi. Madiwani kama kuna msiba, ni wao; iwe kuna sherehe ni wao, watoto kwenda shule, ni wao; kukagua miradi, ni wao; mvua imenyesha, ni wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wakati muafaka, kwenye bajeti ijayo, Serikali iweke ongezeko la posho kwa Wenyeviti wa vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji, Waheshimiwa Madiwani ili na wenyewe wakafanye kazi. Kama maisha ni magumu kwa sekta nyingine na watu wengine, maisha ni magumu sana kwa Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji na Waheshimiwa Madiwani. Hili lizingatiwe na Waheshimiwa Wabunge naomba, kwenye bajeti hii, hicho kipengele lazima kiwekwe kwenye bajeti ya TAMISEMI, ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni vitendea kazi. Ninyi mmezungumza hapa Waheshimiwa Wabunge, watendaji kwanza ni wangapi? Hata asilimia 60 hawafiki. Kwa hiyo, vijiji vingi havina

watendaji. Kata nyingi hazina watendaji, na kama wengine wapo, hawana sifa. Kwa hiyo, ukitaka kuimarisha Serikali za Mitaa, ni vizuri tuangalie hivi unampa nani aendeshe kata? Unampa nani aendeshe Kijiji? Hiyo inaenda sambamba pia kwenye na kwenye mikoa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara nyingi ambazo tunaangalia kwenye mikoa yetu, wanafanya Wakuu wa Mikoa, sasa waulize Makatibu Tawala, wanafanya ziara kwenda kusikiliza watendaji wenye kero kwenye mikoa na halmashauri? Kuna watu wanaonewa sana, yaani hawapati ziara, akienda ziara, posho mnagawana asilimia 80; hujampa posho, huendi. Huo ndiyo ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Makatibu Tawala wafanye ziara kwenye Halmashauri zetu, wawasikilize Watumishi wa Umma, wapunguze changamoto, wapunguze malalamiko ili wafanye kazi kwa moyo. Vilevile katika eneo hili, ni vizuri tuweke utaratibu, hivi Mkurugenzi anapatikanaje? Kuna Wabunge hapa wanalalamika Mkurugenzi hana uwezo kabisa, yupo miaka mitano pale. Sasa wanasubiri maendeleo kwa mtu ambaye hana uwezo! Yaani wewe unapanda mahindi kwenye mwamba, unataka kuvuna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tuangalie watumishi wale na SMT. Kama mtu hana uwezo katika eneo fulani asihamishwe kwenda sehemu ya pili, aondolewe pale awekwe mtu mwenye kwenye nafasi hiyo, mwenye uwezo wa kufanya kazi. Mkitaka matunda na matokeo mazuri, ni lazima muangalie mikoa, Watendaji wa Serikali wenye sifa wale wanaofanya kazi vizuri, wapongezwe. Wezi wote wawajibishwe. Hiyo itasaidia pia kufanya kazi ya utendaji mzuri, na pia kila mtu ajue kwa nini fulani kapata na kwa nini fulani kakosa? Kuwe na vigezo. Hii ni kazi ya Utumishi ya wataalam, hapa siyo siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikifanyika hiyo, Wabunge hapa hatutalalamika, fedha inaenda kwenye Halmashauri inabadilishiwa matumizi kinapangwa kitu kingine. Mbunge ameahidi kazi ya maendeleo, kile ambacho kimesemwa

hakifanyiki, halafu huwezi kumgusa kwa namna ambavyo *setup* imekaa. Kwa hiyo, nilidhani mambo haya yaondolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ziara na semina, nililoliona kwa mfano Uchaguzi wa mwaka 2024, uwekwe utaratibu, Wenyeviti wa Mitaa wakishachaguliwa na vijiji wapewe semina, wapate mafunzo. Madiwani wakichaguliwa mwakani, bajeti iwepo, wafundishwe. Huyu sifa yake, anajua kusoma na kuandika, huyu mwenzake ana *masters,* ana *first degree,* ni mbingu na nchi, hawakutani. Kwa hiyo, kuwapiga *sound* ni rahisi. Ni vizuri tutengeneze watu wetu vizuri kuwajengea uwezo wa ku-*perform* na tunapodai miradi ikae vizuri, maana yake watu tumeandaa wa kusimamia na wenyewe wawe na uelewa pia wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho hapa ni namna ambavyo tunaweza kumalizia shule zetu. Imetengwa bajeti ya TAMISEMI na sasa kuna changamoto kubwa katika Taifa letu. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI anafanya nzuri sana, hatuna shida naye, lakini tunamwomba na Serikali kwa ujumla, barabara ndiyo siasa, barabara ndiyo maisha, barabara ndiyo mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majimbo ya vijijini mvua zimenyesha, hata aliyevuna kidogo hata sokoni hawezi kwenda. Kwa hiyo, ni lazima jambo hili kama Bunge tulichukue kama jambo mahususi, tupate azimio na liungwe mkono, na Waziri aje kwenye Bunge atuoneshe mpango wa muda mfupi wa kutengeneza barabara zetu, mpango wa muda wa kati wa kutengeneza barabara na mpango wa muda mrefu. Mpango wa muda mrefu ni kuongeza bajeti. Tunapendekeza iongezeke fedha kutoka shilingi bilioni 808 iende *1.6 trilion* ili asilimia 70 ya barabara za vijijini ziweze kutengenezwa, na hivyo tutakuwa tumepeleka siasa nzuri na ushindi wa Chama cha Mapinduzi utakuwa shahiri dhahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara kwa mchango wako. Mheshimiwa Florent Laurent

Kyombo atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, na Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia katika taarifa ambayo imewasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Utawala, Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nashukuru na kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Wizara zote ambazo zinasimamiwa na Kamati. Tumeona kazi kubwa ambayo inafanyika katika kipindi cha mwaka mmoja na hizo ni Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na utawala bora; Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano; Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na Wizara ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia nia ya dhati ya Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunaona jinsi alivyodhamiria kuishi kwa misingi ya Utawala Bora, misingi ya haki na misingi ya utii wa sheria. Katika kipindi cha mwaka mmoja, Kamati yetu imepitia Miswada 12. Ndani ya Miswada hiyo 12, kuna sheria zaidi ya 74. Kwa kuangalia hivyo, inatuambia nini? Ni kwamba Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria kusimamia nchi yake katika mfumo wa Utawala Bora, katika mfumo wa utii wa sheria na katika mfumo wa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuishi katika haki hizo maana yake Mheshimiwa Rais anaishi katika Falsafa yake ya *4Rs* ya kuhakikisha kwamba maridhiano yamekuwepo, uvumilivu umekuwepo na ustahilivu, lakini pia *reforms* na *rebuilding* zinakuwepo katika nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona, tumekagua miradi mbalimbali, lakini mahususi nitaongelea miradi miwili, na miradi hiyo yote inalenga kupeleka huduma karibu na wananchi, na pia inalenga kutekeleza haki. Tumeona miradi ya ujenzi wa jengo la Kituo Jumuishi cha Kutoa Hati. Katika eneo hili tunaona katika jengo moja Mahakama ya Mwanzo mpaka Mahakama ya Rufani mwananchi akiingia pale maana yake anapata huduma zake

zote. Pia na Watendaji wetu wa Mahakama, maana yake akihitaji faili kama ni rufani, ahitaji kuandika kesi ambayo imeenda katika Wilaya nyingine au kitongoji kingine, zote ziko ndani ya jengo moja. Hiyo imerahisisha utoaji wa haki za kisheria. Kwa hiyo, tunayo kila sababu ya kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake na wasaidizi wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumeona ujenzi wa Kituo Jumuishi kwa Taasisi za Kisheria. Ukiingia ndani ya jengo moja unamkuta Wakili Mkuu wa Serikali yuko pale, unamkuta Waendesha Mashtaka wako pale, Jeshi la Polisi wako pale, Taasisi zote zinazosimamia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siwezi kusema maneno mengine zaidi ya kusema nia ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya Utawala Bora, nia ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya utii wa sheria, nia ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya haki kwa wananchi wake, tunaiona kwa matendo. Tuna kila sababu pia ya kumpongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria inasimamia Wizara tano kama nilivyotaja, na leo nitajikita katika maeneo makubwa ambayo ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na nitaongelea kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kama muda utaruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza, katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Uratibu na Bunge nitajikita katika Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya. Ni lazima nimpongeze Mheshimiwa Rais na wasaidizi wake katika Wizara hiyo ambao ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, msaidizi wake Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Katibu Mkuu Jimmy na mahususi, Kamishna Jenerali Ndugu yangu Aletas Lyimo, Makamishna Wasaidizi na Watendaji wote wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa imesomwa hapa tumesikia, ongezeko la matumizi ya Madawa ya Kulevya Duniani ni zaidi ya milioni 200 ambayo ni sawasawa na asilimia nne ya watu wote duniani. Tanzania siyo kichaka, tunaendelea pia, suala hili

tunaliona ndani ya nchi yetu, lakini tumekuwa na watumishi ambao chini ya Wizara ya Sera, Bunge na Uratibu chini ya Mamlaka ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya wakijituma usiku na mchana, tumeona wanakagua, tunagundua viwanda vya kutengeneza biscuit za madawa ya kulevya, sehemu mbalimbali wanagundua haya mambo yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaona katika uchukuaji wa sheria katika eneo hili kuna upungufu mkubwa sana. Katika eneo hili tunazo kesi 9,538. Kwa masikitiko makubwa nasema, kesi 16 tu ndiyo zimechukuliwa hatua, na hizo kesi siyo kwamba zimemaliza, yaani nne tu ndiyo zimemalizika kwa Serikali kushinda, nne tu walipata haki yao wakaruhusiwa lakini nne ziko katika hatua za usikilizwaji, tatu ziko katika hatua za kutajwa na moja iko katika hatua ya kusubiri hukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha kesi 1,158 ni za mwaka ulioisha 2023. Sasa tunaenda wapi? Tunawekeza fedha nyingi kwa kuhakikisha tunaandaa utaratibu wa Serikali kuchukua hatua dhidi ya madawa ya kulevya lakini sasa pale wanapogundulika waliofanya hivyo hawapewi haki yao au sheria hazichukuliwi. Kwa kweli ukiangalia kesi 938 na 16 tu ndio zimechukuliwa hatua. Tuna jambo la kujiuliza kama Serikali, tuna jambo la kujiuliza kama Bunge. Tuna jambo la kuhakikisha kwamba tunaisimamia Serikali inahakikisha kwamba wenzetu ambao wanasimamia kesi hizi, haya mashauri; tushauri kitu ambacho kitaisaidia Serikali kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nakuja na ushauri, maana yake ukiziacha kesi hizi, kwanza zinapunguza imani katika mfumo wa haki; lakini pili, ukiangalia kesi hizi kukaa namna hii maana yake tunaendeleza biashara haramu ya madawa ya kulevya. Pia, ukiangalia katika kesi hizi kukaa hivi maana yake jitihada za kupambana na dawa za kulevya zote kwa kweli zinakatishwa tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo hata watumishi wetu …

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, … ambao wanatakiwa kufanya kazi vizuri maana yake watashindwa kufanya kazi kwa wakati…

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mchangiaji mzuri kwa mchango wake na mbali tu hizo jitihada za upambanaji wa dawa za kulevya kushindwa kuungwa mkono kwa watuhumiwa kuchukuliwa hatua stahiki, sasa hivi wamebuni mbinu mpya ya kwenda kuwauzia kemikali bashirifu kwenye zile *center* za wale warahibu wa *drugs.* Mwisho wa siku wanatoka kunywa dawa anarudi tena kutumia kemikali bashirifu ambazo ndio mbaya zaidi, nilikuwa naomba nimpe taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent, taarifa unaipokea?

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa naipokea, ina msingi wa kujenga na kuonyesha lazima tuongeze mbinu za mapambano ili kukabiliana na madawa ya kulevya. Mimi naomba kama ambavyo Kamati tumeshauri, tunaomba Bunge liazimie kuanzisha *division* maalum ya kushughulikia mashauri ya madawa ya kulevya. Tumeona katika maeneo ambapo *division* hizi zimeanzishwa kazi kubwa imeendelea kufanyika kupunguza haya mashauri ambayo yako pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona *division* maalum ya ardhi ambayo iliundwa kwa ajili ya kupambana na mrundikano wa kesi za ardhi inaendelea kufanya kazi vizuri lakini tunaona *division* ya kazi na yenyewe inaendelea kufanya tu vizuri. Kwa hiyo, niombe Bunge lako Tukufu tuanzishe *division* maalum ya kushughulikia mashauri ya dawa za kulevya kusaidia Taifa letu, kusaidia Mheshimiwa Rais wetu ambaye anataka utawala bora, anataka haki na nchi yetu iweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho katika eneo hili naomba nichangie katika Ofisi ya Makamu wa Rais, eneo la muungano na eneo hili naomba nitoe pongezi za dhati kwa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na wasaidizi wake, Mheshimiwa Selemani Jafo, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu. Pia, katika eneo hilo tulikuwa na Hoja za Kamati ambayo ilitakiwa hoja za Muungano 25 ambazo zilikuwepo lakini tunaona asilimia 88 za hoja hizo zote zimejibiwa. Maana yake hoja 22 zote zimejibiwa, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia azimio la pili ilikuwa ni kuhakikisha kwamba taasisi zote za kimuungano zinakuwa na ofisi katika pande zote mbili na tunaona utekelezaji wake hapa ni asilimia 97. Maana yake taasisi 33 zote zina ofisi katika maeneo yote mawili ya muungano na taasisi chache zilizobaki tatu ambazo ni *TIC, NBS* na *TEA* na zenyewe ziko katika hatua za mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia kwa utayari wake wa utawala bora, kwa uongozi wake wa kufuati haki lakini na utii wa sheria; na tunaamini tukiendelea kumuunga mkono na haya yote basi yatatimizwa. Basi tunaiona Tanzania njema ya kesho na leo; na watu wote wataendelea kuishi kwa ustawi wa utii wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru kwa muda wako na naunga mkono hoja ya Kamati na naomba Wabunge wote tuungane kwa ajili ya kuunga mkono hoja za Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Florent kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, ajiandae.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Hoja ya Kamati na nitajielekeza zaidi kwenye Kamati ya Bunge ya Kudumu ya TAMISEMI. Ninamshukuru na

kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya hasa kwa uwekezaji wa fedha nyingi sana kwenye miradi ya maendeleo katika halmashauri za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano ipo mingi, shule za sekondari za mikoa, kila mkoa fedha zimepelekwa na ujenzi unaendelea lakini kupitia *SEQUIP* kila halmashauri inaendelea kupokea fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule; lakini wote tunaona miundombinu ya afya pamoja na vituo vya afya pamoja na hospitali na vifaatiba vimepelekwa kwa wingi. Kwa kweli kazi inafanyika na naamini kabisa mwenye macho haambiwi tazama, tunaona mambo megi ambayo yanafanyika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nichukue nafasi hii pia kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Manaibu Mawaziri na Makatibu Wakuu kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuonyesha katika utekelezaji wa kazi hizo kwenye maeneo mbalimbali tunapoendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye maoni na mapendekezo mbalimbali ambayo yamefanywa na Kamati ya TAMISEMI hasa kwenye upande wa eneo la *TARURA*. Barabara ni siasa kubwa kwenye nchi yetu hasa maeneo ya vijijini na hali tuliyonayo kwa sasa ni mbaya hasa baada ya kipindi hiki cha mvua. *TARURA* ilitengewe shilingi bilioni 818, hivi tunavyozungumza zilizoenda ni bilioni 82 tu ambayo ni sawa na asilimia 12, ndiyo fedha zilizopokelewa. Maana yake ni kwamba kuna fedha zaidi ya asilimia 80 ambazo hazijapelekwa na sasa tuko kwenye kipindi ambacho tunaelekea kumalizia mwaka wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kabla hatujazungumzia ongezeko la bajeti kutoka hii milioni 800 kwenda trilioni 1.6, hizi fedha ambazo mwaka huu zilitengwa, tunaiomba Serikali na tumeiweka kwenye maazimio ipeleke fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara, fedha ambazo zilikuwepo kwenye bajeti iliyopita; na kwenye azimio hili tumesisitiza sana Wizara ya Fedha kuweka vipaumbele vyake sawa sawa kwa sababu hatuoni kipaumbele

kikubwa kwa sasa hivi cha dharura zaidi ya miundombinu ya barabara. Kwenye maeneo mbalimbali ya vijijini, akina mama wanakufa kutokana na kushindwa kusafirisha wagonjwa kwenye maeneo hayo. Mazao yanaoza kwa sababu hatuwezi kusafirisha mazao katika kipindi hiki ambacho barabara zimekatika na kuharibika na changamoto mbalimbali zinazotokana na miundombinu ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hatujajua Wizara ya Fedha ina kipaumbele gani kingine kikubwa zaidi ya miundombinu ya barabara kwa sasa, hadi kusababisha fedha asilimia 12 tu ya bajeti ipelekwe hadi kufikia Desemba, ambapo ni nusu ya mwaka, ambapo tulitarajia fedha ambayo imepelekwa ingekuwa angalau zaidi ya asilima 50. Kwenye azimio letu hili lipo na naomba Bunge likubali kuazimia jambo hili lakini baada ya kuazimiwa jambo hili litekelezwe na Wizara ya Fedha mara moja kwa kuipa *TARURA* fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la elimu yako mambo mawili ya muhimu pamoja na ujenzi wa miundombinu mizuri, halmashauri zimepokea fedha nyingi sana kutoka Serikali Kuu na kwa sababu zimepokea fedha nyingi sana kutoka Serikali Kuu na ujenzi wa madarasa umefanyika vizuri kuna changamoto mbili. Kwanza ni madawati lakini pili ni miundombinu ya vyoo kwenye shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa halmashauri zimekwisha kusaidiwa ni muhimu sasa TAMISEMI kuangalia halmashauri zote kuja na mkakati wa kumaliza tatizo la madawati kwa kupitia mapato ya ndani kwa sababu tayari wameshasaidiwa madawati; kwa sababu tayari wameshasaidiwa miundombinu ya madarasa. Kwa hiyo katika eneo hili, katika bajeti ijayo miundombinu ya vyoo pamoja na madawati iwe ni kipaumbele kwenye sekta ya elimu kwa sababu kama madarasa ni mazuri basi na miundombinu ya vyoo iwe mizuri na madawati yawepo ili watoto wetu waendelee kuwa kwenye mazingira mazuri ya elimu na waweze kuendelea na masomo vizuri. Hili pia tumeliweka kwenye maazimio na nina hakika Bunge litaazimia na kupitisha ili liweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mwenyekiti wa Kamati ya TAMISEMI anawasilisha aliataja suala la halmashauri mbalimbali kujifunza kuhusu kutunza misitu ya asili kwa ajili ya uvunaji wa hewa ya ukaa. Ningependa kutoa mfano mmoja wa Halmashauri ya Kilolo, Hifadhi tu za misitu ya Kijiji, Halmashauri ya Kilolo ni hekta 50,531 lakini hapo nimeacha kutaja hekta za *TFS* ambazo ni 198.599. Ninaamini hii ni moja kati ya halmashauri zenye eneo kubwa sana la hifadhi ya misitu ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale TAMISEMI kuna kitengo nafikiria au idara kuna mtu anashughulika na kuanzisha hii miradi ya uvunaji ya hewa ya ukaa na kuna halmashauri nyingi ambazo zingeweza kukusanya mapato zaidi ya mapato yake ya ndani kwa kupata fedha kutokana na uvunaji wa hewa ya ukaa na tayari kuna halmashauri chache zimeshaanza kunufaika. Tunachojiuliza ni nini kinachelewesha TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Mazingira kuwekeza katika kuhakikisha kwamba halmashauri zote zenye misitu ya asili zinaingia kwenye uvunaji wa hewa ya ukaa ili kujiongezea mapato, kwa sababu jambo hili lingeweza kupunguza sana gharama za unedeshaji wa halmashauri kwa kutoa fedha kwenye Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii jambo limetajwa pale kwenye taarifa yetu na tunasisitiza na kuiomba TAMISEMI pamoja na Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano kuliangalia na kuangalia ni mkakati upi unaweza ukafanywa ili halmashauri zote zenye misitu ya asili na imezitunza kuweza kuingia kwenye uvunaji wa hewa ya ukaa kwa kufuata miongozo ilipo. Ni kwa nini halmashauri chache zipate mabilioni ya pesa na halmashauri zenye misitu mikubwa kuliko hata hizo zinazopata zenyewe hazijaanza. Ni nini kipo hapo? Na kwa nini hakiwezi kutatuliwa? hilo tungeomba liweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoelekea kumalizia nitaje mambo mawili ya muhimu. La kwanza ni suala zima la kuwa na mwongozo mzuri wa posho za viongozi katika ngazi za vijiji na ngazi ya kata, hasa kwa sababu kwa sasa kuna halmashauri nyingi viongozi hao hawapati posho zozote. Kwa hiyo ni lazima tuwe na mwongozo …

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** …ili viongozi hao waweze kupata posho katika…

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** …kwa kufuata mwongozo uliotolewa na TAMISEMI. Kwa sasa inakua ni changamoto kubwa kwa sababu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lazaro…

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** …hakuna mwongozo wowote…

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa kwa Jirani yako.

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Kaka yangu mchangiaji, kwanza Serikali yetu ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iliridhia kabisa Watendaji wa Kata waweze kupewa posho za madaraka, lakini pamoja na hiyo sambamba na hivyo halmashauri nyingi hawawapi posho za madaraka kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Justin Lazaro, taarifa unaipokea? Malizia mchango wako.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea na kuongezea tu pamoja na hilo kwa sababu ni muda mrefu umepita, madiwani pia posho zao hazijafanyiwa mapatio. Kwa hiyo tunatarajia kwenye bajeti ijayo Serikali italeta mapendekezo ya nyongeza ya posho za madiwani lakini na mwongozo mzuri wa ulipaji wa posho kwa viongozi wa ngazi za vijiji na viongozi wa ngazi za vitongoji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja zote mbili, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niwe miongoni mwa wachangiaji katika taarifa zetu hizi mbili ambazo zimewasilishwa na Kamati. Kipekee niwapongeze sana Wenyeviti wetu wote wawili kwa uwasilishaji mzuri kwa niaba ya Kamati zao lakini pia nipongeze Mawaziri na Watendaji wote kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee mimi nitajikita kwenye upande wa Wizara ya TAMISEMI na kwa sababu ya muda, nitaenda moja kwa moja kwenye sehemu ya *TARURA*. Tukiangalia ukurasa wa 37 wa taarifa ya Kamati, imejaribu kutupa kwa kina mchanganuo wa barabara ambazo zinahudumiwa katika nchi hii; barabara za lami, barabara za changarawe na barabara za udongo. Sasa tunaona asilimia zaidi ya 69 ya barabara katika nchi hii zinazohudumiwa na *TARURA* bado ni barabara za udongo, lami ni asilimia 2.23; na changarawe ni asilimia 28.46.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukijaribu kuangalia hali zetu mnazijua, tunaposema udongo, udongo hata ukimwaga maji tu ya kawaida ule udongo unaondoka. Sasa unaweza uka-*imagine* hali ya mvua kama hii ambayo tumekuwepo nayo katika kipindi hiki na ni mateso kiasi gani wananchi wa nchi hii wanapata shida. Kama barabara za lami zinaharibika udongo ukoje? Kwa hiyo picha tunayoondoka nayo hapa, kwa sababu mvua inanyesha nchi nzima maana yake ni kwamba zaidi ya asilimia 70 ya miundombinu ya nchi hii ipo taabani na iko katika hali mbaya, kwa sababu taarifa yenyewe inasema zaidi ya asilimia 69 ni udongo. Maana yake maeneo yote yenye barabara za udongo leo hayaingiliki wala hayafikiki na nyote ni mashahidi tuko hapa wananchi wetu tunajua yanayoendelea majimboni huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kidogo nilitaka tujikite hapa tujaribu kuchambua na kuona ni jinsi gani tunaweza tukawatoa wananchi hawa wa Tanzania katika lindi hili kubwa

ambalo limewakwamisha na zaidi linawarudisha nyuma. Linawarudisha nyuma kwa sababu bila miundombinu mizuri *no matter what you are doing,* mimi kama siwezi kutoka nyumbani leo, umejenga kituo cha afya lakini mvua imenyesha hamna daraja, nafia ndani kwa sababu sintoweza kuvuka kwenda kwenye kituo cha afya. Umejenga shule watoto hawawezi kwenda shule kwa sababu ya miundombinu mibovu. Umejenga masoko na vitu vingine vyote vizuri watashindwa kusafirisha mazao toka mashambani wayafikishe kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo unapokuwa huna miundombinu maana yake unakwama *completely* na unabaki kule chini. Kwa hiyo cha kwanza *focus* yetu kubwa kupitia Wizara hii ya TAMISEMI ni lazima tuangalie jinsi tunaweza tukawasaidia *TARURA* wafanye kazi zao na kazi hazifanyiki bila pesa, maana kazi hizi za ujenzi ni pesa, mafuta yanahitajika kwenye mashine ni pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza ripoti hapa tunasema wakandarasi wanasuasua wengine hawana mitambo, wengine hawana nini; akini nikwambie wakandarasi wa nchi hii ni wazalendo na Wabunge ingebidi tuwapigie makofi kuwapongeza. Kwa sababu wanafanya kazi kubwa na wanamadeni mengi sana ambayo hawajalipwa ni lazima tusema tu, tusipowasemea sisi nani atawasemea? Kwa sababu kama leo ndani ya Bunge ripoti inasema zaidi ya kazi ambazo zimefanyika ni zaidi ya bilioni 339 *exchequer* imekuja zaidi ya bilioni 339 lakini barabara tunachojua kwa *TARURA* walishatangaza mpaka asilimia 80 ya barabara zote walikuwa wametangaza ilibaki asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nina uhakika asilimia 80 ya zile barabara zilizotangazwa wakandarasi wako *site* na wanaendelea na kazi lakini kama watu wamefanya kazi kwa asilimia 80 au hawajafikisha bado wanaendelea, wewe pesa uliyoleta ikawafikia na asilimia 12, leo huyo mkandarasi huyo unamlaumu na nini? Wakandarasi wamekopa kwenye mabenki, ni benki gani itakupa pesa kama hurejeshi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na mpango mzuri wa kuja na hiyo *Samia Infrastructure Bond* lakini kama hatutapanga mpango mzuri wa kuwalipa wakandarasi, mimi nakwambia ukweli watashika hizo barabara lakini barabara zitaishia njiani. Sasa tuombe, tuiombe Serikali hasa Wizara ya Fedha yaani leo unapofanya *prioritization* yako wewe ukifanya vipaumbele vyako wewe, huwezi kufanya vipaumbele ukasahau miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wabunge tunaondoka hapa tunarudi majimboni, inabidi turudi tukafanye ziara tuwaambie wananchi ni vitu gani tunarudi navyo, tukakusanye mawazo yao kwa ajili ya Bunge la Bajeti. Unafikaje huko? Kila mwananchi anakwambia barabara haifikiki, ukirudi leo jimboni unaenda kuongea nini? Ukirudi jimboni unaitisha mkutano watu hawawezi kufika, madaraja hamna barabara zote zimeharibika unawaambia nini? Na ukifika hapo, wakandarasi tena wanaodai huwezi kuwaita kwa sababu wao bado wanakudai pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tulikuwa tunaomba Wizara ya Fedha, katika maazimio ambayo tunayo kabla ya Ijumaa tunapoondoka hapa, hili jambo siyo la kusubiria tuje tupewe taarifa mwakani, kwa sababu ni jambo la kibajeti, tulipitisha hapa tukaongezewa milioni 350. Tukaondoka tukaenda majimboni tukawaambia wananchi, Mheshimiwa Rais kaongeza pesa bilioni 350 kwa kila jimbo tulikuwa tunategemea tupate milioni mia tano, mia tano. Tukachagua na barabara za kwenda kujengwa tukasema kwenye mikutano tukimtaja Rais kwa maendeleo haya na pesa aliyoiongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo pesa hiyo bilioni 350 haijaja hata moja, Wabunge hatujaulizwa barabara, tumejaribu kukaa na mameneja wetu tukapanga zikija tutafanya hivi. Tumeenda tumefanya mikutano tukawaambia wananchi, tukachagua na barabara tulizotaka zikajengwe kwa hiyo milioni 500, unarudije leo ukiwa imebaki miezi minne kwa wananchi kuwaambia ile nilikuambia habari njema ya bilioni 350 haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachonganishwa na Mheshimiwa Rais anachonganishwa kama tunafanya hivi, *if that money wasn't*

*there* ingebidi watuambie haipo lakini hatuwezi kuondoka hapa katika Bunge, tumekaa hapa tumepitisha bajeti tunaenda tunawaambia wananchi kuna pesa imeongezeka *yet* mpaka leo hatuambiwi ni barabara gani zinajengwa, hatuambiwi pesa inakuja lini? *This is not fair,* siyo *fair* kwa Mheshimiwa Rais lakini si *fair* kwa wananchi ambao tunawawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikua naomba hili tulione…

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika maazimio ambayo tunataka tuondoke nayo…

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina wazo, nina wazo la kusaidia *TARURA*. Ukijaribu kuangalia barabara nyingi za vijijini zinajengwa kwa upana.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra, kuna taarifa.

Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe taarifa ni sehemu ya mchangiaji lakini pia inatolewa kwa idhini ya kiti, kwa hiyo Mheshimiwa Tarimba taarifa kuwa ufupi.

**TAARIFA**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wake mzuri sana. Nilitaka nimuongezee tu katika mchango wake kwamba kuomba barabara siyo hisani, barabara ina mkono wa moja kwa moja na uchumi wa Nchi hii. Siyo tu kwamba inakwenda kutusaidia sisi majimboni lakini inasaidia uchumi wa Tanzania ilivyo hivyo Serikali haina hiari kusema ipeleke fedha ama isipeleke mathalan Bunge hili lilitangaza na kutoa maamuzi

kwamba fedha ziende basi Serikali ipeleke, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, taarifa ilitakiwa iwe fupi; Mheshimiwa *Engineer* Ezra taarifa unaipokea?

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea hiyo ni nyama kabisa nyongeza nzuri nimeipokea. Sasa nataka nitoe ushauri wa kitaalamu. Barabara zote za nchi hii *especially* upande wa *TARURA* zinajengwa kwa upana wa mita 6.5 hadi mita saba lakini *standard* ya magari katika dunia na utengenezaji; gari dogo kabisa lina upana wa mita 1.8, zile gari kubwa *semi* zina 2*.4 meters.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unajiuliza huko kijijini unajenga barabara ya mita saba, barabara ya mita sita matokeo yake tairi zinakuwa zinapita tu pale katikati ya barabara huku pembeni majani yameota na huku pembeni majani yameota. Umejenga daraja la upana wa mita saba huko kijijini ni la nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka *TARURA* waende kwenye *standard* zinazoendana na mahitaji ya wananchi kule vijijini. Waweke upana wa barabara *4.5 meters* au *five meters* na daraja likiwa vile tutajenga madaraja mengi na barabara zitakuwa ndefu zaidi. Ina maana hii *plan* ya kwenda kufika mbele zaidi itaweza kufikiwa kwa haraka zaidi, kuliko leo unajenga barabara pana baada ya muda majani yameota huku, yameota huku wakati eneo lote lile lililipiwa. Hiyo nayo bado ni hasara ambayo tunaipata. Kwa hiyo wa-*review* ili waweze kuona kwamba twende kwa barabara finyu lakini zinazoweza kwenda mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeomba kwenye hili. Tunachoomba wakati tunamalizia hapa Ijumaa kwenye maazimio ambayo Bunge linaleta hapa tupate majibu ya shilingi bilioni 350 za nyongeza na tupate majibu ya fedha yetu ya bajeti hii ambayo imeenda asilimia 12. Hizi fedha zinatolewa lini na hiyo iwe ndani ya maazimio ya Bunge Serikali itujibu hapa siku ya Ijumaa wakati Bunge linahitimishwa ili tunaporudi majimboni

tukawaambie wananchi nini kinafanyika kwa habari ya barabara kabla ya mwezi wa saba.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana; Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi. Mimi niseme mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya TAMISEMI na ningependa kuchangia pale alipoishia Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wakati anawasilisha taarifa yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama nchi tuna changamoto kubwa sasa hivi tunayoipitia. Tuna janga na si changamoto, ni janga kubwa sana la uharibifu mkubwa wa miundombinu. Hapa hatupepesi macho, changamoto ni kwamba watu wanaohusika na kutengeneza barabara hawajapelekewa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tuko hapa Wabunge tunashauri, kwenye Kamati tulimwita Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa nini barabara hazitengenezwi? Changamoto ni fedha, wenyewe wameshafanya tathmini wanataka shilingi bilioni 131 kuweza kukabiliana na changamoto ya barabara zilizoharibika na miundombinu yote ya barabara nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayetoa fedha ni Hazina, hapa hayupo Waziri wa Fedha, hakuna Naibu Waziri wa Fedha tutapata wapi haya majibu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi wametoa shilingi bilioni 21 tu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, Serikali ipo Bungeni kwa hiyo usiwe na wasiwasi endelea kuchangia. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilishauri kwenye Kamati aitwe Waziri wa Fedha atuambie tunapata wapi shilingi bilioni 131 kwa ajili ya kutengeneza barabara za nchi hii? Hakuja kwenye Kamati. Nikawa namsubiri nije nimwambie Bungeni, hayupo; sasa nitaenda kumwambia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kitokee nini ili tujue kwamba kuna dharura? Madaraja yameshakatika, barabara zina mashimo, ajali zimetokea. Juzi Shinyanga pale kwangu Mto Mumbu, mtu amesombwa na maji na mafuriko, amekufa. Tunataka kitokee nini ili tujue kwamba jamani tuko kwenye hali ya dharura? Mheshimiwa Aida anasema kwake Nkasi watu wameshakufa kule, Dar es Salaam watu wanakufa; tunataka kitokee nini? Kazi ya Serikali ni kuwahudumia wananchi na kuhakikisha wako salama. Nchi ipo kwenye janga, iko kwenye changamoto, shilingi bilioni 131 zinatakiwa… *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** …mpaka sasa hivi wamepeleka shilingi bilioni 21 tu kwa ajili ya kwenda kutatua hali ya dharura.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ninatambua mchango mzuri wa Mheshimiwa Salome Makamba. Naomba tu nimpe taarifa kwamba kazi ya utengenezaji wa barabara zilizoharibika katika maeneo mbalimbali kutokana na mvua zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi yake kwa mfano Dar es Salaam; Kibamba wamepata, Kawe wamepata na maeneo mbalimbali wamepata. Kwa hiyo nimhakikishie tu kwamba pamoja na kwamba kuna uharibifu mkubwa lakini Serikali haijalala inaendelea kufanya matengenezo ya barabara hizo na hali itakwenda vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana; Mheshimiwa Salome taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi naomba utulie tu nikusaidie kwa sababu tuna changamoto. Nina ripoti ya Mheshimiwa Waziri hapa kuja kwenye Kamati anasema, tathmini imefanyika nchi nzima, halmashauri 184 hali ya uharibifu ili tuweze kurekebisha hiyo hali inatakiwa shilingi bilioni 131. Mpaka sasa hivi Serikali imepeleka shilingi bilioni 21 *out of 131* unasema nchi kazi inaendelea au ndio hao wakandarasi wazawa mnawakopa hela wanafanya kazi wanaendelea kufilisika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *we have a serious problem* sisi kama nchi na tukifanya maigizo *well and good,* lakini kama jambo limeshatishia uhai wa wananchi, kama jambo limeshatishia usalama wa nchi, kama jambo linatingisha uchumi wa nchi hakuna muujiza. Yaani ni kwamba tukirudi hapa bajeti ijayo mtakusanyaje hizo fedha kwa ajili ya kutengeneza bajeti? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Patrobass Katambi.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Mbunge; ni kweli kwamba Watanzania wanapata changamoto kutokana na majanga ambayo yanaendelea. Uhalisia ni kwamba *TMA (Tanzania Meteorological Agency)* ilitangaza uwepo wa mvua za *El Nino,* na uwepo wa mvua hizi umesababisha majanga makubwa karibia nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika fedha iliyokuwa imetengwa ya bajeti ambayo ilikuwa ni kwa ajili ya dharura tume-*burst,* kufikia hatua kwamba fedha zile hazitoshi tena kulingana na uharibifu mkubwa ambao umetokea. Kwa hiyo taarifa yangu ni kwamba Mheshimiwa Mbunge ajue kwenye mazingira ya dharura kuna vitu vinaitwa *natural catastrophes* ambazo ni majanga asilia ambayo hakuna mtu yeyote alipanga mvua za *El Nino* zitokee. Ikitokea majanga kama hayo nchi yoyote inaweka utaratibu wa kuhakikisha inakabiliana nayo. Kwa hiyo ni majanga wala siyo kwamba ni Mpango wa Serikali inapanga hivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana; Mheshimiwa Salome taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hiyo taarifa siipokei, nataka tu nimsaidie kaka yangu pale, Mheshimiwa Katambi. Bajeti iliyopita kwenye *TARURA* waliomba wapewe 1.6 *trillion,* wakapewa shilingi bilioni 800 na ushee tukatenga. Akaja Waziri wa Fedha akatulaghai kwamba anaiongezea *TARURA* shilingi bilioni 350. *As I speak right now* wakili msomi wamepewa shilingi bilioni 89 tu. Ile 800 hawajapewa, tuliyodanganywa hapa wameongezewa 350 hawajapewa, hiyo

hela unayosema inaenda kufanya mambo ya *natural catastrophes* haifiki hata asilimia 10 ya *target* ambayo tunayo. Sasa si tunafanya mzaha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuchukulie jambo la miundombinu ya barabara kwa udharura wake. Kamati ya Miundombinu, Kamati ya TAMISEMI, Kamati ya Bajeti na Kamati ya Fedha ni lazima tukae tuje na msimamo wa Bunge. Nini kifanyike kutatua changamoto ya barabara kwenye hii Nchi? Watu wameshakufa, ajali zimeshatokea, uchumi umeshatetereka inatosha kulifanya jambo hili kuwa ni jambo la dharura na kuchukuliwa kwa uzito wake. Sisi kama Bunge tuishauri Serikali juu ya jambo hili, *unless otherwise* sisi tutaonekana tumeshindwa kuishauri Serikali katika jambo hili la dharura, tutaonekana tumeshindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwa wakandarasi wazawa. Mheshimiwa Waziri amekuja na wazo zuri sana la *TARURA Samia Bond,* lakini nikwambie tu changamoto siyo *bond,* changamoto ni sheria mbovu ambazo zinawabana wakandarasi wetu wanashindwa kufanya kazi za Serikali. Leo mkandarasi atapata kazi ya kujenga barabara anaambiwa nenda kalete *bank guarantee,* anaambiwa nenda kalete sijui nini ya benki. Yaani kabla hajaanza kujenga Barabara asilimia 80 ya fedha zake ameenda kuziweka kama *bond* benki ili aweze kupata *guarantee* akafanye hiyo kazi; atafanyaje kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naelewa miradi mingi hasa inayotekelezwa kwa fedha za wahisani inakuja na masharti magumu lakini *you scratch my back I scratch yours.* Kama wanataka kutupa misaada watupe misaada ambayo inatufaa na inayowanufaisha wakandarasi wetu wazawa. Ni lazima tufanye mapitio ya sheria kuhakikisha Watanzania wananufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachi zote zinazoendelea duniani mtaji wao namba moja ni *population* yao. *Population* ya Watanzania tumefika milioni 60 na kitu. Tukiwawezesha wakandarasi wazawa angalau watano tu (makampuni matano

kwenye kila mkoa) lazima tutoboe, yaani lazima tufanikiwe. Hakuna muujiza kwenye hilo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salome, muda wako umekwisha.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana; Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona na kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Awali ya yote na mimi niunge mkono maazimio yote yaliyowasilishwa hapa na Wenyeviti kwani ni maazimio yaliyolenga kuiboresha na kuisimamia Serikali yetu vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishie hapo alipoishia dada yangu Mheshimiwa Salome Makamba, kipengele hiki cha *TARURA*. Kwanza niwape pole ma-*engineer* wetu nchi nzima. Wataalamu wetu hawa wako tayari kufanya kazi na wanaipenda kazi yao vizuri sana; na namna unavyoona mnavyoongozana nao mnapokagua matatizo unaona nyuso zao zinavyoumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ni kubwa sana kwenye maeneo yetu. Shida hii si mvua tu hizi, yapo maeneo yana mvua karibu msimu mzima wa mwaka. Kwa hiyo maeneo haya yana uharibifu kwa muda mrefu, na ma-*engineer* wetu hawa mara kadhaa wanaandika maandiko kupeleka *TARURA* makao makuu ili wapate fedha kunusuru hali iliyopo kwenye maeneo yetu huku lakini kwa bahati mbaya sana fedha hizo hazitoki, na kama zinatoka zinatoka kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii inatupa wakati mgumu sana sisi Wabunge kwa sababu ni ukweli kabisa tunakaa hapa ndani, tunapitisha bajeti na tunapata ahadi nzuri nzuri lakini utekelezaji unakuwa haupo kabisa. Jambo hili si zuri kwa sababu

baada ya vikao hivi sisi Wabunge tunaenda kuwaambia wananchi kule ni nini kinakuja kutekelezwa. Hatimaye bajeti ya mwaka inaisha hali ya barabara zetu inabaki vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niombe maazimio haya ya Bunge sisi kama Wabunge tunapaswa tuyasimamie kweli kweli pasipo kuoneana aibu, pasipo kuona nani ataniona mimi nasema nini. Lazima tuisimamie Serikali yetu kwa sababu ni Serikali yetu hii. Hakuna mtu mwingine atakayekuja kuisimamia na kuisemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme kama walivyyosema wenzangu, suala la *TARURA* kupata fedha lisiwe suala la kusema kwamba sasa ni shukrani, Hapana, ni wajibu wa Serikali. Taasisi hii tumeiunda wenyewe kwa sababu tunataka itusaidie, tuipe fedha ifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano kwenye Jimbo langu la Mbinga Vijijini. Jimbo hili lina mvua nyingi sana, Jimbo hili lina madaraja mengi sana. Nishukuru kwa awamu hii kidogo barabara zinapitika kwa sababu madaraja yamejengwa. Lakini uko ukanda mmoja bado barabara hazipitiki, mvua ikinyesha tu ujue simu kwako. Mbunge huku kuna shida hii, Mbunge hatupiti. Sasa unashindwa kuelewa hii hali itaenda hadi lini? Ifike sehemu, taasisi yetu hii ni kubwa sana, tuipe fedha. Najua uwezo wa kutekeleza na kutatua matatizo yetu wanayo. Kwa hiyo niombe sana fedha tunazotenga hapa Serikali izipeleke kama zilivyopitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo nataka kuiongelea ni namna tunavyotatua migogoro. Nchi yetu imepangwa vizuri sana; tunaanza kwa mwenyekiti wa kijiji, tunakwenda kata, tunakwenda wilaya, tunaenda mkoa na mpaka huko Wizarani. Maeneo haya yote yalivyotengwa maana yake yana uwezo wa kutatua migogoro. Hata hivyo inashangaza sana, hii migogoro mingine ni ya kawaida sana, lakini wenzetu waliopo kwenye maeneo haya kama walivyoaminiwa hawatatui migogoro hii. Wanasubiri mpaka mtu mwingine atoke huko juu anakuja kutatua ule mgogoro ambao sasa unasababisha mpaka matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro kwangu kule, maarufu unaitwa “ndika.” Nimeuzungumza hapa mara nyingi sana, ni mgogoro wa ardhi. Mgogoro huu chanzo chake ilikuwa panda miti kibiashara. Pale tuna Mkuu wa Wilaya amehangaika sana kuutatua huu mgogoro sana, ukaja haujaisha. Umefika ngazi ya mkoa haujaisha. Lakini cha kushukuru hivi karibuni Mwenyekiti wetu wa Chama aliingia kati tukaenda mimi, yeye Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya tukaumaliza huu mgogoro. Tukaumaliza kwa kusema wananchi warudishiwe maeneo yao wawe tayari kupanda miti hiyo ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni wako viongozi wamerudi, wananchi wale wamejipanga kupanda miti kibiashara, viongozi wale wanaenda wanapiga danadana tena ule mgogoro uanze upya. Sasa wewe kiongozi uko hapa umewekwa kufanya nini? Umewekwa ili uendelee kusumbua hao wananchi? Kwa nini usimalize huu mgogoro ambao Mwenyekiti wa Chama wa Mkoa amesema uishe na tumekubaliana wananchi warudishiwe maeneo yao; kwa nini sasa leo hii wewe pekeyako unasumbua wananchi unaleta danadana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo halikubaliki, halikubaliki kabisa. Viongozi hawa waliopewa dhamana na Serikali ni wajibu wao kumaliza migogoro kwenye maeneo yao. Wasimsubiri Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi aende akamalize migogoro kule, wao wana nafasi zao pale. Wamepewa dhamana na Serikali hii, wamepewa dhamana na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia kumaliza ile migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili jambo kwangu linanisikitisha sana. Ilifika mahali hawa wananchi wako zaidi ya 400 wanasema tunataka kurudisha kadi, tunataka kurudisha kadi za CCM kwa sababu Chama hiki hakitusikilizi. Sasa tumeenda tumewasikiliza, yuko kiongozi mmoja analeta danadana anasema hapana, wasirudishiwe maeneo yao wapewe maeneo mengine. Sasa kwa nini yuko pale? Kwa nini aseme hivi? Kwa nini hakusema wakati tuko pamoja pale? Amesubiri watu tumewaaminisha wananchi kwamba maeneo yenu mnapewa halafu sisi tunaondoka yeye anageuza Kiswahili kule, anamuongopea nani? Nani anayemuongopea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halikubaliki na ninalisema leo hapa tukirudi huko lazima tutagombana sana, lazima tutagombana kwa sababu hatutaki kuwa waswahili kiasi hicho. Mgogoro umeonekana wananchi wamechukuliwa maeneo yao si maeneo ya mtu mwingine yaani shamba langu mimi amepewa mtu mwingine. Sasa kwa nini unapata kigugumizi kunirudishia shamba langu? Kwa hiyo hawa viongozi kwa sababu wamepangwa kiutaratibu watimize wajibu wao, wasisubiri watu kuja kuwafanyia kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumzie hapa ni suala la ujenzi wa vituo vya afya. Nashukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa sababu kwa upande wa jimbo langu mimi mpaka tunaingia awamu ya sita hatukuwa na kituo cha afya, lakini leo hii nashukuru sana, sana, sana, tuna vituo vya afya tulivyovikamilisha vitano. Viko vituo vya afya vile vya tozo viwili lakini tuna vituo vingine tumejenga kupitia mapato ya ndani vitatu tayari tumevikamilisha lakini uhitaji bado ni mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhitaji ni mkubwa kwa sababu Jimbo lile limetawanyika sana lina kata kubwa 29; kwa hiyo kwa vituo vya afya ni vichache sana. Nishukuru kwa mpango wa Mheshimiwa Rais kwa ahadi ile aliyotupa kwamba kila jimbo litapewa kituo cha afya kimoja. Lakini hapa nataka tu kutoa tahadhari kidogo kwamba yako majimbo yana ukubwa tofauti tofauti. Yako majimbo madogo pengine vituo vilivyopo sasa hivi vimeshatosheleza. Hii kauli ya ujumla ya kwamba kila jimbo linaenda kupewa kituo kimoja kimoja pengine tungeitazama kwa jicho jingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kabisa tunaweza kurundika sasa vituo vya afya kijiji kwa kijiji kwenye hayo majimbo mengine. Kwa hiyo ningeomba hapa, na ninapendekeza, wazo kama hilo kwenye majimbo yale makubwa makubwa basi tupeleke hata vituo vya afya viwili badala ya kituo cha afya kimoja. Vivyo hivyo hata pamoja na zile shule za *SEQUIP* yako majimbo sasa hivi wala hawana shida ya shule hizo tayari wameshajitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ushauri wangu katika maeneo kama hayo; kwa mfano kwa jimbo langu mimi tayari kuna kata tatu hazina shule za sekondari. Wananchi hawa wanakwenda kilometa nyingi sana kupata elimu. Kwa hiyo pengine maeneo kama haya najua kwa namna ilivyo yako majimbo yanayofanana na jimbo langu mimi…

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapinga, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa; Mheshimiwa Jackson Kiswaga, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Mheshimiwa Kapinga ni rafiki yangu naomba nimshauri akazane kuomba kwenye jimbo lake asitaje majimbo ya wengine na sisi tuna mahitaji yetu. Akazane kuomba vituo vingi kwake aache na sisi wengine tuendelee na ya kwetu, ni taarifa tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapinga, taarifa unaipokea? Malizia mchango wako.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuipokea taarifa kwa sababu hafanyi utafiti yule. Hafanyi utafiti kwa sababu nilivyomwambia yako majimbo makubwa makubwa. Jimbo lake ni dogo kweli kweli sasa unaipeleka tena shule pale inaenda kufanya nini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Malizia mchango wako.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jimbo langu mimi ni kubwa ndiyo maana nimesema hapa sasa hivi nakosa shule tatu, yeye kwake zote zimetimia. Kwa hiyo Jimbo kama la Kalenga zile shule zinazopaswa kupelekwa kule zirudi kwenye jimbo la mimi. *(Makofi/ Vicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ombi langu lilikuwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia, muda wako umeisha.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu lilikuwa hasa kwenye upande huu wa vituo vya afya na shule tuangalie ukubwa wa maeneo halafu tuvigawe hivyo vituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana na ahsante sana Waheshimiwa Wabunge mliopata nafasi ya kutoa michango yenu tunawapongeza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mchana tutaendelea na mjadala; ataanza Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mheshimiwa Boniphace Butondo, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile na orodha itaendelea jinsi muda unavyokwenda.

Baada ya tangazo hilo fupi nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 07:01 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. ASIA P. MINJA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023 na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

Tunaanza na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia mada iliyopo mezani. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetupa wasaa huu wa kuweza kupata fursa ya kujadili taarifa hii kwa manufaa ya Watanzania wote. Nachukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa pamoja na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI nielezee tu kidogo kwamba Kamati ya TAMISEMI na TAMISEMI kwa ujumla pamoja na Utawala Bora kwa maana ya Utumishi na Utawala Bora ni Kamati muhimu sana pia ni Wizara muhimu sana kwa sababu inahudumia nchi nzima, nizungumzie tu kwamba jukumu hili la TAMISEMI limekuwa na mzigo mkubwa sana na mahitaji makubwa kama nchi, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali na Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na *TARURA;* Wakati tunaunda chombo hiki cha *TARURA* nilikuwepo Bungeni, kilikuwa chombo ambacho hatukukiamini kwamba kitafanya kazi kubwa sana kama kinavyofanya sasa kwenye majimbo yetu yote hapa nchini. *TARURA* ina kazi kubwa, tumeongeza mtandao wa barabara kwenda zaidi kwa wananchi na katika maeneo ambayo ni muhimu sana. Imekuwa kichocheo kikubwa sana kwenye shughuli za kijamii kwa maana ya miundombinu ya barabara ambayo *TARURA* inahudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumshukuru Mungu kwa kutujaalia mvua mwaka huu, Mikoa kadhaa tumepata mvua kubwa sana ukiwemo Mkoa wa Manyara lakini hali ya barabara ni mbaya sana. Naungana na wenzangu wote, Serikali itakapokuja kutupa mrejesho, kwanza itupe kauli ya kupata zile fedha ambazo tayari tulishaomba kwenye bajeti iliyopita pamoja na nyongeza ya fedha shilingi bilioni zaidi ya 300 ili kuweza kurekebisha hali mbaya ya miundombinu iliyotokea kwenye Majimbo yetu, hasa mkoa wa Manyara umeathirika sana mtandao wa barabara kwa sababu mvua imenyesha zaidi ya miezi minne na hadi sasa inanyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Watendaji na Watumishi unakuta wako wachache sana. Eneo hili litazamwe upya tuongezewe fedha, tunaiomba sana Serikali kwa sababu barabara tulizoongeza zinahitaji kufanyiwa matengenezo lakini nyingine zimeathirika na madaraja na miundombinu nyingine kwa ajili ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue tena nafasi hii kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati niongezee eneo la Madiwani, mimi ni Diwani nimetumikia miaka 10, baadae nimekuja sasa hivi ni miaka nane nikiwa Mbunge. Hali ya Madiwani wetu wetu ni mbaya sana kote nchini. Diwani ambaye alikuwa anapewa posho ya shilingi 65,000 mara mbili sasa hivi anapewa shilingi 80,000 kwa maana 40,000 mara mbili. Diwani aliyekuwa anapokea miaka 12 iliyopita 350,000 mpaka leo, hali hii inatisha sana na kwamba viongozi hawa kwa ngazi yao wamesahaulika sana. Tunaiomba Serikali itazame katika bajeti inayokuja ije na mpango mpya wa kuwaongezea fedha au wa kuwaongezea malipo ili kunusuru kada hizi ili tusiwe na tabaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wenyeviti wa Vijiji, mimi Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, yaliletwa majibu mwaka huu kwa swali langu langu la msingi likijibu shilingi bilioni 220 zimetengwa kwa ajili ya kuwahudumia kundi hili la wenyeviti wa vijiji, mitaa na vitongoji kote nchini lakini hadi hivi tunavyoongea Halmashauri chache zenye uwezo ndizo zinazolipa wenyeviti wa vijiji na vitongoji na mitaa kwa ajili ya uwezo wao wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Halmashauri nchini hatuwezi kulipa hata ingekuwa miaka kumi, moja ni Halmashauri ya Mji wa Mbulu, mapato yake ni madogo. Hali hii ya ngazi au tabaka fulani inalipa wenyeviti wake na tabaka fulani haliwalipi inaweka tabaka na chuki kwa viongozi hao wa ngazi za chini. Yeyote ajae akija kule kwenye vijiji na kwenye ziara awe Rais, awe Waziri au awe nani Mwenyeviti wa Kijiji, Kitongoji na Mtaa wanahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zozote zinazotolewa iwe ni miradi ya maendeleo viongozi hao wameteseka wamefanya kazi kwa jinsi walivyoweza, tunasema ni kazi ya kujitolea lakini walau kwenye bajeti inayokuja Serikali yetu sikivu ije na utaratibu wa kuja walau na mpango wa kuwapa posho. Tumejitahidi mambo mengi sana makubwa hili nalo linawezekana panapokuwa na nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la walimu. Tunaipongeza sana Serikali tumejenga shule mpya nyingi sana nchini, shule mpya na madarasa. Moja kwa moja hali hii inachochea uhitaji wa walimu wapya na nyumba za walimu. Hili la walimu wapya tukilinganisha na ajira za miaka iliyopita kundi hili la walimu hatutapata watumishi kwa vyovyote vile na hawataweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yao pia ni mabaya sana. Makazi ya walimu nchini, hali ni mbaya sana kundi hili la walimu, sote tiulioko hapa uwe mtu wa kusoma na kuandika na kuhesabu, uwe mtu wa *PhD,* uwe mtu wa taaluma gani na uwe na shahada mwalimu ndiye aliyekuwa tanuri lako na alikuwa tanuri letu. Naiomba sana Serikali iangalie eneo hili la nyumba za walimu pamoja na maslahi ikiwezekana na ruzuku ya ufundishaji iwepo. Pia, namna ambavyo nyumba zitajengwa na taasisi hizo zinazojenga kwa maana ya *TBA, National Housing* pia Watumishi *Housing* kwenye maeneo ambayo yana changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu anatoka kilomita tano mvua inanyesha anakwenda kufundisha, anarudi nyumbani kupata chai ya asubuhi, baadaye chakula cha mchana, baadaye kurudi shuleni na hatimaye kwenda, mshahara wake ukiufanyia mahesabu unaishia kwenye gharama za kutembea,

kupata huduma pia na maeneo wanayoishi. Hali ya watumishi wetu hawa imekuwa mbaya sana na wao lazima tuwasemee Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Mheshimiwa Rais, alipokuwa Mwanza aliwaunganisha na Waziri wa TAMISEMI akawaahidi ujenzi wa nyumba za Walimu nasi tujiongeze zaidi ya eneo hilo la ahadi ya Mheshimiwa Rais. Taasisi hizi tuzihamasishe kwa maana ya *TBA, National Housing* pia Watumishi *Housing Cooperation* kwa sababu hawa wana fursa ya kujenga jengo na kumkopesha mwalimu na akakatwa muda wote wa utumishi wake akagawiwa kwenye miezi nyumba hiyo mwisho wa siku ikawa ya kwake. Hilo linawezekana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutazame hali ambayo wanakabiliana nayo wanayo madai mengi. Serikali itazame upya, tunaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ililipa madeni mengi, kwanza tuyazuie yasizalishwe mengi lakini pia yale yaliyokwisha kuwepo yaweze kufanyiwa kazi na kulipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mfumo wa ukusanyaji wa mapato ambao siyo mzuri. Serikali itazame upya, tumehama kwenye mfumo tumekuja kupata mashine za kukusanya fedha hizi *POS*. Hizi *POS* zimekuwa na tatizo la ukusanyaji wa mapato. Haiwezekani mashine zinatolewa na ofisi ya Mkurugenzi halafu kesho tunakuta nyingine ni *fake* haziingizi hela kwenye mfumo ama zinachezewa na watumishi bila hatua zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hii hali ya kuwahamisha hamisha watumishi ambao wana dosari zao Serikali iangalie upya kutokuwahamisha iwaondoe kabisa. Hii itasaidia watu kuwa na nidhamu katika kutumikia nafasi zao pia kwa namna ambavyo wanaweza wakawa waadilifu katika utumishi wao wa umma, pia kutokuongeza matatizo kwenye maeneo mengine ambayo yalikuwa yanafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Utawala Bora, tunamshanga sana Mheshimiwa Makonda Katibu Mwenezi wa Itikadi anapofanya ziara. Yale mafuriko, mafaili, mabango na nyaraka zinazopelekwa kwenye ziara za Katibu wa Itikadi na

Uenezi ni dhahiri kuwa ni picha ya wazi tuna kazi ya kutazama upya mfumo mzima wa Utawala Bora katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kiongozi mkubwa anakuja mabango yanaletwa 1,000 kila anakoenda hawezi kufika mahali anakuta ni watu wengi wanajitokeza kutaka ufumbuzi wa matatizo yao.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili muhimu sana litazamwe upya kwa namna inayowezekana ili tuwezeze kufanyia kazi kama Serikali na wananchi wetu waweze kuona umuhimu wa Utawala Bora katika nchi yao na huduma bora lakini pia…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, mengine nitaandika kwa maandishi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana; nilimtaja Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta ajiandae.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia taarifa za Kamati zetu hizi mbili, Kamati ya TAMISEMI pamoja na Kamati ya Utawala Katiba na Sheria. Niende moja kwa moja kwenye kuchangia kwa sababu muda wetu ni mdogo, nitachangia mambo mawili, kwanza ni Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na la pili nitachangia linalogusa pia TAMISEMI juu ya kugawa maeneo ya utawala wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuifanya sasa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ifanye kazi pande zote za Muungano (Tanzania Bara na Zanzibar), kwa mujibu wa marekebisho ya Sheria yake Namba 8 ya Mwaka 2006

inaifanya sasa Tume hii iweze kufanya kazi maeneo yote mawili ya Muungano au ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii ya Haki za Binadamu iko Kikatiba na kwenye Katiba ukurasa wa 108 na 109 majukumu ya Tume hii yametajwa yako mengi na mimi niyataje machache. Moja, ni kufanya shughuli za kupokea malalamiko ya uvunjaji wa haki za binadamu. Jingine ni kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Jingine ni kama ikibidi kufungua mashauri Mahakamani ili kuzuia vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu na jingine ni kuchunguza mienedo ya mtu yeyote anaehusika au taasisi yeyote inayohusika na masharti ya Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu haya ukiyaangalia ni majukumu makubwa, majukumu mazito na ni majukumu yenye upana wake. Ukiangalia nchi yetu kwa kuiangalia Tanzania Bara na Zanzibar nayo ni kubwa sana. Sasa kwa majukumu haya ambayo Tume hii imepewa napata shida kuona utendaji kazi wao kama unaridhisha ili wananchi waweze kufikiwa na Tume hii ya Haki za Binadamu. Kusema ukweli ufikiaji au utendaji kazi wa Tume hii hauwapati wanachi wetu kwa ujumla wake. Moja, ni kwa sababu Tume hii ina Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti na Makamishna na Wasaidizi wa Makamishna halafu wako Dodoma Makao Makuu ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watumishi kwanza ni wachache lakini pia hawapo kwenye Mikoa na Wilaya zetu. Sasa kama wako Dodoma haya malalamiko yaliyosemwa kwenye majukumu yao wanayapata kwa njia ipi. Kama wanayapata wanawezaje kuwafikia hao wanaolalamika kuzingatia uchache walionao na vifaa wanavyovitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kweli nataka kuishauri Serikali kwamba kama tumekubali kuwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora basi Tume hii iwezeshwe kwa namna ya watumishi tuwe na watumishi mpaka kwenye Mikoa au Wilaya ili wananchi wetu wanapopatwa na madhila yanayohusiana na kuvunja kwa haki za binadamu wawe na mahali ambapo wanaweza kupeleka pa karibu zaidi, kuliko

mwananchi kutokea Wilayani kwangu kule Maswa alete hoja yake hapa Dodoma, sasa nashindwa kuelewa itatatuliwa saa ngapi, malalamiko hayo yatatuliwa saa ngapi, shida hizo zitatatuliwa saa ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani *assumption* iliyokuwepo tulipokuwa tunaweka Tume hii ni kwamba Tume hii labda inahusika na viongozi tu lakini kuvunjwa kwa haki za binadamu hakufanywi na viongozi peke yao hata raia wanavunja haki za binadamu. Pia mambo mengine yanatokea kule kwenye maeneo yetu ambako hakuwezi kuonekana kwa urahisi. Kama Tume hii ingejulikana ipo na inafanya kazi kushughulikia matatizo haya, malalamiko hasa ya uvunjaji wa haki za binadamu, Tume hii ingeweza kupunguza sana kitu ambacho mwenzangu aliyenitangulia amesema malalamiko ya wananchi ambayo viongozi wetu wanakutana nayo wanapokuwa wanafanya mikutano yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwamba Tume hii kwanza iongezewe watumishi, Watumishi wake wasifanye kazi kutokea Dodoma peke yake waende Mikoani na Wilayani, pia waongezewe rasilimali fedha. Rasilimali fedha kama haijaongezwa hawawezi kufika huko kwenye maeneo yetu. Jambo la tatu miundombinu kama majengo na vifaa vya TEHAMA viweze kupatikana kwa Tume hii ili waweze kufanya kazi yao vizuri na kuwahudumia wananchi wetu vinginevyo kwa rasilimali chache na kwa uchache wa watumishi waliopo hii Tume itabakia kwenye Katiba na itabakia kwenye maandishi yetu lakini utendaji kazi wao hatuwezi kuuona kama wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende suala la pili la kugawa maeneo ya utawala wa nchi yetu. Naelewa kwa sababu suala hili limekuwa likizungumzwa hapa na Waheshimiwa Wabunge kwa njia ya maswali ya nyongeza na Serikali imekuwa ikijibu hapa kwamba pengine upatikanaji wa fedha utakapokuwepo suala linaweza likatazamwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni kubwa. Nchi yetu sisi ni kubwa kiasi kwamba unaweza ukajumlisha nchi nne za Afrika Mashariki Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi, bado hujapata

eneo la ukubwa wa nchi yetu. Sasa nchi yetu kwa sababu ni kubwa mimi sihesabu kama ni balaa kwa nchi yetu kuwa kubwa, tuhesabu kama ni fursa! Siyo kosa kosa nchi yetu kuwa kubwa. Inavyoelekea ni kwamba tunaona sasa kama ni tatizo, mimi sioni kama ni tatizo, ni fursa na tukijielekeza vizuri bado tunaweza kufanya nchi yetu ikatawalika vizuri na suala la utawala bora na lenyewe likaenda sawa sawa lakini kwa kugawa maeneo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kugawa maeneo ya nchi yetu, wilaya kubwa kama Kilosa ambayo ni zaidi ya Mkoa wa Kilimanjaro, wilaya kubwa kama ya Maswa yenye *square kilometers* zaidi ya 3,000, ni kubwa; sasa maeneo kama haya kuyahudumia kwa watu walioko kule ni shida sana. Ni tabu sana kwa Mkuu wangu wa Wilaya, Mkurugenzi na watumishi wengine waliopelekwa na Serikali kule kuhudumia eneo kubwa lililo pana namna hii, haya maeneo yagawiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunashindwa kuyagawa, basi kwa neno lile la Tawala za Mkoa, kwa kuwa na mkoa au kuwa na wilaya ili tuwe na *DC*, basi tugawe kwa upande huu wa pili, Serikali za Mitaa. Tugawe ziwe halmashauri mbili na maeneo ya vijiji yale makubwa ambayo yanafanana na kata na yenyewe yagawiwe angalau tuwe na halmashauri mbili kwenye eneo la halmashauri moja ambayo ni kubwa na vijiji au kata. Kwa sababu utakuta kata nyingine ni sawa na tarafa kabisa, lakini imeachwa kuwa kata moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tugawe halmashauri, tugawe kata na vijiji. Haya maeneo yakigawiwa, ndiyo maeneo muhimu kwa wananchi wetu kufikishiwa huduma kule kwa ukaribu sana. Tunaweza kufikiria kugawa kuwa na Mkuu wa Mkoa na kuwa na Mkuu wa Wilaya baadaye lakini kuwa na Mkurugenzi na kuwa na Mtendaji wa Kata, kuwa na Mtendaji wa Kijiji ni suala ambalo tunaweza kulifikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kufanya hata kwa awamu kuliko tukiacha maeneo kama yalivyo. Maeneo mengine hayafikiwi kabisa na huduma za Umma, hayafikiwi kabisa na watumishi wa Serikali kwa sababu ya ukubwa wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tumekuwa tukilalamika hapa kwamba rasilimali fedha zinazoenda kule labda hazisimamiwi vizuri, lakini tatizo mojawapo ni ukubwa wa haya maeneo. Tunapeleka miradi mingi. Kwa mfano, mradi uliopelekwa kijiji changu kimoja kinaitwa Mwandu, kilomita 120 kutoka Makao Makuu ya Wilaya, sasa huyu *DC* na Mkurugenzi, Afisa Elimu, Afisa Kilimo atafika saa ngapi kule na kusimamia kazi ya mradi au pesa zilizopelekwa kule ukizingatia pia vifaa kama magari na pikipiki na vyenyewe bado ni pungufu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya maeneo tukiyagawa itakuwa ni karibu kuyahudumia, mtu anaweza kwenda hata kwa pikipiki bila matatizo yoyote. Mtu anaweza akaenda hata kwa *pick-up* bila shida yoyote, mgongo usimuume kwa sababu mwendo atakaoenda ni mfupi. Kama maeneo yatabaki makubwa namna hii, bado watumishi wataendelea kupata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri wa kuyagawa haya maeneo, itarahisisha usimamizi wa shughuli na miradi ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mashimba Ndaki, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa fikra alizonazo Mheshimiwa Ndaki ya kupendekeza kuyagawa haya maeneo zaidi, lakini naomba kumpa taarifa zaidi kwamba mpaka mwaka 2012 Mkoa wa Shinyanga ulikuwa unaibeba Mkoa karibu wote wa Simiyu. Serikali kwa kutambua hayo, iliweza kuugawa Mkoa wa Shinyanga na baadhi ya Wilaya za Shinyanga zilizokuwa tatu zikagawanyika tukapata halmashauri sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri atambue kwamba juhudi zimekuwa zikifanyika, lakini haitakuwa na tija sana iwapo utagawa bado ukashindwa kuweka miundombinu stahiki kuiwezesha Serikali kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumpa hiyo taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante; Mheshimiwa Ndaki taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa sehemu; natambua Mkoa wangu wa Simiyu ulimegwa kutoka Mkoa wa Shinyanga mwaka 2012, lakini hiyo haizuii kugawa wilaya kubwa kuwa halmashauri mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na wilaya kubwa kama ya Maswa, anaifahamu Mheshimiwa Sagini, kubwa, lakini ni halmashauri moja. Huyu Mkurugenzi atatoka damu kifuani kufuatilia miradi kwenye kata zake 36 na vijiji karibu 140 kwenye wilaya hiyo. Tutampa shida bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba hapa ni kwamba, sawa Serikali imefanya juhudi kubwa, lakini bado tunahitaji kuyagawa haya maeneo hata kama ni kwa awamu. Mwaka huu basi halmashauri hizi kubwa tuzigawe ziwe halmashauri mbili. Halmashauri tano kubwa tuzigawe, halmashauri tano nyingine mwaka unaofuata tuzigawe…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, na Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, ajiandae.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili mradi nami niweze kutoa mchango wangu. Kwanza naomba kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara tano ambazo Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria zimekuwa zikitoa taarifa ama tumekuwa tukifanya nazo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya mambo makubwa ambayo wamekuwa wakifanya na katika kipindi hiki wamefanya mambo makubwa sana ni kutoa taarifa njema na hasa katika utekelezaji wa maagizo mbalimbali ambayo katika kipindi cha mwaka mzima uliopita kwa sehemu kubwa sana yameweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni moja kati ya Wizara ambazo ziko chini ya Kamati yetu ya kudumu chini ya Dkt. Mhagama. Vile vile Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na pia Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Mipango, na hii chini ya Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Mheshimiwa Nderiananga wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana katika kusimamia mambo mbalimbali katika Wizara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna Wizara ile ya Katiba na Sheria, unaweza ukaona ni majukumu makubwa ambayo Kamati imekuwa ikifanya wakati wote, lakini tunashukuru kwamba uwezeshwaji wa Bunge kwa maana ya Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake sawa sawa, na mambo mbalimbali, hata ya Miswada mmekuwa mkishuhudia kwamba Kamati imekuwa ikitekeleza wajibu wake vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuanza na upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, yako majukumu makubwa ambayo yamekuwa yanafanyika na hasa suala zima la miradi ya kimaendeleo. Ipo miradi ya kimaendeleo ambayo katika hali ya mapambano ya tabianchi, tuna miradi mikubwa ambayo imekuwa ikisimamiwa kupitia mradi wa *EBA* na Wizara hii imekuwa ikisimamia pakubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ni pamoja na baadhi ya halmashauri hapa nchini ambazo zimekuwa zikihudumiwa. Halmashauri hizi ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu. Miradi mizuri, mikubwa na fedha nyingi zimekuwa zikitolewa katika halmashauri hizi kwa ajili ya mapambano ya hali ya tabianchi. Unaweza ukaona katika Wilaya ya Kishapu tumepokea shilingi bilioni 1.7 katika kipindi cha miaka mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni fedha nyingi sana na moja kati ya mambo makubwa ambayo yamekuwa yakifanyika ni pamoja na kujenga mabwawa makubwa, viwanda vidogo vidogo vya kuchakata ngozi na madume bora ya kisasa ya aina ya borani. Masuala ya uwezeshaji wananchi, ziko mashine zimeanzishwa za kuchakata mafuta na mashine za kuchakata nafaka mbalimbali. Pia wamekuwa wakienda mbali zaidi ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wananchi kupata eneo kwa ajili ya ufugaji wa kisasa na uwekezaji mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yanafanyika mambo makubwa na unaweza kuona kwamba Wizara hii chini ya Mheshimiwa Jafo na ndugu yangu Chilo wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana kusimamia shughuli za miradi hii na imekuwa ni miradi inayowanufaisha sana wananchi na kuwakwamua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia masuala mengine ambayo yanasimamiwa na Wizara hii chini ya Makamu wa Rais, ni pamoja na kushughulikia masuala mazima ya utatuzi wa kero mbalimbali ambazo zimekuwa zikiwepo pande mbili za Muungano. Tangu kuanzishwa kwa utaratibu huu wa kutatua changamoto hizi za Muungano, sote tunafahamu, kati ya changamoto ambazo zilikuwepo 25 mpaka sasa 22 zimeshatatuliwa. Unaweza ukaona tumebakiza mambo makubwa matatu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada kubwa sana inayofanywa na Mawaziri hawa na timu ya wataalam ambao kwa kweli na sisi tunaendelea kuomba Mwenyezi Mungu awasaidie, tuna uhakika baada ya muda mfupi historia kubwa iliyokuwepo kati ya pande

mbili kutokana na hizi changamoto zilizokuwepo, sasa kero hizi za muungano itakuwa ni historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu ukweli ni kwamba amekuwa akiwezesha, kwanza, kuhakikisha kwamba timu hizi za pande zote mbili zinakutana kila wakati na wanapokutana wanatoka na suluhu kila wakati. Kwa hiyo, ni jitihada kubwa sana na hivyo tunauona Muungano wetu unaendelea kustawi na tuna uhakika kwamba baada ya kipindi kifupi sasa tutakuwa tunazungumza kama historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya taasisi 36, taasisi 33 tayari ufumbuzi umeshapatikana. Kuna taasisi tatu tu ambazo zimebaki, lakini unaweza ukaona ni jitihada kubwa sana ambayo imefanywa chini ya usimamizi wa Wizara hii. Pia, yako mambo mengine mengi ambayo ni ya kiutawala wanayokwenda nayo vizuri, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie upande wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Sera na Uratibu, jitihada hizi zinafanyika vizuri sana. Naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Jenista na Naibu Waziri Nderiananga, kazi wanayofanya ni kubwa. Sisi sote ni mashahidi, moja kati ya matukio makubwa ambayo yalipatikana hii juzi na hasa kule Hanang, jitihada kubwa iliyofanyika ya hawa Mawaziri, Katibu Mkuu na viongozi wengine na Wizara nyingine walioshirikiana kwa pamoja, jitihada kubwa ya uokozi imefanyika ikiwa ni pamoja na kurudishia miundombinu katika mji wetu wa Hanang. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaweza ukaona Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naye pia ameweza kufika akazungumza na wahanga. Rais wetu kwa moyo wa upole, kwa moyo wa huruma, kwa kweli ameonyesha jitihada kubwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba miundombinu ya kijiji kile ambacho kimekwanguliwa kabisa na maji hayo sasa unarudishwa. Kwa hiyo, kijiji kile na maeneo hayo ambayo nyumba zake zimeharibiwa, Serikali ya CCM chini ya Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan, ameahidi kuhakikisha kwamba maeneo yale yanarudishwa kama kawaida. Sasa hivi jitihada zimeshaanza kwa ajili ya kuhakikisha maeneo hayo

yanarudishiwa ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba za makazi ya watu hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili tunawapongeza sana kwa kweli kwa jitihada hizo nzuri zinazofanyika. Tunaomba katika maeneo mengine, kwa sababu mvua hizi zinaendelea kunyesha na matukio ya maafa yamekuwa yakijitokeza maeneo mengine, tunaomba wafanye jitihada kubwa za kuhakikisha kwamba uratibu na ufuatiliaji ili mradi Watanzania wajisikie na waone matunda ya Serikali ya CCM wakihudumiwa vizuri, waendelee nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo lingine ambalo ni la madawa ya kulevya. Eneo hili mapambano yake ni makubwa, sisi sote Watanzania tumekuwa mashuhuda. Jitihada za kupambana na madawa ya kulevya zinafanyika kubwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kama Mungu kamjaalia kwa sababu ameteua Kamishna Jenerali ambaye anashughulika na masuala haya ya madawa, ndugu yetu Lyimo, anafanya kazi kubwa sana na Mwenyezi Mungu kwa kweli amlinde ampe afya njema. Nami naomba kumtia moyo kwa moyo wake wa kizalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu yale yanayofanyika ikiwa ni pamoja na kwenda kuyabaini mashamba ya bangi, kukamata madawa ya kulevya ikiwepo unga, heroine na mambo mengine mengi ikiwa ni pamoja na mirungi. Sote tunaona kwa macho yakikamatwa madawa, wakikata mazao ya bangi, jitihada hizi ziko wazi na taarifa zimeonekana ziko wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana kwa sababu tunauona uzalendo wake na sisi tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu, nami namtia moyo Mheshimiwa Rais kwa kweli kwamba aendelee kuwezesha Idara hii inavyotakiwa, nasi kama Wabunge kwa kweli tuna-*support* sana jitihada kubwa inayofanyika kwa ajili ya kuwakomboa Watanzania na hasa wanaoathirika na madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine ambayo nataka nizungumzie kwa kweli, nataka nigusie kwa upande wa TAMISEMI.

Eneo hili la TAMISEMI na hasa upande wa *TARURA* kuna kila sababu ya kuhakikisha suala la fedha tunazokuwa tunatenga ama tunazopitisha kama bajeti kama Bunge ni lazima zipelekwe katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka zaidi ya shilingi bilioni 880, lakini mpaka sasa fedha zilizokwenda kwa kweli ni aibu. Nataka niseme, kazi ya Bunge ni pamoja na kuishauri Serikali na kuielekeza juu ya mambo ya msingi yanayotakiwa kufanyika. Sisi tunasisitiza fedha zitolewe ziende kule zikasaidie halmashauri. Leo ninavyozungumza, Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, kata sita kati ya kata 29 hazipitiki, lakini ni kwa sababu, kwanza, ni ucheleweshaji wa fedha zile ambazo ni za kibajeti zilizokuwa zinatakiwa zipelekwe, hazijapelekwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sasa hivi pamoja na uharibifu wa mvua kubwa zinazoendelea kunyesha, jitihada yoyote haipo. Sasa kama lipo tatizo tunashauri kama Bunge, ni lazima tuwasaidie wananchi. Watanzania wanalia, wanakosa barabara za kusafirisha wagonjwa, wanakosa barabara za kusafiri wao wenyewe, wanakosa barabara za kusafirishia mazao na vitu vingine. Lazima Serikali katika hili isikie na ione umuhimu wa kuhakikisha barabara zinafunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna zile shilingi bilioni 305 zilizoongezwa ambazo kimsingi sisi Wabunge huwa tunashauriana na mameneja wetu wa wilaya kuona ni namna gani tushughulike na matatizo ya barabara. Tunaomba sana fedha hizi na zenyewe zitolewe. Zimesaidia sana katika kipindi kilichopita, tumefungua madaraja, nyingine tumepeleka kwenye lami, miji midogo. Fedha hizi zinapochelewa, zinachelewesha sana jitihada za maendeleo na hasa ufunguzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka kuzungumzia upande wa TAMISEMI ni upande wa Waheshimiwa Madiwani. Mimi ni Diwani kwa mujibu wa taratibu, lakini kinachofanyika siyo. Tangu tumeanza Bunge hili katika kipindi hiki cha mwaka 2020, kila mwaka tumekuwa tukizungumza juu ya jambo hili. Tatizo liko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, tusifike mahali tukaonekana tunavutana. Nashauri sana jambo hili katika kipindi cha mwaka huu wa bajeti tutakaoanza kufanya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba fedha hizi kwa ajili ya kuwasaidia Madiwani ziweze kutengwa na tuwaongezee kiasi cha posho ili mradi na wao weweze kujisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyoko Mezani. Kwanza kabisa, naunga mkono taarifa nzima ya Kamati hii na niseme wazi kwamba nami pia ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa aliyofanya hasa kwa upande wa elimu, afya, barabara na mengi ambayo ameyafanya kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii, hongera sana Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishukuru Serikali anayoiongoza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mchengerwa, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara mbalimbali na vitengo, hongereni kwa kazi kubwa sana mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono kipengele kimojawapo ambacho wenzangu waliotangulia wamekiongea kwa uchungu na kuonyesha ukweli kwamba kinahitaji kufanyiwa kazi, suala la barabara vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* ina umuhimu sana kufanya kazi kwa bidi. Naipongeza pia *TARURA* kwamba inafanya kazi kubwa na ni kutokana na uwezo wanaopewa na Serikali. Kipindi hiki cha mvua, barabara nyingi za vijijini zimeharibika. Kwa msingi huo naunga mkono Maazimio yaliyotolewa na Kamati yangu kwamba Serikali itoe fedha ili barabara zilizoharibika zitengenezwe haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali yetu sikivu kweli itenge fedha haraka sana ili *TARURA* iweze kutengeneza barabara ambazo sisi wote ni mashahidi kwamba mvua aliyotupa Mwenyezi Mungu mwaka huu zimeharibika. Kwa hiyo, zinahitaji kurudishiwa madaraja na kadhalika ili wananchi wa vijijini na hata na mjini pia waweze kufanya kazi zao kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwa upande wa elimu, unapozungumzia shule, ni walimu na wanafunzi, yale mengine yote yanayoongezeka; madarasa na nini ni kusaidia ili elimu itolewe vizuri, lakini unapozungumzia elimu ni walimu na wanafunzi. Ukiangalia kazi kubwa aliyoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia ya kujenga madarasa, kwa kweli ni kazi kubwa sana lakini inahitaji walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, naomba kuchukua nafasi hii pia kuunga mkono Maazimio yaliyotolewa na Kamati kwamba Serikali ifanye iwezavyo, walimu wapatikane ili miundombinu iliyojengwa na Mheshimiwa Dkt. Samia ya madarasa na kadhalika iweze kutumika iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia walimu hasa vijijini, wanakaa mbali sana na ndiyo maana neno linalotumika mara nyingi, ni shule shikizi. Zile shule shikizi ni mahali ambapo ni katikati ambako hakuna shule, hakuna vijiji, wanafunzi wanatembea mwendo mrefu na kwa msingi huo wananchi wanakuja na wazo kwamba hapa tunaanzisha shule shikizi na Serikali au halmashauri inaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema kwamba, madarasa ya wanafunzi yanapatikana, tatizo linakuja nyumba za walimu, wapange wapi? Ninyi wenyewe mnafahamu maeneo ya

vijijini, wapange nyumba wapi? Kwa kipindi kama hiki cha mvua kilichopita, walimu wamepata tabu sana kwenda mwendo wa mbali, apigwe na mvua ili afike kwa wakati afundishe. Kwa hiyo, naunga mkono Azimio lililozungumziwa hapa la kuwa Serikali itenge fedha maalum kwa ajili ya nyumba za walimu ili wakae karibu na shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza lile wazo la *two in one or three in* one hii ambayo itawezesha nyumba kupatikana nyingi iwezekanavyo ili walimu waweze kufika sehemu za kazi kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna jambo ambalo linazungumziwa sana hapa kwamba walimu wengi wamejazana hapa, walimu wengi wamejazana hapa. Siyo kosa lao, ombi langu mimi kwa kuunga mkono Kamati yetu, ni kwamba zitengwe hela za kusawazisha au wanaita msawazo ili walimu walioko sehemu ambayo wako wengi basi wasogezwe sehemu zingine ambazo kuna uhaba, huwezi kumuhamisha Mwalimu bila kumtengea fedha za uhamisho. Tunaomba Serikali itenge fedha maalum kwa ajili ya kuleta msawazo mzuri Walimu waweze kusambaa kwenye maeneo yenye mahitaji *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni la muhimu sana, ni suala la vyoo. Tuna tatizo kubwa sana la vyoo, kwa mfano kama vile sisi Urambo, kuna uhaba wa vyoo, matundu ya vyoo zaidi ya 1411 na mimi naona wananchi wana haki yao kabisa, mahali ambako walianzisha kwa mfano shule shikizi, ni kwamba wanafunzi wanatembea mwendo mrefu. La kwao, kubwa kabisa ni kwamba kuwe na darasa la kuanzia, sawa, lakini wakichanga fedha wananchi kama tunavyojua uwezo wao, darasa likiisha kunakuwa hakuna hela tena za vyoo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tuangalie utaratibu gani ambao tunaweza kuuweka shule zinapojengwa, waanze kwanza na vyoo kwa sababu tunaanza madarasa, yakiisha kunakuwa hakuna vyoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si vizuri wanafunzi wakaenda shuleni kwenye madarasa lakini hakuna vyoo. Kwa hiyo,naomba tuweke Mkakati Maalum wa kuwa na vyoo wakati shule mpya zinapojengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nisingependa nimalize bila kulizungumzia, ni suala la taulo za kike, tumekuja kugundua kwamba, Halmashauri zenye nia nzuri zimetenga fedha kwa ajili ya taulo za kike tukijua kwamba familia nyingi hazina uwezo na hili ni tatizo ambalo linawakwaza wanafunzi wa kike kutokuhudhuria shuleni wakati fulani Fulani, ombi langu ni kwamba, taulo za kike zitengewe bajeti ili Watoto wetu wa kike waweze kusoma vizuri na waendelee na masomo kadri iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeweza kusema maneno mengi lakini Kamati yetu imeleta Taarifa nzuri na tutashukuru kwamba tuone utekelezaji wake. Wajumbe wa Kamati wameshasema kabisa hapana, safari ijayo hatuandiki tena Maazimio kama yale ya kwanza kutengenezwa, yaani hayakufanyiwa kazi. Tunaiomba kabisa Serikali ichukue yale Maazimio, yafanyiwe kazi ili mwakani basi mambo yaendelee vizuri kutokana na jitihada kubwa aliyofanya Mheshimiwa Dkt. Samia ya kuleta maendeleo. Hatua zichukuliwe ili yale mama aliyoamua kuyatendea haki ya kuleta maendeleo ya haraka, basi yaweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naunga mkono Hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, umetumia muda vizuri sana. Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, atafuatiwa na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka ajiandae.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai. Kipekee, nampongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameendelea kuifanya kwenye Majimbo yetu yote. Ukiacha Elimu na Afya na maeneo mengine ya Miundombinu, tumeshuhudia upelekaji wa magari ya ufuatiliaji pamoja na *Ambulance* kwa siku za hivi karibuni. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza na kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mchengerwa, tangia ameanza kuhudumu kwenye Wizara hii pamoja na wasaidizi wake, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, pamoja na Makatibu wote, Katibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu, wameendelea kuwa na kiwango cha *5G*. Endeleeni kupiga kazi, mimi kama Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, naendelea kuunga mkono kazi hii njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kupitia Wizara ya TAMISEMI, kwa kuendelea kufanyia kazi Maazimio na Ushauri wa Kamati kuboresha Elimu Mtandao. Kwa sasa, Serikali inafanya majaribio ya kutoa elimu kwa njia ya mtandao. Tumeshuhudia kama Kamati, Mwalimu mmoja wa Kemia au *Biology* anafundisha kwenye shule tatu kwa wakati mmoja, yeye yuko Kibaha lakini darasa lingine liko Dodoma, na liko eneo lingine. Kwa hiyo, hii ni hatua nzuri na naendelea kuipongeza Serikali kwa kazi hii kubwa ya kuendelea kufanyia kazi maoni ya Kamati pamoja na ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya kuanzishwa kwa Shirika la Kibaha, yalikuwa ni pamoja na kufanya Tafiti kwenye maeneo mbalimbali yakiwemo Elimu. Kazi hii kubwa na nzuri ambayo nimeipongeza hapa, ya kuendelea kuboresha Elimu Mtandao, imefanywa na Shirika letu la Kibaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Elimu Kibaha ndiyo wamefanya kazi hii kubwa na nzuri. Kwa masikitiko, ni kwamba hili Shirika la Elimu Kibaha, tayari imeshatangazwa kuvunjwa. Mapendekezo na Ushauri wa Kamati kwa msimu uliopita, ilikuwa ni kuitaka Serikali iboreshe Shirika la Elimu Kibaha na siyo kuvunjwa. Kwa sababu bado malengo ya kuazishwa kwake yapo na tunayahitaji kama Watanzania. Tunakumbuka kuna Hospitali pale ya Tumbi, ilifanya kazi kubwa na nzuri kuanzia kipindi cha Mwalimu Nyerere, bado kazi ile ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Hospitali ile imerudi kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na jambo hili kwa kweli kama Mjumbe wa Kamati, naona si sawasawa. Bado naiomba Serikali kupitia upya maamuzi yake hayo ya kuvunja Shirika la Elimu Kibaha

ambalo kwa sasa tunaona ipo haja na iko sababu ya kuendelea kuliacha Shirika hili liendelee kufanya Tafiti za Elimu na maeneo mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amandus, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Godwin Kunambi.

**TAARIFA**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza mchangiaji kuhusiana na Shirika la Elimu Kibaha. Mimi ni mdau pale, nimewahi kupita pale *Kibaha Folk Development College* (Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha), kwa kweli Shirika la Elimu Kibaha ni muhimu sana na linatoa watu wengi. Mfano mzuri mimi Mheshimiwa Kunambi niko hapa, ni zao la *Folk Development College* pale Kibaha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amandus, Taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea Taarifa hii nzuri na inayoleta sasa kumbukumbu nzuri ya kazi njema ya Shirika la Elimu Kibaha. Bado naendelea kumuomba Mheshimiwa Mwenyekiti wakati wa kuhitimisha Hoja yake, aone namna atakavyoliweka vizuri ili tuitengeneze kama Azimio la Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwenye *TARURA*, sisi Waheshimiwa Wabunge tunaotokea vijijini, hali yetu kwa kweli ni mbaya. Kuna wakati unalazimika kutokufika Jimboni kwa kutumia gari maana yake lazima uvuke kwenye madaraja yaliyovunjika kwa kutumia namna nyingine ya usafiri kufika ndani ya jimbo lako. Taarifa iliyotolewa hapa, tumeona na tumesikia, Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla wetu namna bajeti ilivyopelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuunga mkono Taarifa hii ya Kamati, Serikali iendelee kupeleka fedha kwa wakati. Hali ni ngumu na hasahasa karibu tunajiandaa kurudi kwenye Majimbo

yetu, wanachi wanatamani kupata majibu kwa Waheshimiwa Wabunge, nini tumesikia kutoka kwa Serikali. Wakipeleka fedha kwa wakati, itaweza kutusaidia zaidi na mambo mengine na shughuli za kimaendeleo zitaendelea kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Nachingwea, siyo Barabara tu za *TARURA*, hata *TANROADS*. Ukitoka Ndanda, huwezi kufika Nachingwea barabara imekatika, ukitoka Masasi, huwezi kufika Nachingwea barabara imekatika, kwa hiyo, achilia mbali Barabara za *TARURA*. Sisi watu wa Nachingwea hatuna mbadala, jana nimepata taarifa basi linaishia Masasi, kutoka hapo wananchi wanavushwa kwenda upande wa pili kwa hiyo hii haileti picha nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwa Mheshimiwa Kuchauka kule Liwale, hali ni mbaya nayo, ukienda huko Mbarali hali ni hivyohivyo. Kwa hiyo niombe sana Serikali, jambo hili ni jambo la dharura na ni lazima tuchukue hatua sasa. Haina mbadala, Wananchi wa Tanzania wanahitaji huduma kila kona. *(Makofi)*

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amandus, Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Lazaro Nyamoga.

**TAARIFA**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza mchangiaji, wakati anaendelea kutaja, nilitaka tu kumtarifu kwamba, hata Kilolo kwenyewe, barabara hazipitiki kabisa maeneo yote na madaraja yamevunjika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amandus, Taarifa ya jirani yako unaipokea?

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kadhia hii, kwenye changamoto hii, hata ukienda Kiteto huko, hali ni hiyohiyo. Tunasema kwa uchungu na tunaiomba Serikali kuchukua hatua sasa, hali yetu siyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, najielekeza kwenye eneo lingine la maboma hasa ya Zahanati na Vituo vya Afya. Wananchi waliitikia wito na kuendelea kuhamasika kujenga majengo ya Zahanati wenyewe kwa nguvu zao lakini na Vituo vya Afya, majengo haya yako mengine yamekaa kwa zaidi ya miaka minne, miaka mitano, miaka miwili na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, hapa nguvu za wananchi zimekwenda, niombe Serikali kuweka Mpango Mahususi, Mpango wa haraka ambao unakwenda kufanya kazi ya kumalizia maboma haya kwa wakati. Zile ni nguvu za wananchi ambazo zimekwenda. Tukifanya hivi maana yake tunawavunja moyo wananchi wetu, hawawezi tena kufanya shughuli zingine, basi tuone nguvu hizi ambazo tayari wameshaziweka kwa kujenga haya majengo…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Hoja za Kamati zote mbili. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, atafwatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa na mimi fursa niweze kuchangia katika hotuba hizi mbili za Wenyeviti wa Kamati muhimu za Kudumu za Bunge. Kwanza naanza kumpongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mhagama, kwa kuwasililisha vizuri Hotuba ya Kamati lakini na ile ya TAMISEMI chini ya Mheshimiwa Dennis Londo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda kuchangia maeneo machache. La kwanza kabisa, naomba kuanza na hili la Maslahi na Posho za Waheshimiwa Madiwani pamoja na Viongozi wa Serikali za Mitaa. Ukifwatilia mjadala wa hapa leo kwenye hizi

Kamati, hasa ya TAMISEMI, utasikia sauti za Waheshimiwa Wabunge wakilizungumzia jambo hili. Mimi kipekee, naipongeza sana Serikali, katika Awamu hii ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweza kuhakikisha kwamba Mheshimiwa Diwani anapata fedha yake, ile posho yake bila kukopwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madiwani walikuwa wakikopwa posho zao lakini hivi sasa angalau wana uhakika wa kupatiwa fedha zile kwa sababu zinalipwa moja kwa moja na Serikali Kuu. Hii ni hatua kubwa na kwa mantiki hiyo, ninaiomba Serikali yangu ya CCM, iendelee kuwa sikivu na iendelee kumtazama mwananchi mnyonge hasa huyu Mheshimiwa Diwani pamoja na Mwenyekiti wa Kijiji na Mtaa ambaye yeye ndiye ana-*deal* moja kwa moja na Miradi ile ambayo sisi tunaipitisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye ndiye anaishi na wananchi kila siku, changamoto zinazojitokeza kwenye jamii yetu yeye ndiye anahangaika nazo. Kwa mazingira hayo, ninarudi tena kuiomba Serikali yetu hii ya CCM ambayo ni sikivu sana, imsikie tena Diwani kilio chake cha kumwongezea ile posho inayompa ya shilingi 350,000 kwa mwezi. Posho ile ni ndogo, ukiangalia hata *currency* tu ya nchi sasa hivi, ukiangalia mfumuko wa bei, thamani ya shilingi hivi sasa, kwenye matumizi ya kawaida tu, shilingi 350,000 ni fedha ndogo sana haikidhi mahitaji ya mtu mzima ambaye tunasema ni kiongozi, tena anasimamia Wataalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Diwani anamsimamia mtu ambaye ni *graduate* kwenye eneo lake lakini yeye analipwa shilingi 300,000. Hawezi kuwa na sauti, hawezi kuwa na *confidence*, anasimamia miradi ya mamilioni ya fedha lakini yeye analipwa shilingi 300,000, hawezi kuwa na *confidence*. Ndiyo unakuta hapo na yeye anaingia katikia ku-*temper* kuhakikisha na yeye anapata chochote kwenye miradi tunayoipeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, endapo ataongezewa kutoka hii shilingi 300,000, ifike hata basi shilingi milioni 1kama kule Zanzibar. Ikishindikana hiyo basi hata nusu yake, apate hata shilingi 700,000, aweze kukidhi, kumudu, kukidhi maisha yake ya kila siku. Naomba hili, Serikali yangu hii iweze kulichukua hili na

kulitazama, huko tunakoelekea kwenye bajeti hii inayokuja hata ile nyingine, kabla ya kwenda kwenye uchaguzi unaokuja, angalau Mheshimiwa Diwani awe ameongezewa kiasi fulani kwenye posho yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo, naomba kuambatanisha na suala la ukubwa wa maeneo yetu ya utawala hasahasa kata na vijiji. Tunazo kata kubwa kwelikweli, ninayo Kata moja inaitwa Ughandi, ni kubwa inakaribia jimbo, ninayo Kata ya Mtinko, kubwa kwelikweli, nina Kata ya Makuro, Ngimo, mpaka kule kwa jirani zangu kule Mkalama kuna Kata inaitwa Mwangeza, kutoka mwanzo wa kata kwenda mwisho wa kata ni kilometa 70. Kata ya Ibaga, ni Kata kubwa yenye vijiji tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, haya maeneo naomba sana Serikali yangu hii, itusikie, iende kuyagawa, tupelekeeni Watendaji wa kata, tupelekeeni Watendaji wa Vijiji ili tumuhudumie mwananchi. Kumfuata Mtendaji wa Kata kutoka kilometa 70, ni umbali mkubwa ukiangalia na hali za maisha za wananchi wetu. Naomba sana tulitazame hili jambo kwa ukaribu ili tuweze kuleta tija kwenye kazi tunazozifanya za kuwahudumia watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia upande mwingine wa Bajeti hizi tunazozipitisha hapa. Tunapitisha bajeti tunasema ziende zikatekeleze miradi ya maendeleo, lakini fedha haziendi kwa wakati kwa hiyo, utekelezaji wa miradi haufanyiki kwa wakati. Wakati mwingine, tunapitisha fedha lakini hakuna kabisa utekelezaji. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, tubadilishe utaratibu, fedha tunazopitisha hapa ziende kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaleta manung'uniko kwa wananchi mathalani hapa kwenye Bajeti hii iliyopita, nilitoa machozi hapa nikililia barabara yangu ile ya Singida – Ilongero Makao Makuu ya Halmashauri, mpaka hapa tunakwenda kwenye bajeti nyingine, fedha hazijaja. Hii inaleta hata mashaka kwa wananchi kule kwamba huenda tumedanganywa lakini kama fedha zingekuja kwa wakati, leo hii tungekuwa tunaifurahia Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana, Serikali ihakikishe fedha tunazozitenga hapa kama Waheshimiwa Wabunge, ziende kwa wakati zikatekeleze ile miradi ya maendeleo, kuna Kituo cha Afya pale Changimu, mpaka leo fedha hamna wakati tulishakubaliana fedha ziende. Kwa hiyo, niombe tunapopitisha vitu hapa, vitekelezeke kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la upungufu wa Watumishi kwenye maeneo yetu, kwenye Sekta ya Afya, Elimu, Utawala, Walimu. Tuna kilio kikubwa sana kwenye maeneo yetu kuhusu Upungufu wa Watumishi, niombe sana…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ahsante sana Mheshimiwa Abeid.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, huu muda ni mchache sana, ile programu ya *Dr. Samia Legal Aid Campaign* ambayo imepelekwa kule na Mheshimiwa Rais wetu kutoa msaada wa Kisheria kwa wananchi wetu kule masikini, ishuke iende mpaka kwenye vijiji, iongezewe *manpower*. Watumishi wale wanasheria wa Halmashauri waende mpaka kule kwa wananchi vijijini ili hii programu iwe na manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, atafwatiwa na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi na nianze mchango wangu jioni hii kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyopambana kuhakikisha wananchi wa nchi hii wanaishi maisha yaliyo bora. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Manaibu Waziri wote wawili, Katibu Mkuu na Makatibu Wakuu kwa namna wanavyoonyesha ushirikiano mkubwa na Kamati yetu ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau kumshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati na Makamu wake pamoja na Sekretarieti ya Kamati, kwa weledi mkubwa uliowezesha ripoti hii kukamilika na kuileta hapa Bungeni leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niaze na jamaa wa *TARURA*, kama mnavyofahamu, mfano mmojawapo wapo, Wilaya yetu ya Liwale, sisi kwetu lami ni msamiati mgumu, ni msamiati ambao haueleweki. Sasa, najaribu kuangalia, hebu Serikali iangalie picha hiyo, kama lami yenyewe tu kuiona ni mtihani mkubwa. Barabara zetu nyingi za udongo na hali hii tuliyonayo leo, kukoje Liwale? Hiyo ichukuliwe kama mfano muone namna gani tunapozungumzia *TARURA, TARURA, TARURA* tunamaanisha nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye Kamati tumezungumza hapa kwamba bajeti ya *TARURA* iongezwe, lakini naenda mbali zaidi, siyo tu iongezwe bajeti, na fedha hizi ambazo zimewekwa kwenye bajeti basi nazo ziende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeonekana hapa shida kubwa ni rasilimali fedha. Wiki nzima hii kila Mwenyekiti kwenye hotuba yake akija hapa anawaambia ongeza watumishi, inataka rasilimali fedha, kila taasisi tunaomba iongezewe bajeti zote unakuta rasilimali fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ombi langu kwa Serikali, kama ambavyo sisi tunasisitiza halmashauri ziongeze wigo wa kukusanya mapato Serikali nao walione hili, kwamba rasilimali fedha sasa hivi hapa nchini kwetu ndilo jambo kubwa tunalopambana nalo. Kwa hiyo ndugu zetu hawa tuliowakasimu Madaraka, kwa maana ya Wizara ya Fedha, waone ni namna gani wanakwenda kuongeza fedha hizi ili rasilimali fedha hii isiwe bidhaa adimu kama ilivyo sasa hivi leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine limegusiwa hapa kwa upande wa afya ni suala la maboma ya zahanati na vituo vya afya; hapa napo mimi nina mchango mdogo. Mimi nafikiri Serikali ije na utaratibu sasa wa kuratibu haya maboma kwamba yanajengwa kwa mtindo gani; kwa sababu

tumeshawahamasisha wananchi wamejenga haya maboma mengi mno. Kinachoonekana sasa kwamba mipango ya Serikali iko nyuma ya mipango ya wananchi. Wananchi wanajenga maboma mengi lakini Serikali uwezo wa kuyahudumia unakuwa ni mdogo. Sasa umefika wakati Serikali wafanye uratibu, labda wapewe wakurugenzi, kwamba kila Mkurugenzi alijenga maboma mangapi kwa mwaka kulingana na uwezo wa Serikali. Lakini kama tukiacha hivi maboma haya yaendelee kujengwa bado tunaendelea kupata lawama kwa wananchi kwa sababu wanajenga maboma mengi lakini uwezo wa kuyahudumia unakuwa ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu elimu. Tunashukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameleta fedha nyingi sana kwenda kuboresha miundombinu ya elimu, na hili jambo hakuna mtu anaweza akapinga ni jambo jema sana lakini bado kuna tatizo la vyoo kwa upande wa elimu. Shule nyingi hata shule za msingi zina matatizo makubwa sana ya vyoo na hapa naomba nitoe ushauri kwamba Serikali kupitia TAMISEMI, ione namna ya kuwawajibisha wakurugenzi wetu iwe ni mojawapo ya vipimo vya Mkurugenzi ni kuona kwamba kwenye halmashauri yake hakuna tatizo la hivi vyoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukiweka kipimo kama *task*, kwamba Mkurugenzi tutampima kwa namna anavyoweza kukabiliana na vyoo shuleni iwe ni mojawapo ya kipimo. Kwa sababu gani nasema hivyo? Kwa sababu sasa hivi kinachoonekana halmashauri nyingi baada ya Mheshimiwa Rais kuwapelekea fedha nyingi za miundombinu ya elimu wako likizo. Kwa hiyo wao wanasubiri wapelekewe bajeti kwamba wewe kwenye halmashauri yako unahitaji vyoo vingapi, unahitaji madarasa mangapi, unahitaji maboma mangapi na vitu kama hivyo. Lakini wapewe *task* sasa kwamba kwenye halmashauri yako nikisikia malalamiko ya vyoo, nikisikia malalamiko ya madawati kuwe na jambo la kujibu kwa hawa watendaji wetu kule kwenye halmashauri zetu, hapo ndipo tunaweza tukakabiliana na tatizo hili la vyoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine kwa upande wa *TARURA,* mimi nafikiri imefika wakati sasa kufikiria Meneja wa Wilaya wa *TARURA* awe na vitendea kazi kama vile ma-*bulldozer* yale au hizi *excavator* zile, kwa sababu gani; kwa mfano mimi kwangu kule kuna Barabara ya udongo unakuta dimbwi lipo katikati ya Barabara kinachohitajika pale ni kijiko tu kuja kuweka mfereji pale maji yale yaondoke yarudishie udongo Barabara ipitike. Sasa Meneja wa *TARURA* anakuambia kumpata mkandarasi kwa kazi ile hakuna mkandarasi ambaye yuko tayari atoke Masasi na *bulldozer* kuja kufukia mashimo mawili, matatu yenye thamani labda mradi tu wa shilingi milioni 50. Kwa hiyo Meneja wa *TARURA* anachofanya ni kusubiri mashimo yawe mengi zaidi angalau apate mradi kuanzia milioni 500 ndipo amwite mkanadarasi aje kufanya kazi kwa sababu kulitoa *bulldozer* kutoka Masasi au kutoka Mtwara kulifikisha Liwale si jambo jepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo mimi nafikiri hivi vifaa kama tulivyofanya kwenye idara ya maji, kwamba kila mkoa kuna lori la maji, basi tuone namna ya kuwawezesha hawa *TARURA*. Hii mitambo midogo midogo ya kufukia mashimo kuanzia zile Barabara za udongo ziwepo kule kwenye halmashauri zetu, kwa sababu miradi hii ni midogo midogo. Kwa mfano mimi nilikuwa mradi wa shilingi milioni 200, yule meneja ametafuta mkandarasi amekosa mwaka mzima, kwa sababu hakuna mkandarasi ambaye yuko tayari atoke umbali mrefu kufata shilingi milioni 200 au 300, *minimum* watakwambia shilingi milioni 500. Kwa hiyo kuwe na mradi zaidi ya shilingi milioni 500, 600 ndipo anaweza kuja kufanya kazi. Kwa hiyo hawa mimi napendekeza wapewe ile mitambo midogo midogo ya kuweza kufukia mashimo kwenye zile Barabara za udongo itakuwa imetusaidia zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea tena kwenye upande wa afya. nashukuru Mheshimiwa Rais amejenga vituo vingi vya afya na hospitali zetu za wilaya mpaka mikoa; na vifaa tiba sasa hivi ni vingi. Lakini tatizo lililozuka kule sasa ni wataalam wa kuhudumia na kutumia vile vifaa lakini sio wataalam peke yake hata kuvifunga. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, malizia.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** … vipo vituo vya afya vingine vyenye vifaatiba zaidi ya miezi sita havijafungwa viko ofisini. Mimi nashauri kwamba tuletewe wataalam vifaa vile vifungwe ili wananchi waendelee kupata huduma nzuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ya Kamati yetu, maazimio yote, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kuna tangazo la wageni walioko Bungeni jioni. Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, Waziri wa Katiba na Sheria kutoka Kata ya Migori Mkoani Iringa, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Kabula Shitobelo Mbunge ambao ni makatibu wa CCM kutoka Wilaya ya Ilemela Mkoa wa Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na kwa ujumla wake, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, kwa hiyo kwa kiwango kikubwa kazi unayoiona iliyoletwa mbele yako inaakisi yale ambayo na mimi kama Mjumbe nimeshiriki. Kwa hiyo, mchango wangu utajikita katika maeneo machache. Nitakwenda kwenye motisha, nitakwenda kwenye michezo na muda ukiruhusu nitakwenda kwenye *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya jumla, kabla sijaja Bungeni nilikuwa nikiangalia kipindi cha *National Geographic*. Kipindi kile niliona wenzetu na adha wanayoipata kutokana na matatizo kama barafu, baridi kali na vitu vingine vya namna hiyo. Nikawa najiuliza sisi kwa bahati nzuri hapa tulipo, msaada wa

Mwenyezi Mungu eneo zuri la kijiografia tulipo na tunalalamika; tukipata mvua tunalalamika, tukikosa mvua tunalalamika, vipi kama tungepata na baridi kali na mabarafu kama yale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu huko duniani kwa kupitia mipango wanajua kuna kipindi cha baridi kali, kuna kipindi cha barafu, kuna kipindi cha mvua kwa hiyo mvua kwao si tatizo ni suala tu la kujua kwa mipango yetu tutakabiliana vipi na mvua na mambo mengine ya namna hiyo. Kwa hiyo nilichokuwa naomba kwanza tumshukuru Mungu kwa kuwa hapa tulipo kijiografia lakini huyu Mwenyezi Mungu tusimpelekee kila aina ya lawama, baadhi ya kazi ni za kufanya sisi wenyewe. Nilikuwa naomba nianze na hilo. Kwa hiyo jitihada zilizobaki ni zetu sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwa watu wa mipango wanatusaidiaje? Ni kweli mimi pia nashiriki katika suala la Chama cha Kibunge cha Idadi ya Watu. Kwa ujumla wake sisi kule kwenye Chama cha Kibunge cha Idadi ya Watu tunasema hivi, kuwa na idadi kubwa ya watu ikitumika vizuri ni fursa lakini kuwa na idadi kubwa ya watu kama hutotumia vizuri ni changamoto. Kwa hiyo kwa sura yangu tafsiri yangu ni nini? Kila mwaka tunapozungumzia habari ya ujenzi wa vyoo, utengenezaji wa madawati, kila mwaka hicho pia ni kipimo cha umaskini. Tunatakiwa kwa kupitia watu wetu wa mipango watusaidie tutoke huko, kwa sababu suala la kujua una idadi gani ya watu, utafanya vipi, maoteo yakoje ni suala la kimipango. Kwa hiyo eneo hilo kwanza nilikuwa naomba sana tujaribu kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitoka hapo, mmezungumzia suala la motisha, mimi eneo la motisha nishukuru kamati kwa maana ya ukurasa wa 21 imezungumzia wale waliofanya vizuri na katika hili nishukuru Mkoa wangu wa Katavi umefanya vizuri kwa ujenzi wa maboma; zaidi ya maboma 500 wanakusudia kuyajenga. Sasa nasemaje kwa maana ya motisha? Wale wanaofanya vizuri tuonyeshe kuwapongeza, kuwatia moyo na ikiwezekana kama kuna namna nyingine ya kuwaruzuku ili watu hawa waendelee kufanya kazi vizuri. Nikilisema hilo ukiacha hilo la kazi nzuri iliyofanywa na eneo hilo, tulipita Mbeya tukakuta kuna shule moja inaitwa Nsalanga, hii Nsalanga pale Mbeya jiji kuna

mwalimu amefanya kazi nzuri kwa kwenye Mradi wa *SEQUIP*. Kazi nzuri kabisa, na kwa kiwango kile kile cha fedha ametengeneza kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba motisha ya watu wanaofanya kazi; na huyu mwalimu kwa ajina anaitwa Mwalimu Pascal Lucas wa Nsalanga naona Mheshimiwa Spika amefurahi ni kweli kazi nzuri, shule nzuri wale watu wamejiongeza wamekuwa ni watundu wabunifu. Mahali pa shule wameweka mpaka badala ya *tiles* wameweka ile kitu wanaita tarazo wamejiongeza walikuwa watundu, wabunifu. Sasa watu kama hawa tuwatie moyo kuwapongeza katika maeneo mbalimbali ili na wengine waige. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hilo hilo la motisha mimi naomba, wenyeviti wa mitaa, wenyeviti wa vijiji, Madiwani wanafanya kazi nzuri tuwape motisha tuwatie moyo hilo ni eneo la motisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo nije eneo la michezo. Tumesema kwa kupitia Kamati yetu. Ujenzi wa viwanja katika maeneo mbalimbali leo tusiwe watu wa kulalamika kwa nini wenzetu wa West Africa wanafanya vizuri ni uwekezaji. Leo ukikuta kila huyu mchezaji mzuri duniani anatoka huko haijaja kwa bahati mbaya, ni kutokana na uwekezaji. Kwa hiyo na mimi naomba eneo la ujenzi wa viwanja tusiache katika maeneo yetu mbalimbali. Niwapongeze Arusha tulipita pale tukakuta wenzetu wa *TARURA* ile chenji iliyobaki wamekwenda kujenga viwanja vizuri vya michezo. Nitoe shime kwa wadau mbalimbali wa michezo waturahisishie kazi hiyo nikiamini tukifanya vizuri eneo hilo la michezo huo ni uwekezaji kama uwekezaji mwingine. Tumeona wachezaji waliofanya vizuri huko duniani wanarudi katika nchi zao wanawekeza; iwe katika shule au katika hospitali. Kwa hiyo kwanza umeanza kwa kuwekeza kwenye michezo baadaye utaiona tija baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi katika eneo la *TARURA* kwa maana ya kumalizia. Sauti ya wengi ni sauti ya Mungu, ukikuta watu wengi kwa nini wote tunazungumzia *TARURA, TARURA, TARURA,* niombe sana watu hawa kuwaongeza fedha mimi kwa

suala la barabara na tatizo lilivyo naichukulia kama ilivyotokezea janga wenzetu hawa wa huku Hanang. Sura ile ilivyotokea na Serikali nzuri ikafanya kazi kwa uharaka ndivyo ilivyo. Kila sehemu ukienda ni tatizo, kila sehemu ukienda ni tatizo. Kwa hiyo hakuna namna zaidi ya kuwaongeza watu hawa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa kwenda kwenye maeneo mengine ya kuboresha, kwa maana ya miradi mingine hiyo ya *AGRI-CONNECT, TACTIC* na *RISE* kwa maana tu huko kote tutafanya kazi ikiwa kwanza hii dharura iliyojitokeza tumei-*address*. Tulichukulie kama janga na watu hawa wapelekewe fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa muda naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Stanslaus Mabula atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Godwin Kunambi ajiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi walau kwa dakika chache niweze kuchangia mambo machache, hasa kwenye sekta hii ya barabara upande wa *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niungane na Wajumbe wote waliopita waliozungumza habari ya barabara, lakini niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati wakiongozwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Londo, kwa kazi nzuri waliyoifanya, hasa kwenye kuichambua na kuieleza vizuri *issue* ya barabara upande wa *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kutazama; Bunge hili limepitisha bajeti siyo mara moja siyo mara mbili namna ambavyo linatamani kuona *TARURA* ikifanya kazi. Kwa bahati mbaya sana hatujafikia malengo wakati wote tuliokubaliana na kupanga hapa ya kuwahudumia wananchi kwenye barabara zao. Kwa mfano tunapozungumza tumepanga bajeti kwa *TARURA* kwa mfano shilingi bilioni 710 ukijumlisha na zile bilioni 107 za wadau lakini nimejaribu kuangalia mtandao wa barabara; *TARURA* peke yake inahudumia barabara za wilayani, mijini na

vijijini zaidi ya kilomita 144,000. Nikajaribu kutafuta uwiano *TARURA* na *TANROADS* ukoje? *TANROADS* wanahudumia barabara zipatazo kilomita 91,532 nchi nzima na katika barabara hizo kilomita 12,197 ni barabara kuu na 21,298 ni barabara za mikoa lakini kilomita 58,037 ni barabara zinazohudumiwa na *TANROADS* wilayani na vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini? *TARURA* hii leo tunaipa nusu ya bajeti sawa na bajeti inayopewa *TANROADS*. Sasa Bunge hili ndilo limeifanya *TANROADS* ikafikia bajeti ya zaidi ya trilioni moja milioni mia nne. Bunge hili ndilo linashindwa kuifanya *TARURA* ifikie kiwango angalau cha trilioni moja na milioni mia sita inayosemwa hapa. Nafahamu tulikotoka kwenye shilingi bilioni 400 mpaka leo tuko shilingi bilioni 700, lakini masikitiko yangu makubwa ni kwamba hata fedha zile ambazo Bunge liliahidiwa zaidi ya shilingi bilioni 350 kupelekwa *TARURA* kwa ajili ya kuimarisha mtandao wa barabara hazijakwenda mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hilo tu, ripoti ya Kamati hapa inasema ni asilimia 12 ya fedha peke yake ndizo zimepokelewa kule *TARURA* kwa ajili ya utekelezaji wa kazi ambayo ni chini ya asilimia 39. Mheshimiwa Rais kafanya kazi kubwa sana, kawekeza sana kwenye sekta ya afya, kawekeza sana kwenye sekta ya elimu. Bahati mbaya sana maeneo yote yaliyoboreshwa kwa ajili ya huduma za kijamii hayawezi kufikika kiurahisi kwa sababu barabara hazipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nikupe mfano, ukichukua Jiji la Mwanza peke yake lina mtandao wa barabara kilometa elfu mia mbili na sabini na kitu. Barabara zilizojengwa zinazoweza kupitika vizuri kwa kiwango cha lami, kiwango cha mawe na kiwango cha changarawe hazizidi kilomita 90 kati ya hizo. Kwa namna yoyote ile bado tunayo kazi kubwa sana Waheshimiwa Wabunge. Ndiyo maana asubuhi nikasema hili jambo sio la Dar es Salaam peke yake hili jambo tulitazame kama jambo la nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge kazi yetu hapa tumesema mara kadhaa tusipopata fedha za kutosha kwenye upande wa barabara na kuiwezesha *TARURA* ifanye kazi

yake vizuri; leo uki-*post* kitu kizuri na cha thamani umejenga kituo cha afya kizuri, umejenga shule nzuri ukaki-*post* kwenye page yako wanaweza kuja watu 10 mpaka 15 wanakueleza habari ya barabara na hawazungumzi kile ulichokiweka pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha ni namna gani wananchi wetu wanatamani maendeleo makubwa tunayoyafanya kwenye sekta za afya, elimu, maji na maeneo mengine tuwekeze hivyo hivyo kwenye Barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani unatoka mjini kilomita mbili ni barabara ya lami halafu unakwenda kilomita 11 barabara ya tope na siyo changarawe na kule unakokwenda umejenga kituo cha afya kizuri, wananchi wanaweza kwenda kupata huduma lakini hawapati. Kwa hiyo mimi nachotaka kusema, na Serikali itusaidie sana, tunakwenda kwenye Bunge la Bajeti sasa hivi. Haiwezekani asilimia 12 peke yake ndiyo fedha iliyotolewa kwa ajili ya kujenga barabara. Leo kazi zimetangazwa asilimia 60 wakandarasi wako *site* hawana hela, asilimia 40 zilikuwa zitangazwe haziwezi kutangazwa kwa sababu fedha hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana na Bunge lako hili kule kwetu tunapotoka sisi kuna maeneo; na nishukuru sana Serikali kwa kutumia miradi ya *TSCP* toka mwaka 2010 mpaka 2014; lakini sasa tuko kwenye miradi ya *TACTIC,* Serikali iwekeze zaidi kwenye kutafuta miradi ya washirika ya namna hii itakayosaidia sana miji yetu kupendeza na kuwa na barabara nyingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mifano mingi ipo, leo hata ukiongea na Mheshimiwa Spika, yuko mbele yangu hapa; Jiji la Mbeya leo ukichukua Mradi wa *TSCP,* ukachukua Mradi wa *TACTIC* ukienda Mwanza uchukue Mradi wa *TACTIC,* Mradi wa *TSCP* ndiyo maeneo ambayo yamesaidia zaidi kwenye uwekezaji wa barabara. Tufanye hivyo tupate fedha ziweze kujenga barabara. Bila hivyo tunapiga *mark time* na thamani ya miradi yetu haitaonekana kwa sababu hatujaitendea haki kwa kuitengenezea miundombinu mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua umenipa dakika tano nikushukuru sana lakini nisisitize Waheshimiwa Wabunge, tunakokwenda bila kuwa na barabara nyingi nzuri tutaadhibiwa kwa sababu ya kukosa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mabula; Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi na Mheshimiwa Agnesta Lambert ajiandae.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa ya mimi leo kuchangia. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kumsahau Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya na kutuwakilisha vema katika Bunge letu hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninataka nichangie mambo machache tu kwenye Wizara hii ya Serikali za Mitaa - TAMISEMI. Kwanza kabisa sisi Wanajimbo la Msalala tunazo shukrani nyingi kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa fedha nyingi sana alizotupatia za maendeleo kwenye Jimbo la Msalala. Ametupatia fedha nyingi kwenye sekta ya afya, tunatakribani ya vituo vipya sita vya afya ametuletea, tuna zaidi ya zahanati 34 zimekamilika lakini juzi nimeenda kukabidhi *ambulance* mpya kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo itaenda kuhudumia wananchi wagonjwa wa Kata ya Isaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hajaishia hapo kwenye sekta ya elimu ametupa fedha nyingi sana, tuna shule zaidi ya saba mpya, hajaishia hapo ametuongeza fedha nyingine ya kujenga Chuo cha Veta bilioni mbili na chuo sasa hivi kinaenda vizuri sana. Hajaishia hapo ametupa fedha za kujenga Chuo cha *Nursing* na chenyewe kimekamilika, hivi karibuni tunaenda kupokea wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya miaka minne, ndani ya miaka mitatu ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan tunaenda kuwa na vyuo viwili kwenye Jimbo la Msalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anatafuta fedha nyingi sana kwa uchungu mkubwa, kwa wivu mkubwa kuhakikisha ya kwamba wananchi wa Jimbo la Msalala na nchi nzima wananufaika na miradi mbalimbali kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kuunga mkono maazimio haya ya Kamati na nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati hii kwa maazimio mazuri kabisa, maazimio yenye afya ambayo ninaimani kabisa kama yataenda kutekelezeka basi kutakuwa na mabadiliko makubwa sana kwenye sekta hii ya TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mimi nakubaliana moja kwa moja na suala zima la mapendekezo ya Kamati ya kupitia upya Kanuni ya uendeshaji wa Mabaraza yetu ili kuona namna gani sasa Waheshimiwa Wabunge wanashiriki vema kwenye shughuli za maendeleo kwenye maeneo hayo. Ukweli usiopingika ni kweli Mheshimiwa Mbunge ni Diwani na ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha lakini kiuhalisia huu uhalisia wa Mheshimiwa Mbunge kuwa Mjumbe wa Kamati ya Fedha na kuwa Mjumbe wa Baraza mara nyingi kalenda ya upangaji wa vikao kwenye maeneo hayo hatushirikishwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Waziri yuko hapo ni namna gani sasa mje na mkakati wa kutoa maelekezo au mwongozo wa kupeleka kule kwenye Halmashauri upangaji wa vikao hivi vya Kamati ya Fedha na Mabaraza uzingatie ratiba ya Waheshimiwa Wabunge kuwepo kule ili tuweze kushiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anakuwa anakuwa vizia Kikao cha Kamati ya Fedha, anavizia Baraza, ukikaa Jimboni muda wote uko Jimboni, lakini ratiba ya Bunge ikitoka tu ukiwa safarini kuelekea Dodoma unapokea *message* kwamba kesho kuna Kamati ya Fedha, kesho kuna Baraza, hivi

wanaogopa nini kutoa ratiba wakati Mheshimiwa Mbunge akiwa yuko Jimboni ili aweze kushiriki kama Mjumbe halali wa Kamati ya Fedha, aweze kushiriki kama Mjumbe wa Baraza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapeleka fedha nyingi sana kule chini na wengi mmeona, ninampongeza Katibu wetu Mwenezi amefanya ziara kwenye maeneo hayo, amekuta changamoto nyingi sana na ninataka niseme na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu yuko hapo. Mheshimiwa Rais anapeleka fedha nyingi sana kwenye Majimbo yetu lakini wasimamizi walioko kwenye maeneo haya na hasa aliowapatia dhamana, hawatimizi majukumu yao ya kusimamia kazi vizuri, wanamuhujumu kwenye maeneo ya miradi huko chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazokwenda huko nitolee mfano kwenye Jimbo langu mimi, tumepokea fedha nyingi sana. Juzi tumebaini wizi wa fedha kiasi cha shilingi milioni mia mbili na wezi wamekatwa wamekula Fedha za *TASAF*, wazee ambao hawawezi kufanya shughuli. Mheshimiwa Rais ametafuta fedha amewapelekea hawa akinamama wanyonge kwa ajili ya *TASAF* lakini baadhi ya watumishi wachache ambao siyo waaminifu wameenda kula zile fedha na nini kimefanyika? Hakuna hatua yeyote iliyochukuliwa isipokuwa ni kwamba kaeni hapa, kila mwisho wa mwezi tutawakata kwenye mshahara wenu laki moja moja. Hivi fedha hizi anazozitafuta Mheshimiwa Rais kwa uchungu, anapeleka huko ili zikawahudumie wananchi, watu baki wanakula fedha na hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu niiombe Serikali ikiwezekana iweze kutoa mwongozo kwa sasa na hasa kwa kipindi hili tulichopo. Mheshimiwa Rais amewaamini watu kule wasimamie shughuli za maendeleo kule chini, lakini watu hao ni ukweli usiyopingika kwa wakati huu wanatumia gari za Serikali ambazo zingetumika kwenda kutatua migogoro, wanatumia mafuta ya Serikali ambayo yangetumika kwenda kutatua migogoro, wanaanza kwenda kutafuta kura na watu hawa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu utoke mwongozo wa kuwaambia kama kuna watu ambao wanahitaji kumsaidia kumsaidia Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sasa wajitokeze

kumsaidia kwa ukweli na wale ambao wanawaza kwenda kugombea Majimbo waache kazi zile waende wakagombee Majimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanatumia fedha za Serikali, wanatumia magari ya Serikali, wanaenda kuanza kukimbizana na Wajumbe kwenye maeneo hayo, niombe sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, hebu Serikali sasa itoe mwongozo wale watakao taka kumsaidia Dkt. Samia Suluhu Hassan ili miradi iweze kukamilika huko chini. Tunaenda kwenye uchaguzi, miradi mingi haikamiliki na wale wazembe ambao wanakula fedha hatua kali zichukuliwe ili kuhakikisha ya kwamba miradi ile inakamilika. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu niombe sana hili liweze kuchukuliwa hatua kali ili tuweze kumsaidia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala zima la vituo vya afya; siku zote mimi huwa nasema katika uanzishwaji wa vituo vya afya hivi huduma inayotolewa kwenye vituo vya afya mara nyingi hakuna huduma inayotolewa bure ni huduma ya malipo. Huwa najiuliza na mara nyingi huwa nakaa nao kuona kwamba kuna utofauti gani kati ya vituo vya afya *(dispensary* za *private)* na vituo vya afya vya Serikali, huduma ni zilezile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali njooni na mkakati wapeni Ma-*DMO* na *in-charge* wa kwenye vituo vya afya hivyo kipimo kwamba kipimo cha *in-charge* kwenye Kituo cha Afya A ni kuhakikisha ya kwamba anakusanya mapato, anasimamia mapato vizuri, pia ahakikishe kwamba dawa zinapatikana wakati wote hiyo inawezekana na ikiwezekana kwa sababu mmeshagatua madaraka yako huko maana yake kwenye mapato lindwa wanaruhusiwa kukusanya mapato na kutumia, waweze basi kuajiri, kwenye vituo vya afya hivyo…

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa ahsante sana, malizia mchango wako, muda wako umeisha.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnesta Lambert na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tumeambiwa tunachangia kwa dakika kumi na mimi naangalia saa yangu hapa naweka pembeni. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, ufuate kengele, itakavyolia ya pili basi utakuwa umehitimisha mchango wako.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mimi nianze na shukrani. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu nimeagizwa na wananchi pia wa Mlimba kumshukuru Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mlimba wameniagiza nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa barabara ya lami kutoka Ifakara kwenda Mbingu - kilomita 62.5. Wananchi wa Mlimba wameniagiza nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa gari ya wagonjwa, wananchi wa Mlimba wameniagiza nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa sekta ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naanza kuchangia. Mimi naanza na mapato ya ndani na matumizi yake ya Halmashauri zetu zote nchini na hapa nitatoa mifano ya Halmashauri mbili *Mrimba DC* na *Dodoma CC;* nianze na *Mlimba DC,* Halmashauri ambayo mimi ndiye Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo changamoto kubwa kwenye Serikali za Mitaa, mimi niliwahi kuwa Mkurugenzi nina-*declare interest* lakini naomba Wakurugenzi wenzangu wanisamehe nchini. Halmashauri nyingi Wakurugenzi wamegeuza kama *comfort zone*. Mkurugenzi anafika ofisini tangu ateuliwe hawezi kuwa hata mbunifu kwenye vyanzo vipya vya mapato ya ndani, Mkurugenzi wa Halmashauri hawezi hata kubadilisha mkao wa kiti. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema haya? Halmashauri zetu nchini zimekuwa tegemezi kwa asilimia zaidi ya

sabini wanategemea Serikali Kuu, asilimia sabini Majiji mengine tutoe mfano Kenya, Rwanda nchi zinazotuzunguka majirani hawa. Majiji yote yanajitegemea kwa mapato ya ndani. Manispaa zote zinajitegemea kwa mapato ya ndani lakini *why not Tanzania?* Kwa nini Tanzania hatuwezi kujitegemea kwenye majiji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa mifano miwili nianze na *Mlimba DC;* kwa miaka mitatu mfululizo nitatoa mapato yetu. Tulianza na bilioni 3.2. Sasa hivi mwaka huu wa fedha tuna bilioni 4.2 tumeongezeka kwa bilioni moja na sasa kwenye makisio mapya ya mwaka fedha ujao tutakwenda kwenye bilioni 4.8. Matumizi yake yakoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kujenga vituo vya afya vitatu kwa mapato ya ndani. Kituo cha Afya cha Chita ni kwa mapato ya ndani. Kituo cha Afya cha Mofu ni kwa mapato ya ndani, Kituo cha Afya cha Igima ni kwa mapato ya ndani. Kwa nini hayafanyiki Halmashauri nyingine? Kweli tunaendelea kupeleka mzigo kubwa Serikali Kuu, nashangaa hata Majiji yanasubiri milioni 500 ya Mama Samia? Kujenga kituo cha afya kimoja kweli *are we serious?* Sasa nataka kusema nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya ubunifu Halmashauri ya Mlimba, ninavyozungumza leo tunalo shamba la miti pale Kata ya Uchindile la ekari 1,300, tunatarajia miaka 10 ijayo sisi tume-*break even* kwa nini wengine hawawezi kufanya? Kwa nini hawafanyi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi Dodoma. Ninatatoa takwimu ya miaka mitatu, mwaka 2016/2017 Dodoma Jiji ilikusanya bilioni 25. Mwaka 2017/2018 ikakusanya bilioni 57, mwaka 2018/2019 ikakusanya bilioni 67, Mwaka 2019/2020 ikakusanya bilioni 71 nikiwa Mkurugenzi wa Jiji. Kwa nini haya hayafanyiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi yake kwa mfano Dodoma Jiji wakati ule tuliona asilimia 70 ilikuwa ni mapato yanatokana na viwanja. Tukasema viwanja vikikosa soko mapato yatakuwaje? Tukaja na Miradi Mikubwa ya Kimkakati Saba na niwaambie Mheshimiwa Naibu Waziri yupo hapa. Soko siyo chanzo cha mapato ni huduma, stendi siyo chanzo cha mapato

ni huduma. Tukaja na miradi saba wakati wangu tukatekeleza miradi miwili, tukajenga hoteli ya Dodoma *City Hotel* kwa bilioni tisa mapato ya ndani na hivi leo wanapata milioni 900 kwa kila mwaka pale mwenye macho anaona, lakini Mji wa Kiserikali tumejenga hoteli… *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuliambia Bunge hili na Tanzania, Mbunge anaeongea ni hazina ya Watanzania, nilitaka kutoa taarifa hiyo. *(Makofi)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea na mchango wako.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Getere, naipokea taarifa yako kwa asilimia 100 na Mungu akubariki kwa kutambua uwezo wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini? Tukajenge hoteli nyingine pale Mji wa Kiserikali, mradi wa bilioni 18 kwa mapato ya ndani na tulipanga Dodoma ndani ya miaka kumi tu-*graduate* ili tutoe mfano kwa Watanzania inawezekana! Mimi sizungumzi sayari nyingine nazungumzia hapa. Tukasema wapo waliosema haa Dodoma ni Mji wa Serikali Makao Makuu, mje mjifunze Mlimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndani Waheshimiwa Wabunge ni Halmashauri gani, Mheshimiwa Mbunge asimame hapa, mnajenga vituo vya afya vitatu kwa mapato ya ndani simama! *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge…

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Kunambi, ili Mbunge asimame anasimama kwa idhini ya Kiti siyo wewe. *(Kicheko)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante sana, nimefuata maelekezo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini? Tufike mahala tuwasaidie Wakurugenzi wa Halmashauri wawe wabunifu. Msingi Mkuu wa Sera ya Ugatuaji Madaraka maana yake Halmashauri zijitegee kwa mapato ya ndani. Sasa leo nasema tunalalamika, kwa hiyo asilimia 90 unategemea mapato ya Serikali Kuu, Fedha ya Maendeleo ya Serikali Kuu! Hivi jamani, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu nisikilize kwa makini.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Taletale.

**TAARIFA**

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa Kaka yangu wa Mlimba, naendelea kusema wewe ni hazina ya Morogoro. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi, taarifa unaipokea?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi, unaipokea taarifa?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuelewane, taarifa ni sehemu ya muda wa uchangiaji, sasa hajapokea taarifa unampa tena taarifa!

Mheshimiwa Kunambi, endelea kuchangia.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunilinda; nataka kusema nini? Changamoto kubwa yetu kama Watanzania, naendelea kusema ni mambo matatu fikra kwa maana ya *mindset, commitment* kwa maana ya utayari kufanya jambo na mwisho uzalendo. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima unapokuwa Mkurugenzi wa Halmashauri au Kiongozi yeyote kwenye Taasisi yeyote ya Umma awe na fikra akiondoka anaacha alama gani? *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unaacha nini kwa watu uliokuwa ukiwaongoza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yangu iko *very positive*. Naomba kutoa taarifa kwa mchangiaji kwa kile ambacho ana-*narrate* naungana naye na naiomba

Serikali kupitia TAMISEMI, taarifa yangu ni hii sasa, vile zinavyokuja fedha kutoka Serikali Kuu wawe wanaangalia uhalisia wa kipato cha Halmashauri husika au Majiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano fedha za UVIKO zilivyogawanyishwa, Dodoma Jiji hapa imepelekewa fedha katika shule sawa sawa na fedha ambazo wamepeleka kule Tarime Mji ambako hamna mapato kabisa. Sasa ili kuweka hii *creativity* ya Wakurugenzi na uhalisia wa vipato katika Majiji au Halmashauri zetu, Serikali Kuu iangalie sasa upelekaji wa fedha katika Halmashauri zetu.

**MWENYEKITI:** Mheshemiwa Esther, ahsante sana.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naungana na wewe kabisa ili iweze kuongeza *creativity* kwenye halmashauri zetu kulingana na uhalisia wa vipato vya Halmashauri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo. Wengi wamezungumzia *TARURA* ni kweli, *TARURA* ndiyo mkombozi wa barabara zetu za vijijini, pamoja na Bunge kupitisha bajeti kwa ajili ya *TARURA* lakini bado fedha za mgao wa kila mwezi wanapewa ndogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi, sawa naona muda umeisha.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina ushahidi mgao wa mwezi uliopita *TARURA* wamepewa bilioni 11 tu na Wizara fulani wamepewa bilioni 20. Morogoro *TARURA* peke yake tulikuwa tunadai madeni ya wakandarasi shilingi bilioni tatu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie Wananchi wa Mlimba wanaomba barabara. Itoshe kusema, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta Lambert, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo na Mheshimiwa Chege ajiandae.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia. Awali ya yote naomba kwa niunge mkono hoja taarifa zote za Kamati mbili kwa maana ya Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Kamati ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa leo nitajikita katika taarifa ya Kamati ya TAMISEMI. Tangia asubuhi wachangiaji wote ambao wamesimama hapa kuchangia taarifa hizi za Kamati *majority* walionesha ni namna gani ambavyo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kutoa fedha nyingi za maendeleo kushuka kule kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo halina ubishani. Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya mambo makubwa kwa wananchi wa huko chini, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametenga fedha nyingi za maendeleo kwenda kwenye Zahanati, kwenye shule kwenye kila namna ya maeneo yote ambayo maendeleo kwa wananchi yanahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya Kamati ya TAMISEMI pamoja na changamoto nyingi ambazo wameelezea wamesema moja kwa moja kwamba miradi ya maendeleo imekuwa haitimii kwa wakati, haikamiliki kwa wakati. Pia katika taarifa hiyo ya TAMISEMI wamesema kwamba, kutokana na miradi hii kutokamilika ni wazi kabisa kwamba kuna watumishi ambao wameshindwa kuwajibika kwa maana hawakutekeleza wajibu wao, hivyo Kamati ikaenda mbali ikashauri kwamba watu hawa wachukuliwe hatua za kinidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanzia hapo kwenda katika mchango wangu. Wote tumekuwa tukifuatilia ziara ya Ndugu Makonda ambaye ni Katibu Mwenezi wa CCM Taifa. Pasipo kificho ukiangalia kwa haraka na kwa karibu sana unaweza ukahisi kwamba uko chini haijawahi kuwepo Serikali kabisa. Unaweza ukadhani kwamba sasa Katibu Mwenezi wa CCM sasa ndiye ambaye anaenda aidha, kutengeneza Serikali au sasa ndiye mkombozi ambaye anashuka kwenda kutatua changamoto na kero za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu wote kwamba wapo wateule wa Rais ambao Mheshimiwa Rais amewaamini kutoka katika idadi ya Watanzania zaidi ya milioni 60, akawapa madaraka kwamba waende huko chini kumsaidia. Nikisema wamepewa madaraka namaanisha akina nani? Ni Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na wataalamu mbalimbali kwenye maeneo hayo ambao wameajiriwa kwa taaluma zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi, Bunge lako ni shahidi, katika ziara ya Ndg. Makonda, badala ya kueleza namna gani Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametekeleza Ilani ya Chama chake, amejikuta hafanyi hayo, mwisho wa siku anaanza kusikiliza na kutatua kero za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua, na wote tunatambua kwamba Wakuu wa Mikoa ndio wasimamizi namba moja wa Shughuli za Serikali kule chini. Ndio wasimamizi namba moja wa fedha za Serikali za maendeleo zinazoshushwa katika maeneo. Vile vile wote tunatambua, kama jinsi ambavyo Mbunge ana Jimbo lake la utawala kwa maana ana Jimbo lake ambalo analisimamia, hivyo hivyo Mkuu wa Mkoa, Mkoa ule ndiyo Jimbo lake la uteuzi ambalo Mheshimiwa Rais amemwamini kwalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na yale mema na mazuri aliyofanya Mheshimiwa Rais ambayo yalipaswa kusikika kule chini, Wakuu wa Mkoa hawa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi, wameshindwa kabisa kutekeleza wajibu wao, kabisa kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mifano michache, nafahamu na wewe unafuatilia mambo haya. Katika mikoa yote ambayo Ndg. Makonda amekwenda, kuna maeneo alifika sehemu, mfano kule Rukwa, mpaka anamwambia Mkurugenzi kwamba, sikuruhusu uambatane na mimi katika msafara wangu huu, nakuacha hapa katika halmashauri yako utatue kwanza changamoto hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara ya Ndg. Makonda hakuna majungu, hakuna kusubiri, ni hapa na hapa; Mkuu wa Mkoa hapo, Mkuu wa Wilaya hapo, Mkurugenzi hapo, wananchi hapo. Jambo hili limefanyika? Mkuu wa Mkoa anasema ndiyo, Mkurugenzi ndiyo, Mkuu wa Wilaya ndiyo. Mmefanya nini? Wanabaki kupiga yowe yowe nyingi, hakuna jambo lolote ambalo wamelifanya kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu kwamba Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi ikiwa atasimama vizuri kumsaidia Rais katika majukumu yake, huwezi kukutana na changamoto za miaka kumi au miaka mitano. Hii ni hujuma ya moja kwa moja kwa Mheshimiwa Rais kutoka kwa wateule hao. Siyo tu hujuma, lakini ni kutowatendea haki Watanzania ambao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amejitoa kwa moyo mweupe kuwatumikia na kuhakikisha changamoto zao zinatatuliwa.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani mwacheni aongee.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Benaya Kapinga.

**TAARIFA**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kumpa taarifa mchangiaji, anachangia vizuri kwa kumpongeza Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi Paul Makonda kwamba anafanya kazi vizuri. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta, unaipokea taarifa? Malizia mchango wako pia muda umekwenda.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sipokei taarifa. Pia hiyo taarifa ni kwamba unakidhalilisha hata Chama chako, unadhalilisha Serikali yenyewe, hapo siyo suala la Makonda anafanya kazi vizuri, hapa ni suala kwamba majukumu ambayo amekwenda kuyafanya Ndg. Makonda ni majukumu ya Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi. Siyo Makonda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wapinzani tulivyoona ziara ya Makonda, tulianza kuogopa sana kwa sababu, Mama Samia Suluhu Hassan, ametekeleza Ilani ya Chama chake. Mama Samia Suluhu Hassan, amefanya mambo makubwa sana kwa wananchi. Kwa hiyo, tulitegemea anakwenda kuelezea namna gani Ilani ile imetekelezwa. Matokeo yake amekwenda kutatua kero za wananchi ambazo walipaswa kuzitatua.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dakika moja tu. Nusu dakika nakuomba.

**MWENYEKITI:** Malizia sekunde kumi Mheshimiwa.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, natambua tuko na Waziri wa TAMISEMI, naona hayupo lakini Manaibu wake wapo, nafahamu mtakuja mbele hapa ku-*wind up* kwa maana ya ninyi kuchangia, napenda kufahamu, kama Serikali kupitia TAMISEMI mmejifunza nini katika ziara hizi za Mheshimiwa Makonda na mnakwenda kufanya nini kuhakikisha Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanawajibishwa kikamilifu kwa sababu hii ni hujuma ya moja kwa moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Chege, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kidogo. Napenda tu kusema naipongeza sana Serikali ya Mama yetu Samia Suluhu kwa maendeleo yaliyopatikana katika kipindi chake cha miaka mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwangu Musoma Mjini karibu changamoto kama siyo zote, basi tunakaribia kuzimaliza. Kwa maana tulikuwa na tatizo la maji, lakini mpaka hivi leo ninavyozungumza mabomba ya mwisho yameshafika kwa ajili ya kumalizia maeneo machache ambayo yalikuwa yamebaki bila maji. Pia namshukuru sana kwa maana tulipata fedha za kutosha, tumeweza kujenga vyumba vizuri vya madarasa, vyumba vipya pamoja na Shule za Msingi na Sekondari. Kwa hiyo, namshukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumeendelea kupata fedha kwa ajili ya kujenga vituo vya afya pamoja na zahanati. Mpaka hivi tunavyozungumza nilikuwa na kero kubwa sana ya stendi, lakini mpaka leo tunavyozungumza, tayari ma-*consultancy* wako *site* kwa ajili ya ku-*design* stendi mpya ambayo itakuwa kwenye Kituo chetu cha Bweri. Hii ni sambamba na barabara za lami ambazo zina-*cover* barabara ya Mtende, barabara ya Shabani kuelekea kule kwenye Kwangwa Hospitali. Hii ni pamoja na Soko la Nyasho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kusema nini? Mambo mengi mazuri kabisa yanaweza kufanyika, lakini yakajitokeza mambo machache sana yakawafanya wananchi na watu wakasahau yale mazuri yote yaliyofanyika. Kwa mfano, kwenye shule zetu za msingi na shule za sekondari, ukienda unakuta kuna vyumba vizuri sana vya madarasa vimejengwa. Sambamba na hilo, viko vyumba ambavyo ni vya zamani na maboma ya zamani. Cha ajabu, utakuta kuna wanafunzi wanakaa kwenye

darasa zuri, lakini wapo wanafunzi wanaokaa kwenye madarasa ya ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unapokuja kuniambia Serikali wanasema hebu iambieni halmashauri itenge fedha. Kwanza, leo halmashauri zetu nyingi zilisha-*paralyze* hazina hata mapato. Kwa hiyo, kwa namna yoyote ile, Serikali mlishasema kwamba hata wananchi sasa tuanze kuwapumzisha kwenye kutoa michango. Sasa, unajiuliza, hali hii tutaivumilia mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachotaka kusema, hebu sasa leo TAMISEMI watuambie wamejipangaje kumaliza vyumba vya madarasa ambavyo havijamalizika. Wamejipangaje kuhakikisha kwamba watoto wetu wote hakuna anayekaa chini? Sambamba na hilo, bado lipo tatizo kubwa la upungufu wa walimu. Unajua kuna hatua ambayo mwanafunzi akiipita ameipita. Leo unakuta kuna baadhi ya walimu *especially* wa sayansi unakuta shule nzima haina mwalimu wa *physics,* kemia na *biology.* Unakuta kwa vyovyote vile kwenye yale matokeo ya *form four* unakuta watoto wengi karibu nusu ya darasa wanapata *division zero. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani pamoja na mambo mazuri ambayo yamefanyika, lazima Serikali ijikite ihakikishe kwamba, kwenye haya madhaifu au huu upungufu uliopo, itenge fedha, vyumba vizuri vya madarasa viwepo, madawati yawepo, walimu wapatikane, watoto wetu wasome ili maisha yao yaendelee kuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, hata kwenye vituo vya afya tunashukuru. Mfano, ukienda pale kwangu kuna Kituo cha Rwamlimi, Serikali imeleta fedha, tumejenga Kituo kizima cha Rwamlimi kimekamilika. Tofauti na hapo, jirani yake tu kuna Kituo cha Afya cha Bweri, kila siku mimi nikisema, hapo Mawaziri wanasema halmashauri itenge fedha. Sasa itatenga fedha mpaka lini? Nashauri tujipange tu tuweze kupeleka fedha ili vile vituo vyote vya afya view vizuri na viweze kutoa huduma nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni kati ya upungufu mkubwa ambao bado upo ambapo pamoja na mafanikio mengi makubwa yaliyofanyika, haya machache yanaendelea kutuchafua. Niwaambie kwamba huku tunakoenda safari hii ndugu zangu wa TAMISEMI, kusema kweli niwaambie kabisa, bahati nzuri tunaonana uso kwa uso. Safari hii rafiki zangu shilingi yenu naenda nayo. Kwa sababu haiwezekani huu upungufu uliopo uendelee kutuchafua wakati tukijipanga vizuri, wala siyo fedha nyingi zinatakiwa, tunaweza kuyamaliza na watu wetu wakaendelea kuishi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, liko jambo ambalo sasa aidha Wizara ya Afya ilitolee tamko au iamue. Sera yetu inasema hivi, mtoto chini ya miaka mitano atibiwe bure, mama mjamzito apate huduma za kujifungua bure. Naamini hata kule kwako hali kama hiyo ipo. Siku moja ilitokea nikaenda tu ghafla kwenye kituo kimoja cha afya nikakuta akinamama wanane wamejifungua, kila mmoja ametoa shilingi 120,000 shilingi 80,000 na kadhalika. Sasa ukimwuliza daktari, anasema Mheshimiwa Mbunge ni kwa sababu hatuna dawa, kwa hiyo, tunalazimika kuwa-*charge* fedha. Sasa tuna sababu gani ya kusema kwamba hizo huduma wanazipata bure, lakini wakati huo huo wakienda kule wanaweza kuwa *charged?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, hata kuna siku moja ambayo nilienda kwenye mkutano, nikasema akina mama wanatibiwa bure, walinistahi tu kwa sababu mimi ni Mbunge wao, lakini ukiona akina mama wamevaa nguo za CCM wanaguna, ni kwa sababu hao wote wanalipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikaamua moja, aidha itoe hizo huduma bure kama ilivyosema na isimamie, na kama haiwezi, basi iwaambie wananchi kwamba wachangie ili wazoee na waone kama ni jambo la kawaida, kuliko kuwaahidi kitu ambacho tunadhani kwamba hatuna uwezo wa kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo sielewi kwamba ni kwa nini limechukua muda mrefu na hata Serikali ilifikia mahali ikasema kwamba limeisha lakini halijaisha, ni mikopo

kwa ajili ya akinamama, watu wenye ulemavu pamoja na vijana. Sasa, zile fedha tulifika mahali Mheshimiwa Rais akasema utaratibu wake hauendi vizuri, kwa hiyo, anasitisha ili Waziri mwenye dhamana apange utaratibu mzuri na hatimaye hizo fedha waweze kukopeshwa. Sasa leo nadhani ni mwaka wa pili, utaratibu kila siku tunaendelea kusema unapangwa, lakini haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yako, hata zile fedha ambazo tumewaambia kwamba zinaendelea kutengwa kule halmashauri, hivi wanatengaje fedha wakati kule Madiwani hawana posho?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimalizie tu kwamba hebu Serikali iweze kulimaliza hilo na iweze kuwaruhusu wale akina mama waweze kukopesheka na maisha yao yaweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jafari Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Niungane na wenzangu kwanza kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia TAMISEMI, kwa niaba ya wananchi wa Kata ya Goride Kijiji cha Nyamusi kwa kutupatia fedha. Sasa nimepigiwa simu na Injinia wa *TARURA* Mkoa, kuwa wametupatia fedha zaidi ya shilingi milioni 92 kwa ajili ya ujenzi wa daraja ambalo lilikuwa linaunganisha wananchi wa Kitongoji cha Mariwa na Kijiji cha Nyamusi. Nachukua nafasi hii kuwashukuru sana kwa sababu katika daraja hili wananchi wengi wamekuwa wakipoteza maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa masikitiko makubwa sana. Kwanza, niseme tu, mimi ni miongoni mwa wale Wabunge ambao hata baada ya Bunge hili kukamilika na kurudi jimboni, sijui ni barabara ipi ambayo inaweza ikanifikisha maeneo ambayo natakiwa kuzungumza na wananchi, kwa sababu barabara zote kati ya 12, barabara nane hazipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Rorya maeneo mengi shughuli kubwa ya kiuchumi tunayoitegemea ni ziwa. Katika barabara 12, barabara nane zinatupeleka maeneo ambayo halmashauri ndiyo inategemea kukusanya mapato, ambayo ni maeneo ya ziwani. Katika barabara 12, barabara nane zote hazipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe kidogo, tarahe 31 mwezi wa Kwanza, ilikuwa ni siku ya Jumatano kilikuwa ni Kikao cha Bunge hili, alisimama Waziri wa Fedha na akaahidi ndani ya Bunge hili baada ya baadhi ya Wabunge kuuliza maswali ya nyongeza na maswali ya msingi. Akasema atahakikisha fedha ya dharura ya utengenezaji wa barabara inakwenda kwenye majimbo ambayo, kwenye maeneo yote ya halmashauri ndani ya nchi hii, ambako barabara hazipitiki. Akaendelea mwishoni akasema, atahakikisha fedha hizi zinakwenda kabla ya Bunge hili kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni siku ya Jumanne, tuna siku mbili zimesalia hakuna fedha yoyote ya dharura iliyokwenda kushughulika na barabara hizi. Wananchi wanateseka, hakuna namna ambayo unaweza ukafika kutoka eneo moja kwenda maeneo mengine. Kwenye halmashauri zetu sisi tunategemea shughuli za kiuchumi magari yaende yakafanye ulanguzi kwenye maeneo ya ziwani, kwa ajili ya kuchukua samaki kwa wavuvi. Magari hayafiki. Mimi ni Mbunge ambaye nimeenda kwenye maeneo hayo, nakwama zaidi ya mara mbili, nasukumwa na wananchi. Una majibu gani ya kuwaambia hawa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema, kwa kuwa hoja ya leo tunaizungumza hapa na tunachangia, Mawaziri watapata nafasi pia ya kuchangia na siyo kuhitimisha hoja, kwa sababu hoja kwa mujibu wa kanuni zinahitimishwa na Wenyeviti

wa Kamati. Naomba kwa ridhaa yako, kwa hizi siku mbili zilizosalia na nitaomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono, tulete Hoja ya Dharura itakayojadili barabara za dharura nchi nzima kwa umoja wake na tutoe maazimio ya moja kwa moja yatakayokwenda Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea hivi tunazungumza, Waheshimiwa Mawaziri watasimama hapa kujibu hoja, bado kule wananchi ni shida. Hebu niambie, leo kama kauli imetoka kwa Waziri wa Fedha mwenye dhamana kwamba atahakikisha kuwa fedha inakwenda kabla ya tarehe 31, mimi leo nakwenda Jimboni nawaambia nini wananchi? Kwa sababu wameisikia Serikali na Waziri mwenye dhamana amesema kabla ya Bunge kwisha fedha zitakuwa zimekwenda. Hakuna fedha maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono, ndani ya hizi siku mbili kama hakuna fedha ya dharura, tulete hoja ndani ya Bunge hili, tujadili kama tulivyokuwa tukifanya maeneo mengine. Tuliwahi kujadili hapa kuhusiana na *issue* za kilimo. Kuna maeneo ambayo wakulima walikuwa na changamoto, tukaleta hoja, tukajadili na Serikali ikapeleka fedha. Kwa maelekezo mahususi au azimio ndani ya Bunge, ninaamini hili linaweza likawa suluhisho kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni *issue* ya Madiwani kusimamia Miradi ya Maendeleo; utakubaliana nami kwamba, hakuna sehemu ambayo haisimamiwi kwa sasa hivi kama miradi ya maendeleo maeneo mengi ninayokwenda nchini. Kwa mfano, kwangu hakuna Diwani anayekwenda kukagua shughuli za kimaendeleo zinazofanyika ndani ya Jimbo. Kwa nini? Kwa sababu hawana fedha, hawana uwezesho wa halmashauri kuwapeleka kukagua yale maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara kwa maana ya TAMISEMI, ipeleke maelekezo mahususi kwamba miradi yote ya maendeleo Madiwani wote wakague kama mnavyofanya ndani ya Bunge. Sisi tunapata nafasi ya kwenda kukagua miradi ya maendeleo, tunakuja kuchangia ndani ya Bunge. Madiwani wasipokwenda kujiridhisha fedha za miradi ya maendeleo maana yake ni nini? Watakuwa wanaletewa makabrasha ndani ya Vikao

vya Madiwani bila kujua huo mradi unaendeleaje. Ndiyo maana unaona miradi haikamiliki, upotevu wa fedha unakuwa mwingi na bahati mbaya sana sisi Wabunge wakati vikao vinafanyika tunakuwa hatupo maeneo ya majimboni, wengi tunakuwa huku. Kwa hiyo, naomba Wizara ya TAMISEMI itoe mwongozo mzuri kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, natambua umenipa dakika tano, mapitio ya kanuni. Nakubaliana kabisa na Kamati yafanyike mapitio ya Kanuni ili angalau Vikao vya Baraza la Madiwani viweze kufanyika wakati ambao Wabunge tupo Majimboni tuweze kushiriki kutoa michango ya kusimamia miradi hii ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chege. Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, atafuatiwa na Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, na Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami nianze kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa na Kamati yetu na pia hoja zote mbili kwa maana iliyoletwa na Kamati ya USEMI na ile ya Utawala na Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli yamezungumzwa mengi sana nami binafsi yangu nataka kuchangia katika baadhi ya maeneo. Serikali ilikuwa inaongeza Bajeti mara kwa mara, na katika maeneo mengi sana tunashuhudia mabadiliko makubwa sana ya kimaendeleo hasa katika maeneo yanayohusu huduma za wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hivyo, pia yako maeneo ambayo kwa kweli tunaweza kusema kwa namna moja au nyingine ongezeko hili la bajeti limeleta mchango ambao uko chanya kabisa kwa maana ya kusaidia wananchi wetu kama ambavyo imeelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, pia nataka niishukuru Kamati kwa kuweza kuangalia mambo ya msingi kabisa ambayo sisi kama Wizara kwa upande wetu yanatupatia nafasi ya kwenda kuboresha zaidi majukumu yetu, na kwa namna moja au nyingine kuendelea kuyafanyia kazi yale ambayo yanaonekana kuwa ni upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu mimi nataka niseme tu kwa niaba ya Serikali naunga mkono sana mawazo yote mazuri yalitolewa na watu wote waliochangia, lakini na mimi nataka niongezee kidogo katika maeneo hayo, kwa mfano katika hili eneo ambalo Kamati imeeleza kwamba walemavu ni kama wamesahaulika

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nilihakikishie Bunge lako, lakini pia kuwaambia umma wa Watanzania pamoja na Bunge lako kwamba, Serikali imeendelea kuwaangalia watu wenye mahitaji maalum katika maana ya ajira, lakini pia katika kuzingatia wanapewa kipaumbele kikubwa, hasa nafikiri katika upendeleo hasa katika eneo hili la utoaji wa ajira. Kupitia Gazeti la Serikali lenye kumbukumbu namba 326 ambalo lilieleza juu ya mabadiliko ya Kanuni ya 17 ya usaili wa katika eneo la watu wenye ulemavu ni kwa kweli, upendeleo mkubwa sana umefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikiri mbele ya Bunge lako kwamba, bado changamoto zipo katika baadhi ya maeneo, lakini kiukweli katika kipindi cha miaka mitatu zaidi ya watu wenye ulemavu 190 wameajiriwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo wanaume 108 na wanawake 82, wote wakiwa ni sehemu ya wafaidikaji. Lakini pamoja na hilo pia, nataka niunge mkono juu ya hoja iliyoelezwa na kamati yetu kuhusiana na malimbikizo ya madeni ya watumishi. Kwa kweli, kibinadamu haipendezi, inauma na ni wajibu wetu kama Serikali, ni wajibu wetu kama Bunge kuendelea kuwasemea watumishi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nipongeze juhudi mbalimbali ambazo zimeendelea kufanywa na Serikali yetu, hasa baada ya kutambulisha mfumo wa mishahara na taarifa za kitumishi ambao kwa lugha ya kitaalamu unaitwa *HCMIS* ambao

mfumo huu umesaidia sana kupunguza madeni, lakini pia na malimbikizo mbalimbali ambayo watumishi wetu walikuwa wanadai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hadi kufikia Disemba, 2023 Serikali imefanikiwa kulipa bilioni 210.67 ikiwa ni sehemu ya madai makubwa ya watumishi zaidi ya 125,147 ambao wamekuwa wanaidai Serikali. nataka nikuhakikishie katika fedha hizo ambazo zimelipwa, ndani ya makundi hayo, Serikali imelipa bilioni 157 kwa watumishi ambao walikuwa wanadai katika malimbikizo ya upandishwaji wa vyeo na kubadilishwa muundo wao wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mengi mazuri yamefanyika katika Serikali na ninataka Bunge lako niendelee kulishawishi kuamini kwamba, Serikali bado inaendelea kufanya mambo mazuri na hayo yanaweza kutafsirika katika eneo kama la bajeti ilivyoongezeka, hasa katika Ofisi yetu ya Rais, Utumishi ambapo asilimia 17 bajeti imeongezeka ambayo tafsiri yake imetafsiriwa katika eneo la kazi na ikiwemo mojawapo kwenye uundaji wa miundo au mifumo ya kiserikali, kuwezesha utoaji huduma nzuri kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hilo tu pia nataka niongee katika eneo moja ambalo limechangiwa na Wabunge wengi, hasa wakiongozwa na Mheshimiwa Janejelly Ntate ambaye alizungumzia hasa juu ya maslahi ya watumishi, hasa wanawake ambao wakipata likizo zao wamekuwa wanapunjwa, lakini wakati mwingine wanapata matatizo makubwa wanapoomba likizo hasa baada ya wenzetu kujifungua watoto njiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza asubuhi juu ya utayari wa Serikali kukutana na wadau katika mabadiliko makubwa tunayokuja kuyafanya kwenye sheria zetu za utumishi, kuweza kuingiza kundi hili maalum ambalo linakwenda kutatua vilio vya walio wengi, akinamama zetu. Tunaamini katika nchi hii ambayo tuliamua kumpa Rais wa kwanza mwanamke, Dkt. Samia Suluhu Hassan awe kiongozi wetu kwa kuleta maendeleo, hatuwezi kuwaacha nyuma hawa ambao wanazaa watoto njiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuona unavyoshika kengele yako, maana yake muda wangu umetosha. Hoja nyingine zote kama zilivyotolewa na Kamati tunachukua, tutakwenda kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, Mheshimiwa Deo Ndejembi ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu na kwanza nichukue fursa hii nimshukuru Mungu kwa kuwa ametujalia tuko hapa, lakini pia nichukue fursa hii nami kwanza niunge hoja mkono kwa Taarifa za Kamati ambazo zimewasilishwa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nichukue fursa hii niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri waliyoichangia, lakini nichukue fursa hii nimshukuru sana Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye maeneo mbalimbali, lakini hasa kwenye jambo la kuuendeleza muungano wetu, lakini katika jambo la kuendeleza kutunza, kuhifadhi mazingira yetu na kupambana dhidi ya athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumezungumzwa mambo mengi, lakini miongoni mwa mambo yaliyozungumzwa ni jambo la hoja ya muungano ambalo kwa upande wa hoja hii Waheshimiwa Wajumbe wamepongeza sana kwa hatua kubwa iliyofikiwa, lakini vilevile kumegusiwa jambo la mazingira hasa kwenye jambo la biashara ya hewa ya ukaa. Nataka niwaambie Waheshimiwa pongezi ambazo wamezitoa, hasa kwenye tasnia ama kwenye eneo hili la muungano ni kwa sababu, kwanza ya juhudi kubwa ambayo Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan anaifanya katika kuendeleza kutuunganisha Watanzania na kuhakikisha kwamba, tunaendelea kuwa kitu kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja za muungano zilikuwa nyingi ama changamoto zilikuwa nyingi, lakini ndani ya kipindi chake Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan zaidi ya hoja 14 amezitatua na leo muungano wetu uko salama na unakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa zaidi katika kuendeleza timu ambayo imeundwa. Timu hii ama Kamati hii ya majadiliano ya hoja za muungano imekuwa inafanya kazi kubwa na ndio maana umefika wakati sasa imetolewa maelekezo kamati hii iwe inakutana ndani ya kipindi cha miezi mitatu; kila miezi mitatu ikutane ili lengo na madhumuni tusiendeleze kulea changamoto za muungano kwa muda mrefu, maana yake zikitokea, tukae tutatue muungano usonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ni busara za viongozi wetu Dkt. Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Pili wa Rais, lakini Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano nao wanafanya kazi kubwa katika kuuboresha na kuutunza Muungano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamezungumzwa jambo hapa la biashara ya hewa ukaa, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira tupo tayari na tumeendelea kuchukua hatua mbalimbali. Moja, tumeshaanzisha tumefungua kituo maalum, kituo ambacho kinatoa taarifa zote sokoine pale, kituo ambacho kinatoa taarifa zote, lakini kituo ambacho kinaendeleza kufanya utafiti. Kituo ambacho kinaendelea kusaidia wawekezaji na watu wengine ambao wako *interested* katika kutaka kujua juu ya suala zima la biashara hii ya hewa ya ukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kutoa elimu, tumeanza kwa Halmashauri, tumekwenda kwa Wakuu wa Mikoa, tumekwenda kwa Wakuu wa Wilaya, tumewapa Wabunge, wawakilishi na sasa tunataka tushuke kwa wananchi mmoja-mmoja, ili waielewe biashara hii ili lengo na madhumuni wananchi waweze kufanya biashara hii, lakini wao wapate kipato na maendeleo kupitia huduma za jamii yapatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tunaendelea kuendelea kuwashauri wananchi kuwaambia kwamba, sisi kwanza tuko tayari kushirikiana nao. Muwekezaji yeyote ambaye yuko *interested* na biashara hii na yuko tayari kufuata sheria na taratibu zilizowekwa kwa sababu, tulishaandaa muongozo na muongozo umeshatoka wa biashara ya hewa ya ukaa maana kule nyuma tulikuwa tunakwenda, lakini tukasema tuandae muongozo maalum ambao utawapa wananchi dira na muelekeo katika kuendeleza biashara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muongozo upo, wawekezaji waje, ili lengo na madhumuni wananchi wapate, lakini na huduma za jamii ziendelee, na tayari iko Mikoa ambayo tumeshaanza kutoa hizo huduma, hospitali zipo, elimu zipo, maji safi yapo na huduma nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi niendelee tu kuunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Ndejembi, Mheshimiwa Hamad Chande ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia afya njema, lakini pili nikushukuru sana wewe. Nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati yetu Mheshimiwa Dennis Londo, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kazi nzuri sana wanayofanya kushauri, kutoa maelekezo na mapendekezo mbalimbali ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na sisi tuwahakikishie kupitia Waziri wetu wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tutahakikisha mapendekezo, ushauri na maelekezo yote ambayo mnayatoa tunayatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba niongee katika maeneo makubwa mawili, nitaanza nae neo la utawala; Waheshimiwa Wabunge wametoa hoja nyingi muhimu na moja ya hoja ni kuhusiana na namna ambavyo watendaji wetu na viongozi wetu katika ngazi za Mikoa na Wilaya hawajaonesha ufanisi katika kutatua kero za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge hapa wamejaribu kulinganisha ziara ya Mwenezi wetu *Comrade Makonda* na namna ambavyo wananchi wanaibuka na hoja nyingi, kero nyingi, ambazo kwa kweli kero nyingi ziko ndani ya uwezo wa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, ziko ndani ya uwezo wa Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, ziko ndani ya uwezo wa Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi na watendaji wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Rais aliwapa dhamana viongozi hao na sisi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tumeendelea kusisitiza na kuchukua hatua kwa watendaji na viongozi wote ambao kimsingi hawatekelezi ipasavyo majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba na sisi tunaendelea kufanya tathmini. Maeneo yote ambayo ambayo tunaona kuna viongozi hawajatekeleza ipasavyo majukumu yao hatustahili kusubiri Mwenezi wa Taifa wa CCM afike kutatua kero za *DC* ambazo *RC* angeweza kuzitatua wakati wamepewa wajibu huo. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, jambo hilo tunalifanyia kazi na tutashauri mamlaka ya uteuzi kwa pale ambapo tutajiridhisha kwamba, hawajatekeleza majuku yao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili lilikuwa ni posho; tunatambua sana kazi kubwa inayofanywa na Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Vijij: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka Bunge hili mwaka wa fedha 2021/2022 lilianzisha kulipa posho kwa Waheshimiwa Madiwani katika Halmashauri 168. Huko nyuma Madiwani

walikuwa wanakopwa posho zao, wanakaa miezi sita bila kulipwa posho, lakini sasa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan analipa posho kwa halmashauri 168, hakuna Diwani akakopwa posho, wote wanalipwa kwa wakati. Tunafahamu tunahitaji kuongeza kiwango cha posho, Serikali inaendelea kuongeza uwezo wa mapato yake, ili tuweze kufanyia kazi suala la posho hizi za Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti ziweze kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la tatu ilikuwa ni susla la utoaji wa posho za watendaji wa kata; niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Serikali ilishatoa maelekezo madhubuti kwamba, Wakurugenzi lazima walipe posho za Maafisa Watendaji wa Kata na wameendelea kulipa. Kwa miezi mitatu iliyopita ni halmashauri 80 kati ya 184 ambazo hazikulipa, na Serikali imeshachukua hatua kwa Wakurugenzi hao, kwanza kuhakikisha wanalipa posho mapema iwezekanavyo, lakini pili kuhakikisha kwamba, wanaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kulipa posho hizo.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Janejelly Ntate.

**TAARIFA**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nina mtandao wote wa Tanzania nzima. Hakuna mahali ambako wamelipa inavyostahili na hakuna mahali ambapo hawadai chini ya miezi kumi, *message* zao ziko humu. Naomba nimpe Taarifa, leo, utoe tamko kwa hawa Wakurugenzi walipe hizi posho. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, taarifa hiyo unaichukua?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea Taarifa ya Mheshimiwa Mbunge, nimesema

kwamba, bado kuna changamoto ya baadhi ya Halmashauri kutolipa posho hizo na tumechukua hatua na tumeelekeza Wakurugenzi kufanya hivyo. Kwa hiyo, tamko ambalo tumelitoa hapa kama Serikali kwamba ni wajibu wa Wakurugenzi kuhakikisha wanalipa posho kwa watendaji wa kata kwa wakati na kuhakikisha wanatenga bajeti za uhakika, ili Maafisa Watendaji wa Kata wapate posho hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee kidogo sekta ya afya; sote hapa, Waheshimiwa Wabunge wamechangia, lakini wote kwa pamoja tumepongeza kazi kubwa sana iliyofanywa na Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yetu ya Awamu ya Sita katika ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, hpspitali za halmashauri, magari ya wagonjwa, vifaa-tiba kila sehemu. Niwahakikishie zoezi hilo ni endelevu, tutahakikisha tunaendelea kujenga vituo hivyo katika bajeti inayofuata, lakini pia kununua vifaa-tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana; Mheshimiwa Deo Ndejembi, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Chande, Mheshimiwa Geophrey Pinda ajindae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kukushukuru wewe pamoja na Bunge lako Tukufu, vilevile nitumie nafasi hii kupongeza sana kazi nzuri ambayo imefanywa na Kamati hizi mbili ambazo hoja zipo Mezani hapa; Kamati ya Utawala, Sheria na Katiba, lakini vilevile Kamati ambayo mimi ni Mjumbe kwa nafasi yangu, Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Niwapongeze Wenyeviti wa Kamati hizi, Dkt. Mhagama pamoja na Mheshimiwa Londo na Wajumbe wa Kamati zote hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo utajikita katika sehemu mbili; sehemu ya kwanza ni miundombinu ya barabara ambayo inasimamiwa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini *(TARURA)* ambao Waheshimiwa Wabunge wengi pia nao

walijikita sana katika michango yao kwenye kuchangia suala zima la barabara zetu za mijini na vijijini hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri changamoto zipo, changamoto hizo zimetokana na athari kubwa iliyoletwa na mvua za *Elnino*, mvua ambazo zilitabiriwa kuja nchini kwetu na zimekuja kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba athari tunayoiona leo ni ndogo kulingana na ambavyo ingekuwa endapo *TARURA* ingekuwa haijafanya kazi yake vizuri katika miaka ya nyuma toka uanzishwaji wake, ni athari ndogo kuliko ambavyo ingekuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hapa *TARURA* ilipoanzishwa mwaka 2017 barabara za lami zilizokuwa chini ya mtandao wao zilikuwa ni kilometa 1,449 hivi sasa tunavyozungumza mwaka huu 2024 mtandao wa lami ni kilometa 3,224 ina maana zimeongezeka, lakini changarawe kutoka kilometa 24,405 hadi kilometa 41,107 lakini vilevile barabara ambazo ni za udongo kutoka kilometa 83,091 kwenda kilometa 100,098.13. Utaona hapa jitihada kubwa ambayo imefanyika na Serikali katika kuhakikisha barabara zetu za mijini na vijijini zinapitika vizuri na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije katika suala ambalo limezungumziwa sana hapa. Suala zima kuhuzu upatikanaji wa fedha; ni kweli, wakati wa kuwasilisha taarifa katika Kamati ya Utekelezaji wa Bajeti ya nusu mwaka fedha ambayo ilikuwa imefika ilikuwa ni bilioni 82 katika taarifa ile iliyowasilishwa kwenye Kamati ya TAMISEMI. Lakini hadi hivi ninavyozungumza sasa jumla ya fedha ambayo *TARURA* imepokea kutoka wenzetu wa Wizara ya Fedha ni bilioni 309. Ni kuonesha ni namna gani ambavyo jitihada inafanyika kuhakikisha barabara zetu zinapitika na zinatengenezwa, hasa kipindi hiki ambacho nyingi zimepata madhara kutokana na mvua ambazo zinanyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sawa na asilimia 43 ya bajeti ambayo imetengwa kwa ajili ya *TARURA,* na tayari jitihada zinaendelea, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa na Waziri wa Fedha Mheshimiwa

Mwigulu Mchemba tayari wamekaa vikao mbalimbali vya kukubaliana ni namna gani tunazidi kupokea fedha na kuwapelekea wenzetu wa *TARURA,* ili barabara zetu ziweze kutengenezwa na kupitika kwa wakati.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ya dharura ambayo ilitengwa kwenye bajeti ilikuwa bilioni 21.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Salome Makamba.

**TAARIFA**

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachojaribu kukisema Mheshimiwa Waziri, anataka kuonesha kwamba, Wabunge au Wajumbe wa Kamati ni waongo au yeye ni muongo, kwa sababu Taarifa ambazo kamati inazo na mimi ni Mjumbe, mpaka tunaingia kwenye Bunge hili, pesa zilizopelekwa ni bilioni 89 tu na zile fedha za dharura. Hiyo bilioni mia tatu na ngapi ni taarifa ambayo anaisema hapa ambayo hakuna Mbunge yeyote katika Bunge hili anaweza kuthibitisha jambo hilo. Yaani anaijua yeye na *most of the time* kama pesa imeingia leo kuna hatihati ikawa ni *exchequer* hiyo, sio hela ambayo…

**MWENYEKTI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba tu yaani anachokisema hakuna anayeweza kukithibitisha, yaani ni *fallacy,* anatuletea hadithi ambayo sisi hatuwezi kukubaliana nayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Salome. Mheshimiwa Naibu Waziri Taarifa unaipokea?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hiyo siipokei kwa sababu nilishasema kwamba Taarifa tuliyowasilisha kwenye Kamati ya nusu mwaka ya utekelezaji wa bajeti, Mheshimiwa Makamba amezungumza, ni sahihi ilikuwa ni bilioni 89, lakini nikikwambia kwamba, *exchequer* ikitolewa na Hazina wenzetu ni sawasawa na fedha ambayo imelipwa kwetu sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naendelea kukupa taarifa ya kwamba, ukiachilia *exchequer* ambayo ni bilioni 309 fedha iliyolipwa ni bilioni 262 hadi siku hii ya leo ambayo ni asilimia 85 ya fedha yote ambayo ilikuwa imetolewa *exchequer,* na bado tunavyozungumza Serikali ipo kazini ni kwamba, fedha hiyo inaendelea kulipwa. Ndio maana nasema taarifa ninazozitoa ni mpaka hivi sasa katika uchangiaji wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambayo ilikuwa imetengwa kwa ajili ya dharura nchi nzima, ilikuwa bilioni 21, na mpaka sasa fedha yote hiyo imepokelewa, lakini baada ya tathmini kwa kumalizia, baada ya tathmini kufanyika iligundulika inahitajika bilioni 65 kwa ajili ya dharura ya hizi mvua ambazo zimeendelea sasa. Hivi sasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango wanakaa katika kuona ni namna gani tunapata hiyo *deficit* ya bilioni 44 katika kipindi hiki kwa ajili ya kutengeneza barabara ambazo zimeathirika sana. Ahsante sana.

**MWENTEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Hamad Chande, atafuatiwa na Mheshimiwa Geophrey Pinda, Mheshimiwa Patrobass Katambi ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na awali ya yote nami niungane na wenzangu katika jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim, Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia rasilimali ya uhai hadi sasa tunaendelea nayo, kwani ndiyo thamani peke yake ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili napenda kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo naifanya katika nchi yetu hii. Nawapongeza sana Wenyeviti ambao wamewasilisha leo taarifa zao. Kwa kweli wamewasilisha kwa ufanisi na weledi mkubwa sana. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nawapongeza Wajumbe wa Kamati hizo pamoja na Wabunge wenzangu kwa namna wanavyochangia hoja katika kujenga Taifa hili. Ni Wabunge wengi ambao wamechangia katika hoja tofautitofauti ambazo ni hoja nzuri na za msingi kabisa. Miongoni mwa hoja hizo zimegusa kwa njia moja ama nyingine Wizara ya Fedha. *So*, niseme kwamba hoja zote ambazo zimetolewa, maoni na ushauri ambao umetolewa tumezipokea kama Serikali na tunaenda kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache kabisa kwa sababu ya muda, naomba nijielekeze tu moja kwa moja kwenye suala zima la miundombinu ya barabara ambayo imetajwa na Wabunge wengi katika Taasisi yetu ya *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi kuongeza bajeti kwa kiasi cha shilingi bilioni 350 ili kutatua changamoto za miundombinu ya barabara katika halmashauri zetu zote nchini. Kwa sasa, Serikali kupitia *TARURA* ipo kwenye hatua za ununuzi ili miradi hiyo iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa miradi ya barabara inatekelezwa kwa kipindi cha miezi sita hadi miezi 18 (mwaka mmoja na nusu). Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, itahakikisha fedha za malipo ya awali *(advance payment)* inalipwa kwa wakati unaostahiki mara tu baada ya mikataba hiyo kusainiwa. Hivyo, naomba nikuhakikishie na nilihakikishie Bunge lako Tukufu pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba, fedha hiyo ya miradi hiyo ambayo imetajwa, kiasi cha shilingi bilioni 350 zitatekelezwa kama ilivyopangwa na ilivyoahidiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nirudie kukuhakikishia kwamba, Wabunge waondoe shaka katika hili.

Fedha hiyo itatolewa kwa wakati kabisa ili kutekeleza miradi hiyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ameshamaliza mchango wake. Tunashukuru sana. Mheshimiwa Geophrey Pinda, atafuatiwa na Mheshimiwa Patrobass Katambi. Mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii. Kwa sehemu kubwa sana nitachangia kwenye Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

Kwanza, napenda kuunga mkono hoja lakini nipongeze Kamati zote mbili ambazo zimetoa wasilisho lake leo, na maalumu kwa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa hoja mbalimbali ambazo zimetolewa mapendekezo na maazimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria inaungana kwa ujumla wake juu ya mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati hii ya Utawala Katiba na Sheria na hasa kwenye maeneo yafuatayo; moja, majengo ya Mahakama ya Mwanzo yaboreshwe kwa kufanyiwa ukarabati. Tunapokea ushauri. Vilevile, tunataka tu kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, majengo mengi ya Mahakama za Mwanzo ni ya miaka mingi sana. Mengi yamejengwa kati ya miaka ya 1950 – 1960. Mengine yamerithiwa. Mahakama hizi zote, hasa zile za majengo yasiyokarabatika, haya tunakwenda kubadili na kuyajenga majengo mapya na kasi ya ujenzi ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili lililotolewa kama ushauri kwa Serikali, Serikali ijenge majengo ya Mahakama za Mwanzo kwenye maeneo ambayo hayana Mahakama za Mwanzo. Zoezi linaendelea. Tayari Mahakama za Mwanzo zipatazo karibia 60 zilishafanyiwa kazi, na kwa kipindi hiki cha fedha 2024/2025, zinakwenda kujengwa Mahakama za Mwanzo 32 katika maeneo mbalimbli hapa nchini. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge ambao maeneo yao hayajafikiwa na majengo mapya, majengo yanakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu katika eneo hili ni matumizi ya TEHAMA. Napenda tu kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge, Mahakama yetu ya Tanzania imefanya mageuzi makubwa sana kwenye eneo la TEHAMA. Mtakubaliana nami, kwamba katika maeneo yote ya Mahakama ambazo zinaanzia ngazi ya wilaya kupanda juu mpaka kwenye Mahakama Jumuishi, Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria imepita kwenye majengo ambayo sasa yako kwenye TEHAMA ya kisasa kabisa. Tuwaahidi tu kwamba, kwenye Mahakama hizi za Mwanzo kadiri zinavyoendelea kufanyiwa marekebisho makubwa ya ujenzi, TEHAMA inaenda kuchukua nafasi yake kwa sababu, karibu Mahakama zote nchini hilo ndilo lengo lake la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye eneo lingine ambalo Kamati imetoa maazimia yake, ni eneo ambalo imeshauri kutumia wale wanasheria wa halmashauri hapa nchini. Ushauri wao umepokelewa ingawa utapitiwa upya kwa sababu, yule mwanasheria wa halmashauri ni mwawakilishi wa *AG* kama ilivyo kwa sisi hapa Bungeni. Kwa hiyo, tunakwenda kupitia yale maeneo ambayo kimsingi yasije yakaleta usumbufu kwa wananchi kwa sababu hawa wanatakiwa kuwa *neutral* wakati watu wawili wanapogombana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na tunashukuru sana na tunaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Patrobass Katambi, atafuatiwa na mtoa hoja, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, kwanza nianze na kukupongeza sana wewe kwa kuendesha vema Bunge lako hili Tukufu.

Pili, niipongeze sana Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Londo tunampongeza sana kwa kazi hiyo kubwa ambayo ameifanya, Mheshimiwa Mhagama

lakini pia Makamu wake na Wajumbe wote wa Kamati. Tunawapongeza na tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja na kwamba tumepokea kwa heshima kubwa mawazo yote, michango, maoni, mapendekezo lakini pia maazimio ya Bunge ambayo yamefikiwa kupitia Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja chache ambazo ni za kufanyia kazi na nyingine zimeendelea kufanyiwa kazi kwa upande wa Serikali. Mojawapo ni uwepo wa kampeni ya kupiga vita dawa za kulevya ili kampeni hizi ziende kwenye ngazi za kuanzia vijiji, vitongoji kwenda ngazi za kata na ngazi za wilaya mpaka mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza sana Kamati kwa ushauri mzuri ambao tunaenda kuuzingatia. Pili, nieleze tu jitihada ambazo Serikali katika kutekeleza hayo imeanza kufanya. Mojawapo kwanza la muhimu sana ni uwepo wa utashi. Utashi madhubuti wa kuchukia dawa za kulevya na kuwa tayari kupigana vita ili zisiwepo, yasiweze kuathiri jamii yetu. Utashi huo unajidhihirisha kupita Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini pia sheria zetu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ambayo ipo kwa mujibu wa sheria. Katika kazi zake, mojawapo pia imekuwa ikifanya kazi za kutanuka katika mikoa na mamlaka zote za Serikali ili kuweza kuhakikisha kwamba tunadhibiti dawa za kulevya. Uwepo wa sheria peke yake ya dawa za kulevya ni ushahidi tosha kwamba tunachukizwa na uwepo wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili tunaloliomba kwa wananchi na Waheshimiwa Wabunge watusaidie, mapigano na mashindano dhidi ya dawa za kulevya ni ya wananchi wote, Watanzania wote wakiwemo viongozi Waheshimiwa Wabunge. Lazima tuchukue jitihada na hatua stahiki kuweza kuhakikisha tunakabiliana nayo. Kwa upande wa Serikali mpango mwigine ambao upo wa kuendelea kupambana na dawa za kulevya ni

mpango endelevu wa utoaji wa elimu. Tumekuwa tukitoa elimu kupitia vyombo vya habari, kwenye redio na televisheni na bajeti za Serikali zimekuwa zikitolewa kwa ajili ya kuhakikisha mamlaka inatekeleza wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo katika eneo la elimu, Mwenge wetu wa Uhuru ambao kila mwaka hukimbizwa nchini kote katika halmashauri 195, umekuwa na ajenda ya kudumu ya vita au mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Kwa hiyo, hata mwaka huu ninayofuraha, niliambie Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge, hata sasa ratiba ya Mwenge imetoka na moja ya ajenda muhimu ya kupambana na dawa za kulevya iko katika Mwenye huu wa Uhuru kama moja ya ajenda au kaulimbiu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika hatua nyingine Serikali ili kuhakikisha tunapambana na dawa za kulevya tumekwishafungua ofisi za kanda zaidi ya kanda nne. Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kati Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Ziwa na maeneo mengine. Shughuli na wajibu mkuu ni kuhakikisha wanapambana na dawa za kulevya na kuweza kuelimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine ambayo imechukuliwa na upande wa Serikali katika kushibisha au kutekeleza hayo maagizo ya Bunge, mojawapo pia ni kutengeneza *clubs* mbalimbali. Zile *clubs* za UKIMWI zilizokuwepo nchini kote pamoja na *clubs* za upambanaji wa masuala ya rushwa katika shule zetu za sekondari na kwenye mamlaka mbalimbali za kijamii katika ngazi za wilaya na mikoa, nayo pia imekuwa ni sehemu mojawapo ya kutusaidia katika kutoa elimu dhidi ya dawa za kulevya na mapambano vidi ya dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ilikuwa inaongelea kuhusu kuongeza vituo vya matibabu hasa kutoa msaada wa kisaikolojia. Tafiti za mwaka 2011 – 2022 inaonesha kwamba tulikuwa tunahitaji mikoa zaidi ya 12. Ninayofuraha kukwambia kwamba katika mikoa tisa toka mwezi Januari 2024, tumeifikia na tumefungua vituo hivyo kwa ajili ya kutoa huduma za masuala ya

uraibu. Mwisho, tayari tuna ofisi za kikanda zaidi ya 16 na tunaendelea kuzifungua na vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ya mwisho ilikuwa kuimarisha udhibiti kwenye maeneo yetu ya mipaka. Siyo tu mipaka, hata kwenye maeneo ya vipenyo vilivyo rasmi na visivyo rasmi tumeshaweka utaratibu mzuri. Hizi *Scanner, Cargo Scanner* na mbinu nyingine za teknolojia ya kisasa ambazo si salama kuzisema hapa. Tanzania tumeendelea kuwa kwenye nafasi nzuri ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya. Kwa sababu ya usiri sitaweza kuzitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nakushukuru lakini pia nisisitize kwa sababu nimekuwa wa mwisho wa kufunga kwenye upande wa Serikali, tuamini kwamba dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali ni njema. Hata hayo maelezo mengi ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge, tunayachukulia kwa uzito mkubwa kwa sababu wananchi wa Tanzania ndio walioiweka Serikali hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan madarakani na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ndiyo iliyoaminika na kwamba tunaenda kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakumbuka kabla ya mafuriko, kipindi cha nyuma Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanatoa shukrani za fedha ambazo tulizipata kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Matokeo ya *El Nino* yameleta athari kubwa, si tu kwenye zile barabara za lami na madaraja, lakini tumeona athari imekuwa kubwa zaidi. Kama Serikali tumeyachukua haya kwa ajili ya kuweza kuhakikisha tunaweka bajeti ambayo itaenda kutibu majeraha yale ambayo yamefikiwa kwenye hayo maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dennis Londo Kuja kuhitimisha hoja yako.

**MHE. DENNIS L. LONDO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa maana imempendeza yeye mjadala huu kuchangiwa na wachangiaji wengi ambao ni wawakilishi wa wananchi, kujadili mambo ambayo yanawagusa wananchi. Walatini wanasema, "*Vox populi, vox Dei*" (Sauti ya Wengi ni sauti ya Mungu). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati tunamshukuru na tunaungana na Wabunge wengine kumshukuru Rais wetu Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Wengi wa wachangiaji wamezungumza mambo makubwa ambayo yanafanyika katika majimbo ya wachangiaji kwenye miundombinu ya elimu, afya na maeneo mengine. Natumia nafasi hii kumshukuru pia Mheshimiwa Spika wa Bunge letu ambaye pia ni Rais wa Mabunge ya *IPU*, Dkt. Tulia Ackson kwa namna na jinsi anavyozilea Kamati zake, Wabunge wake kutupa nafasi ya kuchangia katika ujenzi wa Taifa letu kupitia majukumu ambayo tumeaminiwa na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara ambazo wanasimamia, kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Shukrani zangu ni kwa Wabunge wote 22 ambao wamechangia na wote wameigusa Taarifa yetu ya TAMISEMI. Bila shaka ni kwa Sababu ya Ofisi hii ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inagusa maisha ya wananchi moja kwa moja ambao ni wapigakura wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote ambayo wamezungumza, sisi kama Kamati tuliyaeleza kwenye taarifa yetu. Kubwa kuliko yote ambalo Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia wamepata fursa ya kuelezea, ni kuguswa kwao na kutokuridhishwa kwa kiasi cha fedha ambacho kinaenda kwenye miradi ya kimkakati, hasa barabara na miundombinu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako limepitisha bajeti, lakini kiasi cha fedha ambacho kinaenda, Kamati haikuridhishwa na Wabunge hawakuridhishwa. Ni kweli kwamba ni asilimia 12 tu ya

bajeti ambayo imeidhinishwa ilienda mpaka tarehe 31 Disemba kwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini *(TARURA)*. Kuna mkanganyiko kati ya *exchequer* na *cash flow* ambayo kama Kamati tuliweka msisitizo kwamba tuambieni ni kiasi gani cha fedha ambacho kimeenda kwa wakala kwa ajili ya kulipa wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la barabara na miundombinu yake ni suala la kufa na kupona. Ni siasa lakini pia ni uchumi kwa wananchi wetu na kwa Taifa letu. Si suala la *TRAB* na *TRAT*. Hakuna Rufaa kwa wananchi wetu ambayo wanaweza kukata zaidi ya sisi kama wawakilishi wao kuzungumzia haya ambayo tunayashuhudia kule kwenye halmashauri zetu na wilaya zetu. Sisi tukishindwa hakuna atakaye weza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai ya Kamati na inaungana na wachangiaji wote ambao wamezungumzia ongezeko la bajeti kwa *TARURA*. Tunaishukuru sana Serikali, hata kwenye bajeti iliyopita iliongeza kiasi kikubwa cha fedha kwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini. Changamoto ni kwamba, hilo ongezeko ambalo tumeongeza halikwenda kama ilivyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako liliahidiwa shilingi bilioni 350 za ziada ambazo ilisemwa kwamba zingeweza kwenda kumaliza matatizo ya msingi kwenye barabara zetu. Kiasi hiki pia hakikwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kuna fedha ambazo ni *reinfest* za tozo ambazo pia mara ya mwisho kwenda kwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini ilikuwa ni mwezi wa tisa. Hali hii haiashirii ama haikidhi matumaini na matarajio ya wawakilishi wa wananchi ambao wako kwenye Jumba lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri tunahitaji Serikali kuja na mpango wa dharura ambao unatakwenda kujibu kero kubwa na changamoto kubwa ambayo imetokana na Mvua za *El Nino* ambazo zimeharibu barabara na miundombinu yake katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai ya Kamati kuitaka Serikali kutafuta vyanzo vya uhakika vya mapato ambavyo vitaisaidia Serikali kufikia lengo la trilioni 1.6 kwa miaka minne mfululizo ili tufikie lengo la asilimia 70 ya barabara zetu kuzitoa kwenye udongo kwenda kwenye changarawe, asilimia tatu kwenda lami na kumaliza changamoto ya vivuko kwenye barabara zetu na miundombinu yetu ya barabara, hasa katika maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naongeza muda mpaka tumalize shughuli iliyopo mbele yetu; Mheshimiwa Mwenyekiti endelea. *(Makofi)*

**MHE. DENNIS L. LONDO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, katika hili tungependa kuishauri Serikali kutafuta vyanzo vya fedha pia kuharakisha mchakato wa *TARURA Samia Infrastructure Bond* ili kiwe moja ya vyanzo ambavyo vinaweza vikawa *raised* kwa ajili ya kumaliza changamoto ya barabara na hasa kufikia lengo lile la shilingi trilioni 1.6 kumaliza changamoto ya miundombinu yetu ya barabara kwenye maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wamezungumzia kwa kirefu kuhusiana na mabadiliko makubwa ambayo yanatokea kwenye sekta ya afya na elimu. Ujenzi wa miundombinu lakini ununuzi wa vifaa vya kisasa kama mashine za mionzi na huduma za afya ya kinywa. Pamoja na manunuzi haya bado kuna changamoto ya uhaba wa wataalam pia walizungumzia suala zima la uwezeshaji mkubwa wa Serikali ambao umepelekea Halmashauri zetu kuendelea kuwa tegemezi kwa Serikali Kuu na hivyo kutoa mwanya wa kutumia mapato ya ndani ambayo ilikuwa ni lengo la Serikali kuwapa ahueni kuelekeza fedha hizo kwenye shughuli za maendeleo kama jukumu la TAMISEMI linavyoelekeza maendeleo vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili tunaitaka Serikali kuja na mpango, kuja na mwongozo, kuja na mkakati wa kusimamia fedha za mapato ya ndani kumaliza changamoto ambazo ni umaliziaji wa maboma ya huduma za zahanati, afya na elimu

katika maeneo yetu. Pia kuajiri vibarua ambao wanaweza wakajibu changamoto zetu za muda mfupi wakati Serikali inaangalia changamoto za muda mrefu. Fedha hizi za mapato ya ndani zikitumiwa vizuri zinaweza kumaliza changamoto yetu ya vyoo na madawati ambayo imekuwa ni changamoto kwenye miundombinu ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Shirika la Elimu Kibaha, wakati Scandinavia na Nordic wanatujengea kituo kile, shirika lile la afya walijenga hospitali kubwa, walijenga *FDC* kwa maana ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, walijenga Chuo cha Uunguzi, walijenga sekondari pale lakini walijenga pia chuo ambacho kilikuwa kinafundisha stadi mbalimbali kama ufugaji wa kuku, uvuvi na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika hili lilikuwa ni *model* ambayo ilikuwa na malengo ya kusambaza katika maeneo mengine ya nchi yetu na Afrika kwa ujumla. Shirika hili pamoja na kwamba limetoa wataalam mbalimbali wa kada mbalimbali ni masikitiko ya Kamati yangu kwamba juzi kwenye taarifa ambayo tulikuwa tumeitoa tuliiomba Serikali kupitia taarifa kama hii na Wabunge wamezungumzia hapa umuhimu wa kufuatilia Maazimio ya Bunge, kwamba shirika hili kwa umuhimu wake tuliitaka Serikali iliimarishe. Sasa tunaambiwa kwamba shirika hili ni moja ya mashirika ambayo hayajiendeshi kwa faida linaenda kuvunjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mahali ambapo tulitegemea kwamba shirika hili litupe *cash benefits* isipokuwa huduma, huduma, huduma. Shirika lile lilikuwa ni *package*, kitendo cha kuigawanya hospitali ya Tumbi kwenda Wizara ya Afya, kuchukua shule kupeleka Wizara ya Elimu - TAMISEMI na kugawanya vipande vipande haiendi kukidhi malengo ya msingi ya uanzishwaji wa shirika hilo. Jambo ambalo tunaitaka Serikali kufikiria upya uamuzi huo ambao hatuamini unaenda kukidhi malengo tarajiwa ama malengo halisi ya uanzishwaji wa shirika lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumezungumzia suala zima la utawala bora na katika hili tulikuwa tumezungumzia dhana

nzima ya *D by D,* na wachangiaji wengi walikuwa wamezungumzia idadi ya watu ambao wanatokea kwenye mikutano ya Mwenezi wetu wa Chama Taifa, wakielezea kero na shida mbalimbali. Kimsingi kamati tunaliona hili kama moja ya viashiria vya kufeli huo mfumo wa ugatuaji wa madaraka kwenye ngazi za chini. Ndiyo maana unaweza kuona wengi ambao wanalalamika ni waliodhulumiwa mashamba na ardhi lakini ukiuliza Maafisa Ardhi hawa wanaripoti Wizarani, hawaripoti kwa Mtendaji wa Kijiji, hawaripoti kwa Mtendaji wa Kata, hawaripoti kwa Mkurugenzi wa Wilaya ambaye kwa mujibu wa sera ya ugatuaji wa madaraka *before* huyu ndiyo alikuwa mwajiri, ana mamlaka ya uajiri na mamlaka ya nidhamu ya watumishi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai ya Kamati kuitaka Serikali kwenda kutekeleza kikamilifu Sera ya Ugatuaji wa Madaraka lakini pia kukemea kwa lugha ambayo itasikika na taasisi zake, kupinga jaribio lolote la kuchomoa sehemu ya madaraka ama mamlaka ya TAMISEMI kuamisha mamlaka ya TAMISEMI kwenye taasisi nyingine, badala ya kuimarisha tutaendelea kubomoa na hivyo kumuondoa mwananchi na nguvu ya mwananchi katika kuisimamia Serikali hasa katika ngazi ya chini kwenye Vijiji na Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumzia suala la ubadhilifu na matumizi mabaya ya rasilimali katika ngazi za Halmashauri. Ni rai ya Kamati kwa Serikali tunaiomba kuwe na namna bora sasa ya kuja na muarobaini, kuja na majibu ya uhakika ni lini mambo haya ambayo yanachefua kila mtu binadamu hata na Mwenyezi Mungu yanaenda kumalizika. Vitendo ambavyo vinafanyika, uharibifu ambao unafanyika na ubadhirifu ambao unafanyika si tu kwamba ni hasara kubwa kwa Serikali ambayo inatafuta fedha za kujenga miundombinu katika maeneo mbalimbali kujibu kero na shida za wananchi, zinabomoa Imani ya wananchi kwa Serikali yetu, jambo ambalo halivumiliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maoni yote ambayo tumetoa na maazimio yote, naomba sasa kutoa hoja kwako ili iungwe mkono na Wabunge wote kwamba Maazimio yote ya

Bunge na ushauri wa Wabunge sasa uingie kama sehemu ya Maazimio ya taarifa yetu kama Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu sasa nitawahoji Wabunge kuhusu Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuwa Maazimio ya Bunge.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Maazimio ya Taarifa ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Wote mmeafiki, basi nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Makamu Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge mliopata nafasi ya kuchangia kwenye hoja ya Kamati hii. Tunawapongeza pia upande wa Serikali tunashukuru kwa ufafanuzi na chukueni Maazimio haya ya Bunge na kwenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninamwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Mhagama aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na Mheshimiwa Mwenyekiti wa

Kamati ya TAMISEMI kukushukuru wewe, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge ambao wametupa ushirikiano mkubwa sana kama Kamati. Nitumie pia fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Naibu Mawaziri ambao wamepata fursa yakuchangia taarifa hizi zote mbili ambazo zilikuja mbele yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliyochangia hoja za Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria ambao kwa idadi yao wanafikia sita pamoja na Naibu Mawaziri watatu, walichangia hizi hoja kwa ufasaha sana na Waheshimiwa Wabunge na Naibu Mawaziri wote waliyochangia walipata fursa ya kuunga mkono maeneo yote ambayo kamati yetu ilileta kama mapendekezo kwenye Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo kadhaa ambayo nilitamani niwekee mkazo kwa sababu kwa sehemu kubwa michango yote ya Wabunge na Naibu Mawaziri imejielekeza kuunga mkono hoja pia kulihitajika ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hoja zetu za Kamati, Kamati ilipendekeza kwa Serikali, iliitaka Serikali kupitia Wakala wa Ndege za Serikali kuongeza ndege moja kwa ajili ya matumizi ya viongozi. Ipo kasumba kwa baadhi ya Watanzania wenzetu kuamini kwamba kila aina ya usafiri ni starehe lakini wewe unajua uwekezaji kwenye vyombo vya usafiri siyo wakati wote ni starehe na vyombo vya usafiri siyo wakati wote ni *liability*, wakati mwingine au kwa sehemu kubwa usafiri unaohusu masuala ya utawala ni *asset*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana na mimi ndege ya Serikali F28, ilinunuliwa mwaka 1978 na ilinunuliwa na Baba wa Taifa kwa matumizi ya Serikali kwa maana ya viongozi, in aumri sasa wa zaidi ya miaka 39 bado watu wanaamini kwamba tungeweza kutumia fedha hizi tunazopendekeza kujenga vituo vya afya na zahanati, lakini ili haya yote yaweze kufanyika ni lazima kuhakikisha kwamba viongozi wetu kwanza wanakuwa salama lakini pili wanasafiri kwa haraka ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kujenga nchi kubwa kama Tanzania bila kuhakikisha kwamba wale viongozi wakubwa ambao tunawakabidhi majukumu mazito yakusimamia maslahi mapana ya Taifa letu hawawekewi mazingira salama ya usafiri lakini mazingira yatakayo wawezesha kufanya kazi hizo kwa ufanisi mkubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya awamu ya sita kwa haraka haraka tu imejenga hospitali za Kanda 16, imejenga hospitali za Mikoa 62, imejenga hospitali za Wilaya 351 lakini tunavyo vituo vya afya 1,126, tuna idadi ya zahanati zaidi ya 7,000, tuna shule za sekondari zaidi ya 486. Haya yote yamefanyika ndani ya Awamu hii ya Sita, mambo haya yanahitaji uwezeshwaji mkubwa wa shughuli za kiutawala, kuwawezesha viongozi wetu kuweza kuendelea kuyasimamia haya yaliyokwisha fanikiwa lakini kwenda kuwezesha mengine mengi zaidi ambayo Watanzania tunayahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niliombe Bunge lako liridhie Maazimio haya ya Kamati ya kuitaka Serikali iongeze ndege moja kwa ajili ya kuwezesha shughuli za utawala kwa matumizi ya viongozi ili F28 iweze kupumzishwa ili kurinda usalama na ustawi wa viongozi wetu ambao wanafanya kazi kubwa sana kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ambayo nilitamani niifafanue na niiseme kidogo kwa kina ni hoja hii ya madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya ni janga kubwa sana kwa Taifa letu, hii nashukuru Waheshimiwa Wabunge waliyopata nafasi ya kuchangia wamesema hivyo akiwemo Mheshimiwa Florent Kyombo - Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii lakini pia Mheshimiwa Naibu Waziri Patrobass Katambi, ameelezea kuhusu hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha ukisikiliza takwimu. Kati ya mwaka 2017 mpaka 2020 matumizi ya madawa ya kulevya yameongezeka mara nne, yameongezeka mara nne katika muda huo mfupi lakini idadi ya watumiaji wa madawa ya kulevya kwa takwimu za mwaka 2019 duniani walifikia milioni 200. Sasa milioni 200 tafsiri yake ni nini, hii kwanza ni asilimia nne ya watu

wote waliopo duniani na tafsiri yake nini, tafsiri yake katika kila watu 100 watu wanne wanatumia madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge hapa tupo karibu mia tatu na tisini na kitu, tafsiri yake ni nne mara nne kama watu 16 watakuwa wanatumia madawa ya kulevya. Naeleza tu tafsiri ya kitakwimu, hizi ni tafsiri za kitakwimu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hali hii siyo ya kuifanyia dhihaka, niweke tu taarifa vizuri kwamba huu ni mfano kwamba tuna Wabunge karibu 400 humu ndani na kwa tafsiri ya nne kwa 100 maana yake ni kama watu 16 siyo jambo la kulifanyia dhihaka na wote tunajua madhara ya matumizi ya madawa ya kulevya, Taifa letu linaangamia, Watanzania wanazidi kuwa *useless* katika sekta ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya ukifuatilia hata wale wanaopata huduma za urahibu wapo pia watumishi wa umma ambao wameonekana wanatumia haya madawa ya kulevya, kwa hiyo hatari yake ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilitaka niliombe Bunge lako tumpongeze sana, sana Kamishina Jenerali Arestas James Lyimo ambaye ameonyesha mfano katika usimamizi wa jambo hili, lakini niipongeze sana Serikali katika ujumla wake wamefanya kazi kubwa sana kwenye usimamizi na udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevya pamoja na biashara yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuja na mapendekezo mahsusi au pendekezo mahsusi kwenye eneo hili na misingi ya pendekezo letu ni hii. Mnafahamu kwenye taarifa yetu mmeona yapo mashauri 1,158 ya dawa za kulevya hadi sasa, kati ya hayo ni mashauri 64 pekee ndiyo yamefanyiwa kazi hadi sasa. Kwa hiyo, mnaweza mkaelewa mzigo mkubwa ambao Mahakama zetu zinazo. Kwa hiyo, tumetoa ushauri, tumetaka iundwe *division* maalum ambayo itakuwa inashughulikia mashauri ya madawa ya kulevya, faida zake ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza itawawezesha watoa maamuzi kwa maana ya Mahakimu wetu kubobea kwenye eneo hili la madawa ya kulevya mbinu na mikakati ambayo inatumiwa na wahalifu kwenye eneo hili, pia itawezesha Serikali kutenga rasilimali mahsusi kabisa kwa kushughulikia mashauri ya aina hii ili yaishe kwa wakati ili Watanzania wawe salama zaidi. Nashukuru katika michango ya Waheshimiwa Wabunge hakuna ambaye ameonesha kutoridhika na hoja hii na ninaamini Bunge lako litaipitisha kwa maslahi mapana ya Watanzania lakini kwa usalama wa Taifa letu na watoto wetu. Hayo ni maeneo mawili muhimu ambayo nilitaka niyaseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge pia wameongelea kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kwenye hili niseme tu kifupi kwa sababu muda umeisha, Serikali mnakumbuka tumelizungumza sana suala hili. Watanzania wengi wanalalamika juu ya haki zao kuvunjwa na kwa sehemu kubwa zinavunjwa na baadhi ya taasisi ambazo tumezitungia sheria ya kusimamia mambo mbalimbali. Kwa hiyo, tunaomba sana hizi sekta za taasisi za umma ambazo zimepewa wajibu wa kuwahudumia Watanzania kwa namna moja au nyingine wahakikishe wanalinda haki za binadamu na wanasimamia utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora tumeielekeza ilete taarifa mbele ya Kamati na hapa niombe kusisitiza kwamba tupewe hii taarifa ya Tume ili Kamati ipate mwanya au fursa pana yakuishauri Serikali juu ya malalamiko mengi ambayo Watanzania wanayo juu ya uvunjifu wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mengine ambayo yamekwisha zungumzwa, masuala ya Muungano mnajua *credit* kubwa inaenda kwa Mheshimiwa Rais mwenyewe kuhakikisha kwamba hoja 22 kati ya hoja 25 zinafanyiwa kazi na taasisi 33 kati ya taasisi 36 za Muungano ambazo zilitakiwa ziwe na ofisi Zanzibar, tayari zinaofisi, hayo ni mafanikio makubwa na hii ni *credit* kubwa kwa Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua tunayo Sheria ya Maafa, tumeona namna ambavyo Serikali imeshughulikia maafa na Waheshimiwa Wabunge wamesema hapa, nami niseme tayari tunayo sheria ya kushugulikia maafa nchini, ina miaka kama mitatu hivi, lakini tumetengeneza mfuko kisheria wa kushughulikia maafa nchini. Tunao mkakati mahsusi wa kushughulikia maafa nchini. Kamati imeomba taarifa juu ya utekelezaji wa haya yote ninaamini Serikali itajipanga ilete mbele ya Kamati taarifa hizi ili pia iweze kushauri na ilete mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho lilikuwa msaada wa kisheria kwa kupitia hii *Mama Samia Legal Aid*. Tunajua namna ambavyo imekuwa na faida kubwa kwa Watanzania na hapa imetolewa mifano kivipi leo Watanzania kwa idadi kubwa ile wanakwenda kueleza matatizo yao kwa viongozi wetu wa chama. Ni jambo zuri ni kwamba watanzania wana imani na Chama Cha Mapinduzi, wana imani na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni taswira nzuri lakini nyuma yake kuna changamoto. Changamoto mojawapo ni kwamba hawa wananchi wetu wengi hawajapata nafasi yakusikilizwa, kwa hiyo moja ya namna nzuri ya kutatua changamoto hii ni kuiwezesha *Mama Samia Legal Aid* iweze kufikisha huduma kwa Watanzania walioko vijijini. Kwa hiyo Serikali inapotafakari namna yakutatua changamoto hizi pamoja na zile ambazo Waheshimiwa Wabunge wamesema, iangalie uwezekano wa kuongeza nguvu kwa *Mama Samia Legal Aid* iweze kuwafikia Watanzania wengi zaidi waweze kupata suluhu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Naibu Waziri wa masuala kwa sasa yupo ardhi lakini alikuwa Katiba na Sheria huko nyuma, ameeleza kwamba hatuwezi tukawatumia Maafisa wa Sheria wa Halmashauri kwenye eneo hili lakini sasa ndiyo hatuna watu tufanyeye, Serikali mtupe suluhisho kwenye jambo hili ili tuweze kukabiliana nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba nitoe hoja ya kwamba tunaliomba sasa Bunge lako Tukufu liridhie hoja za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuwa maazimio ya Bunge.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Maazimio ya Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, wote mmeafiki. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati kwa kazi nzuri, Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa kazi nzuri na Waheshimiwa Wabunge mliopata nafasi ya kuchangia pia tunawapongeza wote kwa kazi nzuri na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla wenu. Upande wa Serikali pia tunawapongeza kwa ufafanuzi, myachukue Maazimio ya Bunge na kwenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.00 Usiku Bunge Lilihairishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 14 Februari, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*